**14 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 14 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA- KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Nyamoga.

Na. 325

### Ujenzi wa Barabara Idete - Mngeta Kilolo

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara kutoka Kijiji cha Idete hadi Mgeta?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Idete - Mngeta ni barabara inayojumuisha barabara za Idete - Itonya kilometa 9, Itonya - Mhanga kilometa 4.5 na Mhanga - Mngeta kilometa 17 hivyo kufanya barabara ya Idete - Mngeta kuwa na urefu wa kilometa 30.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuifanyia matengenezo barabara hiyo ambapo katika mwaka 2022/2023 kilometa 13 zimetengenezwa katika kipande cha Mhanga - Mgeta kwa gharama ya shilingi milioni 282.5. Kwa mwaka 2023/2024 zimetengwa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuendelea kukiimarisha kipande cha Mhanga - Mngeta. Aidha, imetengwa shilingi milioni 456.4 kwa ajili ya matengenezo ya kipande cha Kimala – Idunda - Mhanga - Itonya (kilomita 22) na sasa Mkandarasi yupo uwandani anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhudumia miundombinu ya barabara za Wilaya ya Kilolo ili kuhakikisha inaendelea kuwa katika hali nzuri kwa kuendelea kutenga fedha kulingana na bajeti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Wizara ninayo maswali mawili. Swali la kwanza; ziko barabara ambazo zimekatika kata tatu ambazo nimekuwa nikizitaja hapa mara kwa mara. Barabara ya Kimala – Msonza – Masisiwe - Boma la Ng'ombe na Barabara ya Ukwega - Lulindi. Barabara hizi hazipitiki na zimesababisha changamoto kubwa. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za dharura kwa haraka ili matengenezo yaweze kufanyika wananchi wapate mawasiliano?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Barabara ya kutoka Mngeta - Idete ilijibiwa swali ni barabara inayounganisha na Mlimba, Mkoa wa Morogoro na ni barabara muhimu, imetengewa shilingi milioni 100 na haziwezi kutosha. Je, kwenye mipango ya bajeti ijayo ni kiasi gani cha fedha kimetengwa ili barabara hii iweze kukamilika na wananchi waendelee kupita? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge katika kata tatu

Barabara ya Boma la Ng'ombe - Masisiwe barabara hii imeombewa fedha za dharura na nimhakikishie barabara hii itajengwa. Barabara ya Msonza - Kimala yenyewe imetengewa milioni 51.3 katika bajeti ya mwaka huu wa fedha na tayari mkandarasi amepatikana, baada tu ya mvua kukatika kazi ya ujenzi wa barabara hii itaanza. Barabara yake ya Idete - Mngeta na yenyewe ni sehemu ya Barabara ya Mhanga - Mngeta ambayo imeidhinishiwa milioni 100 na ujenzi utaanza wiki ijayo. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara zake hizi alizozitaja na amekuwa akizizungumzia mara kwa mara, lakini hata mimi na yeye tulikaa kuzijadili, nimhakikishie barabara zake hizi zitajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili kuhusiana na hii Barabara ya Idete - Mngeta ambayo imetengewa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi anasema kwamba fedha hii anaona haitoshelezi. Nimhakikishie tayari Serikali imeanza kwa awamu hii tumetenga milioni 100, katika mwaka mwingine wa fedha tutatenga fedha zaidi ili kuhakikisha barabara hii inajengwa kwa viwango na inaweza kuwasaidia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Ikola kwenda Kata ya Isengule imekatika na madaraja yamesombwa na mawasiliano hayapo kwa sasa. Je, ni lini Serikali itaenda kukarabati barabara hiyo ili wananchi waweze kupata huduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha kwamba mawasiliano hayakatiki. Kwa hiyo kwenye maeneo yote ambayo miundombinu imekatika na wananchi wanakosa mawasiliano, basi Serikali inaweka kipaumbele na inachukua ujenzi wa miundombinu hiyo kama dharura. Kwa hiyo nimhakikishie tukitoka

kwenye kipindi hiki cha maswali na majibu mimi na yeye tutazungumza ili kuhakikisha katika mipango ya dharura ya ujenzi wa barabara hizi na barabara hii aliyoitaja iweze kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Juzi tulipokuwa kwenye kikao cha mabalozi pale Mafinga walilalamikia kwamba barabara ya kwenda Kituo cha Afya cha Ifingo mkandarasi amerundika tu kifusi hajaendelea na kazi. Je, ni lini watafanya msukumo ili amalize kazi ile ya muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu hii inajengwa kuhakikisha kwamba huduma za kijamii zinaweza kuwafikia wananchi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mimi na yeye tutazungumza baada ya kutoka hapa ili tuweze kufuatilia ni kitu gani kinakwamisha utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu katika barabara aliyoitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Akheri kuanzia Sing'isi hadi Ndoombo ambayo ujenzi wake unakwenda kwa kusuasua sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameshawahi kunieleza kuhusiana na umuhimu wa barabara hii na nirejee makubaliano tuliyozungumza kati ya mimi na yeye kumhakikishia kwamba, barabara hii itajengwa ili iweze kuwanufaisha wananchi wake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka.

Na. 326

**Ujenzi wa Barabara ya Frank Weston – Misechela – Tunduru**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Frank Weston Tuwemacho – Namasakata hadi Misechela – Tunduru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami kwani barabara za lami zinadumu kwa muda mrefu na zinahitaji matengenezo yasiyo na gharama kubwa. Aidha, *TARURA* inasimamia mtandao wenye jumla ya kilometa 144,429.77 ambapo barabara zenye kiwango cha lami ni kilometa 3,224.12 sawa na 2.23%; kiwango cha changarawe ni kilometa 41,107.52 sawa na 28.46% na kiasi kinachobaki cha urefu wa kilometa 100,098.13 sawa na 69.31% ni barabara za udongo. Kutokana na hali ya fedha iliyopo, kipaumbele cha Serikali ni kujenga barabara zenye mifereji kwa kiwango cha changarawe ili ziweze kupitika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Frank Weston Tuwemacho – Namasakata hadi Misechela ina urefu wa kilometa 62.9 ambapo kati ya hizo kilometa 41.9 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa 21 bado ni za udongo. Mwaka 2022/2023, Serikali ilitenga shilingi milioni 104 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo ambapo kilomita 15 zilichongwa kati ya hizo kilomita tano ziliwekewa changarawe na kalvati mbili zilijengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka huu wa Fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi milioni 225 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo ambapo kilomita 21 zimechongwa. Kati ya hizo kilomita nane zimewekewa changarawe. Aidha, Serikali itaendelea kuihudumia barabara hii kwa kutenga bajeti kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali itatengeneza lini Barabara ya kutoka Mashariki inayopitia Nasomba hadi Lukala, Kata ya Mchesi ili iweze kupitika muda wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara yenye sehemu korofi kwa urefu wa kilometa 16 kutoka Milunde kwa Chami hadi Kalulu kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwenye maswali yake yote mawili, naomba niyajibu kwa pamoja. Serikali itahakikisha inajenga barabara hizi muhimu na Serikali ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan imeongeza bajeti ya barabara za *TARURA,* barabara za wilaya kutoka bilioni 275 mpaka sasa ni bilioni 710. Yote hiyo ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kuhudumia barabara zetu hizi za wilaya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kadri fedha zitakapokuwa zinapatikana, tutahakikisha barabara hizi zinajengwa ili wananchi waweze kuzitumia na uchumi uweze kukua kwa maana barabara hizi zinachochea uchumi kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula, jiandae Sanga.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuwa Barabara ya kutoka Mkuyuni kwenda Tambuka Reli – Butimba - Nyangulugulu mpaka Mahina upembuzi wake na usanifu umeshakamilika kwa 100%, kinachosubiriwa ni kuanza kwa ujenzi wa kiwango cha lami na fedha ilishatengwa. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii kwa ajili ya kusaidia wananchi wanaotumia barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, baada ya mvua kukatika, wakandarasi wataingia uwandani na barabara hiyo itaanza kujengwa. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wako, watapata barabara hii kwa kiwango cha lami hivi karibuni baada tu ya mvua kukatika kwa kuwa wakandarasi wataingia *site*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO D. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Iwawa- Isaplano hadi Nkenja ni barabara ya kiuchumi na Serikali kupitia *TARURA* iliitenga kama sehemu ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami ya kisasa ya majaribio, taarifa tulizonazo ni kwamba imeondoka. Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wa Makete kuhusu barabara hii kujengwa kwenye kiwango cha lami kama ambavyo waliahidi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Iwawa – Isaplano - Nkenja ni miongoni mwa barabara ambazo zipo katika majaribio ya ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia ya kisasa yaani *Eco-roads.* Kwa hiyo, ni kweli barabara hii ilitengewa fedha kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha teknolojia mpya ya lami kwa kilometa 12. Baada ya kufanya *testing* ya udongo ikabainika kwamba teknolojia ile haiendani na udongo wa Makete, lakini sasa hivi Serikali ipo katika

mpango wa kuhakikisha inapatikana teknolojia inayoendana na udongo wa Makete ili barabara hii iweze kujengwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge barabara yake ya kilometa 12 ya Iwawa-Isaplano - Nkenja itajengwa kwa kutumia teknolojia mpya ya ujenzi wa barabara kwa maana ya *Eco-roads*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itaanza kurekebisha barabara zilizopata athari ya mvua hizi katika Jimbo la Mbagala na ukizingatia mvua sasa zimeisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa Serikali inatambua madhara makubwa ambayo yamejitokeza kwenye barabara zetu hizi kutokana na mvua. Nikupe taarifa bajeti maalum ya bilioni 350 imepatikana kwa ajili ya kuhudumia barabara hizi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge, baada ya mvua kuisha katika mwaka mpya wa fedha, tayari ataanza kuona wakandarasi wanaingia *site* kwa ajili ya kuanza kufanya marekebisho ya barabara hizo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deus.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kujenga barabara za mitaa kwa kiwango cha lami katika Mji mdogo wa Laela. Ni lini Serikali itatimiza ahadi hii? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama vile Serikali iivyoahidi ujenzi wa barabara hizo kwa kadri ya upatikanaji wa

fedha, Serikali itahakikisha inakuja kujenga barabara hizo katika jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

Na. 327

**Ujenzi wa Mabweni na Mabwalo katika Shule za Sekondari – Masasi**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Mabweni na Mabwalo katika Shule za Sekondari za Marika, Temeke, Chanikanguo, Anna Abdallah na Mtandi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka kipaumbele katika ujenzi wa mabweni kwenye shule za sekondari za kidato cha tano na sita nchini ambapo katika mwaka 2022/2023, Serikali ilijenga jumla ya mabweni 683 kupitia fedha za mradi wa *SEQUIP*, *Barrick* Tanzania na Serikali Kuu. Aidha, katika mwaka 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.41 kwa ajili ya ukamilishaji wa mabweni 57.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele cha ujenzi wa mabweni na mabwalo ya kidato cha tano na sita kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu kidato cha nne wanapata fursa ya kusoma kidato cha tano na sita. Aidha, Serikali itaendelea na jitihada zake za kuhamasisha wananchi kupitia mamlaka za Serikali za Mitaa kujenga na kuziendesha hosteli katika shule za sekondari za kidato cha kwanza hadi cha nne.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningependa kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali iko tayari kutuunga mkono kwenye ujenzi wa Bwalo kwenye Shule ya Sekondari ya Sululu ambayo tayari wananchi wameshajenga mabweni mawili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tumejenga shule kwenye kila kata, kuna changamoto nyingi sana za watoto wa kike kupata ujauzito, pia na watoto kutopata ufaulu uliotosheleza. Je, Serikali haioni haja ya kuanza kujenga mabweni kwenye shule zetu hizi za sekondari ili watoto waweze kunufaika na ukaaji mabwenini na kukuza taaluma zao pamoja na nidhamu? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeshafanya tathmini ya kuona maboma yanayohitaji kukamilishwa ambayo yapo kwenye sekta ya elimu. Tathmini hiyo imeonesha wastani wa kiasi cha shilingi bilioni 300 kinahitajika, kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inahakikisha inapata fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma haya ambayo wananchi wameyaanza kwa kutumia nguvu zao kuunga mkono jitihada za Serikali. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge boma hili la bweni alilolitaja litajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa ujenzi wa mabweni, kwa ajili ya wanafunzi wetu wa kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, nimesema

kwamba, Serikali itaendelea na jitihada za kuhamasisha wananchi, kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha *hostel* zinaendelea kujengwa kwa ajili ya shule hizi za kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazikumbusha pia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba, wanatenga fedha katika bajeti zao, kwa maana ya katika mapato yao ya ndani ili kujenga miundombinu hii muhimu kwa kuzingatia kuwa huo ndiyo msingi wa ugatuzi kwa maana ya *D by D*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali ilitoa shilingi milioni 80 kujenga Mabweni ya Sekondari ya Nyamang'uta na Sekondari ya Mihingo, lakini mpaka sasa ni miaka mitano mabweni hayo hayajamalizika. Je, ni lini Serikali itamalizia mabweni hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, lengo la Serikali ni kuhakikisha miundombinu muhimu ya mabweni inakamilika na wanafunzi wanaweza kutumia mabweni hayo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, Serikali itahakikisha mabweni hayo aliyoyataja yanakamilika ili wanafunzi waanze kuyatumia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Serikali ilitoa fedha, kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za wananchi ambao walikuwa wamejenga mabweni mawili katika Sekondari ya Iseke na Sekondari ya Kintinku, lakini fedha zile hazikutosha. Je, ni lini Serikali

itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha mabweni hayo ili yawasaidie watoto wa kike? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa miundombinu hii ya mabweni katika shule zetu. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali itaendelea kutafuta fedha na itahakikisha inapata fedha kwa ajili ya kukamilisha mabweni haya ili wanafunzi waweze kuyatumia na wapate mazingira mazuri zaidi ya kusomea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman.

Na. 328

**Kutengeneza Fukwe Zilizoathirika Zanzibar**

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza fukwe za bahari zilizoathirika upande wa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imepanga kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa fukwe zilizoathirika kwa upande wa Zanzibar ambapo jumla ya shilingi 661,000,000 zimetengwa kwa ajili ya miradi hiyo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 300,000,000 zitatumika kukamilisha ujenzi wa matuta ya kuzuia maji ya bahari kuingia sehemu ya mashamba ya mpunga katika Shehiya ya

Mgogoni, Mkoa wa Kusini Pemba, katika Ufukwe wa Sipwese na shilingi 361,000,000 ni kwa ajili ya kufanya tathmini katika Eneo la Nungwi, Visiwani Zanzibar ili kusanifu namna bora ya kudhibiti uharibifu unaoendelea. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, Serikali ina mkakati gani kwenda kurekebisha baadhi ya maeneo ya fukwe yaliyoathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuna baadhi ya maeneo yapo sehemu ya fukwe na yana takataka nyingi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti takataka hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, swali la pili sikulisikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia swali la pili.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo ya fukwe yameathirika na takataka, kwa maana ya uchafu. Sasa je, ni mpango gani upo ama labda mkakati gani endelevu upo kwa ofisi yake kuweza kuondoa takataka hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suleiman, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hatua mbalimbali ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumezichukua katika kuhakikisha kwamba, tunaenda kukabiliana na changamoto kubwa ya athari ya mabadiliko ya tabianchi. Kwanza, ni kuanzisha miradi mbalimbali ambayo inakwenda kusaidia kutatua changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo miradi ya ujenzi wa kuta ili mabadiliko ya maji ya bahari yasiweze kuingia kwenye vipando na maeneo ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kutoa elimu mbalimbali, lengo na madhumuni ni kuwawezesha wananchi kuelewa umuhimu wa kutunza mazingira. Kikubwa zaidi, tayari tunaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuona namna ambavyo tunawashurutisha wananchi waendelee kutunza na kuhifadhi mazingira, ili waepukane na athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la uchafu ama taka ambazo Mheshimiwa amezungumzia; tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia halmashauri, manispaa, mabaraza ya miji na majiji yote, imeshaanza hatua ya kufanya usafi kila mwezi kwa lengo na madhumuni ya kuufanya mji uwe safi kutokana na taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vikosi vya SMZ, hasa Kikosi cha KMKM cha Commodore, Msingiri, tayari kuna hatua mbalimbali wameanza kuzichukua za kufanya usafi katika mji kila mwezi. Lengo na madhumuni ni kuusafisha mji huo, kuondoa taka na uchafu ambao unaweza ukatokea katika Mji wa Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Bishop* Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa sababu ya mvua nyingi zilizonyesha kupita kawaida katika Jimbo la Kawe, Mto Nakasangwe, Mto Tegeta, Mto Mpiji na mito mingine imepanuka na kufikia *almost* mita 300. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ametoa shilingi bilioni moja kwa ajili

ya kutengeneza mito. Je, yupo tayari kwenda pamoja na mimi akaangalie hali halisi ya mito katika Jimbo la Kawe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuona hali ilivyo na kuwasaidia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khalifa Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mtambwe Mkuu ni katika visiwa ambavyo vimeathirika sana na vina makazi ya watu. Je, ni lini utafanyika huo mpango wa kujengewa matuta kuzuia maji ya bahari kutoathiri visiwa hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunatambua kwamba, kuna hiyo changamoto huko Mtambwe. Namwomba tu Mheshimiwa tunamaliza Ukuta wa Sipwese, Kusini Pemba, kisha tutakuja Mtambwe Mkuu, Kaskazini Pemba.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Hali ya uharibifu wa fukwe za bahari zinazoathiriwa na maji Kisiwani Zanzibar inafanana kabisa na hali ya Fukwe za Kisiwa cha Mafia. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuzitengeneza fukwe hizo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tupo tayari

kurekebisha ama kufanya usafi wa maeneo ya fukwe kwa kushirikiana na wananchi na yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge. Tutafanya hivyo kama ambavyo Mheshimiwa amependekeza. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis.

Na. 329

**Huduma za Marekebisho kwa Watoto Wenye Ulemavu**

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha huduma za marekebisho kwa watoto wenye ulemavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha huduma za marekebisho kwa watoto wenye ulemavu Serikali inatekeleza afua mbalimbali kupitia Wizara za Kisekta ikiwemo:-

(i) Kuweka moduli katika mtaala wa mafunzo ya walezi wa watoto ili kuwezesha kufanyika kwa utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu wanapokuwa katika vituo vya kulelea watoto wachanga na watoto wadogo mchana, kaya na familia.

(ii) Vilevile Serikali inawaunganisha watoto husika na huduma stahiki za kijamii zilizo kwenye Wizara za Kisekta kulingana na aina ya ulemavu mathalani; matibabu na

vifaa saidizi, huduma za lishe na kufanya uchangamshi wa awali kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii walio katika Hospitali, Wilaya na Kata ili kupunguza makali ya ulemavu kwa watoto.

(iii) Na hatua ya mwisho ni, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia Maafisa Maendeleo na Ustawi wa Jamii juu ya namna ya kuepuka ulemavu utotoni, elimu ya lishe bora kwa watoto na elimu kuhusu kuwapeleka watoto katika vituo vya kutolea huduma ili waweze kupewa huduma stahiki kulingana na aina ya ulemavu walionao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantatu.

**MHE. MWANTATU MBARAK KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini mbali ya watoto ambao wapo katika vituo pia, kuna watoto ambao wapo katika vijiji na mitaa, hasa vijijini. Pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kutoa elimu kupitia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, je, Serikali ina mpango gani au haioni kuwa, sasa ipo haja ya kutafuta wafanyakazi wa kujitolea katika ngazi ya vijiji wakapewa mafunzo ili huduma hii isogee karibu na jamii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis. Serikali ina mpango wa kufikisha huduma hii ya kuwarekebisha watoto hawa mpaka kwenye ngazi ya familia na jamii na kwamba, inatekeleza mpango wa kuwadahili wahudumu wa ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahudumu hawa wataungana na Maafisa Maendeleo na Maafisa Ustawi wa Jamii na kujengewa uwezo kuwa wanafuatilia kuanzia kwenye ngazi ya familia ili kuweza kuwabaini mapema pamoja na kuzuia kwa kuielimisha jamii, wazazi, walezi na wanafamilia jinsi ya kufanya ili kuepuka

vitu vinavyoweza kusababisha mtoto mwenye ulemavu kupatikana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Rweikiza.

Na. 330

**Mradi wa Maji wa Kemondo – Maruku**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Mradi wa Maji wa Kemondo, Maruku, umechukua muda mrefu kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mradi wa Maji Kemondo, Maruku, unaotekelezwa kwa awamu tatu ambapo awamu ya kwanza imefikia wastani wa 95% na inatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2024 na kunufaisha vijiji vitano vya Rwagati, Kanazi, Katoju, Buganguzi na Minazi. Aidha, awamu ya pili ya mradi huo imeanza utekelezaji ambapo umefikia wastani wa 67% na inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2024 na kunufaisha Vijiji vya Butayabega, Bulinda, Mulahya na Maruku.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya tatu ambayo itahusisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika vijiji vya Kata mbili za Muhutwe na Kanyengereko itaanza baada ya awamu ya pili kukamilika. Kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kulisababishwa na kuchelewa kupokelewa kwa pampu za kusukuma maji zilizoagizwa kutoka Nchini Uturuki ambapo kwa sasa zimepokelewa na kazi ya ufungaji inaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Rweikiza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Katika awamu ya kwanza kuna madeni makubwa sana ya zaidi ya shilingi bilioni tatu ambayo ndicho chanzo cha sababu ya mradi kuchelewa. Je, ni lini madeni haya yatalipwa na Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya pili ya kupeleka maji Kanyangereko na Maruku mkandarasi mmoja alifukuzwa, alishindwa kazi na akaondolewa, mpaka leo ni karibu mwaka mzima tangu ameondolewa. Je, ni lini tutapata mkandarasi wa pili ili kazi iendelee?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Rweikiza kwa kazi kubwa aliyoifanya na kwa kuomba hii miradi. Aliiomba mbele ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais akaridhia kuanzishwa kwa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madai. Serikali inatambua kuwa kuna madai ambayo mkandarasi anadai na ni takribani shilingi bilioni 2.971, ambapo tayari Serikali kupitia Wizara ya Maji tumeshawasilisha Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufanyika haya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipengele cha pili, ni kweli kabisa mkandarasi aliyekuwepo hakuweza kufanya ule mradi kwa ubora uliokuwa unatakiwa, lakini vilevile alikuwa nje ya muda. Kwa sababu hiyo Serikali ilichukua hatua ya kuhakikisha kwamba, tunawasilisha taarifa hii *PPRA* ili kuanza hatua ya pili na sisi Serikali tumeuingiza tena mradi huu katika Bajeti ya 2024/2025. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, hatua za manunuzi

zitakapokamilika, basi mkandarasi atapatikana na kazi ya ujenzi wa mradi huo itaendelea. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwau.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nataka kujua ni lini Mradi wa Maji wa Kintinku, Lusilile, katika Wilaya ya Manyoni ambao unahudumia vijiji 11 utakamilika ili wanawake wa Tarafa ya Kintinku wapate huduma ya maji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maelekezo ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kwamba, miradi yote ambayo imekwama kwa muda mrefu inafanyika na kukamilika kwa wakati ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anaendelea kupambana kuhusu mradi huu aendelee kutupatia ushirikiano ili sisi tuweze kutimiza majukumu yetu na kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata maji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba kuuliza, Miradi ya Maji ya Kijiji cha Kitundueta, Kata ya Muhenda, Mikumi na Kidodi ni lini inaaenda kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilipokee na baada ya kutoka hapa nikutane na Mheshimiwa Londo, ili tuweze kuangalia mradi wake umefikia hatua gani. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri aliahidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni nne, kwa ajili ya Mradi wa Maji katika Wilaya ya Karatu. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jiandae Mheshimiwa Kilave.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, naomba nipate maswali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso rudia swali lako.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri, kwa maana ya Serikali, alitoa ahadi ya kutoa kiasi cha shilingi bilioni nne, kwa ajili ya mradi wa maji katika Wilaya ya Karatu. Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia kwa sababu, lengo ni wananchi wapate maji. Namwahidi kwamba, hili nalipokea na nakwenda kulishughulikia ili kujua ahadi hiyo imefikia katika hatua gani ili kuhakikisha kwamba miradi inaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *DAWASA* wameshindwa kuendeleza visima ambavyo vimechimbwa hasa katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam na hasa Jimbo la Temeke. Kwa nini sasa msivirudishe kwa wananchi ili waviendeleze na kuvifanyia kazi kama mwanzoni kwa sababu, *DAWASA* wameshindwa kabisa kuvifanyia kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nasema mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, *DAWASA* kwa maana ya Wizara ya Maji hatujashindwa, isipokuwa tutaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba, tunatatua changamoto ambazo zinaendelea kujitokeza, lakini tunaamini kwa ushirikiano na Mheshimiwa Mbunge, akiwa ni mdau namba moja katika Jimbo la Temeke, tutahakikisha tunatafuta njia ambayo itarahisisha zaidi kutatua changamoto hiyo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Serikali haiwezi kushindwa jambo lolote isipokuwa utendaji wa kuendesha visima hivi ni wa kiwango cha chini sana. Wakati wananchi walipokuwa wanasimamia visima hivi maji yalikuwa yanatoka, sasa visima vingi maji hayatoki. Kwa hiyo nendeni mkalifanyie kazi.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Hassan Zidadu.

Na. 331

**Kukamilisha Visima vya Maji, Tunduru Kaskazini**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha uchimbaji wa visima vya maji vilivyoanza kuchimbwa katika Jimbo la Tunduru Kaskazini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipanga uchimbaji wa visima 13 katika Wilaya ya Tunduru, hususan katika Jimbo la Tunduru Kaskazini. Hadi sasa visima vitatu vimechimbwa katika Vijiji vya Fundimbanga, Ligunga na Majala. Aidha, taratibu za uchimbaji wa visima 10 katika Vijiji vya Ngapa, Mkanyageni, Malombe, Mkapunda, Namiungo, Sisi-kwa-Sisi, Mtengashari, Tumaini, Mkwajuni na Msamala zinaendelea ambapo uchimbaji wa visima hivyo unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, visima vitatu vilivyochimbwa na visima 10 vitakavyochimbwa vitajengewa vioski ili kutoa huduma ya maji kwa wananchi wakati Serikali inajipanga kujenga miradi mikubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, ni hatua gani imefikiwa kuhakikisha visima 10 vitakavyochimbwa vinakamilika kabla ya mwezi Disemba kwa kuwa mwezi Disemba tayari mvua zinakuwa zimeshanyesha? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge anaendelea kufuatilia miradi hii na tunashirikiana vizuri sana. Ni ukweli usiopingika kwamba Wizara yetu ya Maji

inaendelea kuhakikisha kwamba inatoa huduma inayozingatia ubora unaotakiwa na katika hivyo visima vitatu na vile 10 vingine ambavyo vitakuja kujengwa tutahakikisha vyote vinajengewa vioski ili wananchi waendelee kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipengele cha pili, ni kweli kabisa Serikali imeanza mchakato wa kumpata mzabuni kwa ajili ya mradi unaofuatia wa visima 10 kwa sababu tunatambua kwamba itakapofika Disemba na mvua ikianza tutashindwa kuchimba. Kwa hiyo, sasa tumeshajipanga kuhakikisha kwamba zoezi hilo linakamilika kabla ya Disemba. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha Miradi ya Maji katika Vijiji vya Kisimamkika na Zinga Kibaoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kukamilisha miradi yote inayoendelea nchini ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata fursa ya kupata maji safi na salama. Kwa hiyo, pamoja na nchi nzima maana yake pamoja na vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja tutahakikisha kwamba katika Jimbo lake tunafuatilia kwa ukaribu na wananchi wapate maji safi na salama na kujiepusha na magonjwa ambayo yanaweza yakatokana na maji. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, muda wetu umekwenda tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

Na. 332

**Kuwa na Hospitali Kuu ya Taifa**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakuwa na Hospitali Kuu ya Taifa moja ambayo itatoa huduma zote za afya bila kutegemea hospitali nyingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Issa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali ina Hospitali ya Taifa ambayo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili. Aidha, kwa sasa hatua za kuiboresha hospitali hii zinatekelezwa ili kuweza kutoa huduma zote za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna baadhi ya matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi bado hayapatikani. Je, ni lini Serikali itakamilisha utaratibu wa upatikanaji wa matibabu hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa mifumo ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na ile ya Jakaya Kikwete haisomani na hivyo kupelekea baadhi ya huduma ambazo zinapatikana upande mmoja haziwezi kwenda upande wa pili. Je, ni lini Serikali itahakikisha mifumo hiyo inasomana ili kuokoa maisha ya wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maswali mazuri ya Mheshimiwa Mohamed Said Issa kwamba ni lini sasa tutaanzisha huduma ambazo hazipatikani za ubingwa bobezi. Niseme kwamba tunaendelea kuanzisha huduma mpya kadri zinavyopatikana na utaalam unavyopatikana. Tunawashukuru Wabunge jana waliweza kutupitishia bajeti yetu ndiyo maana unaona sasa kuna huduma mpya ikiwemo za kufanya upasuaji mgumu kwa kutumia roboti, lakini pia na masuala mengine. Kwa hiyo, tutafanya kwa kadri ya upatikanaji wa utaalam na rasilimali fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo nataka kusema, sasa hivi karibu huduma zote zote za ubingwa na ubingwa bobezi zinapatikana katika Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili, kinachotukwamisha kidogo ni miundombinu na tunataraji kutumia zaidi ya shilingi bilioni 500 kuijenga upya miundombinu ya Hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu mifumo ya Muhimbili na Jakaya Kikwete kutosomana, ni kweli nakubaliana naye na jambo ambalo jana pia walitupitishia tunaenda kusimika mfumo mpya wa TEHAMA ambapo sasa hospitali zote zitakuwa zinasomana. Siyo tu masuala ya vipimo kati ya Muhimbili na Jakaya Kikwete, lakini hata kama umefanya kipimo Bombo Tanga nimepewa rufaa kuja Muhimbili kipimo changu na majibu yangu ya Bombo Tanga yataonekana Hospitali ya Taifa Muhimbili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Esther Malleko, kwa niaba yake Mheshimiwa Raymond.

Na. 333

**Kutoa Huduma ya *Ultrasound* bure kwa Wajawazito**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, lini huduma ya *Ultrasound* itatolewa bure kwa wajawazito wanapohudhuria kliniki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inatoa msamaha wa huduma za matibabu kwa makundi maalum ikiwemo akinamama wajawazito. Hivyo, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa sera hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi, Serikali imepitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo itawawezesha makundi yote kupata huduma za vipimo na matibabu bila kikwazo cha fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali, lakini kwa kuwa kipimo hiki cha *ultrasound* ni muhimu sana na sasa hivi vituo vya afya vimejengwa kwenye kila kata. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka *ultrasound machines* kwenye kila kituo cha afya kikiwemo Kituo cha Kata ya Uru Kusini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mama yangu Shally Raymond kwa maswali mazuri, lakini kwa kuwa mstari wa mbele katika kuboresha huduma za akinamama wajawazito, Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kipimo cha *ultrasound* ni muhimu na tunaendelea na zoezi la kusambaza *machine* za

*ultrasound*. Hospitali za wilaya tulishamaliza sasa hivi tunakwenda katika vituo vya afya na tunamshukuru Rais Dkt. Samia kwa kutuwezesha kufanya mapinduzi makubwa ya kusambaza ya hizi *ultrasound machines*, ngazi ya kituo cha afya pia tutafika. Mheshimiwa Shally nitakuja katika Kituo chako cha Afya cha Uru na tutakupatia *ultrasound machine*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tunaipongeza Serikali kwa kupanua mindombinu ya huduma za afya nchini. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kutoa huduma ya saratani ya figo kwa wagonjwa wote katika hospitali za wilaya na mikoa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, rudia swali lako tena kwa sauti, iweke *microphone* yako vizuri.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani wa kutoa huduma ya upimaji wa figo na matibabu yake katika hospitali za mikoa na halmashauri nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu ya saratani katika ngazi ya mikoa na kanda. Swali lake alikuwa anasema twende katika ngazi ya wilaya. Sasa hili kidogo linahitaji uwekezaji kwa sababu matibabu ya saratani yamegawanyika katika sehemu kubwa tatu: sehemu ya kwanza ni upasuaji, sehemu ya pili ni matibabu kwa kutumia tiba kemia *(chemotherapy)* na ya tatu ni *radiotherapy* kwa kutumia mionzi. Kwa hiyo, hatuwezi kupeleka huduma za mionzi katika ngazi ya hospitali za wilaya. Sasa hivi tunachofanya ni kushusha huduma za tiba kemia kutoka *Ocean Road* na hospitali za kanda kwenda katika hospitali za rufaa za

mikoa na tumeanza kwa Mkoa wa Arusha. Kwa hiyo, tutakwenda Mkoa wa Manyara, lakini ngazi ya hospitali ya wilaya bado kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri ameshakuelewa. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wajawazito wengi wanapata huduma kwenye vituo vya afya, nikataka kujua ni lini Serikali itapeleka huduma ya *ultrasound* kwenye vituo vyote vya afya Mkoani Mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Esther Matiko. Kama nilivyosema kati ya jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amelifanya katika kuboresha huduma za afya ni kuboresha huduma za akinamama wajawazito. Kwa hiyo, naahidi chini ya Rais Dkt. Samia kabla hajaondoka tutapeleka *ultrasound machines* katika vituo vya afya vyote nchi nzima, kwa sababu mimba salama ni pamoja na mjamzito kupima ili kujua masuala mbalimbali ya maendeleo ya ujauzito na mtoto.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, muda wetu unakwenda. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

Na. 334

**Uhitaji wa Taa Uwanja wa Ndege Mafia**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka taa Uwanja wa Ndege wa Mafia ili kuwezesha ndege kubwa kupeleka watalii kutembelea Kisiwa cha Mafia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka ujao wa fedha 2024/2025, Serikali ina mpango wa kufunga taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Mafia kwa ajili ya kuwezesha kutolewa kwa huduma za masaa 24 ambapo kutachangamsha uchumi wa Mafia na kukuza utalii nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ya kutia matumaini, naomba kuuliza. Swali la kwanza; je, Serikali au Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutaja kiwango kilichotengwa kwa ajili ya kuanza kazi hii ya kufunga taa katika Kiwanja cha Ndege cha Mafia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Mafia licha ya kwamba hauna taa lakini una uwezo wa kuruhusu ndege kubwa kutua na kwa kuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye Shirika letu la Ndege *ATCL*. Je, ni lini Shirika la *ATCL* litaanza safari ya kwenda Mafia ili kuwawezesha watalii hasa kipindi cha Mwezi wa Kumi mpaka wa Tatu ambapo utalii wa samaki mkubwa anayepatikana kwenye nchi sita tu hapa duniani aina ya samaki potwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyojenga hoja kuhusiana na Uwanja wa Ndege wa Mafia na nimhakikishie swali lake la pili kwamba tumeshaanza tathmini ya kina kufahamu mahitaji na habari za kutosha kuhusiana na Uwanja wa Mafia na tukikamilisha tutapeleka Ndege ya *ATCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza kuhusiana na habari aliyozungumza, kwanza nimkumbushe Serikali inafahamu umuhimu mkubwa sana wa Kiwanja cha Ndege cha Mafia

kilichojengwa miaka mingi iliyopita kuanzia wakati wa mkoloni na tumefanya kazi kubwa pale. Tulirekebisha *runway* tukajenga ambayo ina urefu wa mita 1,500 na upana wa mita 30, tukaongeza eneo la kuegesha ndege kiasi kwamba ndege sita ndogo *Caravan C208* zinaweza kutua pale. Kama hiyo haitoshi, tunapozungumza hapa tunafanya usanifu kwa ajili ya kuongeza jengo la abiria ili liwe na uwezo wa kubeba abiria zaidi kwa sababu jengo lililopo linabeba abiria 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, katika mwaka huu wa fedha nimeshamtamkia, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia inao mpango na inakwenda kuweka taa za kuongozea ndege katika kiwanja hicho. Atupe muda tu tutakwenda kukamilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Kahama unapokea watu zaidi ya 200 kwa siku. Je, Serikali ina mpango gani wa kuupanua na kuujenga kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Kahama ni moja ya viwanja muhimu kwa Taifa letu na kwa kushirikiana na wadau tumeshajenga jengo la abiria zuri sana. Tuko kwenye hatua za tathmini ili kuhakikisha kwamba tunajenga njia kwa ajili ya kuruka na kutua ndege.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Waziri ametueleza kwamba Uwanja wa Ndege wa Kahama uko kwenye *process,* sasa ni lini wakati wanasubiri mchakato huo wataanza kuleta safari za Ndege za *ATCL* ambazo zitatua Kahama? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ameleta kama ushauri, tumepokea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea muda wetu umekwisha. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

Na. 335

**Usalama wa Abiria Wanaotumia Meli ya *MV Victoria***

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itahakikisha usalama wa abiria na mali zao kwa wasafiri wanaotumia Meli ya *MV Victoria* ndani ya Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa abiria na mali zao kwa wasafiri wanaotumia meli ya *MV Victoria* ndani ya Ziwa Victoria ni suala la muda wote na ni kipaumbele namba moja kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* inahakikisha usalama wa abiria na mali zao kwa wasafiri wanaotumia vyombo vyote vya majini, ikiwemo meli ya *MV Victoria* ndani ya Ziwa Victoria kwa kukagua meli hizo mara kwa mara na kuzipatia vyeti vya ubora, ambapo kwa cheti hicho inamaanisha meli imekidhi vigezo vya usalama kwa abiria na mali zao, ulinzi na utunzaji wa mazingira majini. Aidha, meli zote ikiwemo *MV Victoria* zinasisitizwa kuwa na vifaa vya uokozi ambapo abiria melini hutangaziwa uwepo wa vifaa hivyo na jinsi ya kuvitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, *TASAC* inaendelea na mikutano ya uelewa na kufanya kaguzi za kushtukiza kwa meli na kuhakikisha manahodha na wafanyakazi wengine wote

wamepata mafunzo ya umahiri na kuwa na vyeti hai vinavyotolewa na *TASAC*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Meli ya *MV Victoria* husafirisha abiria kwa madaraja matatu, daraja la tatu, daraja la pili na daraja la kwanza. Mimi nilisafiri na meli hiyo kupitia daraja la kwanza, nikalala usingizi nilipoamka saa saba badala ya watu wawili nilikuta tupo watu sita. Sasa napenda kujua ni taratibu gani zinatumika ili hao watu wa *TASAC* au kama ni *Marine Service* wanahakikisha usalama wa abiria kwa kufuata taratibu zilizowekwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; huko nyuma Afisa Kazi wa Mkoa alikuwa katika daraja la kwanza kwenye meli, alifuatwa ndani ya meli, akachukuliwa na akatupwa ndani ya maji akafariki. Je, *Marine Service* au kama ni *TASAC* sasa wako tayari kuweka ulinzi thabiti ndani ya meli kuhakikisha kwamba kunakuwa na usalama wa kutosha hasa ule usiku mkuu maana hii meli inasafiri usiku ndani ya maji? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpe pole Mheshimiwa Mbunge kama alivyoeleza kwa aliyoyasema Bungeni, lakini nimhakikishie na nitumie nafasi hii kutoa maelekezo maalum kwa Wakala wa Meli pamoja na *TASAC* kuhakikisha kwamba wanadumisha ulinzi na usalama kwa abiria kwa vyombo vyote majini siyo tu Ziwa Victoria na maeneo mengine yote ikiwemo Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na kwingineko kote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Michael Kembaki.

Na. 336

**Changamoto ya Wachimbaji Mgodi wa Kebaga – Tarime**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa Vibali kwa Wachimbaji Wadogo na kutozwa mapato kwenye mchanga Mgodi wa Kebaga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mgodi wa Kebaga kuna umiliki wa leseni namba *PML000851* na *000852* zinazomilikiwa na Bibi Virginia Mkandala na Bwana Samson Gesase. Mgodi huo ulikuwa na changamoto ya kukosa Meneja wa Mgodi hivyo kushindwa kudhibiti uchimbaji na uchenjuaji wa madini katika eneo hilo. Hivyo, Tume ya Madini iliweka utaratibu wa kusimamia mgao wa mawe ambapo vibali vya ugawaji vilikuwa vikitegemea utayari na wito kutoka kwa wamiliki wa leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hapakuwa na utaratibu mzuri wa kusimamia hatua zote za uzalishaji, Tume ya Madini ililazimika kutoza tozo za Serikali kwenye hatua za ugawaji wa mawe. Mgodi huo kwa sasa umeboresha usimamizi kwa kuteua Meneja wa Mgodi ambaye anasimamia shughuli zote za uzalishaji. Hivyo, kuanzia tarehe 1 Aprili, 2024 yaani mwezi uliopita Tume ya Madini imesitisha zoezi la mgao wa mawe na shughuli za uzalishaji katika mgodi huo zinaendelea kufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura 123.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze Serikali kwa majibu mazuri na namna ambavyo wameweza kutatua changamoto za wachimbaji wadogo katika Mgodi wa Kebaga. Pamoja na majibu hayo

mazuri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kumekuwepo na Mgodi wa *Barrick* ambao unafanya utafiti katika Kata za Ketare, Turwa pamoja na Kenyamanyori, lakini wamekuwa wakiwapa wenyeji wenye maeneo shilingi 20,000. Je, nini mwongozo wa Serikali kuhusiana na malipo hayo madogo yanayofanywa na Mgodi wa *Barrick*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; upo wasiwasi mkubwa ambao wanao wale wachimbaji wadogo katika eneo la Tarime Mjini kutokana na ujio wa *Barrick* katika maeneo yao. Je, Serikali inawahakikishia nini hawa wachimbaji wadogo ili kuhakikisha kwamba wanakuwa salama wasiingiliwe au wasipate hasara kutokana na ujio wa *Barrick*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kembaki kwa jinsi anavyowatetea wananchi wake wa Jimbo la Tarime Mjini. Pia, nitumie nafasi hii kumjulisha kwamba Barrick wanapofanya utafiti katika maeneo yao ya leseni na tafiti zile zinapopita katika maeneo yenye mazao au bidhaa za wananchi katika yale maeneo ambayo bado wananchi wanaishi huwa wanapita wakiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ambaye wataalam wake wa Sekta ya Ardhi hufanya tathmini ili kujua kwamba mazao yaliyoharibiwa yana thamani kiasi gani na hufidiwa kwa mujibu wa kiwango cha uharibifu uliofanyika katika sehemu walizopita katika tafiti zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, *Barrick* inapoendelea na tafiti zake na wanapofanya tafiti mpaka nje ya maeneo ya leseni yao kwa maana ya maeneo ya wachimbaji wadogo, hawawezi kufanya kitu chochote kinyume na taratibu zilizowekwa na sheria za nchi, ikiwemo Sheria ya Madini, Sura ya 123, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali. Kama atahitaji eneo la mtu atalifidia, kama analifanya ili aweze kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo, maana yake kumekuwa na hiyo dhana ya kuwasaidia utafiti na mitaji, basi hiyo ndiyo dhana, lakini wananchi wa maeneo hayo niwape faraja kwamba, hakuna

kipande chao kitakachochukuliwa na mwekezaji kinyume na sheria au sehemu ambayo amepewa kihalali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la wachimbaji wadogo Nywarwana, Kata ya Kibasuka, Serikali inachukua kodi katika maeneo yale, lakini hakuna choo wala barabara ya kupita. Nini mwongozo wa Mheshimiwa Naibu Waziri katika eneo lile ili wachukue kodi halali, lakini pia watoe huduma za kijamii katika eneo lile kwani lina watu wengi sana na wanachafua mazingira? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Waitara kwamba nikitoka kujibu maswali hapa tukutane ili niweze kujua changamoto hiyo imesababishwa na nini, kwa sababu haiwezekani tozo zichukuliwe halafu huduma muhimu kwa wananchi zisitolewe, kwa hiyo, hilo nitalifuatilia baada ya hapa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaenda Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Vincent Mbogo.

Na 337

**Wananchi Kuliwa na Mamba Ziwa Tanganyika**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka wavu maeneo ambayo wananchi wanapoteza maisha kwa kuliwa na Mamba wanapofuata maji katika Ziwa Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu ndani ya Bunge. Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na matukio ya mamba kujeruhi na kusababisha vifo vya watu hususan kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa maeneo yenye maziwa, mito na mabwawa. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau imeandaa na inaendelea kutekeleza mkakati wa Taifa wa kusimamia migongano baina ya binadamu na wanyamapori. moja ya malengo ya kimkakati ni kuwajengea uwezo wananchi kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za kujilinda na kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo mamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mkakati huo, Serikali imekwishajenga vizimba vya mfano kwa ajili ya kuzuia mamba katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Aidha, Serikali imeandaa mpango wa kuendeleza ujenzi wa vizimba vya mfano vya kuzuia mamba katika maeneo mengine nchini yenye changamoto hiyo yakiwemo maeneo ya Ziwa Tanganyika kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nina swali la nyongeza. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kujenga vizimba vya mfano hasa maeneo hatarishi katika Kata ya Wampembe katika Kijiji cha Izinga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kwenda kutimiza jukumu hilo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea muda wetu umekwisha. Mheshimiwa Francis Mtinga.

Mheshimiwa Francis uko Bungeni au uko wapi?

Na 338

**Mapungufu katika Sheria ya Kifuta Machozi**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaifanyia marekebisho Sheria ya Kifuta Machozi kwa madhara yanayosababishwa na wanyamapori kwani iliyopo inawakandamiza wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikilipa kifuta jasho na kifuta machozi kama mkono wa pole au faraja kwa wananchi wanaopata madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa lengo la kuimarisha mtazamo chanya kwa wananchi juu ya shughuli za uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori nchini. Malipo hayo yamekuwa yakifanyika kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011 na kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya mapitio ya Kanuni za Kifuta Jasho na Machozi za Mwaka 2011 kwa lengo la kuboresha viwango vya malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushauriana na Wizara ya Fedha kama mdau muhimu katika kufanikisha suala hili, inafanyia kazi viwango vipya vya kifuta jasho na kifuta machozi ili kuviingiza kwenye Kanuni zinazofanyiwa marekebisho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yanayotia moyo ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapa pole wananchi wa Kata ya Mwangeza kwa jinsi ambavyo wamekuwa

wakiathirika na tembo, lakini bado hawapati huduma inayostahili kutoka Serikali. Swali la kwanza; Serikali haioni kwamba suala hili sasa linapaswa kuletwa kama sheria ili lifanyiwe mabadiliko badala ya kufanyiwa mabadiliko kama Kanuni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa jambo hili limekuwa likipigiwa kelele na Wabunge humu ndani kila kona. Serikali haioni kwamba, sasa suala hili linapaswa kuletwa kwa hati ya dharura ili Sheria hii ya kifuta jasho itazamwe ambayo inaawaathiri sana wananchi wa Tanzania? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mtinga, yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni zinapotumika ni sehemu ya utekelezaji wa sheria. Naomba kurudia, Kanuni zinapotumika ni utekelezaji wa sheria ambazo Bunge hili limezitunga. Ni kweli kwamba, yapo maeneo ambayo Sheria ya Uhifadhi na Sheria ya Wanyamapori imepitwa na wakati, Serikali iko kwenye mchakato wa kufanyia mapitio na kwa kadri muda utakavyokubaliana na vipindi vya Bunge, Serikali itawasilisha marekebisho hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda, maswali yamekwisha na muda umekwisha na orodha ya wageni bado haijaletwa mezani. Kwa hiyo, tunaendelea na ratiba zingine. Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Fungu Na. 99 – Mifugo na Fungu Na. 64 - Uvuvi, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa Fungu Na. 99 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu ya siku ya leo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Pia, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti kuwa Naibu Waziri na Dkt. Edwin Mhede kuwa Naibu Katibu Mkuu upande wa Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini ushirikiano wetu na mchango wa viongozi hawa vitaongeza kasi na kuleta mageuzi chanya himilivu ya kisekta ambayo ni mojawapo ya falsafa ya *4R* za Mheshimiwa Rais kuelekea ujenzi wa uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu wote natoa pongezi kwa Viongozi Wakuu wa Serikali akiwemo Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, kwa utendaji wao wa kazi uliotukuka na unaomfanya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kuendelea kutoa mchango wake muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu na hivyo kung’ara katika duru za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vema na kwa umahiri mkubwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo ni moja ya sababu zinazolifanya Bunge letu liaminiwe, hata Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, akiwa ni mwanamke wa kwanza kutoka Barani Afrika na wa tatu Duniani kushika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuongoza Kamati zao katika kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri kwa kuendelea kuwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nawashukuru viongozi, wajumbe wote na Sekretarieti yao kwa ushauri wao ulioiwezesha Wizara yangu kufanya maboresho stahiki. Tunaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya usimamizi na ushauri ili kuendeleza na kukuza mchango wa Sekta za Mifugo na Uvuvi kwenye uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri na ubunifu uliosaidia kuboresha usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, nawapongeza Profesa Riziki Silas Shemdoe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Profesa Daniel Elius Mushi, Naibu Katibu Mkuu Mifugo; Dkt. Edwin Paul Mhede, Naibu Katibu Mkuu Uvuvi; na Ndugu Agnes Kisaka Meena, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu katika Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya uhamisho, Mama Meena alikuwa Naibu Katibu Mkuu katika Wizara yetu, nawashukuru kwa kuwa viongozi na watendaji wazuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi, pia nawashukuru kwa uongozi wao uliotukuka kwa kusimamia utendaji kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nawashukuru kwa dhati ya moyo wangu watumishi wote wa Wizara yangu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naishukuru familia yangu, hususani mke wangu kipenzi Ndugu Mariam Abdallah Ibrahim na watoto wangu, kwa kuendelea kuniombea na kunivumilia muda mwingi ninapokuwa kazini kutimiza majukumu yangu ya Kibunge na Kitaifa na kwa kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu ya utumishi wangu kwa Watanzania. Aidha, nawashukuru kwa namna ya kipekee wananchi wa Jimbo la Mkuranga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuwatumikia na kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Naomba nichukue fursa hii kuwaahidi kuwa nitaendelea kuwa mtumishi wao na muda wote nitadumu katika kuwatumikia kwa umahiri na moyo wa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa salamu zangu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar kwa kuondokewa na Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.  Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakili aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani, Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.  Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole pia kwa wananchi wote waliokumbwa na mafuriko na maporomoko ya udongo yaliyotokea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kama vile Hanang', Rufiji, Kibiti, Kilwa, Kilosa, Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na maeneo mengine nchini ikiwemo na Jimbo langu la Mkuranga na pale jirani zangu Wilayani Mafia walipopatwa na maafa. Nawapa pole na kuwaombea ili Mwenyezi Mungu awape subira na kuwafanyia wepesi katika kuyajenga maisha yao upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2023/2024, kwa Fungu Na. 99 na Fungu Na. 64, mpango na bajeti ya Fungu Na. 99 Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2024/2025, baada ya kuunganishwa kwa Fungu Na. 99 na Fungu Na. 64 na kuwa Fungu moja Na. 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana katika vishikwambi vya Waheshimiwa Wabunge na tovuti ya Wizara. Aidha, naomba muhtasari huu kwa pamoja na taarifa yangu niliyowasilisha iingizwe kwenye *Hansard* zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo. Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024; maeneo ya kipaumbele katika mwaka 2023/2024. Katika mwaka 2023/2024, Wizara ilianza kutekeleza mpango wa mabadiliko ya Sekta ya Mifugo ili kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na pato la Taifa na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa ni kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo ambazo nimekuja nazo hapa, vyakula vya mifugo, maji kwa ajili ya mifugo, kuimarisha afya ya mifugo, kuboresha huduma za ugani, kuimarisha programu ya jenga kesho iliyobora *(BBT),* kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo, kuwezesha uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake kama ambavyo leo unaweza ukaona namna ambavyo Tanzania kwa mara ya kwanza imefikia hatua ya kutengeneza maziwa ya unga na kiwanda cha kizalendo cha *ASAS* ambayo leo nimekuja hapa kuwaonesha Waheshimiwa

Wabunge kazi kubwa na nzuri inayofanywa. Pia kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli katika sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha Zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Mwaka 2023/2024; katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu Na. 99 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 112. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 50.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 23.9 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 26.2 ni matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 61.9 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikijumuisha shilingi bilioni 56.6 fedha za ndani na shilingi bilioni 5.3 fedha za nje. Hadi Aprili, 2024 jumla ya shilingi bilioni 44.5 zimetolewa sawa na 39.7%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Bajeti ya Kawaida na Maendeleo; hadi Aprili, 2024, shilingi bilioni 32.1 zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na 64.1% ya shilingi bilioni 50.1 zilizotengwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 18.63 zimetumika kulipa mishahara na shilingi bilioni 13.45 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2024 shilingi bilioni 12.44 zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na 20.1% ya shilingi bilioni 61.9 zilizotengwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 12.4 ni fedha za ndani na shilingi milioni 40 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makusanyo ya maduhuli. Katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 99 ilitarajia kukusanya shilingi bilioni 42.1. Hadi kufikia Aprili, kiasi cha shilingi bilioni 22.6 sawa na 53.68% zimekusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya Sekta ya Mifugo; katika mwaka 2023/2024 Wizara imeendelea kusimamia shughuli za mifugo na kuwezesha uzalishaji ambapo idadi ya mifugo nchini imeongezeka kutoka ng'ombe milioni 36.6 hadi ng'ombe milioni 37.9; mbuzi kutoka milioni 26.6 hadi milioni 27.6; na kondoo kutoka milioni 9.1 hadi milioni 9.4. Idadi ya kuku imeongezeka kutoka

milioni 97.9 hadi milioni 103.1, ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 45.1 hadi milioni 47.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni 52.9 hadi milioni 55.7 na nguruwe wameongezeka kutoka milioni 3.7 hadi milioni 3.9. Aidha, Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2023 ilikua kwa asilimia tano na kuchangia 6.7% kwenye pato la Taifa letu. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, jumla ya ng'ombe 2,957,724 na mbuzi pamoja na kondoo 2,828,248 wenye thamani ya shilingi trilioni 3.4 waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini, ikilinganishwa na ng'ombe 2,218,293 na mbuzi 2,121,187 waliokuwa na thamani ya shilingi trilioni 1.7 waliouzwa katika mwaka wa 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa minadani limetokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika soko la ndani na soko la nje pamoja na hamasa ya uvunaji wa mifugo miongoni mwa wafugaji. Uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani 803,264.3 mwaka 2022/2023 hadi tani 963,856.55 mwaka 2023/2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la 16.7%. Kiambatanisho namba mbili kinajieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya hizo nyama ya ng'ombe ilikuwa ni tani 612,808.50, mbuzi tani 134,403.35, kondoo tani 28,290, kuku tani 132,442.28 na nguruwe tani 55,912.42 kwa mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani 544,983.8, mbuzi tani 91,893.8, kondoo tani 21,888.5, kuku tani 96,915 na nguruwe tani 47,583.1 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji katika kukinga mifugo dhidi ya magonjwa, wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi. Sasa Serikali inatoa ruzuku ya dawa ya kuogesha mifugo ambapo tani 56,000 katika mikoa 25 na mashamba ya Wizara na taasisi zake zenye thamani ya shilingi bilioni 2.5 ambayo imepunguza vifo vya mifugo kwa asilimia nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya vipande 1,542,916 vya ngozi vyenye uzito wa kilo 5,777,669.5 vyenye thamani ya shilingi bilioni saba viliuzwa nje ya nchi yetu ikilinganishwa na vipande vya ngozi 748,009 vyenye uzito wa kilo 3,591,396 vyenye thamani ya shilingi bilioni 5.5 vilivyouzwa nje ya nchi katika mwaka 2022/2023. Aidha, mauzo ya ngozi kwenda nje ya nchi yameongezeka kutokana na mahitaji ya soko la ngozi isiyosindikwa kuongezeka katika Nchi za Afrika ya Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2023/2024, jumla ya vifaranga 95,584,347 vya kuku vilizalishwa na kusambazwa nchini ikilinganishwa na jumla ya vifaranga 83,845,967 vilivyozalishwa mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la 12.3%. Kati ya vifaranga hivyo, vifaranga vya kuku wa nyama ni 73,481,572, vifaranga chotara ni 14,163,396 na kuku wa mayai ni 7,939,379 ikilinganishwa na vifaranga vya kuku wa nyama 64,457,555, chotara 12,424,064 na kuku wa mayai 6,964,348 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho katika mashamba ya Serikali umeongezeka kutoka tani 22.2 za mbegu za malisho aina ya nyasi na mikundekunde mwaka 2022/2023 hadi tani 127 katika mwaka 2023/2024. Aidha, jumla ya marobota 267,695 ya *hay* yamevunwa katika mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na marobota 248,209 yaliyovunwa katika mwaka 2022/2023. Ongezeko hili limetokana na uwekezaji wa mashine na usambazaji wa dhana na vifaa kwenye mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jumla ya tani 728.6 za *silage* zimezalishwa. Vilevile, uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kufikia tani 1,880,000 mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na tani 1,580,000 mwaka 2022/2023. Ongezeko hili limetokana na Serikali kuendelea kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa Sekta Binafsi ili kuwezesha nchi kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona kwa mara ya kwanza tumefanikiwa kutengeneza mbegu ambazo zinaingia

madukani kwenda kuuzwa kwa ajili ya wafugaji. Mbegu hizi kwa mara ya kwanza zitauzwa katika maduka ya dhana za kilimo, mifugo na uvuvi. Haya ni mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Mifugo (Sera, Sheria na Kanuni). Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ambapo rasimu ya kwanza iliyoboreshwa ipo katika hatua za maamuzi ya Serikali. Aidha, Wizara imekamilisha nyaraka za kuunganisha Bodi ya Nyama na Bodi ya Maziwa na kupendekeza kuundwa kwa chombo maalum kitakachosimamia uendelezaji wa mazao na miundombinu ya mifugo ambapo zipo kwenye hatua za mapitio katika ngazi za Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeandaa Mpango Mkuu wa Mifugo, Uvuvi na Kilimo Mazao *(Agricultural Transformation Master Plan 2050)* ambao utatoa dira ya mabadiliko katika Sekta hizi za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji mbegu bora na masoko. Katika mwaka wa 2023/2024, Wizara kupitia Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji *(NAIC)* imezalisha dozi 111,844 za mbegu za ng'ombe na kusambaza dozi 67,958. Aidha, Wizara imewajengea uwezo wahimilishaji 196 kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuratibu, kuwezesha na kusimamia shughuli za utafiti wa mifugo nchini ambapo imefanya tathmini katika vituo saba vya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(TALIRI)* na uratibu wa taasisi nyingine 11 zinazofanya utafiti unaohusiana na mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la tathmini hiyo ilikuwa ni kubaini tafiti mbalimbali zinazofanyika pamoja na uzingatiwaji wa sheria, kanuni, miongozo na utekelezaji wa Ajenda ya Utafiti wa Mifugo Nchini ya Mwaka 2020/2025. Aidha, tafiti hizi zimechangia katika utatuzi wa changamoto mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa mifugo ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa mbari za mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mifugo, upatikanaji wa mbegu bora za malisho na uboreshaji wa malisho ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kufanya uratibu katika vyuo 21 vya mafunzo ya mifugo nchini ikihusisha tathmini ya mafunzo katika kampasi tisa zilizo chini ya Wakala ya Mafunzo ya Mifugo Tanzania *(LITA)* na vyuo binafsi 12. Lengo likiwa ni kuona uzingatiwaji wa utumiaji wa mitaala ya Wizara, uwiano wa wakufunzi na wanafunzi na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchanjaji wa mifugo katika mwaka wa 2023/2024. Serikali imeendelea kuratibu utoaji wa chanjo ya mifugo nchini ambapo hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya dozi 616,070,986 za chanjo ya mifugo zimetumika dhidi ya magonjwa 13 ya kipaumbele kama ilivyobainishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu, Ibara ya 66.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2023/2024 ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengineo, Wizara ilipanga kujenga jumla ya majosho 246 yenye thamani ya shilingi 5,658,000,000 katika halmashauri 65. Fedha ambazo zilihamishiwa kwenye halmashauri ili kuwezesha ufanisi, tija na umiliki wa miradi hii kwa halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uogeshaji wa mifugo unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya michovyo 1,342,932,142 ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng'ombe 660,725,421, mbuzi 453,142,239, kondoo 201,975,117 na punda 27,089,368. Michovyo hii ni sawa na 75% ya lengo la michovyo bilioni 1.8 kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2024 Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* imezalisha ndama 1,361 na kusambaza mitamba 201 kwa wafugaji ili kuboresha kosaafu za mifugo yetu. Pia, imezalisha na kuuza tani 186 za nyama, imenenepesha na kuchinja ng'ombe 1,534, imefyeka na kuondoa vichaka hekta 445 katika Ranchi za Kongwa, Ruvu na *West Kilimanjaro* kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho na imezalisha jumla ya marobota 52,500 ya malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, imewezesha kutoa ushauri wa kitaalam na imetoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 505 kutoka katika myuo vya mafunzo ya mifugo nchini. Katika mwaka wa 2023/2024, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imeratibu mauzo ya nyama nje ya nchi ambapo kiasi cha tani 13,745.38 zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 56.6 zimepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi hiki ni sawa na ongezeko la 12.3% ikilinganishwa na tani 12,243.8 zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 51.9 zilizouzwa katika mwaka 2022/2023. Katika mwaka 2023/2024, Bodi ya Maziwa imesajili jumla ya wadau 411 wa maziwa. Idadi hii ni sawa na 103% ya wadau 400 waliokuwa wamelengwa. Pia, bodi imefanya ukaguzi kwa wafanyabiashara 867 kati ya wafanyabiashara 1,200 waliokuwa wamelengwa sawa na 72.3% na hatua stahiki zilichukuliwa kwa wale waliokiuka sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi iliyopelekea kuanza uzalishaji wa maziwa ya unga hapa nchini itakayopelekea kupunguza uagizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi yetu. Maelezo ya kina yanapatikana katika Ibara ya 77 hadi 79 kwenye Hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania *(TVLA)* kupitia Taasisi ya Kuzalisha Chanjo *(TVI)* imezalisha na kusambaza chanjo za mifugo dozi 62,173,850 za magonjwa mbalimbali ya kipaumbele. Aidha, Wakala imefanya uchunguzi wa magonjwa ya wanyama kwenye sampuli 21,667, kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo kwenye sampuli zisizopungua 2,550 na kutoa vibali 54 vya kuingiza viuatilifu vya mifugo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, *TALIRI* imeendelea kufanya tafiti za kuboresha mbari za mifugo na malisho ambapo jumla ya miradi 54 ya utafiti imeendelea kutekelezwa. Aidha, matokeo ya tafiti hizo ni kuibuliwa na kusambazwa kwa teknolojia ambapo jumla ya mifugo iliyoboreshwa 268 ilizalishwa. Kati ya mifugo hiyo iliyozalishwa, 120 ilisambazwa katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Pwani na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *TALIRI* iliwezesha upatikanaji wa ithibati ya mbegu za malisho aina tano ambazo zitaanza kuuzwa katika maduka ya pembejeo nchini kote ili wafugaji waende wakanunue, wapande mashambani na kuepuka migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Wakala ya Mafunzo ya Mifugo *(LITA)* imedahili wanafunzi 4,454 katika ngazi ya astashahada na stashahada katika kampasi nane za Wakala ikilinganishwa na wanafunzi 4,036 waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi hiyo ni ongezeko la wanafunzi 418 sawa na 10%. Aidha, wakala imeendelea na mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau 600 katika Sekta ya Mifugo kuhusu mifugo na mazao yatokanayo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi imetekeleza maeneo saba ya kipaumbele ambayo utekelezaji wake umezingatia Dira ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kipaumbele yaliyozingatiwa yalikuwa ni kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni za Sekta ya Uvuvi, kuimarisha taasisi za uvuvi ili kuongeza ushiriki katika uchumi wa bluu, kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu, kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji, kuimarisha udhibiti ubora wa mazao ya uvuvi na masoko na kuimarisha huduma za ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbemaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa 1.9% na ilichangia 1.8% katika Pato la Taifa letu. Aidha, Sekta inatoa ajira kwa Watanzania zaidi ya milioni sita pamoja na ajira ya moja kwa moja kwa wavuvi 198,475 na wakuzaji viumbemaji 35,986. Ajira hizi zimewezesha familia kupata kipato pamoja na kuongeza usalama wa chakula na lishe ambapo sekta huchangia 30% ya protini inayotokana na

wanyama. Aidha, inakadiriwa kwamba kiwango cha ulaji wa samaki umefikia kilo 7.9 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 hadi kufikia Aprili, Sekta ya Uvuvi imezalisha jumla ya tani 472,579.34 za mazao ya uvuvi. Kati ya hizo, tani 429,168.39 ni kutoka katika maji ya asili na tani 43,410.95 ni kutoka katika ukuzaji viumbemaji. Kufuatia uzalishaji huo, jumla ya tani 41,271.07 za mazao ya uvuvi na samaki hai 134,572 wa mapambo waliuzwa nje ya nchi. Vilevile, Sekta inachangia katika shughuli za uhifadhi wa rasilimali za uvuvi na utalii ambapo hadi sasa kuna hifadhi tatu za bahari na maeneo tengefu 15 yanayohifadhiwa kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari *(MPRU)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 183.9. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 49.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 134 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2024 jumla ya shilingi bilioni 103.2 sawa na 56.1% zilipokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili, 2024, jumla ya shilingi bilioni 21.9 sawa na 44% zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 11.2 ni fedha za mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 10.7 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 134 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 110 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 23.7 ni fedha za nje. Hadi Aprili, 2024 jumla ya shilingi bilioni 81.2 sawa na 60.4% kutoka vyanzo vya ndani zimetumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 41.0 kupitia Fungu 64. Hadi kufikia Aprili, 2024, shilingi bilioni 24.7 sawa na 60.16% ya lengo la mwaka zilikusanywa kupitia Sekta ya Uvuvi, hii ni sawa na 72% ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 34 hadi Aprili, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 Wizara imekamilisha kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura Na. 388 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura 280, ambayo yaliwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupitishwa na Kamati ya Baraza la Mawaziri. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Kanuni za Ukuzaji Viumbe Maji ambayo imepitiwa na wadau mbalimbali. Tayari rasimu hiyo imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki na kupata maoni. Pia Wizara inaendelea na mapitio ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, Wizara imekamilisha nyaraka za kuanzisha chombo cha kusimamia shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji ambacho kitakuwa na jukumu la kuendeleza, kusimamia, kudhibiti na kuhifadhi rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji nchini ambapo zipo kwenye hatua za mapitio katika ngazi za Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya tani 472,579.34 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.94 zilivunwa ikilinganishwa na tani 426,555.46 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.86 zilizovunwa 2022/2023. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi, kwa maana ya idadi ya wavuvi, aina na idadi ya vyombo vya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea kuimarisha ukusanyaji, uchakataji na usimamizi wa taarifa na takwimu za uvuvi kwa lengo la kuratibu shughuli za usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Katika kipindi hicho, wavuvi 198,475 na vyombo vya uvuvi 58,820 vilitumika katika shughuli za uvuvi ikilinganishwa na wavuvi 197,763 na vyombo vya uvuvi 58,448 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha biashara ya mazao ya uvuvi katika soko la nje ya nchi yetu. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya tani 41,271 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 134,572 wenye thamani ya shilingi bilioni 515.78 waliuzwa nje ya nchi na kuliingizia

Taifa mrabaha wa shilingi bilioni 14.44; ikilinganishwa na tani 29,466.98 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 150,308, wenye thamani ya shilingi bilioni 453, waliouzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrabaha wa shilingi bilioni 12.56 katika mwaka 2022/2023; ikiwa ni ongezeko la 40% la mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo siku kazi 2,912 za doria, sawa na 37.3% ya lengo la mwaka la kufanya doria siku za kazi 8,400 zilifanyika. Matokeo ya doria ilikuwa ni kukamatwa kwa zana haramu za uvuvi na kuwachukulia hatua za kisheria waliotenda vitendo hivyo. Taarifa zaidi inapatikana katika ibara ya 106 hadi 115 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ilisaini Mkataba wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Uvuvi katika Ziwa Tanganyika tarehe 16 Disemba, 2021, unaohusisha nchi nne zinazozunguka Ziwa; ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Tanzania na Zambia. Mkataba huo pamoja na masuala mengine unahusisha kupumzisha shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti kila mwaka. Lengo la kupumzisha ziwa ni kuruhusu kuzaliana, kuimarika kwa baioanuai na kuongeza uzalishaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara inaendelea kutekeleza mkataba huu ambao leo nimekuja nao hapa, pamoja na kuanzisha shughuli mbadala ambapo wadau wa uvuvi 6,898 walifikiwa. Pia, vizimba 29 vya wafugaji wa samaki ambavyo viliahidiwa vimekopeshwa bila ya riba kwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika. Kazi hii itaendelea katika Mwaka huu wa Fedha wa 2024/2025 kama shughuli mbadala za baada ya kupumzisha ziwa ili wavuvi wa Ziwa Tanganyika na wao wawe na shughuli za kuwapatia kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa samaki na bidhaa za uvuvi

kwenye mipaka, maeneo ya viwanja vya ndege na masoko ya samaki nchini kote. Aidha, kaguzi za kawaida 9,201 zilifanyika katika viwanda 21 vya kuchakata samaki, vituo 37 vya kuhifadhia samaki hai wa mapambo, mialo 33 ya kupokelea samaki, masoko matatu, maghala 70 ya kuhifadhi mazao yaliyokaushwa, vituo 17 vya kugandisha samaki, viwanda 17 vya mabondo, meli tatu za uvuvi na kambamiti na meli moja ya uvuvi wa bahari kuu vyote vilikaguliwa. Vilevile ukaguzi ulifanyika katika vyombo 1,470 vya kusafirisha mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekarabati miundombinu ikiwemo, mitambo ya kuzalisha barafu na vichanja vya kuanika samaki ili kuongeza ubora na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi. Maelezo ya kina yanapatikana katika ibara ya 116 hadi 115 ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Maabara ya Taifa ya Uvuvi ilipokea na kufanya uchunguzi wa jumla ya sampuli 1,982 za samaki, mazao ya uvuvi na mazingira. Maabara iliwezesha nchi kuuza tani 41,271 za samaki na mazao ya uvuvi katika masoko ya kimataifa zenye thamani ya Dola za Marekani 206.6. Aidha, maabara ilifanyiwa ukaguzi na Bodi ya Ithibati ya *SADC*. Naomba hapa nisisitize, maabara imekagua samaki wetu pale Ziwa Victoria, baharini na Ziwa Tanganyika; na hapa wataalam wapo na nataka niwaambie Watanzania kupitia muhtasari wa taarifa hii ya bajeti ya kwamba, samaki wetu ni salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2024, uzalishaji wa mazao ya ukuzaji wa viumbe maji umefikia tani 43,410 kutoka tani 33,525 za mwaka 2022/2023. Uzalishaji huo unajumuisha tani 34,828 za samaki, tani 8,545 za mwani mkavu, tani 30 za kambakochi, tani tano za kambamiti, tani 2.5 za kaa, tani 1.5 za majongoo bahari na vipande vya lulu 250. Aidha, idadi ya miundombinu ya uzalishaji wa viumbe maji imeongezeka hadi kufikia mabwawa 34,417, vizimba 1,215 na vitotoleshi vya kuzalisha vifaranga 41 ikilinganishwa na mabwawa 32,878, vizimba 993 na vitotoleshi 39 mtawalia kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, uzalishaji wa vifaranga vya samaki umefikia 66,684,806 ikilinganishwa na vifaranga 35,967,180 kwa mwaka 2022/2023. Aidha, matumizi ya vyakula vya samaki nchini yameongezeka kutoka tani 4,337.9 mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 7,335.7, zinazojumuisha tani 3,309 zilizozalishwa ndani ya nchi yetu na tani 4,025 zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Aprili 2024, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imetoa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, uhifadhi na uongezaji wa thamani katika zao la mwani kwa wakulima 2,615. Tunashukuru kwamba baadhi ya wakulima hawa leo wako katika maonyesho ya Wiki ya Protini hapa Bungeni kutoa ushuhuda wa kazi nzuri na kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na jemedari wetu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia *TAFIRI* imefanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika maji ya Bahari ya Hindi na maziwa makuu. Matokeo ya tafiti hizo katika baadhi ya maeneo ikiwemo Ziwa Tanganyika yameonesha kupungua sana kwa samaki. Matokeo haya yameiwezesha Wizara kuweka mikakati madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi ili kufikia lengo la kuongeza wingi wa uzalishaji wa samaki nchini. Maelezo ya kina yanapatikana katika ibara ya 131 ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, *FETA* imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 1,116 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada yanayotilia mkazo umahiri kwa vitendo na kuondokana na mfumo wa zamani wa uwezo kwa maarifa. Aidha, *FETA* ambaye ni wakala wa mafunzo ya uvuvi nchini imewezesha mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uelewa na kukuza ujuzi kwa washiriki 4,035 katika maeneo ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Uvuvi Nchini *(TAFICO)* imesaini mkataba na Serikali ya Japan wa ujenzi wa meli moja ya uvuvi wa bahari kuu. Uundaji wa meli hii tayari

umeanza na unatarajia kukamilika mwezi Disemba, 2025. Aidha, ukarabati wa miundombinu ya majengo ya Shirika la Uvuvi Tanzania umefikia 75%.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TAFICO* pia imenunua mtambo wa barafu za chenga wenye uwezo wa kuzalisha tani tano kwa siku ili kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi. Vilevile Shirika linaendelea na tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii kwa ajili ya ununuzi wa meli nne za uvuvi wa bahari kuu na kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi kupitia programu ya kuendeleza kilimo. Kiwanda hiki kitajengwa pale Kilwa Masoko panapojengwa bandari ya uvuvi. Shirika letu la Uvuvi *TAFICO*, limefufuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu *(DSFA)* ilifanya ukaguzi wa meli 75 za uvuvi. Kati ya hizo meli 67 zilichukua leseni na meli nane zilipewa vibali na ruhusa, hivyo kuwezesha makusanyo ya shilingi bilioni 9.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.8 zilizokusanywa kutokana na leseni 51 za mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 2.9, sawa na 42.6%. Aidha, mamlaka imeendelea kutumia Mifumo ya Ufuatiliaji wa Mienendo ya Meli *(VMS)* na kuweka uangalizi wa uvuvi. Tunalishukuru sana Bunge kwa maelekezo na sasa tunaona pia *DSFA* imeanza kuongeza mapato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu yaani *MPRU* iliendelea kutekeleza jukumu la ulinzi na usimamizi wa rasilimali za bahari, ikiwa ni pamoja na kuainisha maeneo mapya ya hifadhi za bahari katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Mkoani Lindi. Aidha, doria 420 za kwenye maji na nchi kavu zilifanyika ili kudhibiti uharibifu wa mifumo ya ikolojia ya rasilimali za uvuvi za bahari yetu. Katika hili tumefanikiwa sana. Tulikuwa na tatizo kubwa la upigaji wa mabomu baharini; hivi tunavyozungumza hakuna upigaji wa mabomu. Natoa tahadhari kwa wapiga mabomu wote, atakayejaribu mkono wa sheria utamfikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko unaotarajia kukamilika mwaka 2025, ambapo hadi Aprili, 2024, ujenzi umefikia 53%. Maelezo ya kina yanapatikana katika ibara ya 150 ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu *(ECF);* katika mwaka 2023/2024, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua programu maalum ya kuwawezesha wavuvi na wakuzaji viumbe maji. Programu hiyo inatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* kupitia dirisha la *ECF*. Aidha, kupitia programu hiyo boti za kisasa za uvuvi 160 na vifaa vyake zimekopeshwa kwa wanufaika 3,295 wa moja kwa moja bila riba. Pia, katika awamu ya kwanza, vizimba 222 vya kufugia samaki na pembejeo zake vimetolewa kwa wanufaika 1,214 wa moja kwa moja. Mikopo hiyo inatolewa kupitia Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora kwa Vijana na Wanawake *(BBT);* Wizara ilipokea maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuanzisha Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora *(BBT)* inayolenga kuwajengea uwezo vijana na wanawake kujiajiri na kuajiri wengine. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) imeendelea na utekelezaji wa programu hiyo. Ninayo furaha kwamba miongoni mwa waalikwa wetu ni vijana wa *BBT,* wako hapa, wamekuja kutoa ushuhuda wa kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maelekezo hayo Sekta ya Mifugo imeanzisha vituo nane vya vijana na wanawake kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuanzisha na kuendesha miradi ya ufugaji kibiashara. Aidha, mafunzo yametolewa kwa wanufaika 235, ambapo kati yao 74 wamepata ajira Serikalini na 161 wanaendelea na mafunzo. Aidha, kupitia programu hiyo jumla ya ng'ombe 3,388 wamenenepeshwa na kuuzwa kwa

thamani ya shilingi bilioni 1.97 na kupata faida ya shilingi milioni 199.57. Pesa hizi ni za walengwa wa *BBT* na zitaingizwa katika akaunti zao moja kwa moja kama sehemu ya mtaji wa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, vijana wanaendelea na utekelezaji wa programu hiyo hadi Juni mwaka huu ambapo watakuwa tayari kwenda kuanza ufugaji wa kibiashara kupitia vitalu vilivyoandaliwa na Wizara katika ranchi za *NARCO* za Kitengule na Kagoma. Ili kuboresha usimamizi na kuongeza umiliki Wizara imehamasisha jukumu la kusimamia na kuendesha vituo nane vya *BBT* mifugo vilivyopangwa kutekelezwa mwaka 2023/2024 kwa Sekretarieti za Mikoa ya Tabora, Arusha, Morogoro, Pwani na Mtwara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hitimisha na uombe pesa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mpango wa Bajeti wa mwaka 2024/2025; katika mwaka 2024/2025, maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2024/2025 pia yamezingatia falsafa ya *4R* za Mheshimiwa Rais inayosisitiza uwepo wa maridhiano, uhimilivu, mageuzi na kujenga upya ili kujenga uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika kutekeleza maono hayo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwaka huu tena tunafanya kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo kwa kutoa chanjo kwa magonjwa 13 ya kipaumbele, kuendelea na taratibu za uundwaji wa chombo cha kusimamia uendelezaji wa miundombinu, kuanza kutekeleza mradi wa mageuzi katika tasnia ya maziwa, mabadiliko ya tabia nchi kwa miaka mitano ambapo utanufaisha walengwa wasiopungua 600,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi utahusisha kununua ng'ombe wa kisasa 17,200, kujenga mabanda ya ng'ombe ya kisasa 5,000, kujenga mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua katika kaya 22,400, kununua na kusanikisha mitambo 2,800 ya *biogas*, kujenga vituo 950 vya kukusanya maziwa, kununua dozi 929,000

za chanjo za mifugo na kujenga kilometa 140 za barabara katika maeneo ya mradi ya kwenda kukusanyia maziwa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakwenda kuanzisha Mradi Maalum wa *guest house* katika *Ranch* yetu ya Mkata ili kuondoa migogoro ya wafugaji na wakulima ili wafugaji waweze kwenda kunenepeshea mifugo yao pale katika *ranch* yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa uvuvi, Wizara imejiandaa na vipaumbele ambavyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko; Kuendelea na taratibu za uundwaji wa chombo cha kusimamia uendelezaji wa rasilimali za uvuvi; Kuendelea na taratibu ya kununua meli nne kupitia *TAFICO;* Kujenga kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi kupitia *TAFICO;* Kuwezesha ununuzi wa boti 450 kutoka 160 za mwaka uliopita; Kuwezesha vikundi 300 vya vikundi vya vijana; Kununua meli moja ya mafunzo itakayosimamiwa na Chuo chetu cha *VETA* kupitia Mradi wa *TASFARM;* pamoja na kununua vizimba 497 tutakavyovigawa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara inaomba kutumia jumla ya fedha za Kitanzania shilingi 460,333,000,602. Kati ya fedha hizo, shilingi 97,215,432,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 363,118,000,170 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za matumizi ya kawaida shilingi 97,000,000,000; mishahara shilingi 41,000,000,000 na matumizi mengineyo shilingi 52,000,000,000. Fedha za matumizi ya maendeleo shilingi 363,118,000,170; fedha za ndani ni shilingi 242,078,803,000 na fedha za nje ni shilingi 121,039,000,367.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza na unaweza ukaona, kutoka shilingi 169,000,000,000 wakati Mheshimiwa Rais anaingia mwaka 2021/2022 mpaka shilingi

460,000,000,000, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MB.), WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyochambua na kutoa ushauri kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2023/2024, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/2024. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu, liridhie na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2024/2025. **Shukrani na Pongezi**

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uhai, afya njema na kutuwezesha kushiriki mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Mbili, ikiwa ni mkutano mahsusi wa Bunge wa kuamua mambo yenye mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutimiza kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake na kwa kuliongoza Taifa letu kwa weledi, umahiri na mafanikio mkubwa. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti (Mb.), kuwa Naibu Waziri, na Dkt. Edwin Paul Mhede kuwa Naibu Katibu Mkuu – Sekta ya Uvuvi, ambapo kwa ushirikiano wetu tunaamini mchango wa viongozi hawa utapelekea kuleta mageuzi chanya ya kisekta, ambayo ni mojawapo ya falsafa ya 4R za Mheshimiwa Rais kuelekea ujenzi wa uchumi jumuishi.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali; akiwemo Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa, na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, kwa utendaji wao uliotukuka unaomfanya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kuendelea kutoa mchango wake muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu na hivyo kung'aa katika duru za Kitaifa na Kimataifa.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jambo ambalo ni moja ya sababu zilizofanya uaminiwe na kuchaguliwa kuwa Rais wa **31** wa Umoja wa Mabunge Duniani, ukiwa ni mwanamke wa kwanza kutoka Barani Afrika na watatu Duniani kushika nafasi hiyo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia kwa umahiri mkubwa wa kuendesha shughuli za Bunge. Pia, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuongoza Kamati zao katika kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.), Mbunge wa Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri (Mb.), kwa kuendelea kuwa Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati. Vilevile, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ninawashukuru viongozi, wajumbe wote, na Sekretarieti ya Kamati hii kwa kufanya uchambuzi makini wa Bajeti yetu. Ushauri wao umewezesha Wizara yangu kufanya maboresho stahiki. Hakika, Mheshimiwa Spika unayo Kamati ambayo ni msaada kwetu. Aidha, kwa upande wetu, tunaahidi kuendelea kuipa kamati ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi

na ushauri ili kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuongeza mchango wake kwa uchumi wa Taifa.

**6.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti (Mb.), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri na ubunifu uliosaidia kuboresha usimamizi wa Sekta za Mifugo na Uvuvi. Aidha, nawapongeza Prof. Riziki Silas Shemdoe (Katibu Mkuu-Wizara ya Mifugo na Uvuvi), Prof. Daniel Elius Mushi (Naibu Katibu Mkuu-Sekta ya Mifugo), Dkt. Edwin Paul Mhede (Naibu Katibu Mkuu - Sekta ya Uvuvi) na Bi, Agnes Kisaka Meena (Naibu Katibu Mkuu - Wizara ya Maji) aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Sekta ya Uvuvi) kabla ya uhamisho, kwa kuwa viongozi na watendaji wazuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Pia, ninawashukuru watendaji wa Wizara kwa utendaji mzuri na ushirikiano wanaotupatia uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kikamilifu.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** natambua mchango wa Sekta Binafsi, unaojumuisha wawekezaji wakubwa na wadogo wakiwemo wafugaji, wavuvi, wachakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi ambao wameendela kufanya uzalishaji kwenye sekta za mifugo na uvuvi. Aidha, uzalishaji wao umeendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza sekta hizo muhimu kwa kuzalisha protini kwa ajili ya ustawi wa afya ya jamii na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa nchi yetu. Vilevile, ninapenda kuwashukuru washirika wa maendeleo, taasisi za fedha na Asasi Zisizo za Kiserikali kwa kuendelea kutuunga mkono katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Tunawashukuru, na tunaahidi kuendelea kuwahudumia na kushirikiana nao.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, naishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi Bi. Mariam Abdallah Ibrahim na watoto wangu, kwa kuendelea kuniombea na kunivumilia ninapokuwa muda mwingi kazini kwa majukumu yangu ya Kibunge na Kitaifa na kwa kuwa mara zote wamebaki kuwa marafiki wa kweli wanaonitia moyo katika utekelezaji wa majukumu ya utumshi wangu kwa Watanzania. Aidha, ninawashukuru kwa dhati na kwa namna ya kipekee wananchi wa Jimbo la Mkuranga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia

katika kuwatumikia na kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo letu. Naomba nichukue fursa hii kuwaahidi kuwa nitaendelea kuwa mtumishi wenu na muda wote nitadumu katika kuwatumikia kwa umahiri na moyo wa dhati.

**Salamu za Pole**

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Watanzania wote kwa kuondokewa na Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakili aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninatoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na mafuriko na maporomoko ya udongo yaliyotokea maeneo ya Rufiji, Kibiti, Kilwa, Kilosa, Dar es Salaam, Arusha, Hanang', Mbeya na maeneo mengine nchini yaliyopatwa na maafa. Ninawapa pole sana.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024, kwa Fungu **99** na **64** na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2024/2025 kwa Fungu **99**, baada ya kuunganishwa kwa Fungu **99** na **64** kuwa Fungu moja **99**.

## B. SEKTA YA MIFUGO


### Hali Halisi ya Sekta ya Mifugo

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, idadi ya mifugo nchini imeongezeka kutoka ng'ombe milioni **36.6** hadi ng'ombe milioni **37.9**, mbuzi kutoka milioni **26.6** hadi milioni **27.6**, na kondoo kutoa milioni **9.1** hadi milioni **9.4**. Pia, kuku wameongezeka kutoka milioni **97.9** hadi milioni **103.1** ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni **45.1** hadi milioni **47.4**, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni **52.9** hadi milioni **55.7** na nguruwe wameongezeka kutoka milioni **3.7** hadi milioni **3.9** (**Kiambatisho Na.1**). Aidha, Sekta ya Mifugo kwa mwaka 2022 ilikua kwa asilimia **5** na kuchangia asilimia **6.7** kwenye Pato la Taifa.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya ng'ombe **2,957,724** na mbuzi na kondoo **2,828,248** wenye thamani ya Shilingi trilioni **3.4**, waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **2,218,293** na mbuzi na kondoo **2,121,187** waliokuwa na thamani ya Shilingi trilioni **1.7** waliouzwa katika mwaka 2022/2023. Ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa minadani limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika soko la ndani na nje ya nchi pamoja na hamasa ya uvunaji wa mifugo.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani **803,264.3** (mwaka 2022/2023), hadi tani **963,856.55** (mwaka 2023/2024), ikiwa ni sawa na ongezeko la asimilia **16.7** (**Kiambatisho Na. 2**). Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe tani **612,808.50**; mbuzi tani **134,403.35**; kondoo tani **28,290.00**; kuku tani **132,442.28**, na nguruwe tani **55,912.42** kwa mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani **544,983.8**; mbuzi tani **91,893.8**; kondoo tani **21,888.05**; kuku tani **96,915.6** na nguruwe tani **47,583.1** kwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limechangiwa na wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao na kukua kwa soko la nyama la ndani na nje ya nchi (**Kielelezo Na. 1).**

***Kielelezo Na. 1 Uzalishaji wa Nyama (Tani) kwa Mwaka 2023/2024 Ikilinganishwa na Mwaka 2022/2023***




***Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi, 2024***

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, jumla ya vifaranga vya kuku **95,584,347** vimezalishwa na kusambazwa nchini ikilinganishwa na jumla ya vifaranga **83,845,967** vilivyozalishwa mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la asilimia **12.3**. Kati ya vifaranga hivyo, vifaranga vya kuku wa nyama ni **73,481,572**; chotara **14,163,396;** na kuku wa mayai **7,939,379**; ikilinganisha na vifaranga vya kuku wa nyama **64,457,555**; chotara **12,424,064** na kuku wa mayai **6,964,348** kwa mwaka 2022/23.

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai bilioni **5.50,** mwaka 2022/2023 hadi mayai bilioni **6.41**, mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia **16.55 (Kiambatisho Na 2).** Ongezeko hilo limesababishwa na kuimarika kwa vituo **28** vya kutotolesha vifaranga vya kuku vilivyopo nchini, mashamba **25** ya kuku wazazi, kuongezeka kwa ufugaji wa kuku wa mayai na hatua mbalimbali ambazo zimeendelea kucukuliwa za kudhibiti uingizaji holela wa vifaranga kutoka nje ya nchi **(Kiambatisho Na 3)**.

**18.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni **3.60**, mwaka 2022/2023, hadi kufikia lita bilioni

**3.97,** mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia **10.3** ambapo kati ya lita hizo, lita milioni **34.69** zimetokana na maziwa ya mbuzi na lita bilioni **3.93** zimetokana na maziwa ya ng'ombe. Aidha, lita bilioni **2.64** zinatokana na ng'ombe wa asili na lita bilioni **1.30** zimetokana na ng'ombe wa maziwa walioboreshwa (**Kiambatisho Na 2)**. Vilevile, usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita milioni **77.90,** mwaka 2022/2023, hadi kufikia lita milioni **81.80,** mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia **5.01 (Kiambatisho Na 4)**. Pia, ukusanyaji wa maziwa kupitia vituo vya kukusanyia maziwa, umeongezeka kutoka lita milioni **71.80,** mwaka 2022/2023, hadi kufikia lita milioni **93.40,** mwaka 2023/2024. Ongezeko la uzalishaji wa maziwa limechangiwa na utoaji elimu ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa kibiashara hapa nchini, kuongezeka kwa ng'ombe wa maziwa walioboreshwa pamoja na vituo vya kukusanyia maziwa vilivyofikia **258** mwaka 2023/2024 kutoka **246** mwaka 2022/2023.

**19.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha uzalishaji wa mazao ya mifugo na kuhamasisha ulaji mazao hayo nchini. Aidha, ulaji wa mazao ya mifugo, kwa mtu kwa mwaka, umeongezeka kutoka wastani wa lita **62** hadi lita **67.5** za maziwa, kilo **15** hadi kilo **16** za nyama, na mayai **106** hadi mayai **107**. Ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa soko la ndani la mazao ya mifugo. Pamoja na ongezeko hilo, ulaji wa mazao hayo uko chini ukilinganisha na viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ambavyo ni lita **200** za maziwa, kilo **50** za nyama na mayai **300** kwa mtu kwa mwaka.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho katika Mashamba ya Serikali umeongezeka kutoka tani **22.7,** za mbegu za malisho aina ya nyasi, vipando na mikunde, mwaka 2022/2023, hadi tani **127.8** mwaka 2023/2024. Pia, jumla ya marobota **267,695,** ya hei yamevunwa katika mwaka 2023/2024, ikilinganishwa na marobota **248,209,** yaliyovunwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hili limetokana na uwekezaji wa mashine na usambazaji wa zana na vifaa kwenye mashamba hayo. Vilevile, jumla ya tani **728.6** za saileji zimezalishwa. Aidha, uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka

kufikia tani **1,880,000,** mwaka 2023/2024**,** ukilinganisha na tani **1,580,000,** mwaka 2022/2023. Ongezeko hili limetokana na Serikali kuendelea kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa Sekta Binafsi ili kuwezesha nchi kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya vyakula vya mifugo.

**21.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024, Wizara, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kupitia uchanjaji, uogeshaji mifugo na utoaji elimu kuhusu udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya dozi **616,070,986** zimetumika kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa **13** ya kipaumbele. Aidha, uchanjaji wa mifugo umesaidia kupungua kwa matukio ya magonjwa yanayovuka mipaka na kuiwezesha Tanzania kukidhi matakwa ya biashara ya mifugo na mazao yake kulingana na matakwa ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Biashara Duniani (WTO).

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 – SEKTA YA MIFUGO

### Bajeti iliyoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo - Sekta ya Mifugo

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya **Shilingi 112,046,777,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 50,122,670,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 61,924,107,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2024, jumla ya **Shilingi 44,517,993,057.94** zimetolewa, sawa na asilimia **39.70.**

### Matumizi ya Kawaida

**23.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika bajeti ya mwaka 2023/2024, Sekta ya Mifugo iliidhinishiwa kutumia Shilingi **50,122,670,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **23,939,807,000** ni Mishahara na Shilingi **26,182,863,000** ni Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya Shilingi **32,080,170,763.71**


zimepokelewa ambazo ni sawa na asilimia **64.1** ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Katika fedha zilizopokelewa Shilingi **18,630,838,737.53,** sawa na asilimia **77.9** kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi **13,449,332,026.18** sawa na asilimia **51.4** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Miradi ya Maendeleo**

***24. Mheshimiwa Spika***, katika bajeti ya mwaka 2023/24, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) iliidhinishiwa Shilingi **61,924,107,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **56,592,173,000** ni fedha za ndani na Shilingi **5,331,934,000** ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya Shilingi **12,437,822,294.23** zimepokelewa ambazo ni sawa na asilimia **20.10** ya bajeti ya maendeleo. Katika Fedha zilizopokelewa Shilingi **12,397,422,294.23** ni fedha za ndani, sawa na asilimia **21.90** na Shilingi **40,000,000** ni fedha za nje, sawa na asilimia **0.8** ya fedha iliyoidhinishwa.

**Makusanyo ya Maduhuli ya Sekta ya Mifugo**

**25. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu **99,** ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **42,105,000,000**. Hadi kufikia Aprili, 2024, kiasi cha Shilingi **22,586,244,129.42** zimekusanywa sawa na asilimia **64.37** ya lengo la kukusanya Shilingi **35,087,500,000** kwa kipindi husika na asilimia **53.64** ya lengo la mwaka (**Kiambatisho Na. 5**). Upungufu huu umechangiwa na mapungufu yaliyokuwa kwenye mfumo wa *Local Government Revenue Collection Information System* (LGRCIS) katika ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara katika minada ya awali (**Kielelezo Na. 2**).




***Kielelezo NA. 2: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka 2023/2024 Sekta ya Mifugo***

**26**. ***Mheshimiwa Spika,*** vyanzo vikuu vya makusanyo ya Sekta ya Mifugo ni pamoja na tozo za huduma za mifugo (veterinary charges); vibali vya usafirishaji mifugo; ushuru wa soko; tozo za kusafirisha mifugo nje ya nchi (export duty); mauzo ya mitamba na mauzo ya mbegu na kimiminika cha hewa ya naitrojeni.

**Maeneo ya Vipaumbele katika Mwaka 2023/2024**

**27. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99 imetekeleza maeneo 10 ya vipaumbele ambayo utekelezaji wake umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Mifugo. Aidha, vipaumbele hivyo ni pamoja na: -

(i) Kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta ya Mifugo;

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo ili kuboresha mbari za mifugo;

(iii) Kuimarisha upatikanaji wa malisho, vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo;

(iv) Kuimarisha Afya ya Mifugo;

(v) Kuboresha Huduma za Ugani;

(vi) Kuimarisha programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT);

(vii) Kuimarisha Huduma za Utafiti na Mafunzo ya Taaluma za Mifugo;

(viii) Kuwezesha uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake;

(ix) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO); na

(x) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli katika Sekta.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 utekelezaji wa vipaumbele hivyo umewezesha Wizara kupata mafanikio na matokeo kama yalivyooainishwa hapa chini: -

**Sera, Sheria na Kanuni Katika Sekta ya Mifugo**

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara ya mifugo na mazao yake, Wizara imefanya marekebisho ya kanuni moja (1) ya Magonjwa ya Wanyama *The Animal Diseases (Animals and Animal Products Movement Control) Regulations of 2023* (*GN.No.448K/2023)*. Aidha, Wizara imeandaa Notisi ya Uteuzi wa Madaktari wa Mifugo kwa ngazi za Mikoa na Wilaya *The Animal Diseases (Appointment of District and Regional Veterinary Officers) Regulations of 2024 (G.N No.229/2024);* Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Nsimbo kimeanzishwa kupitia notisi *(Tanzania Livestock Research Institute (Establishment of Nsimbo Research Center)* iliyotolewa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza zenye *G.N No. 228/2024* na *No.227/2024;* pamoja na Notisi ya Wakaguzi wa Ustawi wa Wanyama *(Animal Welfare (Inspectors) Notice,2024)*, yenye *G.N No. 318/2024.*

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 kwa kuzingatia ushauri

uliotolewa na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Aidha, Wizara imekamilisha rasimu ya andiko la kuunganisha Bodi za Nyama na Maziwa na kupendekeza kuundwa kwa chombo maalum kitacho simamia uendelezaji wa mazao na miundombinu ya Mifugo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeandaa Mpango Mkuu wa Mifugo, Uvuvi na Kilimo Mazao, (Agricultural Transformation Masterplan - 2050) ambao utatoa dira ya mabadiliko katika sekta hizo.

**Uzalishaji na Uboreshaji wa Mbari za Mifugo**

**Huduma ya Uhimilishaji**

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) imezalisha dozi **111,844** za mbegu za ng'ombe na kusambaza dozi **67,958** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM). Pia, Wizara imewajengea uwezo wahimilishaji **196** kutoka katika MSM. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji ambapo hadi kufikia Aprili, 2024, ng'ombe **67,355,** wamehimilishwa ikilinganishwa na ng'ombe **60,697** waliohimilishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 katika mikoa **26** (**Kiambatisho Na. 6**).

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea na mkakati wa uhifadhi wa mbari za asili kwa kununua madume **25** ya ng'ombe wa asili ikiwemo Fipa, Gogo, Iringa red, Singida white, Ankole, Tarime, Sukuma na Maasai yatakayotumika kuvuna mbegu kwa ajili kuanzisha uhifadhi wa vinasaba vya mbari za mifugo wa asili iliyo hatarini kutoweka hapa nchini. Aidha, dume moja lina uwezo wa kuzalisha dozi **100,000** kwa mwaka, hivyo madume **25** yanategemewa kuzalisha dozi **2,500,000** kwa mwaka.

**Ugawaji wa Madume Bora ya Mbegu**

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuboresha mbari za ng'ombe ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa na nyama, Wizara ipo katika hatua za mwisho za ununuzi wa madume bora

**200** ya ng'ombe aina ya borani ambayo yatasambazwa kwa wafugaji kupitia vikundi vya Wafugaji katika halmashauri **10**.

**Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba**

**34.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2023/2024, jumla ya mitamba bora **735** ya maziwa wamezalishwa kwenye mashamba matano **(5)** ya Serikali na mitamba **183** imesambazwa kwa wafugaji. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya Nangaramo na Ngerengere kwa kununua ng'ombe wazazi **400** aina ya Borani kwa ajili ya kuzalisha mitamba bora. Pia, jumla ya mitamba bora **3,066** ya maziwa imezalishwa katika mashamba makubwa nane (**8**) kutoka katika Sekta Binafsi. Uzalishaji na usambazaji huu wa mitamba bora wa maziwa unategemea kuchangia kuongeza uzalishaji na unywaji wa maziwa nchini.

**Uzalishaji wa Kuku wa Nyama na Mayai**

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, jumla ya vifaranga vya kuku **95,584,347** vimezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hivyo, vifaranga vya kuku wa nyama **73,481,572**, kuku chotara **14,163,396** na kuku wa mayai **7,939,379,** ikilinganishwa na jumla ya vifaranga **83,845,967** vilivyozalishwa mwaka 2022/2023. Vilevile, uuzaji wa kuku na mazao yake umeendelea kuongezeka, kwa mwaka 2023/2024 jumla ya vifaranga vya kuku **2,701,429** vimeuzwa nchi za Zambia, Ubelgiji, Kenya, Ufaransa, Poland na Uingereza **(Kiambatisho Na. 7)**.

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha Tasnia ya kuku nchini kwa kuongeza uzalishaji wa kuku wazazi halisi kupitia kampuni ya Aviagen East Africa Limited iliyopo mkoani Kilimanjaro. Shamba hili ni la kuku wazazi halisi (grandparent stock) limeanza kuzalisha vifaranga aina ya Rosi na kuuza ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya vifaranga vya kuku wazazi (Parent Stock DoC) **515,174** wamezalishwa, kati ya hao takribani vifaranga **468,340** vya kuku wazazi halisi vimeuzwa katika nchi za Uganda, Kenya, Congo DRC, Rwanda, Burundi, Eritrea, Ethiopia, Djibout, Somalia na Sudan Kusini.

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imetoa vibali **71** vya kuingiza vifaranga vya kuku wazazi nchini kwa wadau waliosajiliwa kwenye mnyororo wa thamani ya kuku ambapo jumla ya vifaranga **1,371,746** vimeingizwa nchini **(Kiambatisho Na. 8).** Kati ya hivyo, vifaranga wa mayai (Commercial Layers Day Old Chicks - DOC) ni **527,710,** vifaranga vya kuku wazazi wa mayai (Layers Parent Stock - PS) ni **244,736,** vifaranga wa kuku wazazi chotara (PS Dual purpose DOC) **45,742,** na vifaranga wa kuku wazazi wa nyama **(**PS Broiler DOC**) 499,950.** Aidha, Jumla ya vifaranga vya kuku wazazi halisi (Grand Parent Stock DOC) **53,292** na jumla ya mayai **904,280** ya kuanguliwa (hatching eggs for parent stock) yameingizwa nchini **(Kiambatisho Na. 9)**.

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imefanikiwa kusajili jumla ya mawakala **85** wa usambazaji vifaranga nchini kwa lengo la kuimarisha na kuondoa changamoto ya udanganyifu unaofanywa na baadhi ya mawakala wasio waaminifu. Aidha, Wizara imetambua vitotoleshi **170** visivyo rasmi katika mikoa **11** vyenye kutotolesha jumla ya vifaranga **236,469** kwa mwezi sawa na vifaranga **2,837,628** kwa mwaka kwa lengo la kupunguza utotoleshaji holela wa vifaranga.

**Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, **2024**, jumla ya ng'ombe **2,957,724** na mbuzi/kondoo **2,828,248,** wenye thamani ya Shilingi trilioni **3.4,** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **2,218,293**, mbuzi/kondoo **2,121,187** wenye thamani ya Shilingi trilioni **1.7** waliouzwa katika mwaka **2022/2023**. Ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa minadani limetokana na hamasa ya uvunaji wa mifugo na kuimarika kwa soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali imeendelea kudhibiti utoroshaji wa mifugo katika minada ya mipakani kwa kuimarisha vituo vitano vya utoaji huduma na elimu juu ya biashara ya mifugo na mazao yake katika maeneo ya Handeni (Ndelema), Monduli (Makuyuni), Busega (Lamadi), Misenyi (Kyaka), na Momba (Tunduma).

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha utendaji wa NARCO, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Mabadiliko wa Miaka Mitatu (2022/2023 hadi 2024/2025) wenye vipengele vitano ambavyo ni: - uboreshaji wa mbari za mifugo, uendelezaji wa malisho na vyakula vya mifugo, unenepeshaji wa mifugo, skimu za unenepeshaji kupitia vijana na wanawake na uendelezaji wa masoko. Aidha, utekelezaji wa maeneo hayo umehusisha uwekezaji wa Shilingi 4,645,000,000 zilizotengwa kutoka serikalini mwaka 2022/2023 kwa ajili ya ununuzi wa ng'ombe wazazi **800**, mbuzi **2,000**, kondoo **2,000**, vifaa shamba, Mbegu za malisho na kununua magari 4 katika ranchi za Kongwa, West Kilimanjaro, Mzeri na Ruvu ranch. Uwekezaji huu utaiwezesha NARCO kutumia maeneo yake kikamilifu na kuongeza tija.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Bodi ya Nyama, imeendelea kusimamia na kuratibu biashara ya nyama kwenda nje ya nchi ambapo, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya tani **13,745.38** (zikiwemo tani **1,024.33** za nyama ya ngómbe, tani **9,982.67** za mbuzi, tani **3,195.09** za kondoo, tani **32.35** za kuku na tani **10.94** za nguruwe (**Kiambatisho Na.10**), zenye thamani ya Dola za Marekani milioni **56.6,** zimeuzwa nje ya nchi, ikilinganishwa na tani **12,243.8** zenye thamani ya Dola za Marekani milioni **51.9** kwa mwaka 2022/2023. Mauzo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia **12.3** ikilinganishwa na mwaka 2022/2023. Aidha, nyama ya mbuzi imeendelea kuongoza kwa kuchangia asilimia **72.6** mauzo ya nyama nje. Hii ni kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa **Dkt.** Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongeza mashirikiano na fursa za kibiashara nje ya nchi, masoko ya nyama ya yameendelea kuongezeka kufikia nchi **12** ambazo ni Bahrain, Comoro, Hong Kong, Jordan, Kenya, Kuwait, Oman, Qatar, Rwanda, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Vietnam.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa imeendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa kupitia vyombo vya habari na maonesho mbalimbali yakiwemo ya Wiki ya Unywaji Maziwa, Maonesho ya Saba saba, Nane Nane, Siku ya Chakula Duniani na Programu ya Unywaji wa Maziwa

Shuleni. Aidha, wadau **35** wa maziwa wamewezeshwa kushiriki Maonesho ya Saba Saba na Nane Nane. Vilevile, Bodi imeratibu na kusimamia Wiki ya Unywaji Maziwa Shuleni kitaifa iliyofanyika Septemba 2023, mkoani Mwanza ambapo jumla ya wanafunzi **12,506** walishiriki na kunywa lita **3,126.5** za maziwa. Hadi April 2024, programu hiyo inatekelezwa katika shule **136,** zenye jumla ya wanafunzi **101,104** (**Kiambatisho Na.11**).

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, uzalishaji wa maziwa umefikia lita bilioni **3.97** ikilinganishwa na lita bilioni **3.6** mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la asilimia **10.3**. Aidha, usindikaji wa maziwa umefikia lita milioni **81.8** mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na lita **77.3** mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la asilimia **5.8**. Ongezeko la uzalishaji wa maziwa limechangiwa na juhudi za Serikali za utoaji elimu ya ufugaji bora kupitia huduma za ugani. Pia, ukusanyaji wa maziwa kupitia Vituo vya Kukusanyia Maziwa umeongezeka kutoka lita milioni **71.80,** mwaka 2022/2023 hadi kufikia lita milioni **93.4** mwaka 2023/2024. Vilevile, Bodi imetoa vibali **782** vya kuingiza maziwa nchini ambapo jumla ya lita **11,747,150** za maziwa, zenye thamani ya Shilingi **23,423,652,811.8,** zimeingizwa nchini ili kukidhi mahitaji ya maziwa yaliyosindikwa hususan maziwa ya unga. Aidha, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi iliyopelekea kuanza kwa uzalishaji wa maziwa ya unga hapa nchini. Uwekezaji huu utachangia kupunguza uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa mara ya kwanza imeandaa Mpango Kazi wa utekelezaji wa programu ya Unywaji Maziwa Shuleni na kufanikiwa kutengeneza nakala **4,000** ambapo nakala **1,300** zimesambazwa kwa wadau wanaojishughulisha na utekelezaji wa mpango huo. Sambamba na uandaaji wa mpango huo, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) wametengeneza na kusambaza vibanda vya maziwa shuleni (school milk access points) katika shule nane (**8)** zenye jumla ya wanafunzi **6,994** zikiwemo mbili (**2**) za jiji la Dodoma, nne (**4**) mkoani Mbeya na mbili (**2**) katika Manispaa ya Morogoro. Idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kufikiwa katika kipindi cha miaka

mitano (2023/2024-2027/2028) ya utekelezaji wa mpango kazi huu ni **1,609,687**.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, jumla ya vipande vya ngozi milioni **14.69** (ng'ombe milioni **4.6**, mbuzi milioni **7.5** na kondoo milioni **2.6**), vyenye thamani ya Shilingi bilioni **32.1,** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni **14.1** (ng'ombe milioni **4.4**, mbuzi milioni **7.2** na kondoo milioni **2.5**), vyenye thamani ya Shilingi bilioni **31.1,** vilivyozalishwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limechangiwa na wafugaji kupatiwa mafunzo kuhusu ufugaji wa kisasa na kibiashara wa mifugo na uhamasishaji kuhusu uvunaji wa mifugo kwa wakati.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya vipande **1,542,916** vya ngozi vyenye uzito wa kilo **5,777,669.5** (ng'ombe vipande **1,034,447**, Mbuzi vipande **355,928** na Kondoo vipande **152,541**) vyenye thamani ya Shilingi bilioni **7** viliuzwa katika nchi za Nigeria, Togo, Kenya, Ethiopia na Pakistan ikilinganishwa na vipande vya ngozi **748,009** vyenye uzito wa kilo **3,591,396** (ng'ombe vipande **748,009**) vyenye thamani ya Shilingi bilioni **5.50** vilivyouzwa katika nchi za Nigeria, Ghana, Togo na Pakistan mwaka 2022/2023. Aidha, mauzo ya ngozi kwenda nje ya nchi yameongezeka kutokana na mahitaji ya soko la ngozi isiyosindikwa kuongezeka katika nchi za Nigeria na Togo. Pia, Wizara imewawezesha wamiliki wa machinjio za kisasa zilizo chini ya EPZA kwa kuwaondolea kodi ya kusafirisha ngozi nje ya nchi. Hatua hii imeleta mafaniko ya kupata soko la ngozi ya mbuzi na kondoo nje ya nchi ambayo imekosa soko la ndani.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya ngozi imeendelea kusimamia biashara na ubora wa ngozi kwa kusajili na kutoa leseni kwa maghala **30** ya ngozi kwa kampuni za wafanyabiashara wanaosafirisha ngozi kwenda nje ya nchi. Aidha, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Sekta Binafsi kutoa mafunzo kuhusu uendelezaji wa zao la ngozi nchini. Wachunaji wa ngozi **213** na wataalam wa mifugo **16** wamejengewa uwezo kuhusu uchunaji bora wa ngozi unaozingatia mahitaji ya soko kutoka katika Mikoa mitano (**5**).

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika ngozi ambapo hadi Aprili, 2024 kuna viwanda vitatu (**3**) vinavyofanyakazi ambavyo ni: Himo Tanners and Planters (Kilimanjaro), ACE Leather (T) Ltd. (Morogoro) na Phiss Tanners (Pwani). Viwanda hivyo vinasindika jumla ya vipande **198,100** vya ngozi ya ng'ombe na **717,000** vya ngozi ya mbuzi na kondoo vyenye thamani ya Shilingi bilioni **21.5** (**Kiambatisho Na. 12)**. Aidha, Wizara imefanikiwa kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa malighafi bora kwa kuwaunganisha wamiliki wa viwanda vya kusindika ngozi na wazalishaji wa ngozi. Pia, jumla vya vipande **10,550** vya ngozi ya ng'ombe na **409,229** vya kondoo na mbuzi vilivyosindikwa hadi ya hatua ya kati (wet blue) vimeuzwa katika nchi za Pakistan na Ethiopia kwa thamani ya Shilingi **860,315,600**.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 jumla ya jozi za viatu **3,028,700** zimezalishwa ikilinganishwa na jozi **2,927,500** zilizozalishwa mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limetokana kuongezeka kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs) **151** wanaotengeneza bidhaa za ngozi pamoja na ongezeko la upatikanaji wa ngozi bora (**Kiambatisho Na.13**).

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea na ujenzi na ukarabati wa minada **26** ya awali, upili na mpakani. Kati ya minada hiyo, minada saba (7) ya Mhunze (Kishapu), Gwandi (Chemba), Nyanguge (Magu), Buhungulwa (Kwimba), Mkongeni (Mvomero), Waso (Ngorongoro) na Kintinku (Manyoni) imekamilika. Aidha, minada **19** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kukamilika kwa ujenzi huu kutachangia kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo na kupunguza upotevu wa maduhuli kupitia utoroshaji wa mifugo.

**Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imefanikiwa kuendelea kuimarisha upatikanaji wa maji kwa mifugo ambapo imekamilisha ujenzi wa mabwawa matatu (**3)** ya Kongwa (Morogoro), Naalarami (Monduli) na Vinyenze (Kibaha) ambayo

yanakadiriwa kuhifadhi wastani wa lita milioni **100** za maji na yana uwezo wa kunywesha mifugo **3,500** kwa siku kila moja.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta **81,625.9** za maeneo ya malisho katika vijiji **194** vya Mikoa ya Kigoma, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu, Tanga, Shinyanga, Singida, Rukwa, Arusha, Morogoro, Pwani, Iringa, Dodoma, Tabora na Njombe kupitia Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na kufanya maeneo yaliyotengwa kufikia hekta **3,466,111.43** kutoka hekta **3,384,485.5** mwaka 2022/2023. (**Kiambatisho Na. 14**)

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuhakikisha maeneo ya malisho yaliyotengwa kwenye vijiji yanaendelezwa, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Tanzania People and Wildlife* (TPW) imezijengea uwezo kamati 50 za usimamizi wa maeneo ya malisho katika vijiji **61,** na kufanya tathmini, usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malisho kwenye Wilaya za Simanjiro **(3)**, Babati **(5)**, Monduli **(22)** Ngorongoro **(2),** Longido **(25)** Same **(2)** na Mwanga **(2).** Vilevile, Wizara imefanya kazi ya kuondoa vichaka na mimea vamizi kwenye maeneo ya malisho yenye ukubwa wa ekari **7,279** kwenye Vijiji 17 katika Wilaya za Monduli **(4)**, Longido **(11)**, Babati **(1)** na Simanjiro **(1)** pamoja na kuzuia mmomonyoko wa udongo kwenye maeneo ya malisho kwa kufukia makorongo yenye zaidi ya ukubwa wa kilomita **100** katika kongani ya Muriatata inayoundwa na vijiji vya Armanie, Engushai, Mundarara na Kiseriani katika Halmashauri ya Longido. Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la *Heifer International* vikundi vya vijana na wanawake **769** vyenye jumla ya wana vikundi **15,453** vimejengewa uwezo sambamba na kuanzisha mashamba darasa ya malisho **161** katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Mwanza, Mara, Kagera pamoja na Zanzibar**.**

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kushiriki katika utatuzi wa Migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ili kuwezesha wafugaji kujikita katika ufugaji bora na wenye tija. Katika mwaka 2023/2024, jumla ya migogoro **14** inayohusu

wafugaji na maeneo ya hifadhi, maeneo ya Serikali na taasisi, wakulima na Ranchi za Kampuni za Taifa (NARCO) imepokelewa ambapo kwa ushirikiano na Wizara za kisekta migogoro **8** imetatuliwa katika Mikoa ya Kagera **(2),** Morogoro **(4),** Mbeya **(1)** na Mara **(1).** Aidha, Rasimu ya mkakati wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imeandaliwa.

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuongeza upatikanaji wa mbegu na malisho ya mifugo ambapo jumla ya tani **127.8** za mbegu za malisho aina ya nyasi na mikundekunde zimezalishwa kutoka mashamba ya serikali na Sekta Binafsi ikilinganishwa na tani **22.7** zilizozalishwa mwaka 2022/2023. Pia, Jumla ya marobota ya hei **267,695** yamevunwa kutoka katika mashamba ya Serikali na binafsi ikilinganishwa na marobota **248,209** mwaka 2022/2023. Vilevile, jumla ya tani **728.6** za saileji zimezalishwa katika mashamba ya Serikali na binafsi. Ongezeko hili limetokana na uwekezaji wa mashine, zana na vifaa shamba.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa malisho, jumla ya tani **38.9** za mbegu za malisho aina ya Napier iliyoboreshwa (Juncao) zilinunuliwa na kusambazwa katika maeneo ya Msomera tani **5**, Kongwa Ranchi tani **20**, Ruvu Ranchi tani **3.9,** na tani **10** katika mikoa ya Morogoro, Pwani na Tanga. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa mashamba darasa ya malisho **150** yenye ukubwa wa ekari **865** katika Halmashauri **71** ambapo jumla ya tani **5** za mbegu za nyasi aina ya *Rhodes* zimesambazwa katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Rukwa, Katavi, Kigoma, Kagera Geita, Shinyanga, Simiyu, Singida Pwani, Arusha, Manyara, Songwe, Ruvuma na Lindi.

**Rasilimali za Vyakula vya Mifugo**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imefanya ukaguzi wa maeneo **250** ya kuzalisha, **416** ya kuuza na **81** ya kuhifadhi rasilimali za vyakula vya mifugo ambapo maeneo mapya **29** ya kuzalisha vyakula vya mifugo yamesajiliwa katika mikoa ya Arusha **(5),** Dar es Salaam **(12),**

Morogoro **(2),** Pwani **(7),** Mwanza **(1),** Katavi **(1)** na Dodoma **(1)** Ili kuongeza ubora na usalama wa vyakula vya mifugo. Aidha, kaguzi hizo zimebaini ongezeko la viwanda vya kuzalisha vyakula vya mifugo kutoka **221** mwaka **2022/2023** hadi **250** mwaka **2023/2024**. (**Kiambatisho Na.15**)

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kutoka tani **1,580,000** mwaka 2022/2023, hadi tani **1,880,000** mwaka 2023/2024, ambapo ongezeko hili limetokana na Serikali kuendelea kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa Sekta Binafsi.

**Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani wa Mifugo**

**Utafiti**

***59. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuratibu, kuwezesha na kusimamia shughuli za Utafiti wa Mifugo nchini ambapo imefanya tathmini katika vituo saba **(7)** vya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo **Tanzania** (TALIRI) na uratibu wa Taasisi zingine kumi na moja **(11)** zinazofanya utafiti unaohusiana na Mifugo nchini. Lengo la Tathmini likiwa kubaini tafiti mbalimbali zinazofanyika pamoja na uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na utekelezaji wa Agenda ya Utafiti wa Mifugo nchini ya mwaka 2020-2025. Aidha, tafiti hizi zilizofanyika zimechangia katika utatuzi wa changamoto mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa mifugo ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa mbari za mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mifugo, upatikanaji wa mbegu bora za malisho na uboreshaji wa malisho ya asili.

**Mafunzo**

***60. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kufanya uratibu katika vyuo vya Mafunzo ya Mifugo kumi na tatu (13) nchini ikihusisha tathmini ya mafunzo katika kampasi nane (9) zilizo chini ya Wakala ya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA) na vyuo Binafsi kumi na mbili (12). Lengo likiwa ni kuona uzingatiwaji wa utumiaji wa mitaala ya wizara, uwiano wa

wakufunzi na wanafunzi, miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Tathmini hiyo ilibaini kuwa vyuo hivyo vinazingatia mitaala na miongozo **(**Maelezo ya kina kuhusu LITA yanapatikana ibara 86-88).

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo Endelevu (Sustainable Agriculture Tanzania – SAT) inaendelea na zoezi la kuhuisha Mitaala mitatu (**3**) ya mifugo ambayo ni afya na uzalishaji wa mifugo, Teknolojia ya maabara za veterinari na usimamizi wa nyanda za malisho na udhibiti wa mbung'o. Lengo la zoezi hili ni kuwezesha vijana wanaosoma mafunzo ya mifugo kukidhi mahitaji muhimu ya wadau, mabadiliko ya teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukidhi soko la ajira.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya nje, imeratibu na kuwezesha wanafunzi **69** kwenda nchini Israel kwa mafunzo ya mafunzo ya utarajali (Internship programme) kuhusu shughuli za ufugaji. Kati ya hao **12** kutoka Kampasi za LITA na **57** kutoka Vyuo vya Binafsi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia mradi wa *Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination* (TANIPAC) imeendesha mafunzo ya Sumukuvu kwa Wakufunzi kutoka katika Vyuo **20** vikiwemo Kampasi Nane **(8)** chini ya LITA na Vyuo vya Binafsi **12** vinavyotumia Mtaala wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Huduma za Ugani**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imewezesha Mafunzo Rejea kwa Maafisa Ugani **1,058** katika Kanda Nane (**8**) ikihusisha Mikoa **26** na Halmashauri **184.** Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Sekta binafsi, wadau wa maendeleo na Asasi zisizo za Kiserikali, imewapa mafunzo rejea jumla ya Wafugaji **250,000** wakiwemo wafugaji wa mfano **620** kupitia mradi wa TIP3 unaotekelezwa na Heifer International Tanzania ambapo lengo mahususi likiwa ni ufugaji wa Kibiashara na tija. Aidha Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na Utekelezaji wa Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building a Better Tomorrow

BBT); Uboreshaji wa Koosafu za mifugo, Udhibiti wa Magonjwa na tiba kwa mifugo; Matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ugani (MIMIS, M-Kilimo na Ugani Kiganjani); Upatikanaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho na Vyakula vya mifugo.

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta imeendelea kusambaza teknolojia za ufugaji bora, uzalishaji, usindikaji wa mazao yatokanayo na mifugo, hifadhi ya malisho pamoja na upatikanaji wa masoko kupitia maonesho na maadhimisho mbalimbali. Aidha, jumla ya wadau **67,832** wamefikiwa kupitia maonesho ya Kimataifa ya Biashara – Saba Saba, maadhimisho ya wakulima - Nane Nane na Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani. Pia, jumla ya vipeperushi **4,279** na vitabu **290** vya ufugaji bora wa mifugo vilisambazwa kwa wadau.

**Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo Upatikanaji na Usambazaji wa Chanjo**

**65.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/24, ili kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini, jumla ya dozi za chanjo **695,978,188** zimetumika ambapo kati ya hizo, dozi **520,153,000** zimeingizwa kutoka nje ya nchi na dozi **175,825,188** zimezalishwa ndani ya nchi kwa ajili ya kuchanja magonjwa **13** ya kipaumbele. Kati ya dozi hizo zilizozalishwa nchini, dozi **62,173850** zimetengenezwa na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) na dozi **113,651,338** zimezalishwa na Sekta Binafsi.

**Uchanjaji wa Mifugo**

**66.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024, Wizara, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo kupitia uchanjaji, uogeshaji mifugo na utoaji elimu kuhusu udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya dozi **616,070,986** zimetumika kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa **13** ya kipaumbele ambayo ni: Kimeta kwa ng'ombe mbuzi na kondoo dozi **1,521,495**; Kichaa cha mbwa na paka dozi **991,346;** Homa ya Mapafu ya Ng'ombe dozi **5,734,881**; Ugonjwa wa Miguu na

Midomo (FMD) ng'ombe dozi **2,523,786**; Sotoka ya Mbuzi na Kondoo dozi **3,780,210**; Mdondo dozi **296,479,000**; Gumboro dozi **220,829,000;** Ndigana Kali dozi **95,681** na Mahepe (*Marecks*) dozi **61,243,770;** Chambavu (BQ) dozi **883,100;** Ugonjwa wa Kutupa Mimba (Brucellosis) dozi **53,975**; Mapele ya Ngozi (LSD) dozi **106,011** na Ndui ya Kuku (*Fowl pox*) dozi **21,828,713** (**Kiambatisho Na.16**). Aidha, uchanjaji wa mifugo umesaidia kupungua kwa matukio ya magonjwa yanayovuka mipaka kutoka asilimia **3.5,** mwaka 2022/2023 hadi asilimia **2.5,** mwaka 2023/2024 na kuiwezesha Tanzania kukidhi matakwa ya biashara ya mifugo na mazao yake kulingana na matakwa ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Biashara Duniani (WTO).

**Ujenzi wa Majosho na Uogeshaji wa Mifugo**

**67. Mheshimiwa *Spika*,** katika mwaka 2023/2024, ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengine, Wizara ilipanga kujenga jumla ya majosho **246** yenye thamani ya **Shilingi 5,658,000,000** katika Halmashauri **65,** fedha hizi zilihamishiwa kwenye Halmashauri ili kuwezesha ufanisi, tija na umiliki wa miradi kwa Halmashauri (**Kiambatisho Na.17**). Aidha, uogeshaji wa mifugo unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya michovyo **1,342,932,142** ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng'ombe **660,725,421**, mbuzi **453,142,239**, kondoo **201,975,117** na punda **27,089,365**. Michovyo hii ni sawa na asilimia **75** ya lengo la michovyo bilioni **1.8** kwa mwaka 2023/24.

**68. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara yatokanayo na magonjwa yanayoambukiza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, ambapo imekagua jumla ya mifugo **8,320,065** (ng'ombe **816,375** mbuzi **493,872**, kondoo **182,014,** nguruwe **207,592** na kuku **6,620,252**). Aidha, jumla ya ng'ombe **12,840**, mbuzi na kondoo **198,374**, ngamia **10** wamekaguliwa na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, mifugo **78,120** wakiwemo ng'ombe **5122,** mbuzi na kondoo **72,819**, ngamia **16** na nguruwe **163** wamekaguliwa na kuingizwa nchini kwa ajili ya uzalishaji. Pia, Wizara inaendelea kutumia mfumo wa utoaji wa taarifa kwa

kutumia simu janja (EMA-i) ambao umewezesha utoaji wa taarifa za matukio ya magonjwa kwa wakati katika Halmashauri **114**. Mfumo huu umewezesha ufuatiliaji wa magonjwa ambapo taarifa zinaonesha kupungua kwa matukio ya magonjwa yanayovuka mipaka kutoka asilimia **3.5** mwaka 2022/2023 hadi asilimia **2.5** mwaka 2023/2024.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali kupitia Baraza la Veterinari Tanzania, imefanya ukaguzi wa vituo **837** vya kutolea huduma za afya ya wanyama katika Halmashauri **66**. Aidha, vyuo vitatu (3) vya mafunzo ya afya na uzalishaji wa wanyama ambavyo ni Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Afya Chato (Geita), Taasisi ya Mafunzo ya Kilimo Igabiro (Kagera) na KARUCO (Kagera) vimekaguliwa.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania limesajili madaktari wa wanyama **25** kati ya **70** waliotarajiwa kusajiliwa na kufanya idadi yao kufikia **956** ambapo wanaume ni **852** na wanawake ni **104**. Aidha, wataalam wasaidizi **377** wa afya ya wanyama wameandikishwa na kufanya idadi yao kufikia **5,418** ambapo kati yao wanaume ni **3,663** na wanawake ni **1,755**. Vile vile, leseni **35** zimetolewa kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara na kufanya wakaguzi wa nyama kufikia **933**, wahimilishaji **85** na wataalam wa maabara **82**. Pia, vituo **139** vya kutolea huduma za afya ya wanyama vilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia **2,479**.

**71.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Baraza la Veterinari linaendelea kusimamia mafunzo ya uanagenzi kwa wahitimu wa shahada ya udaktari wa Wanyama. Aidha, jumla ya madaktari wa Wanyama wahitimu **162** wanaendelea na mafunzo hayo katika vituo **66** vilivyopo katika maeneo mbalimbali ndani ya Tanzania bara na Zanzibar. Pia, mitihani ya kuandikishwa imefanyika kwa wahitimu **965** wa stashahada ya afya na uzalishaji wa Wanyama kwa ajili ya

kupata sifa ya kuandishwa na kuweza kutoa huduma za afya ya mifugo.

## C. TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MIFUGO

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kupitia Taasisi zake sita ambazo ni Bodi ya Nyama Tanzania (**TMB**), Bodi ya Maziwa Tanzania (**TDB)**, Kampuni ya Ranchi za Taifa (**NARCO**), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (**TALIR**I), Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (**LITA**), na Wakala ya Maabara ya Veterinari (**TVLA**). Taasisi hizi zimewezesha upatikanani wa huduma kwa wadau wa Sekta kwa haraka ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa teknolojia na utatuzi wa changamoto katika mnyororo wa thamani wa Mifugo. Baadhi ya kazi na majukumu yaliyotekelezwa na Taasisi hizo ni kama ifuatavyo;

### Kampuni ya Ranchi za Taifa

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2023/2024 Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) iliweza kuzalisha ndama **1,361**; kusambaza mitamba **201** kwa wafugaji ili kuboresha kosaafu za mifugo; kuzalisha na kuuza tani **186** za nyama; kunenepesha na kuchinja ng'ombe **1,534**; kufyeka na kuondoa vichaka hekta 445 katika Ranchi za Kongwa, Ruvu na West Kilimanjaro kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho; kuzalisha jumla ya robota **52,500** za malisho; kuwezesha kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji **276** katika vijiji vinavyozunguka Ranchi za NARCO; na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi **505** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini.

### Bodi ya Nyama ya Tanzania

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) imeendelea kusimamia, kuratibu na kuendeleza shughuli mbalimbali zinazofanyika katikaTasnia ya nyama nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, hadi kufikia Aprili, 2024, Bodi imefanya jumla ya kaguzi **8,701** kwa wadau mbalimbali wanaofanya shughuli za uzalishaji katika mnyororo wa thamani wa nyama. Idadi hiyo ni sawa na asilimia **96.68** ya lengo

la mwaka wa **2023/2024** la kukagua wadau **9,000**. Aidha, ukaguzi na Utambuzi huo umefanyika katika mikoa **18** ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Tabora, Shinyanga, Kigoma, Mwanza, Kagera, Mara, Dar-es-salaam, Pwani, Mtwara, Mbeya, Ruvuma. Songwe, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Ukaguzi huo umekuwa ukifanyika kwa lengo la kuhakikisha nyama na bidhaa zake zinazoingia sokoni zinakuwa bora na salama ili kulinda afya za watumiaji wa bidhaa hizo.

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, katika kuhakikisha biashara ya nyama inaratibiwa na wahusika wanatambulika, Wizara kupitia Bodi ya Nyama Tanzania imesajili jumla ya wadau wapya **3,038** hadi kufikia Aprili, 2024. Idadi hiyo inajumuisha wazalishaji wa mifugo **66,** wafanyabiashara wa mifugo **141,** minada **12,** machinjio **56,** magari maalumu ya kubeba nyama **208,** wasindikaji na wasambazaji wa nyama **55,** maduka na maeneo ya kufanyia biashara ya nyama **2,396.** Wadau hawa **3,038** waliosajiliwa ni sawa na asilimia **67.12** ya lengo la mwaka 2023/2024 la kusajili jumla ya wadau **4,527**. Aidha, kufikia Aprili, 2024, Bodi imehuisha usajili wa wadau **3,594** kati ya lengo la kuhuisha wadau **4,542**. Idadi hiyo ya wadau ni sawa na asilimia **79.13** ya malengo ya mwaka.

**76.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, ili kuhakikisha nyama na bidhaa zake zinazoingia sokoni zinakuwa bora, salama na kulinda afya za watumiaji pamoja na kuongeza thamani ya nyama, Bodi imeendesha mafunzo kwa wasindikaji na wauzaji wa nyama wapatao **10,175**, ambao ni sawa na asilimia **84.16** ya lengo la kuwafikia wadau **12,090** Mafunzo hayo yalitolewa katika mikoa **18** ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Tabora, Shinyanga, Kigoma, Mwanza, Kagera, Mara, Dar-es-salaam, Pwani, Mtwara, Mbeya, Ruvuma, Songwe, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

**Bodi ya Maziwa**

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) imeendelea kusimamia, kuratibu na kuendeleza Tasnia ya Maziwa nchini ambapo imefanya ukaguzi kwa wafanyabiashara **867** kati ya **1,200** waliolengwa

sawa na asilimia **72.3** katika Kanda ya Mashariki **327**, Kanda ya Kaskazini **102**, Kanda ya Kati **165**, Kanda ya Ziwa **121** na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini **152** na hatua stahiki zilichukuliwa kwa mujibu wa sheria na kanuni kwa wale waliokiuka sheria.

**78.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024, Bodi pia imesajili jumla ya wadau **4 1 1** wa maziwa kati ya **400** waliolengwa sawa na asilimia **103** wakiwemo wazalishaji **148**, wasindikaji **52**, wafanyabiashara **89**, waingizaji **24** wa maziwa nchini, wauzaji wanne ( **4** ) wa maziwa nchi za nje, wasambazaji tisa ( **9)**, wakusanyaji **12**, maghala **48** ya kuhifadhia maziwa, wauzaji watatu (**3**)wa pembejeo zinazohusika na uzalishaji maziwa, wachuuzi **14** na wasafirishaji nane (**8**) wa maziwa. Katika zoezi hilo, elimu kuhusu Sheria ya Tasnia ya maziwa na Kanuni zake ilitolewa.

**79.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, vilevile, Bodi imetoa mafunzo kwa wadau wa maziwa **1,040** kati ya **2,000,** sawa na asilimia **52** ya waliolengwa wakiwemo wafugaji **655** wa ng'ombe wa maziwa, wasafirishaji **85** wa maziwa, wasindikaji **64** wa maziwa, wauzaji **175** wa maziwa na wasimamizi **61** wa vituo vya kukusanyia maziwa katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha na Tanga.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari (TVLA)**

**80.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2023/2024, Wakala ya Maabara ya Veterinari (TVLA) kupitia Taasisi ya kuzalisha chanjo (TVI) iliyopo Kibaha mkoani Pwani imezalisha na kusambaza chanjo za mifugo dozi **62,173,850** dhidi ya magonjwa mbalimbali ya kipaumbele kama ifuatavyo: dozi **689,100** za kimeta, dozi **133,250** za Chambavu, dozi **1,650** za Ugonjwa wa Kutupa Mimba, dozi **1,367,500** za Homa ya Mapafu ya Ngombe, dozi **289,400** za Homa ya Mapafu ya Mbuzi, dozi **357,250** za mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu na dozi **59,335,700** za Mdondo. Aidha, katika mwaka 2023/2024, Wakala ya Maabara za Veterinari imefanya uchunguzi wa magonjwa ya wanyama kwenye sampuli **21,667**, Kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo kwenye sampuli **2,550** na kutoa vibali **54** vya kuingiza viuatilifu vya mifugo nchini.

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya kiwanda cha uzalishaji chanjo kwa kuweka mtandao wa intaneti ya mkongo wa Taifa na kufunga vifaa vya kisasa vya maabara. Aidha, Serikali imeanza ujenzi wa jengo la kisasa la maabara kwa ajili ya uzalishaji wa chanjo za magonjwa yasababishwayo na virusi. Pia, Serikali imeendelea na Utafiti wa chanjo mbili ambazo ni Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ambao hadi sasa upo katika hatua mbalimbali.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, TALIRI imeendelea kufanya tafiti za kuboresha mbari za mifugo na malisho ambapo jumla ya miradi **54** ya utafiti inaendelea kutekelezwa. Aidha, matokeo ya tafiti hizo ni kuibuliwa na kusambazwa kwa teknolojia, ambapo jumla ya mifugo iliyoboreshwa **268** ilizalishwa wakiwemo ng'ombe chotara wa nyama ambao wana sifa ya ukuaji wa haraka na uzalishaji wa nyama nyingi, ng'ombe chotara wa maziwa, wenye uwezo wa kuzalisha hadi lita **15** za maziwa kwa siku, na mbuzi wa kuzalisha nyama na maziwa (dual purpose). Kati ya mifugo hiyo iliyozalishwa, **120** ilisambazwa katika mikoa ya Dodoma (Dodoma Jiji, Bahi, Mpwapwa na Kongwa), Tanga (Muheza na Tanga Jiji); Mbeya (Mbeya Jiji); Pwani (Mkuranga), Dar-es-Salaam (Ilala), Arusha (Longido na Meru) na Morogoro (Morogoro DC). Mifugo hii inasambazwa kwa ajili ya uboreshaji wa makundi ya mifugo ya wafugaji katika maeneo mbalimbali ya nchi.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI inaendelea kuhifadhi na kutunza mbari za mifugo ya asili yenye sifa maalumu zikiwemo ukuaji, uhimilivu wa magonjwa na uzalishaji kwa ajili ya utafiti. Katika mwaka 2023/2024, jumla ya mbuzi **51** na kondoo **83** wenye sifa maalumu walizalishwa. Aidha, jumla ya mbuzi **188** na kondoo **71** chotara walizalishwa ambapo mbuzi **122** na kondoo **56** chotara walisambazwa katika mikoa ya Kilimanjaro (Siha), Dodoma (Dodoma Jiji, Mpwapwa na Bahi); Pwani (Kisarawe na Mkuranga); Mbeya (Mbeya Jiji); Dar-es-Salaam (Ilala) na Arusha (Longido na Meru).

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya uzalishaji wa kuku wa asili walioboreshwa aina ya Horasi unafanyika kupitia mradi wa *Tropical Poultry Genetic Solution* (TPGS) ambapo jumla ya mayai **5,032** yalinunuliwa kutoka kwa wafugaji na vifaranga **3,042** vimetotolewa na kutunzwa katika kituo cha TALIRI Naliendele. Aidha, zoezi la uzalishaji na uchaguzi wa kuku wenye sifa bora miongoni mwa kuku jamii ya horasi linaendelea kwa lengo la kupata kizazi chenye sifa bora kwa ajili ya kusambaza kwa wafugaji nchi nzima. Jamii hii ya kuku ina uwezo wa kuzalisha nyama na mayai kwa kiwango sawa au kinachokaribia cha kuku wa kigeni.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** TALIRI inaendelea kufanya utafiti, uzalishaji na usambazaji wa teknolojia bora za malisho na mbegu za malisho ambapo jumla ya kilo **5,298** za mbegu za nyasi (punje) zimezalishwa na kilo **2,451** zimesambazwa; kilo **1,372** za mbegu za nyasi (vipando) zimezalishwa na kilo **918.5** zimesambazwa katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, Taasisi imezalisha jumla ya marobota **24,398** ya nyasi kavu (hay) na marobota **17,824** yaliuzwa kwa wadau wa mifugo katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Mbeya na Iringa. Pia, Wizara kupitia TALIRI imekamilisha usajili wa aina tano **(5)** za mbegu za malisho na kupata ithibati kutoka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (Tanzania Official Seed Certification Institute -TOSCI).

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI imeanzisha Kituo cha Utafiti wa Mifugo Kanda ya Magharibi kilichopo katika Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi ambapo maandalizi mbalimbali ya kuanza utekelezaji wa shughuli za utafiti ikiwemo ununuzi wa vifaa shamba na ujenzi wa miundombinu yanaendelea. Aidha, lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuhakikisha wadau katika kanda zote za kiikolojia nchini wananufaika na matokeo ya tafiti za mifugo zinazofanywa na TALIRI.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

**87.** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) imeendelea kuimarisha Kampasi za mafunzo ambapo katika mwaka 2023/2024 imekamilisha ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za

mihadhara, zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **250** kila moja, katika Kampasi za Morogoro na Mpwapwa. Aidha, ufungaji wa viti **150** katika awamu ya kwanza umekamilika kwenye kumbi mpya za mihadhara katika Kampasi ya Mabuki. Vilevile, utekelezaji wa miradi mipya ya ujenzi wa kumbi tatu (**3**) za mihadhara, hostel tano (**5**) za wanafunzi na jengo moja la utawala umeanza katika kampasi za Tengeru, Kikulula, Buhuri, Madaba na Kampasi mpya ya Songwe.

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, LITA imedahili wanafunzi **4,454** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika kampasi nane **(8)** za Wakala ukilinganisha na wanafunzi **4,036** waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2022/2023. Idadi hiyo ni ongezeko la wanafunzi **418**, sawa na ongezeko la asilimia **10**.

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wakala imeendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wadau mbalimbali katika Sekta ya Mifugo ambapo Mafunzo ya usindikaji wa maziwa kwa wajasiriamali **16** kutoka Taasisi ya Dodoma Halisi yamefanyika katika Kampasi ya Mpwapwa; Mafunzo rejea ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa yamefanyika kwa wanufaika **556** waliojumuisha wafugaji na maafisa ugani wa mifugo kupitia mradi wa Maziwa Faida kwa ufadhili wa Serikali ya Ireland katika Kampasi ya Buhuri Tanga; Mafunzo rejea kwa wakufunzi **28** na watafiti sita (**6**) juu ya mbinu sahihi za utoaji wa mafunzo ya muda mfupi na huduma za ushauri kwa wafugaji na wadau wengine katika Kampasi ya LITA Buhuri; na Mafunzo ya afya na uzalishaji wa Mifugo kwa wahudumu wa mifugo jamii (WAMIJA) **21** katika kampasi ya LITA Tengeru. Aidha, kaya za wafugaji **2,719** zimefikiwa na kupewa huduma za ushauri na wanafunzi wa Kampasi zote za LITA kupitia somo la *outreach* na mafunzo kwa vitendo uwandani.

## D. SEKTA YA UVUVI

### Hali Halisi ya Sekta ya Uvuvi

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi imeendelea kuwa miongoni mwa Sekta muhimu za kiuchumi

nchini zinazochangia katika Pato la Taifa. Sekta ya Uvuvi inajumuisha shughuli za uvuvi katika maji ya asili, ukuzaji viumbe maji na uhifadhi wa bahari na maeneo tengefu. Katika mwaka 2022, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa asilimia **1.9** na ilichangia asilimia **1.8** katika Pato la Taifa. Aidha, Sekta inatoa ajira kwa watanzania zaidi ya milioni **6.0** pamoja na ajira za moja kwa moja kwa wavuvi **198,475** na wakuzaji viumbe maji **35,986.** Uzalishaji uliofanywa na waajiriwa hawa umewezesha familia kupata kipato pamoja na kuongeza usalama wa chakula na lishe ambapo Sekta huchangia asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama. Pia, inakadiriwa kwamba, kwa wastani, kila mtanzania anakula kiasi cha kilo **7.9** kwa mtu kwa mwaka.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, Sekta ya Uvuvi imezalisha jumla ya **tani 472,579.34** za mazao ya uvuvi. Kati ya hizo, tani **429,168.39** zilivunwa kwenye maji ya asili na tani **43,410.95** ni kutoka ukuzaji viumbe maji. Kufuatia uzalishaji huo, jumla ya tani **41,271.07** za mazao ya uvuvi na samaki hai **134,572** wa mapambo ziliuzwa nje ya nchi. Aidha, katika kipindi hiki jumla ya tani **12.90** za samaki na bidhaa za uvuvi zimeingizwa nchini. Vilevile, Sekta inahifadhi rasilimali za uvuvi na kuendeleza utalii wa fukwe kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) kinachosimamia hifadhi tatu (**3**) za bahari na maeneo tengefu **15.**

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imefanikiwa kuendeleza miundombinu ya uvuvi ikiwemo ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko (Lindi); ujenzi wa masoko saba (7) ya mazao ya uvuvi; mialo mitatu (3) ya kupokelea samaki; kukamilisha ujenzi wa vituo vinne (4) vya ukuzaji viumbe maji; kukamilisha ujenzi wa ofisi za vituo vitatu (**3**) vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi; kufanya upembuzi yakinifu wa vituo vinne (**4**) vya ukuzaji viumbe maji; kukamilisha ujenzi wa kituo cha kusambaza teknolojia za uvuvi na ukuzaji viumbe maji; na kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa soko la samaki Kigamboni. Aidha, miundombinu hii itaimarishwa kwa kujenga mitambo ya kuhifadhia mazao ya uvuvi kama vile vyumba vya ubaridi na mitambo ya kuzalisha barafu. Vilevile, Serikali imeendelea na ujenzi wa mashamba darasa katika Halmashauri sita (6) nchini.

## F. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 – SEKTA YA UVUVI

### Bajeti iliyoidhinishwa kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo - Sekta ya Uvuvi

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya **Shilingi 183,874,156,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 49,462,296,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 134,411,860,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2024, jumla ya **Shilingi 103,173,799,111.45** zimetolewa, sawa na asilimia **56.1** ya fedha zilizotengwa.

### Matumizi ya Kawaida

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu 64 lilitengewa jumla ya **Shilingi 49,462,296,000** ambapo, **Shilingi 15,368,951,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na **Shilingi 34,093,345,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi Aprili, 2024, jumla ya **Shilingi 21,965,932,353.90** zimetolewa, sawa na asilimia **44.4** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 11,207,887,242.90** ni fedha za mishahara ya watumishi (PE) na **Shilingi 10,758,045,111.00** ni fedha za matumizi mengineyo.


### Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo

**95.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa kiasi cha **Shilingi 134,411,860,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo **Shilingi 110,682,025,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 23,729,835,000** ni fedha za nje. Hadi Aprili, 2024, jumla ya Shilingi **81,207,866,757.55,** sawa na asilimia **60.4** kutoka vyanzo vya ndani na nje, zimetumika.

**Makusanyo ya Maduhuli ya Sekta ya Uvuvi**

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi **41,000,000,000,** kupitia Fungu 64. Hadi kufikia Aprili, 2024, Shilingi **24,667,345,822.65**, sawa na asilimia **60.16,** ya lengo la mwaka zilikusanywa kupitia Sekta ya Uvuvi, ambayo pia ni sawa na asilimia **80.2** ya lengo la kukusanya Shilingi **30,750,000,000** hadi Aprili, 2024 (**Kiambatisho Na. 18**). Aidha, miongoni mwa sababu za kutofikia lengo ni pamoja na kupungua kwa malighafi kwenye viwanda vya kuchakata samaki kutokana na kuimarika kwa biashara ya samaki katika soko la ndani.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, fedha hizi zimekusanywa kutoka vyanzo vifuatavyo: leseni za kusafirisha samaki na mazao yake nje ya nchi (Export Licences); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi ndani ya nchi (Import Licences); mrabaha wa kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi (Export Royalty); mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (Import Royalty); leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu; tozo ya maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti; kibali cha kusafirisha mazao ya uvuvi ndani ya nchi (movement permit); mauzo ya vifaranga vya samaki; na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria za uvuvi (**Kielelezo Na. 3)**.




**Kielelezo NA. 3:** ***Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Hadi Aprili, 2024***

***Sekta ya Uvuvi*** **Vipaumbele vya Sekta ya Uvuvi (Fungu 64) kwa Mwaka 2023/2024**

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi, Fungu 64 imetekeleza maeneo saba (**7**) ya kipaumbele ambayo utekelezaji wake umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III 2021/2022 – 2025/2026); Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; na Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi 2021/2022 – 2036/2037. Aidha, utekelezaji umezingatia Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Uvuvi ili kuifungamanisha Sekta na dhana ya Uchumi wa Buluu, hususan matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi ikiwemo uvuvi kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Utekelezaji wa vipaumbele hivi umewezesha Sekta kupata mafanikio na matokeo ambayo yameelezwa katika hotuba yangu.  Aidha, vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Uvuvi;

(ii) Kuimarisha taasisi za uvuvi ili kuongeza ushiriki katika Uchumi wa Buluu;

(iii) Kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu;

(iv) Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi;

(v) Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji;

(vi) Kuimarisha uthibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi na masoko; na

(vii) Kuimarisha huduma za ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

**Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta ya Uvuvi**

**99.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 kupitia sheria na kanuni mbalimbali za Sekta ya Uvuvi. Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura Na. 388 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura 280, ambazo ziliwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kupitishwa na Kamati ya Baraza la Mawaziri. Pia, Wizara imeandaa rasimu ya Kanuni za Ukuzaji Viumbe Maji ambayo imepitiwa na wadau mbalimbali na tayari rasimu hiyo imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki na kupata maoni yake. Vilevile, Wizara inaendelea na mapitio ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009.


**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi Wizara imekamilisha andiko la kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji ambayo itakuwa na jukumu la kuendeleza, kusimamia, kudhibiti na kuhifadhi rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji. Hatua hii inalenga kuondoa shughuli za operesheni na usimamizi wa kila siku wa rasilimali za uvuvi ili Wizara ifanye kazi za kusimamia na kuratibu uteklezaji wa Sera ya Uvuvi.

**Uzalishaji, Usimamizi na Biashara ya Mazao ya Uvuvi na Viumbe Maji**

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa lengo la kuwezesha wadau kufanya uzalishaji na biashara ya mazao ya uvuvi kwa ufanisi ili kuchangia Pato la Taifa, lishe, usalama wa chakula na ajira. Katika kuendela kusimamia jukumu hili, katika mwaka 2023/2024, Wizara imetekeleza afua mbalimbali kama ifuatavyo:-

**Uzalishaji wa Samaki katika Maji ya Asili na Biashara ya Mazao ya Uvuvi**

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya tani **472,579.34** za samaki, zenye thamani ya Shilingi **trilion**i **2.94,** zilivunwa ikilinganishwa na tani **426,555.46** za samaki, zenye thamani ya Shilingi **trilioni 2.86,** zilizokuwa zimevunwa katika kipindi kama hiki, mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo (asilimia **0.61**) lilichangiwa na kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi (idadi ya wavuvi, aina na idadi ya vyombo vya uvuvi). Aidha, kati ya tani **429,168.39** zilizovunwa kwenye maji ya asili, tani **265,412.19,** sawa na asilimia **61.8** zilivunwa kutoka Ziwa Victoria; tani **78,130.12** (**18.2%)** kutoka Ziwa Tanganyika; **57,590.12** (**13.4%)** Ukanda wa Bahari ya Hindi; tani **10,340.88** (**2.4%)** Ziwa Nyasa; na tani **5,619.78** (**1.3%**) kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu. Vilevile, tani **5,274.54** (**1.2%)** na tani **5,081.74** (**1.2%**) zilivunwa kutoka Bwawa la Mtera na Ziwa Rukwa, mtawalia. (**Kielelezo Na. 4**).




***Kielelezo Na. 4: Uzalishaji wa samaki (%) katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 kwenye Maji ya Asili (Wizara ya Mifugo na Uvuvi)***

**103.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea kuimarisha ukusanyaji, uchakataji na usimamizi wa taarifa na takwimu za uvuvi kwa lengo la kuratibu shughuli za usimamizi wa rasilimali za uvuvi nchini. Katika kipindi hicho, wavuvi **198,475** na vyombo vya uvuvi **58,820** vilitumika katika shughuli za uvuvi ikilinganishwa na wavuvi **197,763** na vyombo vya uvuvi **58,448** kwa mwaka 2022/2023 (**Kiambatisho Na.19**).

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha biashara ya mazao ya uvuvi katika soko la nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya tani **41,271.07** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **134,572,** wenye thamani ya Shilingi **bilioni 515.78,** waliuzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrabaha wa Shilingi **bilioni 14.44,** ikilinganishwa na tani **29,466.98** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **150,308,** wenye thamani ya Shilingi **bilioni 453.80,** waliouzwa nje ya nchi na kuingizia Taifa mrabaha wa Shilingi **bilioni 12.56** katika

mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia **40.05** la mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi (**Kiambatisho Na.20**)

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya tani **12.90** za samaki, zenye thamani ya Shilingi milioni **252.41** zimeingizwa nchini na kuliingizia Taifa mrabaha wa Shilingi milioni **54.15** ikilinganishwa na tani **6.92** za samaki, zenye thamani ya Shilingi **milioni 224.03,** zilizoingizwa nchini na kuliingizia Taifa mrabaha wa Shilingi milioni **38.94** katika mwaka 2022/2023 (**Kiambatisho Na. 21**).

**Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi**

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Bahari ya Hindi, mabwawa ya Nyumba ya Mungu na Mtera ambapo siku kazi **2,912** za doria, sawa na asilimia **37.3** ya lengo la mwaka la kufanya doria siku kazi **8,400**, zilifanyika. Matokeo ya doria ilikuwa kukamatwa kwa zana haramu za uvuvi kama ifuatavyo; makokoro **326,** nyavu za makila **418** zenye macho chini ya inchi **6**, nyavu **1,609** za timba, mita **202,060** za kamba za kokoro, *ring net* **12** zenye macho chini ya mm **8**, vyandarua **16**, samaki wachanga kilo 6,477, mitumbwi **241**, injini za kupachika **66**, kasia **53** na watuhumiwa **830** ambapo hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa dhidi yao.

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti uvuvi kwenye mazalia ya samaki, matumizi ya zana na mbinu haramu za uvuvi ikiwemo nyavu haramu, vilipuzi (blast fishing), pamoja na kudhibiti uvuvi wa samaki wachanga. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanikiwa kwa kudhibiti uvuvi wa haramu wa kutumia vilipuzi (blast fishing) katika ukanda wa pwani ya bahari yetu.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara katika kutekeleza Mkataba wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika Charter) imetoa elimu kwa wadau

wa uvuvi **6,898** kuhusu upumzishwaji wa shughuli za uvuvi katika ziwa kwa kipindi cha miezi mitatu (3) kuanzia tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti, 2024. Utekelezaji wa mkataba huu unalenga kuruhusu samaki kuzaliana, kuimarika kwa bioanuai na kuongeza uzalishaji wa samaki ili kuwa na uvuvi wenye tija na endelevu. Aidha, jumla ya vizimba 29 vya kufugia samaki vimekopeshwa kwa wavuvi bila riba kama shughuli mbadala wakati wa kupumzisha ziwa.

**109. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali ya World Wild Life Fund for Nature (WWF) na Mwambao Coastal Community Network (MCCN) imeandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mwamba Darasa la Uvuvi wa Pweza – Tanzania. Mwongozo huo unalenga kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali na kuongeza ubora na thamani ya pweza nchini.

**110. *Mheshimiwa Spika***, Wizara katika kuongeza ubora na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi imekarabati soko la samaki Moa - Mkinga pamoja na kusanikisha mitambo mitatu (**3**) ya kuzalisha barafu yenye uwezo wa kuzalisha kilo **150** kwa siku. Aidha, vikundi vya wanawake wanaofanya biashara ya mazao ya uvuvi vimepatiwa majokofu nane (**8)** yanayotumia nishati ya jua (uwezo wa lita **150** kila moja) katika vijiji vya Moa (**4**), Jasini (**2**) na Ndumbani (**2**). Pia, imejenga vichanja vitano (**5**) katika Kijiji cha Moa (**2**) na Jasini (**3**) vyenye uwezo wa kuanika takribani tani **1.8** za dagaa kwa mara moja. Ukarabati wa soko na ujenzi wa chanja ulifadhiliwa na Shirika la *Wildlife Conservation Society* (WCS-Tanzania).

**111. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya *The Nature Conservancy*-TNC imetoa mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi, ukusanyaji takwimu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa eCAS, usimamizi wa rasilimali za uvuvi, utatuzi wa migogoro, uongozi na usimamizi wa fedha kwa wanachama **1,328** wa vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) katika Wilaya za Nkasi, Uvinza na Tanganyika.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Kilimo na Chakula la U*moja wa Mataifa (FAO) imewezesha BMU nane (8) za Halmashauri ya Mkinga kuandaa mipango ya usimamizi wa mavuvi ya *pweza*, samaki wa tabaka la juu, na samaki wa mwambani kwa kuzingatia dhana ya ikolojia na mazingira kwa lengo la kuimarisha **usima**mizi wa mavuvi ya kipaumbele. Pia, BMU **21** za Wilaya ya ***Mkinga zimepewa m***afunzo kuhusu sheria na kanuni za uvuvi, usimamizi wa rasilimali za uvuvi, athari za uvuvi haramu pamoja na kuwezeshwa vifaa vya doria na ukusanyaji takwimu za uvuvi kwa njia ya kielektroniki.

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la WCS imejenga uwezo kwa kutoa vifaa vya doria ikiwemo makoti ya mvua **42**, makoti okozi **46**, kamera tatu (**3**), darubini nne (**4**) na vifaa vya huduma ya kwanza pamoja na simu janja sita (**6**) kwa BMUs za Jasini, Ndumbani na Moa katika Wilaya ya Mkinga ili viweze kusimamia rasilimali za uvuvi na kupambana na uvuvi haramu katika maeneo yao. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mwambao Coastal Network Tanzania imetoa boti tatu (**3**) za kisasa za doria na vifaa vya uokozi kwa Kamati za Usimamizi wa Eneo la Pamoja la Uvuvi (CFMAs) ya BOMAMAHANDAKI (Mkinga - **2**) na PAMBWEBO (Pangani - 1) Mkoani Tanga.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imevijengea uwezo vikundi **31** vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi (Beach Management Units - BMUs) vya Wilaya za Mkuranga (**11**), Kilwa (Kusini **10**), Lindi Manispaa (**6**) na Mtama (**4**) kwa kuvipatia mafunzo ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi, ujasiriamali, ukusanyaji wa takwimu za uvuvi, kufunga miamba kwa muda kwa ajili ya mavuvi ya pweza, doria, sheria na kanuni za uvuvi. Pia, maeneo sita (**6**) ya Usimamizi wa pamoja yameanzishwa katika Wilaya za Lindi (**3**) na Kilwa (**3**) ili kuimarisha usimamizi wa uvuvi. Pia, wanawake **200** wamehamasishwa kuanzisha vikundi vya akina mama vya usimamizi wa mazingira na rasilimali za uvuvi ili kuongeza ushiriki wa wanawake na ufanisi wa usimamizi ambapo vikundi nane (**8**) vyenye wanachama **200** vimeanzishwa katika Halmashauri za Wilaya ya Pangani na Mafia. Mafunzo hayo yalitolewa kwa ufadhili wa Shirika la *Seasense*.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilisaini Mkataba wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika Charter) tarehe 16/12/2021 unaohusisha nchi nne zinazozunguka Ziwa Tanganyika za Burundi, D.R Congo, Tanzania na Zambia. Mkataba huo, pamoja na masuala mengine, unahusisha kupumzisha shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa kipindi cha miezi mitatu (3) kuanzia tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti kila mwaka. Lengo la kupumzisha ziwa ni kuruhusu samaki kuzaliana, kuimarika kwa bioanuai na kuongeza uzalishaji wa samaki. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza Mkataba huo ambapo hadi sasa imetoa elimu kwa wadau wa uvuvi 6,898 kuhusu umuhimu wa upumzishwaji wa shughuli za uvuvi katika ziwa. Aidha, jumla ya vizimba 29 vya kufugia samaki vimekopeshwa bila riba kwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika kama shughuli mbadala wakati wa kupumzisha ziwa.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa samaki na bidhaa za uvuvi kwenye mipaka, maeneo ya viwanja vya ndege, na masoko ya samaki nchini kote. Aidha, kaguzi za kawaida **9,201** zilifanyika katika viwanda **21** vya kuchakata samaki; vituo **37** vya kuhifadhia samaki hai wa mapambo; mialo **33** ya kupokelea samaki**;** masoko **3**; maghala **70** ya kuhifadhia mazao yaliyokaushwa; vituo **17** vya kugandisha samaki; viwanda **17** vya mabondo; meli nne (**4**) za uvuvi; na vyombo **1,470** vya kusafirisha mazao ya uvuvi.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, kaguzi za kina **114** zimefanyika kwenye viwanda, maghala ya kuhifadhia samaki, vituo vya kugandisha samaki, magari ya kusafirisha samaki, mialo ya kupokelea samaki pamoja na masoko. Vilevile, kaguzi **5,891** za uhakiki wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi zilifanyika na vyeti vya afya kutolewa kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imewezesha ujenzi wa vichanja **14** vya kuanikia dagaa kwa vijiji vya Kalungu nne (**4**), Manda Uhuru tano (**5**) na Manda Kerenge tano (**5**) katika Wilaya ya Nkasi kwa lengo la kuongeza ubora na kupunguza upotevu wa mazao

ya uvuvi. Chanja hizo zina urefu wa mita **20** na upana wa mita mbili (**2**) na zina uwezo wa kuanika wastani kilo **120** za dagaa kila moja. Ujenzi wa miundombinu hiyo ulifadhiliwa na Shirika la *The Nature Conservancy* (TNC). Pia, Wizara imewezesha kikundi cha wanawake wanaochakata mazao ya uvuvi wilayani Muleba kwa kujenga vichanja vinne (**4**) vya kukaushia dagaa kwa ufadhili wa Shirika la EMEDO.

**Maabara ya Taifa ya Uvuvi**

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi imeendelea kufanya uchunguzi wa sampuli **1,982** za samaki kutoka kwenye mialo, maghala ya kuhifadhia samaki, vituo vya kugandishia samaki, na masoko ya mazao ya uvuvi, mazingira, na sampuli za maji ili kubaini uwepo wa vimelea na kemikali hatarishi kwa afya ya walaji na kikidhi matakwa ya masoko ya kitaifa na kimataifa. Matokeo ya uchunguzi yanaonesha samaki wanaozalishwa nchini na kutoka nje ya nchi wako salama kwa afya ya walaji. Aidha, matokeo hayo yamechangia nchi kuuza tani **41,271.07** za samaki na mazao ya uvuvi katika masoko ya kimataifa zenye thamani ya Dola za Marekani **206,597,922.24**. Aidha, Maabara ilifanyiwa ukaguzi na Bodi ya ithibati ya SADC (*SADC Accreditation Service* - SADCAS) na kupewa ithibati ya ISO/IEC 17025:2017, na kuendelea kukidhi viwango vya ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi katika masoko ya kitaifa na kimataifa.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika ukuzaji viumbe maji. Hadi kufikia Aprili, 2024, uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe maji umefikia tani **43,415.95** kutoka tani **33,525.46** za mwaka 2022/2023. Uzalishaji huu unajumuisha tani **34,828.5** za samaki, tani **8,550.75** za mwani mkavu, tani **30** za kambakoche, tani **5.20** za kambamiti, tani **2.5** za kaa, tani **1.5** za majongoo bahari na vipande **250** vya lulu. Vilevile, idadi ya miundombinu ya uzalishaji wa viumbe maji imeongezeka hadi kufikia mabwawa **34,417**, vizimba **1,215** na vitotoleshi vya kuzalisha vifaranga **41**

ikilinganishwa na mabwawa **32,878**, vizimba **993** na vitotoleshi **39** mtawalia kwa mwaka 2022/2023.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, uzalishaji wa vifaranga vya samaki umefikia **66,684,806** ikilinganishwa na vifaranga **35,967,180** vilivyozalishwa mwaka 2022/2023 **(Kiambatisho Na. 22).** Aidha, matumizi ya chakula cha samaki nchini yameongezeka kutoka tani **4,337.9**, mwaka 2022/2023 hadi tani **7,911.4**, zinazojumuisha tani **3,455.4** zilizozalishwa nchini na tani **4,456.0** zilizoagizwa kutoka nje ya nchi (**Kiambatisho Na.23**).

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika ukuzaji viumbe maji kwa kuainisha maeneo **98** yenye ukubwa mita za mraba milioni **220** ambayo yanafaa kwa ufugaji samaki kwa vizimba na kuyafanyia tathmini ya kimkakati ya mazingira katika mikoa mitano **(5)** inayozunguka Ziwa Victoria. Lengo ni kupunguza gharama za uwekezaji kwa wananchi na kuhakikisha kuwa shughuli za ufugaji samaki kwa vizimba zinafanyika bila kuathiri mazingira na kuepusha migogoro.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa vibali kwa ajili ya shughuli mbalimbali za ukuzaji viumbe maji. Hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara imetoa vibali **44** vya kuingiza chakula kutoka nje ya nchi kwa Kampuni **15** na kuwezesha kampuni hizo kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)* na ushuru wa forodha. Vile vile, Wizara imetoa vibali vya kusafirisha samaki wazazi (*YY – tilapia broodstock*) **1,430** kwenda nje ya nchi. Aidha, Wizara imetoa vibali vya ufugaji jongoo bahari kwa vikundi **55** (Mtwara **17**, Lindi **19**, Pwani **9** na Tanga **10**) na Sekta Binafsi **15** (Mtwara **12** na Mafia **3**) ili kuwawezesha kunufaika na fursa za Uchumi wa Buluu (**Kiambatisho Na.24**).

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kuwa shughuli za ukuzaji viumbe maji zinatekelezwa kwa kuzingatia sheria na kanuni bora, Wizara imefanya ukaguzi wa vizimba **610**, mabwawa **215**, matanki **12,** vitotoleshi sita **(6)** na viwanda vya chakula cha samaki viwili **(2)** katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Morogoro na Simiyu.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili 2024, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imetoa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, uhifadhi na uongezaji thamani zao wa mwani kwa wakulima **2,615** (Tanga - **669**, Lindi - **746**, Mtwara – **652**, Pwani - **427** na Dar es salaam - **121**). Vile vile, jumla ya wakulima wa mwani **520** kutoka katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara walipatiwa vifaa vya usalama kazini vinavyojumusha kofia (**520**), viatu (**219**) na buti (**301**) na nyundo (**90**) zenye thamani ya Shilingi milioni **45**.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2024, katika kuongeza upatikanaji wa samaki na kuboresha lishe kwa wananchi wanaoshi mbali na maeneo ya mavuvi, Wizara imepandikiza vifaranga **465,000** vya samaki katika mabwawa ya asili yaliyopo Kilosa - Bwawa la Iyovi-Kidatu (**10,000**); Mvomero - Bwawa la mradi wa *Ecosystem Based Adaption for Rural Resilience - EBARR* (**10,000**); Ifakara - Lambo la Chagugu (**4,000**), bwawa la Kisawasawa (**2,000**) na bwawa la kikundi cha Usamaria (**2,000**), Mufindi - Bwawa la Ngwazi (**224,000**), Rungwe – Bwawa la Ndwati (**164,000**), Mbinga (**20,000**) na Wanging'ombe – Bwawa la Sakalenga (**33,600**).

**Huduma za Ugani wa Uvuvi**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutambua na kuhamasisha jamii kujiunga na vikundi ambapo vikundi **457** vya wakulima wa mwani, wafugaji wa majongoo bahari na wanenepeshaji wa kaa, vyenye jumla ya wanachama **8,665** vimetambuliwa. Hatua hii itarahisisha utoaji wa huduma za Ugani nchini kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji. Aidha, mafunzo rejea yametolewa kwa Maafisa Ugani **161** kutoka Halmashauri za Pangani, Bagamoyo, Muheza, Tanga Jiji, Kigamboni na Mkuranga. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi wa programu ya BBT, usimamizi wa rasilimali za uvuvi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ugani (M-Kilimo na Ugani Kiganjani). Aidha, mpaka sasa jumla ya maswali **3,515** yanayohusu uvuvi na ukuzaji viumbe maji yamepokelewa na kujibiwa kupitia mfumo wa M–Kilimo.

**128. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wadau wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji nchini ambapo jumla ya wadau **6,493** kutoka katika mikoa ya Geita, Mwanza, Kagera, Mara, Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani na Simiyu wamepatiwa mafunzo. Mafunzo hayo yalihusu; fursa zilizopo kwenye Sekta ya Uvuvi **(1,856),** Utunzaji wa mazingira ya shughuli za uvuvi **(1,497),** Sheria, Kanuni na Miongozo ya uvuvi **(1,473)** na njia bora za uhifadhi na uchakataji wa mazao ya uvuvi **(1,667).** Aidha, wadau **80,617** walipatiwa elimu na maelezo mbalimbali juu ya shughuli za Sekta za Mifugo na Uvuvi pamoja na teknolojia mbalimbali za Mifugo na Uvuvi kupitia maonesho ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, wadau **38,578** wamepatiwa elimu katika maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba), wadau **1,115** katika maonesho ya siku ya chakula duniani na siku ya Mvuvi (Mvuvi day) na wadau **41,739** katika maonesho ya Nane nane.

**TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UVUVI**

**129. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara katika Sekta ya Uvuvi imeendelea kutekeleza majukumu yake kupitia Taasisi zake tano (5) ambazo ni Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (**TAFIRI**), Wakala ya Mafunzo ya Uvuvi (**FETA**), Shirika la Uvuvi Tanzania (**TAFICO**), Kitengo cha Hifadhi ya Maeneo Tengefu (**MPRU**) Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (**DSFA**). Taasisi hizi zimewezesha upatikanaji wa huduma kwa wadau wa Sekta ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa teknolojia na utatuzi wa changamoto katika mnyororo wa thamani wa mazao ya uvuvi. Aidha, baadhi ya kazi na majukumu yaliyotekelezwa na Taasisi hizo yamebainishwa hapa chini:-

**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania - TAFIRI**

**Utafiti Bahari ya Hindi**

**130. *Mheshimiwa* Spika**, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia TAFIRI ilifanya utafiti wa ikolojia ya Bahari ya Hindi kwenye maji ya Tanzania kwa kutumia meli ya kisasa ya R/V Dr Fridtjof Nansen kutoka nchini Norway. Jumla ya aina **836** za samaki zilipatikana

ikiwa ni pamoja na aina mpya **20** za samaki zilitambuliwa. Aidha, utafiti huu umebaini uwepo wa tani **46,481** za samaki wa tabaka la chini na tani **12,517** za samaki wa tabaka la juu, aina ya dagaa na kibua, katika eneo la Bahari lenye kina kuanzia mita **20** mpaka **1,000.**

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024 TAFIRI imefanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa dagaa na kibua katika maji ya ndani ya eneo la Bahari ya Hindi katika maji yenye kina cha mita **5** mpaka **50** ambapo matokeo yanaonesha kuwepo kwa jumla ya tani **113,287** za samaki wa tabaka la juu aina ya dagaa na kibua.

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TAFIRI imekamilisha kutengeneza programu tumizi na lango la ujumbe wa simu inayowezesha wavuvi wa ukanda wa Pwani kupokea taarifa za maeneo ya uvuvi yenye samaki wengi kupitia simu zao za mkononi ili kuongeza tija na kupunguza gharama. Sambamba na hilo, Wizara inakamilisha uwekaji wa vivutia samaki (FADs) 10 katika maeneo ya Pwani ili kuwawezesha wavuvi wadogo kuongeza mavuno na kipato.

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TAFIRI imekamilisha utafiti wa kutambua uharibifu na upotevu wa mazao ya uvuvi, hasa dagaa wa baharini, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria na kugundua kuwa kuna upotevu wa asilimia **40** kuanzia kwenye hatua ya kuvua, kusafirisha, kutunza na hata kwenye mauzo. Kutokana na utafiti huu, Wizara imeandaa Mpango Mkakati (Multidimensional Solutions Strategy for the Reduction of Food Loss and Waste in the Dagaa Fisheries in the United Republic of Tanzania) unaolenga kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi hadi kufikia asilimia **24** ifikapo mwaka 2030.

**Utafiti Ziwa Tanganyika**

**134.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI imekamilisha utafiti wa wingi na mtawanyo wa samaki katika Ziwa Tanganyika. Matokeo ya awamu yameonesha kuna tani **144,690** za samaki wa tabaka la juu katika eneo la kilomita za mraba **13,495** lililofanyiwa utafiti.

Aidha, matokeo yameonesha kuwa wingi wa samaki (biomass) umepungua kwa asilimia **8** ikilinganishwa na makadirio ya wingi wa tani **157,493** za samaki mwaka **1995**. Utafiti pia umeonesha kuwa eneo la kaskazini (Kigoma) kuna kiwango kidogo cha samaki (tani **30,966**) ikilinganishwa na tani **60,796** eneo la kati (Buhingu mpaka Kalya), na **52,928** kwa eneo la kusini mwa ziwa. Matokeo ya utafiti yatawezesha Wizara kuweka mikakati madhubuti ya kufikia lengo la kuongeza wingi na uzalishaji wa samaki.

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI imekamilisha utafiti wa matumizi ya nyavu aina ya makila ya freemaya zinazotumika kuvua samaki aina ya migebuka Ziwa Tanganyika. Matokeo yameonesha kuwa nyavu hizo zinavua samaki wadogo chini ya kiwango kinachokubaliwa kisheria na kuwa samaki hao wanaharibika upesi, hivyo kuongeza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutoa elimu kwa wavuvi kuhusu athari za kutumia nyavu hizo.

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI pia, imekamilisha utafiti wa kutathmini bioanuwai ya samaki katika vijiji **19** vya Wilaya ya Nkasi ambapo kwa kushirikiana na wananchi maeneo ya mazalia ya samaki yalitambuliwa katika maeneo ya vijiji hivyo. Utafiti huu umewezesha kutambuliwa kwa maeneo yenye bioanuwai kubwa kama vile Korongwe, Ninde na Kisiwa cha Mandakerenge kilichopo eneo la Kipili. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau, likiwemo Shirika la The Nature Conservancy, inalenga kuhifadhi maeneo hayo ili kuchochea uvuvi endelevu, kuongeza uzalishaji wa samaki, usalama wa chakula na kipato kwa wavuvi.

**Tafiti za Ukuzaji Viumbe Maji**

**137.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia TAFIRI ilitekeleza programu ya tathmini ya Kimkakati ya Mazingira kwa ajili ya kuainisha maeneo yanayofaa kufanya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Victoria. Katika awamu ya kwanza, maeneo **39** katika mikoa ya Kagera na Mwanza yamefanyiwa tathmini kuchunguza kama yanafaa kwa ufugaji wa samaki ambapo maeneo **36,** kati ya hayo, yalionekana

yanafaa kwa ufugaji kwa njia ya vizimba. Aidha, tathmini ya maeneo mengine **81** katika mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Geita na Kagera imefanyika na uthibitishwaji wa maeneo haya upo katika hatua za mwisho.

**138.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia TAFIRI imefanya utafiti wa ufuatiliaji wa aina za samaki wanaofugwa wenye tija katika mabwawa na vitotoleshi kwa kutumia teknolojia ya vinasabamazingira (eDNA) kwa nia ya kuboresha ufugaji samaki nchini. Aidha, utafiti huu umewezesha kutambua aina ya samaki wa asili na samaki wa kigeni wanaofugwa kwenye maeneo mbalimbali ya Bonde la Ziwa Victoria. Wafugaji **60** walifundishwa namna ya kutambua aina ya samaki anayefaa kufugwa ili kuondokana na changamoto ya kufuga samaki wasiokua vizuri au waliodumaa. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia kuwekwa mikakati ya kuepukana na ufugaji samaki wenye vinasaba vilivyochafuliwa na hivyo kutokuwa na tija kwa mfugaji na kuondokana na tatizo la uchafuzi wa vinasaba vya aina nyingine ya samaki kwenye maji ya asili.

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI inaendelea na utafiti wa bioanuwai na mazingira katika Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kutambua maeneo yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika Bwala hilo. Utafiti huu unategemewa kuiwezesha Wizara na wananchi, katika eneo la Nyumba ya Mungu, kusimamia na kufanya uvuvi endelevu.

**Wakala ya Mafunzo ya Uvuvi – FETA**

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kufaidika na fursa za Uchumi wa Buluu na kuwa na wataalam wenye mtazamo wa kujiajiri katika Tasnia ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji, FETA imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi **1,116** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada yanayotilia mkazo umahiri kwa vitendo.

**141.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, FETA imewezesha mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uelewa na kukuza ujuzi kwa washiriki **4,035** katika maeneo ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kama ifuatavyo: mbinu bora za ufugaji wa samaki

wa kibiashara (**1,949**); ufugaji wa Majongoo Bahari (**293**); unenepeshaji wa Kaa (**123**); na kilimo cha mwani (**472**). Aidha, mafunzo yametolewa kuhusu mnyororo wa thamani na mazao yake (**551**); kupunguza uharibifu wa mazao ya uvuvi baada ya mavuno (**334**); ufundi stadi wa matengenezo ya majokofu na vipoza hewa (**95**); na mafunzo ya uendeshaji na usalama wa vyombo vidogo katika maziwa na bahari (**133**). Vilevile, FETA kupitia programu ya BBT inaendeleza ujuzi kwa vijana na wanawake **60** (Mbegani – **25** na Mikindani – **35**). Pia, wakufunzi **25** wamejengewa uwezo kuhusu masuala ya ujasiriamali, masoko, ubunifu na fedha.

**142. *Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha mafunzo yanayotolewa kuendana na uhitaji wa soko na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, na kutoa wahitimu wenye vipaji, ubunifu na utayari wa kujiajiri, katika mwaka 2023/2024, FETA imeendelea na maboresho ya kimkakati kama ifuatavyo: kupitia mitaala yake saba **(7)** ya mafunzo ya muda mrefu ili kuihuisha; kuandaa mitaala mipya **12** ya mafunzo ya muda mrefu; na kuandaa mitaala tisa **(9)** ya mafunzo ya muda mfupi.

**143. *Mheshimiwa Spika***, Utoaji mafunzo katika Kampasi ya FETA Kibirizi - Kigoma ulisimama kwa muda wa mwezi mmoja kutokana kina cha maji kuongezeka katika Ziwa Tanganyika na kusababisha madarasa, maabara, maktaba, na ofisi kujaa maji na kutoweza kutumika. Aidha, Wizara inaishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuipatia FETA madarasa ya Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima, yaliyopo katika Kata ya Buzebazeba, Kigoma na kuwezesha masomo kuendelea kuanzia tarehe 15 Aprili, 2024. Pia, FETA inaendelea kutafuta eneo lingine kwa ajili ya ujenzi na uwekezaji wa miundombinu ya kudumu ya kutolea mafunzo.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

**144. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2023/2024**,** Serikali imeendelea kuimarisha Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), ambapo kupitia ufadhili wa Programu ya Kuendeleza Uchumi na Jamii (*Economic and Social Development Programme - ESDP)* ya

Japan, mkataba wa ujenzi wa meli moja (**1**) ya uvuvi wa bahari kuu umesainiwa na ujenzi wa meli umeanza Mei, 2024 na unategemewa kukamilika ifikapo Disemba, 2025. Kukamilika kwa meli hii kutaiwezesha TAFICO kuanza uvuvi wa bahari kuu na kufungua fursa zaidi katika uchumi wa buluu. Vilevile, ukarabati wa miundombinu ya majengo umefikia asilimia **75.**

**145.** ***Mheshimiwa Spika*****,** TAFICO imenunua mtambo wa barafu za chenga wenye uwezo wa kuzalisha tani tano (**5**) kwa siku, jenereta; na gari moja (**1**) la ufutiliaji na usimamizi wa miradi. Vilevile, Shirika linaendelea na tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii kwa ajili ya ununuzi wa meli za uvuvi wa Bahari Kuu na ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi.

**Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA)**

**146.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) imeendelea kusimamia shughuli za uvuvi wa bahari kuu, ambapo hadi kufikia Aprili, 2024, DSFA imetoa leseni **67** za uvuvi wa bahari kuu ambapo meli moja **(1)** ya ndani na meli **66** za nje; na kutoa vibali vinne (**4**) vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania na leseni nne **(4)** za meli saidizi. Utoaji wa leseni hizo umewezesha makusanyo ya Shilingi bilioni **9.7** ikilinganishwa na Shilingi bilioni **6.8** zilizokusanywa kutokana na leseni **51** zilizotolewa mwaka 2022/2023 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni **2.9,** sawa na asilimia **42.6**. **(Kiambatisho Na. 25)**. Aidha, kuimarika kwa makusanyo hayo kulitokana na ongezeko la ukataji wa leseni za uvuvi wa bahari kuu na juhudi mahsusi zilizofanywa na Serikali ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo ya kimkakati na wamiliki wa meli na uwepo wa mazingira rafiki ya uwekezaji.

**147.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvuliwa na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi kwa wavuvi wadogo, Wizara kwa kushirikiana na ALBACORA Group imenunua na kusanikisha mtambo wa kuzalisha barafu katika soko la samaki la Malindi – Unguja wenye uwezo wa kuzalisha tani tano (**5**) za barafu kwa siku. Pia, taratibu za kusanikisha mtambo wa pili Dar es Salaam zinaendelea. Vilevile,

ALBACORA Group imefanikiwa kushusha jumla ya tani **125** za samaki wasiolengwa (*bycatch*) na imewezesha mafunzo ya vitendo na ajira kwa mabaharia sita (**6**) wa Kitanzania (Tanzania Bara - **3** na Zanzibar - **3**).

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uvuvi wa bahari kuu na makubaliano ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za uvuvi kwenye bahari kuu, Mamlaka imeendelea kutumia mifumo ya ufuatiliaji wa mienendo ya meli (Vessel Monitoring System - VMS na Automatic Identification System – AIS) na kuweka Waangalizi wa Uvuvi (Fishery Observers). Vilevile, Mamlaka ilifanya ukaguzi katika meli **75** za uvuvi kati ya hizo meli **67** zilichukua leseni na meli saidizi nane (**8**) zilipewa vibali. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na nchi jirani na Nchi Wanachama wa Kamisheni ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Commission - IOC) imefanya doria ya kwenye maji kwa kutumia meli na ndege zisizo na rubani (Drones).

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) iliendelea kutekeleza jukumu la ulinzi na usimamizi wa rasilimali za bahari katika maeneo ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu ikiwa ni pamoja na kuainisha maeneo mapya ya hifadhi za bahari katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Mkoani Lindi. Aidha, MPRU imezindua kamati ya kitaifa ya kuhifadhi matumbawe na Mpango wa Kitaifa wa Kuhifadhi Kasa kwa kushirikiana na Shirika la Seasense. Pia, doria **420** za kwenye maji na nchi kavu zilifanyika ili kudhibiti uharibifu wa mifumo ya ikolojia ya rasilimali muhimu za bahari. Pia, MPRU imeshiriki katika mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabia Nchi **COP 28 Dubai** na kupokea mikakati mbalimbali ya uhifadhi wa bahari ili kuhakikisha rasilimali bahari zinasaidia kizazi cha sasa na kijacho. Pamoja na hilo utalii wa bahari katika hifadhi umeendelea kuimarika kupitia program za *Royal Tour* na kupelekea kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka **38,160** mwaka 2022/2023, hadi **40,088** 2023/2024. Pia, kwa mara ya kwanza, Hifadhi ya Mafia imepokea meli kubwa za watalii

(*Cruise Ship Tourism*) zikiwemo meli ya *The World* iliyoleta watalii **442**, *The cloud* **220**, na *Le bougainville* **200**. Utalii huo umeingizia MPRU mapato ya Shilingi **2,175,500,625** zilizowezesha uendeshaji wa shughuli za uhifadhi.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Uvuvi**

**Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Programu ya ASDP II**

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko unaotarajia kukamilika mwaka 2025, ambao hadi Aprili, 2024 ujenzi umefikia asilimia **53**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha uchimbaji wa kuongeza kina cha maji baharini; Utengenezaji wa *slab* **308**; ujenzi wa *beam* **272**; uchimbaji wa eneo ili kuondoa udongo usiofaa na kujaza udongo unaofaa kwa ajili ya ujenzi. Aidha, ujenzi wa nguzo **113** kati ya **160** umekamilika na ujenzi wa majengo ya utawala na uzio upo katika hatua ya msingi.

**151. Mheshimiwa *Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara inaendelea na ujenzi wa mialo mitatu (**3**) ya Chifunfu – Sengrema, Igombe – Ilemela, na KayenzeIlemela, Igabilo-Bukoba. Pia, Wizara imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Ruhila - Songea, Nyengedi - Lindi na Rubambagwe – Geita. Ujenzi wa awamu ya kwanza ya kituo cha Ruvula Mtwara umefikia asilimia 95.

**Mradi wa Mkopo wa Masharti Nafuu (Extended Credit Facility- ECF)**

**152.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2023/2024, Mhe. **Dkt.** Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua programu maalum ya kuwawezesha wavuvi na wakuzaji viumbe maji. Programu hiyo inatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani kupitia dirisha la ECF. Aidha, kupitia programu hiyo boti za kisasa za uvuvi **160** na vifaa vyake zimekopeshwa bila riba kwa wanufaika **3,295**

(**Kiambatisho Na.26**). Pia, awamu ya kwanza, vizimba **222** vya kufugia samaki na pembejeo zake zimetolewa kwa wanufaika **1,214.** Mikopo hiyo inatolewa kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) (**Kiambatisho Na. 27**).

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya masoko, mialo na uanzishaji wa mashamba darasa ya ukuzaji viumbe maji ili kuongeza uzalishaji, ubora, na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi. Aidha ujenzi wa soko la Kasanga – Kalambo umefikia asilimia **90**; soko la Zingibari –Mkinga asilimia **20.** na mwalo wa Chato beach asilimia **90**. Vilevile, uanzishaji wa mashamba darasa **10** ya ufugaji samaki katika Halmashauri za Njombe, Iringa, Songea, Ruangwa, Kongwa, Tandahimba, Rombo, Same, Moshi na Mkuranga upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora kwa Vijana na Wanawake**

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipokea maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu kuanzisha Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) inayolenga kuwajengea uwezo vijana na wanawake kujiajiri na kuajiri wengine. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imeendelea na utekelezaji wa Programu hiyo.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia maelekezo hayo, Sekta ya Mifugo, imeanzisha vituo nane (**8**) vya vijana na wanawake kwa lengo kuwajengea uwezo wa kuanzisha na kuendesha miradi ya ufugaji kibiashara. Aidha, mafunzo yametolewa kwa wanufaika **235** ambapo, kati ya hao, **74** wamepata ajira Serikalini na **161** wanaendelea na Programu.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Programu hiyo, jumla ya ng'ombe **3,388** wamenenepeshwa na kuuzwa kwa thamani ya Shilingi **1,970,604,200** na kupata faida ya Shilingi **199,572,612.25.** Aidha, vijana wanaendelea na utekelezaji wa programu hiyo hadi Juni, 2024 ambapo watakuwa tayari kwenda kuanza ufugaji wa

kibiashara kupitia vitalu vilivyoandaliwa na Wizara katika Ranchi za NARCO za Kitengule na Kagoma.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, ili kuongeza wigo wa ushirikishwaji wa vijana na wanawake, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri imeanzisha vituo vipya vya BBT katika mikoa mitano (5) ya Tabora, Arusha, Morogoro, Pwani na Mtwara**.**

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Programu hiyo inalenga kuongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa kuwapatia mafunzo kwa vitendo, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko. Jumla ya wanufaika **500** (vijana na wanawake) wamepatiwa mafunzo ambapo wanufaika **200** wamehitimu na **300** wanaendelea na mafunzo katika vituo **15** vilivyopo Ukanda wa Ziwa Victoria (**10),** Ukanda wa Pwani (**4**) na Zanzibar (**1**). (**Kiambatisho Na. 28**).

**Changamoto na Mikakati katika Sekta za Mifugo na Uvuvi**

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta za Mifugo na Uvuvi zimeendelea kukabiliwa na changamoto mabalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Mapungufu yaliyokuwa kwenye mfumo wa LGRCIS katika ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara katika minada ya awali.

(ii) Uwepo wa vipenyo vingi katika maeneo ya mipakani hali inayochangia utoroshaji wa mifugo kwenda nchi jirani.

(iii) Kuendelea kuwepo kwa magonjwa ya mifugo yanayoathiri biashara ya mifugo na mazao yake na kukosekana kwa mfumo rasmi wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo.

(iv) Ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi. Hali hii imesababisha kupungua kwa samaki katika bahari, maziwa na mito,

uharibifu wa mazalia ya samaki na uharibifu wa mazingira kwa ujumla;

(v) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa unaokadiriwa kufikia asilimia 30 - 40 hususan katika maeneo ya vijijini ambako miundombinu ya umeme na minyororo ya ubaridi ni hafifu;

(vi) Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa Bahari Kuu na usindikaji wa mazao ya uvuvi ambao unaathiri mchango wa sekta katika pato la Taifa;

(vii) Uhaba wa maafisa ugani wa mifugo na uvuvi ikilinganishwa na mahitaji ya wataalam hao katika Halmashauri; na

(viii) Uhaba wa vifaranga na vyakula vya samaki vyenye ubora;

**160. *Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Wizara kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI imeanza kutumia mfumo wa TAUSI badala ya mfumo wa LGRCIS kukusanya maduhuli kwenye minada ya awali kwa kutoa hati ya malipo jumuishi (split control number).

(ii) Kuimarisha vituo 47 vya ukaguzi vya mipakani na kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti utoroshwaji wa mifugo na mazao ya mifugo inayosafirishwa nje ya nchi bila kulipia vibali.

(iii) Kufanya kampeni ya kitaifa na zoezi la chanjo kwa magonjwa ya kipaumbele na utambuzi wa mifugo

(iv) Kuanzisha na Mamlaka ya Kusimamia Rasilimali za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji;

(v) Kushirikiana na OR-TAMISEMI na Sekta Binafsi kuimarisha na kujenga miundombinu muhimu ya uvuvi ikiwemo masoko na mialo;

(vi) Kukamilisha ujenzi wa bandari za uvuvi za Kilwa Masoko na Bagamoyo, pamoja na ununuzi wa meli za uvuvi wa Bahari Kuu;

(vii) Kuendelea kushirikiana na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma kutenga nafasi za ajira kwa maafisa ugani na kuandaa kanuni zikazoruhusu watoa huduma binafsi za ugani; na

(viii) Kuimarisha vituo vya ukuzaji viumbe maji na kuha na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika vitotoleshi ili kuongeza uzalishaji vifaranga.

## G. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025

### Vipaumbele vya Mpango na Bajeti

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Mpango na Bajeti ya Wizara utatekelezwa kupitia Fungu 99 (Mifugo na Uvuvi) baada ya kuunganishwa kwa fungu 64 (Sekta ya Uvuvi) na fungu 99 (Sekta ya Mifugo).

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mambo mengine maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/2025 yamezingatia falsafa ya 4R ya Mheshimiwa Rais inayosisitiza uwepo wa maridhiano (Reconciliation) uhimilivu (Resilience), mageuzi (Reforms) na kujenga (Rebuilding) katika kujenga uchumi jumuishi. Aidha, kwa upande wa **Maridhiano** tumejielekeza kutatua migogoro baina ya watumiaji wa rasilimali za mifugo na uvuvi kwa kuanzisha miradi ya uzalishaji wa malisho na kutenga ardhi ya nyanda za malisho. Vilevile, ili kuleta **Uhimilivu** Wizara itatekeleza miradi ya vizimba, kilimo cha mwani na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Pia, katika kuleta **Mageuzi** ya sekta za mifugo na uvuvi, wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeanzisha Mpango Mkuu wa Mageuzi ya sekta za Mifugo, Uvuvi na Kilimo Mazao (Agricultural

Transformation Masterplan - 2050). Aidha, katika **Kujenga Upya**, Wizara itaendelea kuimarisha uhifadhi na maeneo tengefu ya bahari.

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025 maeneo ya kipaumbele ya Mpango na Bajeti ya Wizara yatakayotekelezwa ni:- Kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi; Kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi; Kuhamasisha uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi; na Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika sekta za mifugo na uvuvi.

**Miradi na Shughuli Zitakazotekelezwa**

**Sekta ya Mifugo**

**164.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara itatekeleza miradi na shughuli zifuatazo:

(i) Kufanya kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo kwa kutoa chanjo kwa magojwa 13 ya kipaumbele;

(ii) Kukamilisha kuundwa kwa chombo maalum kitakacho simamia uendelezaji wa mazao na miundombinu ya Mifugo;

(iii) Kuanza kutekeleza Mradi wa Mageuzi katika Tasnia ya Maziwa na Mabadiliko ya Tabianchi (T-CSDTP) wa miaka mitano (**5)** wenye kunufaisha walengwa **58,000**. Mradi utahusisha kununua ng'ombe wa maziwa **17,200**; kujenga mabanda **5,000** ya ng'ombe; kujenga mfumo wa uvunaji maji ya mvua katika kaya **22,400**; kununua na kusanikisha mitambo **2,800** ya biogesi; kujenga vituo **950** vya kukusanya maziwa; kununua dozi **929,000** za chanjo za mifugo; na kujenga kilomita **140** za barabara

(iv) Kuanzisha kambi moja ya Mifugo (Livestock Guest house) katika Ranchi ya Mkata;

(v) Kununua na kusambaza madume **60** ya mbari bora za mifugo aina ya Brahman ili kuongeza uzalishaji na tija katika mnyororo wa thamani wa mifugo na mazao yake;

(vi) Kujenga kituo cha mafunzo ya wadau wa mnyororo wa thamani wa malisho aina ya mabingobingo (Juncao);

(vii) Kuboresha na kuendeleza hekta **20,000** za maeneo ya malisho katika eneo la Msomera, Kitwai na Saunyi;

(viii) Kukamilisha ujenzi wa mabwawa saba **(7)** na visima virefu vitatu **(3)**;

(ix) Kuwezesha uendeshaji wa mashamba ya kuzalisha malisho na mbegu za malisho;

(x) Kuwezesha FETA na LITA kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;

(xi) Kuziwezesha LITA na FETA kutekeleza Programu ya elimu na ujuzi wa kazi za uzalishaji (Education and Skills for Productive Jobs Program-for-Results - Phase II);

(xii) Kuwezesha mradi wa Maziwa Faida TALIRI Tanga na African Dairy Genetic Gain katika Mikoa saba (**7**) nchini;

(xiii) Kuiwezesha TALIRI na TAFIRI kufanya tafiti mbalimbali;

(xiv) Kukarabati miundombinu ya kituo cha karantini cha Kwala ili kuwezesha biashara za kimataifa; na

(xv) Kuzalisha chanjo za mifugo kupitia Wakala ya maabara ya Veterinari (TVLA).

**Sekta ya Uvuvi**

**165. *Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa nguzo muhimu za uzalishaji hapa nchini. Kwa sasa usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwenye bahari na maziwa hususan maji ya ndani (Inner

Seas) na maji ya kitaifa (Territorial Waters) unategemea zaidi mbinu za doria na operesheni ambazo matokeo yake ni ya muda mfupi na vitendo viovu vya uvuvi haramu hujirudia. Vile vile, mbinu hizi zinasababisha changamoto nyingi ambapo waheshimiwa wabunge na wananchi wameendelea kupaza sauti.

**166. *Mheshimiwa Spika,*** tunakusudia tuandike historia ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais shupavu wa Awamu ya Sita kwa kumaliza kadhia ya uvuvi haramu kwa kuweka na kutekeleza mikakati madhubuti ya muda mfupi na mrefu. Mkakati mmojawapo ni kutumia teknolojia za kisasa ambazo pamoja na kudhibiti (control) zitazuia (deterrence) uhalifu wa uvuvi katika bahari na maziwa yetu. Teknolojia hizo ni kama vile matumizi ya ndege maalum zisizokuwa na rubani (drones) ambazo zina uwezo wa kusafiri kilomita **100** kwa muda wa saa mbili (**2**) na kuchukua picha za kiwango cha juu (high resolution videos) za uhalifu wa uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi. Teknolojia hii itaongeza ufanisi na kupunguza matumizi ya rasilimali fedha na muda.

**167. *Mheshimiwa Spika***, Wizara pia, inakusudia kuanza kutumia mfumo wa ufuatiliaji wa kielektroniki ambao utafungwa katika vyombo vyote vya uvuvi zikiwemo boti za kisasa zilizotolewa hivi karibuni. Mfumo huu utafuatilia mienendo yote ya wavuvi nchini ikiwemo kuweka kumbukumbu za mavuvi. Pamoja na kuzuia uvuvi haramu, mfumo huu utasaidia kuweka usalama wa wavuvi na wananchi ambao wanapata matatizo wakiwa maeneo ya maji yetu. Aidha, Wizara itaweka mipaka na kulinda mazalia na makuzi ya samaki (critical habitats) kwa kuweka maboya maalum, hatua hii itazuia uharibifu wa mazalia ya samaki ambayo ndio chanzo cha utunzaji wa demografia ya samaki ndani ya maji yetu.

**168. *Mheshimiwa Spika,*** tutaendelea kuwekeza katika teknolojia sahihi zitakazowezesha uendelevu wa rasilimali zetu adhimu za uvuvi kwa maslahi mapana ya sasa na vizazi vijavyo. Aidha, katika mwaka 2024/2025, Wizara itatekeleza miradi na shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa – Masoko na kufanya maandalizi ya awali ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Bagamoyo;

(ii) Kukamilisha uanzishaji wa chombo cha kusimamia na kuendeleza rasilimali za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji;

(iii) Kuendelea na taratibu za ununuzi wa Meli nne **(4)** za uvuvi wa Bahari Kuu kupitia TAFICO;

(iv) Kujenga kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi na kiwanda cha kuzalisha vyakula vya samaki;

(v) Kuwezesha ununuzi wa boti **450** na zana za uvuvi kupitia dirisha la ECF na Mradi wa TASFAM;

(vi) Kuwezesha vikundi **300** kwa ajili ya kilimo cha mwani, ufugaji wa kaa na majongoo bahari;

(vii) Kununua meli moja (**1**) ya mafunzo ya uvuvi kupitia mradi wa TASFAM;

(viii) Kununua maboya **60**, ndege saba (**7**) zisizo na rubani (drones) na kusanikisha mfumo wa ufuatiliaji wa vyombo vya uvuvi;

(ix) Kuwezesha ununuzi wa vizimba **497** kupitia ECF; na

(x) Kuanzisha mashamba darasa **20** ya ukuzaji viumbe maji katika Halmashauri **20.** Kuzalisha vifaranga vya samaki.......

**Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta za Mifugo na Uvuvi**

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuratibu na kuboresha utekelezaji wa Sera, Sheria na kanuni zinazosimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi ikiwemo kuendelea na mapitio ya Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006, Kanuni ya Uvuvi ya Mwaka 2009, kufanya tafsiri ya kanuni mbalimbali na kutoa elimu ya Sheria kwa wadau wa mifugo na uvuvi. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza afua na mikakati iliyobainishwa katika Mpango Mkuu wa Sekta ya Kilimo (Agricultural

Transformation Masterplan - 2050) ili kufikia matokeo tarajiwa katika sekta za mifugo na uvuvi.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025**

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, **Fungu 99,** inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **69,105,000,000,** kati ya fedha hizo, Shilingi **36,105,000,000** zitatokana na vyanzo vya mifugo na Shilingi **33,000,000,000** vyanzo vya uvuvi. Vyanzo vikuu vya makusanyo hayo ni pamoja na tozo ya ukaguzi wa mifugo; ushuru wa masoko; tozo za vibali vya kusafirisha mifugo, samaki na mazao yake; leseni za kusafirisha samaki na mazao yake; ushuru wa mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi na mifugo nchini; Ushuru wa mrabaha wa mauzo nje ya nchi na tozo za maabara.

**Mchanganuo wa makusanyo umeainishwa katika jedwali hapa chini:**

| GFS Code | GFS Code Description | Annual Budget Estimates |
|---|---|---|
| **Kifungu 7001: Veterinary Services** | | |
| 11510106 | Export Duty | 420,000,000 |
| 14210137 | Receipt from Veterinary Charges | 13,607,000,000 |
| 14220168 | Compounding Fee | 216,666,666 |
| 14220174 | Livestock Movement Permit | 14,000,000,000 |
| **Jumla Ndogo – 7001** | | **28,243,666,666** |
| **Kifungu 8001 : Livestock Production and Marketing** | | |
| 14220168 | Compounding Fees | 216,666,667 |
| 14220175 | Livestock Market Fees | 5,595,000,000 |
| 14220190 | Receipt from Sale of Semens and Liquid Nitrogen | 430,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 14220191 | Receipts from Sale of Heifers | 880,000,000 |
| **Jumla Ndogo – 8001** | | **7,121,666,667** |
| **Kifungu 8002 : Grazing Land and Animal Feed Resources Development** | | |
| 14220168 | Compounding Fees | 216,666,667 |
| 14220193 | Receipts from sale of Seeds and Hay | 200,000,000 |
| **GFS Code** | **GFS Code Description** | **Annual Budget Estimates** |
| 14220217 | Movement Permits fee other than livestock market | 323,000,000 |
| **Jumla Ndogo – 8002** | | **739,666,667** |
| **Kifungu 9001: Maendeleo ya Uvuvi** | | |
| 14210147 | Fishing Licences & Export | 2,059,000,000 |
| 14210148 | Export Royalty | 17,796,000,000 |
| 14210149 | EEZ Licenses | 2,814,000,000 |
| 14220161 | Miscellaneous Receipts | 237,000,000 |
| 14220168 | Compound fees | 943,000,000 |
| 14220213 | Prawn Fishing Licenses | 212,000,000 |
| 14220216 | Receipts from sale of Laboratory& Inspection Services | 1,900,000,000 |
| 14220217 | Movement permit | 6,679,000,000 |
| 14220222 | Import Royalty | 30,000,000 |
| **Jumla Ndogo – 9001** | | **32,670,000,00** |

| | | |
|---|---|---|
| | | **0** |
| **Kifungu 9002: Ukuzaji Viumbe maji** | | |
| 1422019 4 | Receipts from Sale of Fish and Fingerlings | 330,000,000 |
| **Jumla Ndogo – 9002** | | **330,000,000** |
| | | **69,105,000,000** |

**Uboreshaji Mbari za Mifugo**

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara imepanga kuboresha mbari za mifugo kwa kununua madume bora **60** aina ya Brahman na kuyasambaza kwa vikundi vya wafugaji. Aidha, wahimilishaji **178** kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa watajengewa uwezo ili waweze kutoa huduma ya uhimilishaji.

**Uendelezaji wa Mifugo na Mazao yake**

**172.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara imepanga kuanzisha kambi moja (1) ya mifugo wageni (Livestock Guest House) katika Ranchi ya Mkata kupitia mpango wa vitalu vilivyoboreshwa kwa kuwekewa miundombinu muhimu ya ufugaji ikiwa ni pamoja na malisho, maji na huduma za ugani. Mpango huu utasaidia kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo: Kuzalisha ndama **6,059** kutokana na majike wazazi **7,574**; Kuweka uzio wa fensi katika eneo la nyanda za malisho lenye ukubwa wa kilometa za mraba **40** katika ranchi ya Kongwa, Mkata, Mzeri, Ruvu na Missenyi; kutekeleza mradi wa unenepeshaji wa ng'ombe **4,800** katika ranchi za Kongwa, Ruvu na Mzeri; kuuza tani **1,134.8** ya nyama bora ya ''Kongwa beef'' kupitia maduka ya Kampuni; kuzalisha marobota **66,000** ya hei katika ranchi ya Kongwa, Ruvu na Mzeri kwenye eneo la ekari **825;** kuuza madume bora **346** ya ng'ombe aina ya Boran kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya kuboresha kosaafu za mifugo yao;

kununua madume bora **184** ya ng'ombe aina ya borani kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji katika ranchi ya Kalambo; kulima ekari **150** katika Ranchi za Kongwa na Ruvu kwa ajili ya kuzalisha malisho aina ya Mabingobingo yaliyoboreshwa (JUNCAO).

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) imepanga kuwajengea uwezo wadau wa maziwa **102** na wakaguzi wa maziwa **49** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Aidha, mafunzo kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa yatatolewa kwa vikundi **1,200** vya wafugaji sanjari na kufanya ukaguzi wa wadau **1,050** na kuwezesha usajili wa wadau 400 na vyama vya ushirika vinne **(4).**

**175.** ***Mheshimiwa Spika***, ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara itakamilisha ujenzi wa minada saba **(7)** na vituo 10 vya kukusanyia maziwa ili kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo na mazao yake nchini.

**Bodi ya Nyama**

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025 Wizara kupitia Bodi ya Nyama itaendelea kuthibiti ubora na biashara ya nyama kwa kuwajengea uwezo wazalishaji **300** wa mifugo na wadau **12,090.** Aidha, itafanya ukaguzi kwa wadau **12,075** kwa lengo la kulinda afya za watumiaji wa bidhaa za nyama na kusajili wadau **5,097**.

**Bodi ya Maziwa**

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa itasajili wadau **1,000** wa maziwa ili kuongeza urasimishaji wa biashara ya maziwa, ukaguzi wa wadau **1,200** ili kuimarisha uzingatiaji wa Sheria ya Maziwa Sura 262 ya Mwaka 2004, itajenga uwezo kwa wadau **500** na kuwezesha uanzishwaji na uimarishaji wa vyama viwili (**2**) vya ushirika wa maziwa ili kuongeza uzalishaji wa maziwa. Aidha, itawajengea uwezo wakaguzi **185** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha usimamizi.

**Huduma za Mifugo Chanjo na Uchanjaji wa Mifugo**

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itafanya kampeni maalum na zoezi la chanjo ya magonjwa ya kipaumbele kwa kuchanja zaidi ya asilimia 70 ya mifugo. Kampeni hii inalenga kudhibiti magonjwa na kukuza biashara ya mifugo na mazao yake ikiwa ni pamoja na kutokomeza ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR) na homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP) ambayo yanasababisha vifo vingi vya wanyama na hasara kwa wafugaji. Vile vile, kampeni hii itawezesha kukidhi matakwa ya biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi.

**Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake**

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, ili kulinda afya ya jamii dhidi ya magonjwa yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu, Wizara itaendelea na ukaguzi wa mifugo na mazao yake kwenye minada, machinjio, vituo vya ukaguzi vya ndani ya nchi na mipakani. Aidha, Wizara itaratibu ukaguzi wa mifugo na mazao mbalimbali ya wanyama yanayosafirishwa nje ya nchi. Vilevile, Wizara inatarajia kukagua na kuidhinisha nyama ya ng'ombe tani **2,200,** mbuzi na kondoo tani **15,000** kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. Pia, Wizara itakarabati miundombinu ya Kituo cha karantini cha Kwala kilichopo eneo la Kibaha, mkoani Pwani ili kukuza biashara ya mifugo kimataifa na kulinda afya ya jamii kutokana na magonjwa yanayoweza kuambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara itaendelea kushikiriana na sekta mbalimbali zikiwemo sekta za afya, kilimo na mazingira katika kudhibiti magonjwa ya kuambukiza yanayoathiri binadamu kutoka kwa wanyama ikiwemo kichaa cha mbwa, kimeta, homa ya bonde la ufa, ugonjwa wa kutupa mimba, ugonjwa wa malale na ugonjwa wa mafua makali ya ndege. Pia, Wizara itaendelea kudhibiti matumizi holela ya dawa za mifugo ili kuzuia tatizo la usugu wa dawa za kutibu magonjwa ya mifugo kwa baadhi ya vimelea vya magonjwa.

**Ustawi wa Wanyama**

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kutoa elimu ya ustawi wa wanyama kwa wakaguzi **70** na wadau **5,000** ili kuwajengea uelewa juu ya haki za Wanyama ili kuboresha uzingatiaji wa Sheria ya Ustawi wa wanyama Sura Na. 154 na Kanuni zake.

**182.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kudhibiti magonjwa na kuwezesha biashara salama ya mifugo ndani na nje ya nchi, kwa kuiwezesha Wakala ya Maabara ya Veterinari kuendelea na ujenzi wa maabara ya virusi pamoja na ununuzi wa vifaa vya maabara ya virusi, ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa chanjo.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania**

**183.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025,Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania imepanga kuzalisha chanjo za mifugo dozi milioni **85.3** ambapo dozi milioni **78** zitalenga kuzuia Ugonjwa wa Kideri/Mdondo kwa kuku; **dozi 800,000** dhidi ya mchanganyiko wa magonjwa ya Kimeta na Chambavu; dozi milioni **4.2** za Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe; dozi milioni **1.1** za Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi; **dozi 600,000** dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta; **dozi 550,000** za Ugonjwa wa Chambavu; na **dozi 17,000** za Ugonjwa wa Kutupa Mimba. Aidha, Wizara itaendelea kufanya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kwenye jumla ya sampuli **30,000** za wanyama, kuhakiki ubora wa vyakula vya mifugo kwenye sampuli **5,000** kutoka kwa wazalishaji, kufanya usajili mpya kwa aina **tatu (3)** za viuatilifu, kuhuisha **vibali 30** vya waingizaji wa viuatilifu nchini na kuhuisha leseni **200** za wauzaji wa viuatilifu. Pia, Wizara kupitia Wakala itatoa elimu na ufuatiliaji wa uzalishaji wa vyakula vya mifugo kwa wazalishaji **200** katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma. Vile vile Wakala itasajili na kuanza matumizi ya Chanjo ya Ugonjwa wa Mdondo/Kideri iitwayo TEMEVAC iliyotengenezwa kwa mfumo wa kidonge baada ya kufaulu majaribio ya ndani na uwandani, lengo likiwa ni kuwezesha kuwa na chanjo yenye muda mrefu wa matumizi

(Shelf life) na kuwezesha matumizi kwenye ufugaji mkubwa wa kuku kibiashara.

**184.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari itaendelea na ujenzi wa jengo la Maabara ya kisasa yenye hadhi ya GMP (Good Manufacturing Process) katika Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) ili kuzalisha chanjo za Magonjwa ya Mifugo yanayosababishwa na Virusi. Aidha, Wakala itaanza ujenzi wa jengo jipya la Maabara na Ofisi katika kituo cha Wakala - Dodoma ili kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa kimaabara. Pia, Wakala itaendelea na utafiti wa utengenezaji wa chanjo mpya tatu (3) dhidi ya magonjwa ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, Kichaa cha Mbwa na Mapele ngozi ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utengenezaji

**Baraza la Veterinari Tanzania**

**185.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania itafanya ukaguzi wa vituo **2,195** vya huduma ya afya ya wanyama; kukagua vituo **300** vinavyotoa na vinavyotarajia kutoa mafunzo ya afya na uzalishaji wa mifugo; kusajili madaktari **80** wa wanyama; kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi **1,500;** kutoa leseni **300** kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara ya veterinari; kusajili vituo **300** vya kutolea huduma ya afya ya wanyama katika Halmashauri 184; na Baraza litaendesha mitihani kwa madaktari wahitimu kutoka nje ya nchi na mitihani ya kuandikishwa kwa wahitimu **1**,**500** wa stashahada ya afya na uzalishaji wa mifugo.

**Uendelezaji wa maeneo ya malisho**

**186.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara itatoa mafunzo kwa wakaguzi **80** wa vyakula vya mifugo kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na kufanya ukaguzi wa maeneo **100** ya kuuzia, kuhifadhia na kuzalisha rasilimali za vyakula vya mifugo.

**187.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025 Wizara itawezesha mashamba ya Serikali (Vikuge na Langwira) kwa kuyapatia zana mbalimbali zikiwemo mashine na vifaa shamba;

kuwezesha ujenzi wa ghala la kuhifadhia malisho na kukaushia mbegu za malisho ili kuongeza uzalishaji wa malisho. Aidha, Wizara itakarabati miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la malisho Langwira na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la malisho la Vikuge.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Wizara, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Tume ya Taifa ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi itapima na kuweka mipaka eneo la malisho lenye ukubwa wa hekta **500,000** kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, Wizara itaondoa vichaka eneo lenye ukubwa wa hekta **2,000;** kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Mlunduzi na ghala la kuhifadhia malisho katika eneo la Msomera.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itakamilisha ujenzi wa visima viwili (**2**) vya Kinamwigulu (Maswa) na Kapelekasinde (Momba) na mabwawa manne (**4**) ya Kwekikwembe (Kilindi), Lerumo (Simanjiro), Kaiwang (Kiteto), na Msomera (Handeni). Aidha, kukamilika kwa miundombinu hii ya maji itasaidia kupunguza vifo vya mifugo wakati wa ukame na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa maji.

**Usimamizi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi**

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu sahihi za uvuvi, kutoa mafunzo kwa wakusanyaji takwimu za uvuvi pamoja na kufanya sensa za uvuvi katika maziwa ya Nyasa na Rukwa; na maji madogo (Nyumba ya Mungu, Ziwa Babati, Eyasi, Natron na Tlawi) ili kupanga mipango madhubuti na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa maeneo ya mazalia ya samaki kwa kuyatambua na kuweka alama kwa kutumia maboya. Kwa awamu ya kwanza jumla ya maboya 40 yatawekwa katika Ziwa Victoria kwa lengo la kuhifadhi, kulinda bioanuai, samaki na kuongeza uzalishaji. Aidha, Wizara

itaendelea kuimarisha usimamizi wa uvuvi wa pweza kwa kuhamasisha jamii za wavuvi kupumzisha miamba kwa hiari.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuimarisha vituo **37** vya doria, vikundi vya usimamizi shirikishi (BMUs), mashirikiano na taasisi mbalimbali pamoja na kufanya doria zenye siku kazi **8,400** ili kudhibiti uvuvi na biashara haramu na kuchochea uvuvi endelevu katika maeneo yote ya uvuvi.

**Uthibiti Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kusimamia uthibiti ubora, viwango na masoko ya mazao ya uvuvi kwa kuwajengea uwezo wakaguzi na wadau **300**; kuimarisha vituo **20** vya uthibiti ubora, viwango na masoko ya mazao ya uvuvi; kufanya kaguzi za kawaida **9,200**, kaguzi za kila robo mwaka **800** na kaguzi nne (**4**) za Kikanda na Kimataifa ili kufikia viwango vya masoko ya samaki na mazao yake.

**Maabara ya Uvuvi**

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaimarisha huduma za Maabara ya Taifa ya Uvuvi kwa kukarabati na kununua mitambo na vitendanishi vya uchunguzi wa kimaabara ili kuendelea kukidhi kiwango (ISO/IEC 17025:2017) cha umahiri wa upimaji, na ustawi wa ithibati ya maabara. Aidha, Maabara itafanya uchunguzi wa sampuli **3,500** za samaki, mazao ya uvuvi na mazingira yake ili kukidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama na kuiwezesha nchi kuuza samaki na mazao ya uvuvi katika masoko ya kitaifa na kimataifa.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na uzalishaji wa vifaranga kwa kusimamia na kuendesha vituo tano (**5**) vya ukuzaji viumbe maji (Ruhila – Ruvuma, Kingolwira – Morogoro, Mwamapuli – Tabora, Machui – Tanga na Nyengedi – Lindi) ili viweze kuzalisha

vifaranga **milioni 3**. Aidha, Wizara itaanza kufanya mapitio ya Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji (2018 - 2025) kwa lengo la kufanya maboresho yatakayo changia kuongeza uzalishaji wa mazao ya viumbe maji nchini. Vile vile, Wizara itafanya kaguzi na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za uzalishaji na udhibiti wa magonjwa katika maeneo ya ukuzaji wa viumbe maji, vitotoleshi na viwanda vya kutengeneza chakula cha samaki katika mikoa sita (**6**).

**Miradi ya Maendeleo chini ya Programu ya ASDP II**

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuimarisha uendeshaji wa vituo vitano (**5**) vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji (Machui, Ruhila, Nyengedi, Mwamapuli na Kingolwira) kwa kuvipatia vitendea kazi ili kuongeza ufanisi na tija. Aidha, Wizara itaendelea kuainisha na kuendeleza maeneo ya ufugaji samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Tanganyika na Nyasa. Vilevile Wizara itajenga mabwawa mawili (**2**) ya kufugia samaki katika shule moja nchini kwa lengo la kuimarisha lishe na kuhamasisha ufugaji wa samaki.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kutekeleza Mradi wa Ufugaji Samaki na Kilimo cha Mwani kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu ya zana na pembejeo za ufugaji samaki kwa vizimba na kilimo cha mwani kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Aidha, vizimba **270** vitatolewa pamoja na ujenzi wa mashamba darasa **20** katika Halmashauri **20** kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ufugaji samaki kwa vitendo.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko – Lindi; Maandalizi ya awali ya ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Bagamoyo; kununua na kusambaza maboti **180** na zana za uvuvi kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania; Kukamilisha ujenzi wa masoko saba **(7)** ya Tunduma, Kyamkwikwi, Masunche, Manda, Nyamikoma, Zingibari na Kasanga na mialo mitatu **(3)** ya Chato Beach, Kalungu na Ng'ombo. Aidha, na

kuimarisha Vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwa kuvinunulia boti 5 na injini zake, ndege moja (1) isiyokuwa na rubani kwa ajili ya doria (*surveillance drone*) na, mizani maalum mitano (5) ya kupimia uzito wa mazao ya uvuvi kwenye masoko na vituo vya ukaguzi.

**199.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2024/2025 Serikali itatekeleza Mradi wa Mageuzi ya Tasnia ya Maziwa kwa kuzingatia mabadiliko ya Tabianchi wenye lengo la kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa, kuimarisha upatikanaji wa malisho, udhibiti wa magonjwa ya mifugo na kuboresha huduma za ugani. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni ili kuboresha lishe kwa watoto na kuchochea ujumuishaji wa vyakula vitokanavyo na mazao ya mifugo.

**Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP)**

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, ili kuimarisha miundombinu ya vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji, Wizara itaendelea na ujenzi, ukarabati na Pangani-Tanga**;** kukamilisha ujenzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji – Rubambagwe; kujenga vichanja 40, ujenzi wa mahema mawili (2) ya kukaushia dagaa kwa mionzi ya jua (*solar drier*) na vyumba vitatu (**3**) vya ubaridi katika Halmashauri ya Wilaya ya Pangani na Manispaa ya Lindi.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)**

**201.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia MPRU itaboresha uwezo wa utoaji huduma, usimamizi wa ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa ofisi na vitendea kazi katika Vituo vya Mafia, Tanga, Mtwara na Dar es Salaam kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Tanga Coelecanth Marine Park (TACMP), Tanga Marine Reserves -TMRS na Maziwe; na kudumisha usafi wa njia za asili katika hifadhi na magofu ya kihistoria ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa. Vilevile, Wizara kupitia MPRU itafanya mikutano ya uhamasishaji ya washikadau kuhusu kufuata sheria zinazohusiana na usimamizi wa MPAs; kuwezesha

ukusanyaji wa mapato katika MBREMP na kushiriki katika maonyesho ya Saba saba, Karibu Arusha na SITE.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia MPRU itakuza maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na utalii kwa kutayarisha hati **(5)** za masoko; kuanzisha na kudumisha kanzidata ya utalii; kuboresha usimamizi wa mifumo ya ikolojia ya baharini na bioanuwai. Aidha, itatangaza maeneo mapya ya hifadhi ili kukuza utalii nchini. Aidha, Kitengo kitafanya upembuzi yakinifu na mashauriano pamoja na wadau ili kutambua maeneo yanayofaa kuanzisha au kufanya upanuzi wa MPAs.

**Shirika la Uvuvi Tanzania**

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025**,** Serikali itaendelea kuimarisha TAFICO kwa kufanya uwekezaji wa kimkakati ikiwemo kununua meli mbili (**2**) za uvuvi wa bahari kuu na kujenga kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki na kiwanda cha kuchakata mazao ya uvuvi. Aidha, mpango huu unalenga kushirikisha sekta binafsi kwa ajili ya kuchagiza uwekezaji, kuongeza ufanisi, matumizi ya teknolojia za kisasa na hivyo kuchangia katika kuongeza ajira, ukuaji wa uchumi na pato la taifa kwa ujumla. Vilevile, Wizara itaendelea na ukarabati wa miundombinu ya uendeshaji wa shirika ikiwemo chumba cha ubaridi na ukarabati wa gati.

**Utafiti, Mafunzo na Ugani**

**Utafiti na Mafunzo**

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha vijana na wanawake kwenye ufugaji wa kibiashara na kuongeza upatikanaji wa malighafi nchini, Wizara itaendelea na utekelezaji wa programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) kwa kuimarisha vituo nane (**8)** vilivyopo na kuanzisha vituo vipya vitano **(5**) ambapo vijana na wanawake **390** watanufaika katika Sekta ya Mifugo **.** Aidha, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi mafunzo ya stadi za ukuzaji wa viumbe maji yatatolewa kwa vijana na wanawake **300**.

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi nane (**8)** za Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) na kampasi tano (**5**) za Wakala ya Mafunzo ya Uvuvi (FETA). Aidha, Wizara itaratibu na kuwezesha mafunzo kwa Wakufunzi kutoka Kampasi za LITA na vyuo **12** vya Binafsi vinavyotumia Mitaala ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Pia, Wizara itaendelea kuratibu Vituo saba (**7)** vya TALIRI, vitano (**5)** vya TAFIRI na Taasisi **11** zinazofanya Tafiti katika kuhakikisha tafiti zinazofanyika zinakidhi vigezo na kuzingatia Agenda ya Utafiti wa Mifugo na Uvuvi na mahitaji ya kisera.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2024/2025 Wizara kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) itaendelea kuwalea vijana **161** wa BBT waliopatiwa vitalu vya kuendelea na ufugaji wa mifugo kibiashara katika Ranchi za Kitengule na Kagoma, Mkoani Kagera. Aidha, Wizara itaendelea kuwaunganisha vijana hao na fursa mbalimbali ikiwemo mikopo kutoka Taasisi za kifedha pamoja na Masoko ili kuwawezesha kukuza mitaji ya kuendesha biashara ya mifugo.

**Taasisi za Utafiti wa Mifugo na Uvuvi (TALIRI na TAFIRI)**

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TALIRI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea na utekelezaji wa mradi wa African Asian Dairy Genetic Gain (AADGG) katika Mikoa saba (7) nchini kwa ajili ya kuboresha mbari za ng'ombe wa maziwa; mradi wa unenepeshaji wa mbuzi na uzalishaji wa malisho (BBT Kongwa Ranchi); mradi wa *Environment Cow GHG Emission* katika Mikoa miwili ya Kilimanjaro na Arusha kwa ajili ya kupunguza madhara ya hewa ukaa; mradi wa Maziwa Faida Mkoani Tanga kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa maziwa. Vilevile, Wizara kupitia TAFIRI itaendelea kuainisha maeneo ya ufugaji samaki kwa vizimba katika Ziwa Tanganyika na Nyasa.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu sahihi za uvuvi, kutoa mafunzo kwa wakusanyaji takwimu za uvuvi

pamoja na kufanya sensa za uvuvi katika maziwa ya Nyasa na Rukwa; na maji madogo (Nyumba ya Mungu, Ziwa Babati, Eyasi, Natron na Tlawi) ili kupanga mipango madhubuti na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi za TALIRI na TAFIRI zitaendelea kufanya tafiti katika maeneo ya kiupaumbele ambayo ni: uzalishaji na uendelezaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na nguruwe; uchambuzi na uhifadhi wa kosaafu za mifugo mbalimbali ya asili; uendelezaji wa malisho na uzalishaji wa mbegu za malisho, lishe na ubora wa vyakula vya mifugo na kufanya utafiti wa wingi na matawanyiko wa samaki katika Bahari ya Hindi kwa upande wa TAFIRI.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo na Uvuvi (LITA na FETA)**

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) na Wakala ya Mafunzo ya Uvuvi (FETA) zinatarajia kudahili wanafunzi **5,300** na kuendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi **13**. Aidha, Wakala ya kwa kushirikiana na wadau zitatekeleza programu ya elimu na ujuzi wa kazi za uzalishaji (Education and Skills for Productive Jobs Program-for-Results - Phase II); Kujenga Kituo cha kubadilishana teknolojia (African Modern Agriculture Technology Exchange Training Centre); na kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika kampasi za Gabimori, Mikindani na Nyegezi.

**Huduma za Ugani**

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha uhaulishaji wa maarifa na teknolojia mpya kwa wafugaji, wavuvi na wakuzaji viumbe maji, katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Maonesho ya Kimataifa ya Kibiashara (Saba Saba), Nane Nane, Siku ya Ushirika Duniani; Madhimisho ya Siku ya Chakula Duniani; na Siku ya Mvuvi imepanga kuwafikia wadau **50,000**. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya Ushirika vya Wafugaji **(20)** na Wavuvi **(10)** katika Halmashauri **20** nchini. Vilevile, itahuisha Mwongozo wa Utoaji Huduma za Ugani wa Mifugo na Uvuvi.

## H. MASUALA MTAMBUKA

### Utekelezaji kwa Mwaka 2023/2024 ya Masuala Mtambuka

### Ushiriki wa Sekta Binafsi

**212.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi imeendelea kushirikiana na wadau wa Sekta Binafsi wakiwemo, wazalishaji, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara wengine wa mazao ya mifugo na uvuvi. Kupitia ushirikiano huo, wadau wa mifugo na uvuvi wameunganishwa na taasisi za fedha. Hadi kufikia Aprili mwaka 2024, benki ya TADB imetoa mkopo wa Shilingi **bilioni 15.82,** benki ya NMB imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi **bilioni 67.9** na benki ya CRDB Shilingi **bilioni 66.59**. Mikopo hiyo ilielekezwa kwenye maeneo ya ufugaji wa ngómbe, kuku, nguruwe na samaki; uzalishaji wa malisho na vyakula vya mifugo, kilimo cha mwani; unenepeshaji wa mifugo na uchakataji wa mazao ya mifugo na uvuvi.

**213.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kuibua maeneo mapya ya uwekezaji; kuwajengea uwezo wafugaji na wavuvi ili wafanye shughuli zao kibiashara; kushiriki katika kufanya tafiti ya minyororo ya thamani na masoko; kuwaunganisha wafugaji na wavuvi na taasisi za kifedha.

### Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, jumla ya watumishi 103 wamepandishwa vyeo; watumishi 14 wamebadilishwa kada; 108 wameajiriwa; 22 wamehama; 13 wamehamia. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza Mwongozo wa Kudhibiti VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma kwa kutoa elimu kwa watumishi **921** kuhusu VVU/UKIMWI, magonjwa yasiyoambukizwa na kuhamasisha upimaji wa afya. Pia, watumishi **921** wamehamasishwa na kushiriki

mabonanza ya michezo na mashindano ya SHIMIWI, ili kupunguza Magonjwa Yasiyoambukiza.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara imeomba kupatiwa Ikama yenye jumla ya nafasi **668** kwa ajili ya ajira mpya **150**, uhamisho **86**, uteuzi **11**, upandishwaji vyeo **410**, na ubadilishwaji wa kada **11**. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya kutekeleza Mwongozo wa Kudhibiti VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma kwa kutoa elimu kwa watumishi **1,157** kuhusu VVU/UKIMWI, Magonjwa yasiyoambukizwa na kuhamasisha upimaji wa afya. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa kwa kuelimisha watumishi kuhusu Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma.

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**216.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuhamasisha ufugaji unaozingatia utunzaji wa mazingira na kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ambapo jumla ya wafugaji **204** kutoka vijiji sita (**6**) vya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda (Mara) wamepewa mafunzo kuhusu ufugaji endelevu unaohimili Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, Wizara imeandaa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira katika ukarabati wa machinjio ya Kizota – Dodoma; Pia, ukaguzi wa kimazingira katika mnada wa Upili wa Pugu, Dar-es-Salaam umefanyika na jumla ya miti **1,050** ya kivuli na kuzuia mmomonyoko wa ardhi imepandwa.

**217.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari, maziwa na mito ili kuwa na uvuvi endelevu ambapo jumla ya wavuvi **110** wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo walijengewa uelewa juu ya mbinu za kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu baharini na nchi kavu. Pia, jumla ya wavuvi **277** (**128** kutoka ziwa Babati na **149** kutoka ziwa Manyara) walijengewa uelewa wa uvuvi endelevu na matumizi ya zana za uvuvi zinazokubalika kisheria.

**218.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta zilizoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ambapo majengo ya ofisi za vituo vya ulinzi na usimamizi wa raslimali za uvuvi vya Kigoma, Buhingu (Uvinza), Ikola (Tanganyika), Kasanga (Kalambo) pamoja na mialo mitatu (3) iliyoboreshwa ya Kibirizi (Kigoma), Ikola (Uvinza), na Kilando (Nkasi) imezama baada ya mvua kubwa iliyosababisha kuongezeka kwa kina cha maji katika Ziwa Tanganyika.

**219.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu ufugaji na uvuvi endelevu, sheria za uhifadhi wa mazingira na mbinu za kustahimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa wavuvi na wafugaji **1,500**. Aidha, Wizara itaratibu na kusimamia Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) kwenye miradi **15** ya maendeleo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia, Wizara itajenga mtambo mmoja (**1**) wa biogesi katika viwanja vya maonesho ya Nane Nane Nzuguni - Dodoma. Vilevile, Wizara itajenga uelewa kwa wadau **500** katika Ziwa Nyasa juu ya hatua za kuchukua ili kupunguza athari kwa mazingira zitokanazo na shughuli za uvuvi na ufugaji wa mifugo usio endelevu.

**Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

**220.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma ambapo imeratibu usimamizi na utoaji wa vibali **16,778** vya kusafirisha mifugo na mazao yake kupitia mfumo wa *Mifugo Integrated Management Information System* (MIMIS) na Mfumo wa TAUSI unaotumika kwenye minada ya awali ya mifugo iliyopo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara imeendelea na usanifu na uandaaji wa mfumo wa utambuzi na usajili wa mifugo nchini, ambapo utakapo kamilika utambuzi na usajili utafanyika kwa kutumia simu ya kiganjani. Aidha, Wizara imeboresha mfumo wa maduhuli (FiRCIS) ili kupunguza muda wa kuhudumia wateja kutoka siku 21 hadi saba (7) pamoja na kudhibiti upotevu wa maduhuli ambao ungetokana na udanganyifu wa nyaraka.

**221.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kusanifu, kutengeneza, kusimamia vibali vya kusafirisha mifugo, mazao ya uvuvi na mifugo ndani na nje ya nchi na kutoa msaada wa kiufundi kwa mifumo ya TEHAMA ya Wizara ikiwemo FiRCIS, LGRCIS, MUSE, GePG, MIMIS, pamoja na kufunga miundombinu na vifaa vya TEHAMA kati ya Wizara na vituo vyake.

**Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa**

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara imesaini Hati ya Mashirikiano (MoU) na Jeshi la Kujenga Taifa yenye lengo la kukuza na kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi katika mnyororo wa thamani kwa ajili ya kuchangia usalama wa chakula ikiwa ni pamoja na kukuza uchumi kwa Vijana na Wanawake. Aidha, Wizara, pia, imesaini Hati ya Mashirikiano (MoU) na wadau wa kuku na ndege wafugwao yenye lengo la kutanua soko na kuchagiza ukuaji wa sekta. Utekelezaji wa Mashirikiano unaendelea na Wizara imezindua kamati ya kusimamia utekelezaji wa mashirikiano hayo.

**223.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imesaini hati ya mashirikiano (MoU) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Rwanda juu ya uendelezaji wa Tasnia ya Maziwa. Mashirikiano hayo yatahusisha ujenzi wa kiwanda cha kusindika maziwa mkoani Mwanza sambamba na ujenzi wa vituo vya kukusanya maziwa kwa ajili ya kiwanda hicho. Aidha, kutokana na uwepo wa Mradi wa TI3P ambao unatekelezwa kwa pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Wizara yangu kupitia Bodi ya Maziwa na mashirika ya *Heifer International* na *Land O'lakes Venture 37* vyama vya ushirika vya wafugaji vinaundwa na vile vilivyopo kuimarishwa kufanya uzalishaji wa maziwa wenye tija kwa kutoa mafunzo ya ubora na kukusanya maziwa katika maeneo rasmi. Mradi huu pia utawezesha kupatikana kwa maziwa katika kiwanda kinachotarijiwa kujengwa.

**224.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi kwa kushiriki katika mikutano

na vikao mbalimbali vya kikanda na kimataifa. Baadhi ya mikutano hiyo ni pamoja na Kikao kazi cha kilichounda Jukwaa la Afya Moja katika ukusanyaji na utoaji wa taarifa zinazohusu magonjwa yanayoenezwa kati ya binadamu na wanyama chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na *Southern African Center for Infectious Disease Surveillance (SACIDS);* Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (LVFO) vilivyojadili na kuweka mipango ya kudhibiti uvuvi haramu, usimamizi wa uvuvi na ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba; Vikao vya Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (LTA) kwa ajili ya utekelezaji wa Mkataba wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi na maandalizi ya sensa ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika; pamoja na Mkutano wa Jukwaa la Mifumo Afrika (AGRF) uliofanyika Dar es Salaam na kufungua fursa za masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi pamoja na fursa za uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

**225.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Wizara inashirikiana na taasisi za kikanda na kimataifa zikiwemo:- Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC), Taasisi ya Uvuvi Ziwa Victoria (Lake Victoria Fisheries Organization - LVFO),Taasis ya Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), Taasisi ya Sayansi za Bahari Magharibi mwa Bahari ya Hindi (Western Indian Ocean Marine Science Association - WIOMSA), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Commision - SWIOFC), Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika Authority - LTA), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Tuna Commission - IOTC), Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (Indian Ocean Rim Association - IORA), Kamisheni ya Usimamizi wa Nyangumi (International Whaling Commission - IWC), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Commission - IOC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness - AWARFA), Shirika la Afya Duniani (World Health Organization - WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (World Organization for Animal Health - WOAH), Shirika la Chakula

na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ireland (TEAGASC), Serikali ya Uholanzi na Serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (*Economic and Social Development Programme – ESDP*), *Trade Mark East Africa* - TMEA na *Overseas Fishery Cooperation Foundation (OFCF) of Japan*. (weka kimakundi)

**226.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2023/2024, Wizara imesaini hati mbili **(2)** za mashirikiano (MoU) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China yanayolenga kuendeleza teknolojia, kuendeleza na kuboresha mbinu za usimamizi na matumizi ya rasilimali za uvuvi, ulinzi wa ikolojia ya mazingira na uhifadhi wa viumbe maji. Pia, Wizara imesaini hati ya mashirikiano na Jamhuri ya Indonesia, lengo la mashirikiano haya ni kuendeleza na kukuza ushirikiano katika nchi hizi mbili **(2)** katika kuendeleza tasnia ya ukuzaji viumbe maji,usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi na kubadilishana uzoefu katika kuzuia uvuvi haramu, uvuvi usioratibiwa na uvuvi usiotolewa taarifa.

**227.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha mahusiano katika uwekezaji, masoko na tafiti zinazohusu Sekta za Mifugo na Uvuvi.

## HITIMISHO

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2022/2023 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za Kitaifa na

Kimataifa, taasisi zwakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

**229.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutumia fursa hii kuzitambua na kuzishukuru nchi za Japan, Korea Kusini, Uingereza, Uholanzi, Ireland, Saudi Arabia, United Arab Emirates (UAE), Oman, Norway, Jumuiya ya Ulaya, Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Ethiopia, Comoro na Misri; kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Naomba pia kutambua na kuzishukuru jumuiya za kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Shirika la Maendeleo la Kiserikali la Nchi za Afrika Mashariki (IGAD), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).

**230.** ***Mheshimiwa Spika***, Aidha, ninazishukuru taasisi zinazoendelea kutuunga mkono kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:- Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (Lake Victoria 141 Fisheries Organization - LVFO), Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (Lake Tanganyika Authority - LTA), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Tuna Commission - IOTC), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Commision - SWIOFC), Jumuiya ya Nchi zilizopo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (Indian Ocean Rim Association - IORA), Western Indian Ocean Marine Science Association (WIOMSA), Kamisheni ya Kimataifa ya Usimamizi wa Nyangumi (International Whaling Commission - IWC), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Commission - IOC), na Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness -AWARFA).

**231.** ***Mheshimiwa Spika***, nitambue pia mchango wa mashirika mengine tunayoshirikiana nayo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ambayo ni: Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Kiatomiki (International Atomic Energy), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Misaada la Poland (Polish Aid), Shirika la Umoja

wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ireland (TEAGASC), Serikali ya 142 Uholanzi na Serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (Economic and Social Development Programme – ESDP), na Overseas Fishery Cooperation Foundation (OFCF) of Japan.

**232.** ***Mheshimiwa Spika***, nazishukuru pia taasisi za Kifedha na Wadau wa Maendeleo kwa ushirikiano wao hasa, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo ya Uswisi (SDC), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GIZ), United Nations University (UNU), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA); na mashirika ya IAEA, UNIDO, ILRI, CIAT, ASARECA, CCARDESA na GEF kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**233.** ***Mheshimiwa* Spika**, Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za Bill and Melinda Gates Foundation, World Wide Fund for Nature (WWF), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, OXFARM, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Building Resources Across Communities (BRAC), World Society for Protection 143 of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), British Gas International, Sea Sense, SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC), pamoja na Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**234.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt.** Samia Suluhu Hassan, kwa namna

anavyoliongoza Taifa letu na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nina imani kuwa ndani ya uongozi wake tutahakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 unatekelezwa kikamilifu hususan katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii tena kuwashukuru na kuwapongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa maoni yao na ushauri unaolenga kuboresha na kuimarisha Sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia niwashukuru wadau mbalimbali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, wafugaji na wavuvi hususan wanaozingatia Sheria katika utendaji wa kazi zao kote nchini kwa kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Napenda kuwaahidi kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuunga mkono juhudi za wafugaji, wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa bidhaa za mifugo na uvuvi.

**236.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kurejea tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti (Mb), Mbunge wa Jimbo la Misungwi, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri na ushirikiano wake katika kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, natoa pia shukrani zangu kwa **Prof.** Riziki Silas Shemdoe, Katibu Mkuu, **Dkt.** Daniel Elius Mushi Naibu Katibu Mkuu (Mifugo) na **Dkt.** Edwin Paul Mhede Naibu Katibu Mkuu (Uvuvi), Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi nzuri wanazozifanya.

**237.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mkuranga ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na ya Taifa letu, nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo ili niweze kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi.

**I. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025**

| | | |
|---|---|---|
| **i)** | **Fedha za matumizi ya Kawaida:** | **Shilingi 97,215,432,000** |
| | Mishahara | Shilingi 44,847,492,000 |
| | Matumizi Mengineyo (OC) | Shilingi 52,367,940,000 |
| **ii)** | **Fedha za Matumizi ya Maendeleo:** | **Shilingi 363,118,170,000** |
| | Fedha za Ndani | Shilingi 242,078,803,000 |
| | Fedha za Nje | Shilingi 121,039,367,000 |

**238.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara inaomba kutumia jumla ya Shilingi **460,333,602,000** kati ya fedha hizo, Shilingi **97,215,432,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **363,118,170,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.** Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya wizara: www.mifugouvuvi.go.tz.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsante Mheshimiwa Waziri na hongera kwa kazi nzuri, Ilala hujaleta boti bado. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na orodha ya wageni imeletwa na wageni ni wengi, inabidi tuwapunguze hawa ili waingie wengine. Nachukua jukumu la kuwatangaza wageni wote waliohudhuria Bunge hili. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii:

Wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika, wageni 10 wa Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Bunge la Zambia wakiongozwa na Mheshimiwa Darius Mulunda, Mwenyekiti wa Kamati na Kiongozi wa Msafara. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kambamba S. Mulenga, Mjumbe; Mheshimiwa Edgar Sing'ombe, Mjumbe; Mheshimiwa Elliot Kamondo, Mjumbe; Mheshimiwa Lukas Simumba, Mjumbe; Mheshimiwa Mwene Luhamba, Mjumbe; Mheshimiwa Christopher Shakafuswa; Mjumbe; Mheshimiwa Misheck Mutelo, Mjumbe; Mheshimiwa Misheck Nyambose, Mjumbe; na Mheshimiwa Moses Chuba, Katibu wa Msafara. Karibuni kwenye Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Profesa Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu; Dkt. Daniel Mushi, Naibu Katibu Mkuu, Mifugo; Dkt. Edwin Mhede, Naibu Katibu Mkuu, Uvuvi; Mheshimiwa Balozi Dkt. Ahmada El Badaoui, Balozi wa Comoro; Ndugu Mark Tsoxo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala ya Mafunzo ya Mifugo – *LITA;* Profesa Sebastian Chenyambuga, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo – *TALIRI;* Ndugu Priska Lwangili, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uvuvi *TAFICO;* Profesa Lugano Kusiluka, Mwenyekiti wa Baraza la Veterinari Tanzania; Ndugu Philbert Mponzi, Mwakilishi wa *CEO NMB;* Dkt. Salum Soud Hamed, Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Uvuvi – SMZ; Ndugu Yohana Kaduma, Mkurugenzi Mkuu *Private Agriculture Support Services;* na Ndugu Florence Martin Turuka, Katibu Baraza la Kumshauri Rais kuhusu masuala ya Chakula na Kilimo. *(Makofi)*

Wengine ni Sheikh Ally Ngeruko, Naibu Kadhi Mkuu wa Tanzania; Sheikh Khamis Mtupa, Sheikh wa Mkoa wa Pwani; Sheikh Mustafa Rajabu, Sheikh wa Mkoa wa Dodoma; Sheikh Walid Alhad Kawambwa, Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam; Sheikh Walid simama tena bwana, wewe ndiye Sheikh wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Ahsanteni. *(Makofi)*

Wapo pia Padre Ayubu Mwang'onda, Baba Paroko Kanisa Katoliki Mkuranga; Ndugu Frank Nyabundege, Mkurugenzi

Mtendaji; Ndugu Charles Tulahi, *Assistance Representative FAO and Co-chair of Agriculture Working Group*; Profesa Raphael Chibuda, Makamu Mkuu wa Chuo cha Sokoine cha Kilimo; Ndugu Fuad Abri, Mkurugenzi Mtendaji wa Asas; Ndugu Mzee Khamis Ulega, baba mzazi wa Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Waziri wa Mifugo; karibu baba umezaa chema. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Maya Khamis Kassim, dada wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Asha Abdallah Ibrahim, dada wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Zaitun Ulega, dada wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Khadija Abdallah Ibrahim, dada wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Spika ni Mheshimiwa Mzee Joseph Butiku, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, karibu sana Mzee Butiku. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha, Askofu Mussa Masanja Magwesela, Askofu Mkuu wa *African Inland Church Tanzania* na Askofu wa Dayosisi ya Mwanza; na Mchungaji Japhet Tengule Kafugo, Mchungaji Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Mwanza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Kundo Andrea Mathew, Naibu Waziri wa Maji, Baba Askofu Liberatus Sangu, Askofu wa Jimbo la Shinyanga, Baba Askofu karibu. *(Makofi)*

Wageni wengine nane wa Mheshimiwa Spika ni Wajumbe wa Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM). *(Makofi)*

Wageni wengine saba wa Mheshimiwa Kundo Andrea Mathew, Naibu Waziri wa Maji, Mapadre kutoka Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi, mtoto wake kutoka Mlalo, Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Mkundi, mvuvi kutoka Ukerewe. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hawa Chakoma, mdau wa maendeleo ya watoto kutoka *Watoto Foundation* ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, kaka yake kutoka Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani kutoka Ushetu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, mvuvi kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ndugu yake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Kigwangala kutoka Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Deus Sangu, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kutoka Sumbawanga. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, wafugaji kutoka Mvomero Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Boniphace Getere kutoka Chama cha Wafugaji Tanzania. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Khamis Taletale, wafugaji kutoka Morogoro Kusini. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa George Malima, Makatibu Muhtasi wa Baba Askofu kutoka Dayosisi ya Kanisa la Anglikana Tanzania. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Katani Katani, Watendaji wa Kata kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba wakiongozwa na Afisa Tawala wa Halmashauri Bi Saumu Bakar. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo:-

Akinamama wazee 18 waliosoma Ashira kwenye miaka ya 1960 na 1970 wa *Ashira Alumni Club 60+;* Wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; na wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Mt. Yohana cha Jijini Dodoma *(St. John's University of Tanzania)*. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na kundi la Waheshimiwa Mabalozi wa Nchi za Afrika *(African Diplomatic Group)*, imeandaa mashindano ya mbio za ridhaa *(African Marathon Day)* kilometa tano na kilometa 15, tarehe 18 Mei, 2024, Jijini Dar es Salaam. Lengo la maadhimisho hayo ni kuelekea kilele cha Siku ya Afrika *(Africa Day)* ambayo huadhimishwa kila ifikapo tarehe 25 Mei ya kila mwaka.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wanaalikwa kushiriki kwenye mbio hizo. Aidha, washiriki wanaweza kufanya usajili kupitia kiungo kifuatacho ambacho kipo kwenye vishkwambi vyenu. Ada ya kushiriki ni shilingi 30,000/= kwa kila mshiriki ambayo inalipwa kupitia Lipa Namba 54281965 *M-Pesa*. Kwa mawasiliano zaidi, wanaweza kuwasiliana na Bwana Ismail Abdallah kwa namba 0713 407 543 au afike eneo la mapokezi, Ofisi ya Bunge, Jengo la Utawala.

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa *Jubilee Life Insurance* wapo katika viwanja vya Bunge kuonesha huduma zao za Bima wanazotoa kuanzia tarehe 13 – 17 Mei, 2024. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenda kutembelea maonyesho hayo.

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na

Jeshi la Zimamoto, wameweka banda la maonyesho katika viwanja vya Bunge kuanzia tarehe 13 – 21 Mei, 2024. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenda kutembelea banda hilo na kupata elimu.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Iddi Kassim kuhusu masuala ya tozo kwenye mashamba, Serikali itatoa maelezo. Kwa hiyo Serikali mjiandae *immediately* baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo kutoa taarifa yake.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KUDUMU YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizaya hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kutokana na ufinyu wa muda, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelezo ya Jumla, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu Msingi wa Uchambuzi, Muundo wa taarifa na njia zilizotumika kutekeleza jukumu la shughuli hii ya bajeti;

(ii) Sehemu ya Pili inatoa maelezo kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri kutokana na uchambuzi na kuhitimisha maudhui ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelezo kamili kuhusu Uchambuzi na Tathmini; sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, tarehe 21 Machi, 2024, Kamati ilikutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika maelezo hayo Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa majukumu, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo - Fungu 99 ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 42,105,000,000. Hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 17,330,279,726, sawa na 41.16% ya lengo la makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, Fungu 64 lengo lilikuwa ni kukusanya jumla ya shilingi 41,000,000,000 kutoka vyanzo mbalimbali kama vilivyobainishwa katika Taarifa. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi 17,897,169,912.78 ambayo ni sawa na 43.7% ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(i) Jumla ya makusanyo ya maduhuli hadi kufikia Februari, 2024 yamefikia 42.4% ya lengo;

(ii) Sekta ya Mifugo iliyokadiriwa kuchangia 51% ya makusanyo ya Wizara imechangia 49%; na

(iii) Sekta ya Uvuvi iliyokuwa imekadiriwa kuchangia 49% ya Makusanyo, imechangia 51%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya ukusanyaji wa maduhuli inaonesha kuwa ni vigumu kwa Wizara kufikia lengo lililowekwa la ukusanyaji wa maduhuli. Aidha, pamoja na ukusanyaji usio na mwelekeo wa kufikia lengo, Sekta ya Uvuvi imejitahidi sana kulinganishwa na Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 194,335,967,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi 165,274,198,000 na fedha za nje ni shilingi 29, 061,769,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati imebaini kuwa hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024 Wizara ilipokea 41.56% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge hili Tufuku. Hali hiyo inaonesha kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi hicho ulikuwa nyuma kwa 58.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ni wazi kuwa, utekezaji wa miradi iliyopangwa na Serikali kupitia Wizara hii haiwezi kufikiwa. Hali hiyo, siyo nzuri na inaweza kusababisha Sekta ya Mifugo kushindwa kuchangia vyema katika Pato la Taifa, kukuza ajira na kupunguza umasikini miongoni mwa Watanzania waliojiajiri katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitatu ya Tanga, Dar e salaam na Pwani na kukagua baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na Serikali kupitia Wizara hii:-

(i) Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo katika mpaka wa Horohoro, Tanga.

(ii) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* na

(iii) Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo lililopo Vikuge, Kibaha, Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ziara hiyo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo yameonesha mambo yafuatayo:-

(a) Katika Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo Horohoro, Tanga, Kamati imebaini kuwa:-

(i) Kumekuwa na utoroshaji wa mifugo kwa kupitia njia za panya kwenda nchi jirani ya Kenya. Aidha, bado idadi ya mifugo inayouzwa katika Mnada wa Horohoro ni ndogo, jambo linalopunguza mapato ya Serikali.

(ii) Ushuru wa mifugo kwenye Mnada wa Horohoro ni mkubwa ambapo ng'ombe mmoja anatozwa shilingi elfu thelathini, hali inayochochea utoroshwaji wa mifugo kupitia njia za panya.

(iii) Pamoja na Halmashauri ya Mkinga na Serikali ya Kijiji kutoa eneo la kujenga mnada bado hawanufaiki na mapato yanayotokana na mnada huo. Hali hii inatokana na utaratibu wa Serikali Kuu kuchukua mapato yote yanayotokana na mnada.

(iv) Kukosekana kwa ulinzi katika eneo la mnada kunahatarisha usalama wa watu, mifugo na majengo wakati na baada ya shughuli za uuzaji wa mifugo.

(v) Kukosekana kwa majengo ya ofisi, Kituo cha Polisi na miundombinu ya maji katika eneo la mnada kuna hatarisha usalama wa afya za watumiaji wa mnada huo na

(vi) Pamoja na eneo la mnada kuwa kubwa hakuna mpango wowote wa kuwa na malisho ya mifugo wakati wafugaji wakiwa wanasubiri kuuza mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo ni dhahiri kuwa, lengo la Mradi wa Kuimarisha Biashara ya Mifugo na Kuongeza Mapato haliwezi kufikiwa. Kamati ina maoni kwamba, changamoto hizo zinapaswa kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi *(TAFICO)*. Kamati imebaini kuwa:-

(i) Baadhi ya Majengo ya *TAFICO* yaliyo pembezoni mwa bahari yako hatarini kuanguka kutokana na maji kula kingo za ardhi.

(ii) *TAFICO* kukabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo na upungufu wa zana za kutosha kama vile meli za uvuvi.

(iii) Mtiririko usioridhisha wa fedha zilizoidhinishwa, kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hali hiyo inasababisha kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwenendo huu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni vigumu kwa taasisi hiyo kufikia dira yake ya kuwa kituo bora cha utafiti na ushauri elekezi katika Ukanda wa Mashariki ya Kusini mwa Afrika. Aidha, *TAFICO*

haitoweza kuendeleza uvuvi wa kibiashara na Sekta ya Uvuvi Nchini kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo Vikuge, Mkoani Pwani. Kamati imebaini kuwa:-

(i) Ukosefu wa miundombinu ya kukaushia na kuhifadhia mbegu za malisho, hali inayosababisha upotevu wa malisho na mbegu kuharibika.

(ii) Ukosefu wa miundombinu ya kuhifadhia malisho baada ya kuvuna na kabla ya kuuzwa kwa wanunuzi hali inayochangia hasara kutokana na malisho kuharibika.

(iii) Ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji hali iliyosababisha shamba kupunguza uzalishaji hasa kipindi cha kiangazi.

(iv) Uchakavu wa mitambo na vifaa ikiwemo matrekta, mashine za kukata majani hali inayoathiri ufanisi na tija katika shamba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matokeo hayo tija ya mradi na manufaa kwa wafugaji hayawezi kupatikana inavyostahili. Kamati ina maoni kuwa, ipo haja ya kuongeza usimamizi wa mradi huu kwa lengo la kusaidia manufaa makubwa kwa wafugaji. Aidha, Serikali inapaswa kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huu, ili kuendeleza kupata tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla kamati inapongeza sana jitihada za Serikali za kuendeleza kuwafikishia wananchi miradi mbalimbali ambayo ina lengo la kutatua changamoto zinazowakabili, hasa katika Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Sekta ya Mifugo (Fungu 99) na Uvuvi (Fungu 64) zilitengewa jumla ya shilingi 292,520,933,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kutekeleza

Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2024 Wizara ilipokea 38.55% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha Sekta zote mbili (Sekta ya Uvuvi na Sekta ya Mifugo) hazitarajiwi kukamilisha majukumu yake yaliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2023 na 2024. Aidha, pamoja na kuwa mwenendo wa jumla unaonesha hali ngumu ya upatikanaji wa fedha, Sekta ya Uvuvi imekabiliwa na hali ngumu zaidi ukilinganisha na Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo inahatarisha mchango wa sekta hizo katika Uchumi wa Taifa. Aidha, hali hiyo inaathiri ustawi wa watu ambao shughuli zao kuu za uchumi zimeegemea katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kamati ina maoni kuwa, upo umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa, fedha zilizobaki kwa ajili ya sekta hizo zinapatikana kabla ya tarehe Moja Julai, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu hizo kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa wakati, ili utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati. Mfano wa ushauri wa Kamati uliozingitawi ni kuhusu uendeshaji wa Vituo vya *BBT* na ufugaji bora wa kisasa. Taarifa ya Wizara inaonesha kwamba, Vituo vya *BBT* vimeanzishwa na vijana waliopo katika vituo hivyo wanafundishwa mbinu za ufugaji bora, ili kuzalisha mifugo inayokidhi mahitaji na soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri, yapo maeneo mengine ya ushauri wa kamati ambayo hayajafanyiwa kazi inavyostahili. Kwa mfano, kamati ilishauri kuwa, Serikali ianzishe mamlaka mpya ya usimamizi wa Miradi ya Wizara hii, lakini Taarifa ya Wizara inaonesha kwamba,

hatua iliyofikiwa ni maandalizi ya andiko la kuanzisha chombo maalumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati haijaridhishwa na hatua hiyo kwa kuwa, imetimia miezi nane tangu ushauri kutolewa na Wizara kuendelea kuwa kwenye andiko. Athari yake ni kusababisha fedha za Serikali kupotea, miradi kutokuwa na tija na wananchi kutokunufaika na miradi hiyo kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Maduhuli. Matokeo ya uchambuzi huu yanaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara hii yamepungua kwa 14.5% ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(ii) Kutokana na mwenendo wa ukasanyaji wa maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 halina uwezokano wa kutimizwa. Sababu za mtazamo huu hadi kufikia kipindi cha takribani 66% ya muda wa utekelezaji, lengo lililofikiwa kwa 42.4% tu. Kasi hiyo ya ukusanyaji ilikuwa nyuma kwa lengo kwa 24%, lakini punguzo la lengo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 halifiki 24%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida makadirio ya jumla ya bajeti ya nchi huzingatia makadirio ya makusanyo kwa sekta moja moja. Uwekaji wa lengo la makusanyo usiyozingatia uhalisia unaweza kuathiri uhalisia wa bajeti ya matumizi. Kwa msingi huo kamati ina maoni kuwa, ni vizuri kila sekta inapokadiria ukusanyaji wa maduhuli izingatie uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madirio ya Matumizi ya Kawaida. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio yamepungua kwa asilimia mbili ulinganisha na mwaka unaoisha.

(ii) Kutokana na uzoefu wa upatikanaji wa fedha wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaokwisha kiasi cha fedha kinachodaliwa kwa matumizi ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 kinaweza kisipatikane kama kilivyoombwa.

(iii) Makadirio ya matumizi kwa Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi yamejumuishwa katika Fungu moja (Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi). Uzoefu huu ni tofauti kabisa na Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambapo kila sekta ilikuwa ina fungu linalojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati ilizingatia maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kubaini kuwa, bajeti ya Wizara hii ilipaswa kuendelea kuongezwa. Sababu yake ni kuwa, ilani ilitambua umuhimu wa kuongeza tija katika ufugaji na uvuvi, kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi, hata hivyo uchambuzi umeonesha tofauti na matarajio hayo ya Ilani. Maoni ya Kamati ni kwamba, Sekta ya Uvuvi na Mifugo zinapaswa kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Matumizi na Maendeleo. Kamati ilichambua Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo na kubaini mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yameongezeka kwa 79% ikilinganishwa na Mwaka 2023/2024.

(ii) Utegemezi wa vyanzo vya nje vya bajeti ya maendeleo katika Wizara hii umeongezeka kwa 17% ukilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika mwaka wa

fedha unaoisha 15% ya bajeti ya maendeleo ilikuwa ni fedha za nje, lakini kwa Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, 32% ya Bajeti ya Maendeleo ni fedha za nje.

(iii) Pamoja na kuwa uhakika wa upatikanaji wa fedha za nje kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulithibitika kuwa mdogo, ongezeko la uwiano wa fedha za nje haliendani na uhalisia uliojitokeza katika utekezaji wa bajeti ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kwa mfano, Sekta ya Mifugo ilipokea 0.7% ya makadirio ya fedha za nje.

(iv) Uzoefu wa jumla wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha unaoisha ulionyesha kuwa, katika kipindi cha utekelezaji cha 66% Wizara ilipata fedha za maendeleo kwa kiasi cha 41% tu ya makadirio. Kwa hali hiyo uzoefu unaonyesha kuwa, upatikanaji wa fedha umekuwa mgumu kwa 25%, hali hiyo inathibisha kuwa ongezeko la bajeti kwa 79% linaweza lisiwe na uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa matokeo hayo makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yana sura ya kuongeza ufanisi katika sekta hizo. Hata hivyo iwapo changamoto ya upatikanaji wa fedha iliyojitokeza katika mwa fedha ulioisha haitapatiwa ufumbuzi, makadirio haya yanaweza yasiwe na maana. Kamati ina maoni kuwa, upo umuhimu wa Serikali kuongeza mkazo katika upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo chini ya sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ili kubaini matokeo ya bajeti yaliyojadiliwa katika Fungu 99, Kamati ilifanya mapitio ya maeneo ya vipaumbele katika Bajeti ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na mapitio hayo Kamati ilibaini kuwa:-

(i) Maeneo yote ya vipaumbele yaliyobainishwa na Wizara yanaendana na mwelekeo wa nchi na mahitaji ya jamii.

(ii) Iwapo vipaumbele hivyo vitazingatiwa ipasavyo, Sekta ya Mifugo na Uvuvi zitaongeza mchango katika Uchumi wa Taifa, maendeleo ya nchi na ustawi wa watu nchini.

(iii) Iwapo upatikanaji wa fedha zitakazoidhinishwa kutokana na makadirio hayo utakuwa wa kusuasua, vipaumbele hivyo vitabaki na muonekano unaovutia, lakini usiokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, kwa vipaumbele hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inastahili pongezi kubwa kwa nia yake ya kuboresha sekta hiyo. Aidha, Serikali kwa ujumla wake inahitaji kuzingatia umuhimu wa vipaumbele hivyo, ili kuboresha zaidi Sekta ya Uvuvi na Mifugo kwa lengo la kupata mchango mkubwa katika uchumi wa nchi. Kwa mtazamo huo, ipo haja ya kusisitiza zaidi upatikanaji wa fedha zinazoombwa wakati wa utekelezaji. Mbali na hivyo, mchango wa sekta hizo utakuwa wa mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Madhumuni ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kuliwezesha Bunge kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa namna yenye manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Jumla. Maoni na ushauri katika sehemu hii unatokana na kuzingatia vipaumbele vilivyobainishwa na Wizara kwa kulinganisha na hali halisi ya Sekta. Kwa msingi huo kamati ina maoni yafuatayo:-

(a) Wingi wa tozo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi unakwamisha maendeleo ya Sekta hizi nchini na kusababisha maisha ya wafugaji na wavuvi kuendelea kuwa duni. Ili kutatua changamoto hiyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kupunguza tozo ambazo ni kero na vikwazo kwa maendeleo ya Sekta hii na kusababisha umasikini kwa wafugaji na wavuvi. *(Makofi)*

(b) Mtiririko usioridhisha wa fedha kutoka HAZINA, hususan fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, unakwamisha utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo mradi wa *BBT* (Mifugo na Uvuvi). Ili kukabiliana na changamoto hii Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Wizara hii zinapatikana kwa wakati. *(Makofi)*

(c) Utaratibu wa kuanzisha miradi mingi kwa pamoja na kushindwa kuikamilisha na usimamizi hafifu wa utekelezaji unachangia matokeo yasiyoridhisha ya miradi katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Ili kukabiliana na changamoto hii Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali iweke na kuzingatia vipaumbele katika utekelezaji wa miradi ili ikamilike kwa wakati na kuepuka ongezeko la gharama za miradi;

(ii) Iandaliwe mikakati ya kusimamia miradi kikamilifu ili tija iliyokusudiwa ipatikane;

(d) Kukosekana kwa Mamlaka za Usimamizi wa Utekelezaji wa Miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni jambo linalochangia kuzorota kwa Sekta hizo. Aidha, hali hiyo imepunguza mchango wa Sekta za Uvuvi na Mifugo katika Pato la Taifa, ustawi wa watu na maendeleo kwa ujumla. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri kwamba, Serikali ikamilishe mchakato wa kuanzisha Mamlaka Mpya ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri Maalum wa Kamati Kisekta (Sekta ya Mifugo). Katika Sekta ya Mifugo kamati ina maoni na ushauri kama iufuatavyo:-

(a) Utoroshwaji wa Mifugo kwa njia za panya ni jambo lisilofaa kwa uchumi wa nchi. Hali hiyo inaikosesha Serikali mapato na kuvuruga takwimu muhimu, kwa ajili ya

mipango ya nchi. Ili kukabiliana na tatizo hilo, kamati inashauri kwamba:-

(i) Minada ya mifugo ijengwe katika maeneo ya mipakani na iwekewe ulinzi, ili kudhibiti utoroshwaji wa mifugo kwenda nje ya nchi.

(ii) Ushuru unaotozwa katika minada ya mifugo ufanyiwe mapitio kwa lengo la kubaini kiwango cha ushuru kinachoweza kuwavutia wafugaji kuuza mifugo yao kwenye minada hiyo.

(iii) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kwamba, Halmashauri nchini zinaweka mikakati ya kulinda maeneo yote ya mipaka, ili kuzuia utoroshwaji wa mifugo. Aidha, Halmashauri za Wilaya na Vijiji zinufaike na mapato yanayotokana na minada iliyopo kwenye maeneo yao.

(iv) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, isukume mazungumzo miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kukubaliana namna bora ya kutumia minada ya mifugo ya mipakani.

(b) Uhaba wa malisho hasa kipindi cha ukame unaathiri mifugo na kusababisha Wafugaji walazimike kutafuta malisho kwa kuhamahama. Hali hii inachangia kupoteza ubora wa mifugo, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na uharibifu wa mazingira. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri kwamba:-

(i) Serikali iongeze bajeti, kwa ajili ya uanzishwaji wa maeneo ya mashamba ya malisho na mbegu za malisho.

(ii) Miundombinu ya mashamba ya mbegu na malisho iboreshwe, ili kuongeza tija katika

uzalishaji. Aidha, barabara zinazofika kwenye mashamba ya mbegu ya malisho ziboreshwe, ili ziweze kupitika wakati wote.

(iii) Serikali itengeneze miundombinu ya kukaushia malisho katika mashamba, ili kudhibiti upotevu. Sambamba na hilo, maghala ya kuhifadhia malisho baada ya kuvunwa yajengwe na kuendelezwa na Serikali ijenge miundombinu ya umwagiliaji, ili kuhamasisha na kuongeza uzalishaji wa malisho hasa kipindi cha kiangazi.

(c) Kutofanyika kwa utambuzi wa mifugo, kunasababisha dosari katika udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, uimarishaji wa usalama wa chakula, dosari za udhibiti wa biashara ya mifugo na mazao yake na udhibiti duni wa wizi wa mifugo. Ili kutatua tatizo hili, Kamati inashauri kwamba, Serikali ifanye utambuzi (sensa), ili kujua takwimu sahihi za aina, idadi, mtawanyiko na taarifa nyingine muhimu zinazohusu mifugo nchini. Aidha, Serikali ihakikishe inasimamia utoaji wa chanjo ya mifugo nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi; katika Sekta ya Uvuvi Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(a) Uhaba wa samaki katika bahari, maziwa, mabwawa na mito unasababishwa kwa kiasi kikubwa na uvuvi haramu ambao unaathiri mazalia na biashara ya samaki nchini. Ili kukabiliana na changamoto hii, kamati inashauri kuwa, Serikali iwahamasishe wadau na Sekta binafsi kushiriki katika udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya samaki.

(b) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa (*post-harvest losses*) unakadiriwa kufikia 30% hadi 40%, hususan katika maeneo ya vijijini. Upotevu huu umesababisha Sekta hii kutochangia ipasavyo katika Pato la Taifa tofauti na ukubwa wake. Kamati inashauri kuwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itoe elimu ya namna ya kuhifadhi mazao

ya uvuvi baada ya kuvunwa. Aidha, Wizara ijenge miundombinu ya kuhifadhia samaki kama vile vituo vya kuzalisha barafu katika maeneo ya uvuvi. *(Makofi)*

(c) Sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu yanapotea kutokana na ukosefu wa nyenzo za uvuvi katika eneo hilo. Aidha, njia ya kukabiliana na ukosefu wa nyenzo kwa kutoa leseni kwa meli za kigeni inaongeza upotevu wa mapato. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kununua meli nne za uvuvi, ili zisaidie kufanya uvuvi kwenye eneo la bahari kuu na kuongeza mapato ya nchi.

(ii) Serikali iendelee kuimarisha doria za mara kwa mara kwenye eneo la uvuvi la bahari kuu, ili kudhibiti uvuvi haramu.

(iii) Serikali ishirikishe Sekta Binafsi na kuiwekea mazingira rafiki, kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya uchakataji na usindikaji wa mazao ya uvuvi, ili kukuza mchango wa Sekta hii katika Pato la Taifa.

(iv) Serikali iongeze bajeti ya *TAFICO* na kuwezesha kupata watumishi wa kutosha, ili Shirika hilo liweze kutekeleza majukumu yake inavyostahili.

(v) Uhaba wa vifaranga vya samaki na chakula bora cha samaki nchini unarudisha nyuma juhudi za Serikali kuhamasisha wananchi kujikita katika ufugaji wa Samaki. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, kamati inashauri kwamba, Serikali ishirikishe Sekta Binafsi katika uzalishaji wa chakula na vifaranga vya samaki kwa gharama nafuu, ili kusaidia kuhamasisha wananchi hasa vijana kujikita katika ufugaji wa samaki wa vizimba, kupunguza tatizo la ajira na kuongeza pato kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Kama inavyofahamika kwamba, Sekta za Mifugo na Uvuvi ni za uzalishaji ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa Sekta ya Viwanda. Aidha, Katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Ibara ya 9(C), Ukurasa wa 7, Serikali iliahidi kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi, ili kuweka uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Ibara ya 43 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ukurasa wa 54, Serikali imeahidi kuimarisha Sekta ya Uvuvi kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu, ili iweze kuhimili ushindani na kuifanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuachana na uagizaji kutoka nje pamoja na kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mifugo inachangia asilimia saba ya pato la Taifa. Pato hilo linatokana na uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Vilevile, Sekta ya Uvuvi inachangia takribani 1.8% ya pato la Taifa. Zaidi ya Watanzania milioni 4.5 wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na shughuli mbalimbali zikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na baba na mama lishe. Aidha, Sekta ya Uvuvi huchangia 30% ya protini yote inayotokana na mazao ya wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, endapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi itapewa fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya uwekezaji kikamilifu na kutumia vizuri rasilimali nyingi zilizopo nchini, Wizara hii ina uwezo wa kufanikisha mipango mbalimbali ya Serikali na kutengeneza faida ikilinganishwa na gharama zitakazowekezwa, hali itakayopelekea fafugaji kunufaika na mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao, natamani kuwatambua kwa majina, lakini kwa kuzingatia ufinyu wa muda, naomba yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika kwa kuniamini kuweza kuwasilisha Taarifa hii kwa niaba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mbunge), Naibu Waziri, Mheshimiwa Alexander Mnyeti (Mbunge), kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha kutekeleza majukumu yake. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Riziki Shemdoe, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Kamati kwa kuhakikisha sekta za mifugo na uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa Shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**14 MEI, 2024**

# TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu Msingi wa Uchambuzi, Muundo wa taarifa na njia zilizotumika kutekeleza jukumu la kushughulikia bajeti hii;

(ii) Sehemu ya Pili inatoa maelezo kamili kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri kutokana na uchambuzi na kuhitimisha maudhui ya Taarifa hii.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi na Uwasilishaji wa Taarifa Hii

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6(1)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka masharti yaliyoitaka Kamati kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, yaliitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024 ili kulinganisha na Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Kamati za Kisekta kuchambua Taarifa za Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, shughuli ya Bunge kujadili hoja hii leo imestahili kutanguliwa na uchambuzi kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 184 (5) ya Kanuni za Bunge, Waziri Mtoa Hoja na Kamati hii tulitakiwa kuweka mezani nakala ya Taarifa zinazohusika kabla ya kuanza mjadala. Nafurahi kwamba, mapema asubuhi, nakala ya Taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Aidha, Kanuni ya 184 (6) ya Kanuni za Bunge imetaka maoni ya Kamati yatolewe Bungeni baada ya Waziri anayehusika kuwasilisha hotuba yake. Ninashukuru kwamba, kwa sasa, tumepewa nafasi ya kuiwasilisha Taarifa hii ili iweze kuzingatiwa na Bunge wakati wa kujadili hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi na Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaoripotiwa katika Taarifa hii unagusa utekelezaji wa bajeti katika Mafungu mawili; **Fungu 99** Sekta ya Mifugo na **Fungu 64** Sekta ya Uvuvi kwa mwaka 2023/2024. Aidha, kwa upande wa Makadirio kwa mwaka wa fedha 2024/2025 uchambuzi umefanyika kwa **Fungu 99** - Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Hali hiyo imezingatia uamuzi wa Serikali wa kuunganisha Makadirio ya Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi chini ya **Fungu moja 99** – Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla wake, uchambuzi huu umegusa mambo makuu yafuatayo:-

(i) Hali ya jumla ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(ii) Tathmini ya jumla ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati;

(iv) Tathmini ya Ukusanyaji wa maduhuli; na

(v) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) iliyotaka matokeo ya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti yatumike kufanya ulinganisho na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo uliiwezesha Kamati kupata mambo ya kuzingatia kuhusu hoja inayojadiliwa leo.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 MAELEZO KAMILI KUHUSU UCHAMBUZI NA TATHMINI
### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Mifugo na

Uvuvi. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 21 Machi, 2024 Kamati ilikutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika maelezo hayo Kamati ilibaini mambo mbalimbali kuhusu ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa majukumu, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

#### 2.2.1 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, **Sekta ya Mifugo** - Fungu 99 ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 42,105,000,000**. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 17,330,279,726** sawa na **asilimia 41.16** ya lengo la makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta ya Uvuvi Fungu 64 lengo lilikuwa ni kukusanya jumla ya **Shilingi 41,000,000,000** kutoka vyanzo mbalimbali kama vilivyobainishwa katika Taarifa. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 17,897,169,912.78** ambayo ni sawa na **asilimia 43.7** ya lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua maduhuli hayo kwa kila fungu ili kujiridhisha na juhudi za ukusanyaji wa maduhuli. Matokeo ya uchambuzi yanaonekana katika **Kielelezo Na. 1**.

**Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli 2023/2024**

| Fungu | Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2023/2024 | Makusanyo ya Maduhuli hadi Kufikia Februari, 2024 | Asilimia ya Makusanyo |
|---|---|---|---|
| **Fungu 99** – Sekta ya Mifugo | **42,105,000,000** | **17,330,279,726.00** | 41.16 |
| **Fungu 64**- Sekta ya Uvuvi | 41,000,000,000 | 17,897,169,912.78 | 43.7 |
| **JUMLA KUU** | **83,105,000,000** | **35,227,449,639** | **42.4** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu 99 na Fungu 64*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(i) Jumla ya makusanyo ya maduhuli hadi kufikia Februari, 2024 yamefikia **asilimia 42.4** ya lengo;

(ii) Sekta ya Mifugo iliyokadiriwa kuchangia **asilimia 51** ya makusanyo ya Wizara imechangia **asilimia 49**; na

(iii) Sekta ya Uvuvi iliyokuwa imekadiriwa kuchangia **asilimia 49** ya makusanyo imechangia **asilimia 51**;

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya ukusanyaji wa maduhuli inaonesha kuwa ni vigumu kwa Wizara kufikia lengo lililowekwa la ukusanyaji wa maduhuli. Aidha, pamoja na ukusanyaji usio na mwelekeo wa kufikia lengo, Sekta ya Uvuvi imejitahidi ikilinganishwa na Sekta ya Mifugo.

### 2.2.2 Mwenendo na Mtiririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa kiasi cha **Shilingi 194,335,967,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **Shilingi 165,274,198,000.00**; na Fedha za Nje ni **Shilingi 29,061,769,000.00**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2024, Wizara ilipokea **asilimia 41.56** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hiyo inaonesha kuwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi hicho ulikuwa nyuma kwa **asilimia 58.4. (Kielelezo Na. 2).**

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo na mtririko wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2023/2024**

| MTIRIRIKO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO HADI FEBRUARI, 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **MIRADI** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2023/2024** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2024** | **Asilimia ya Fedha zilizopokelewa** |
| Fedha za Ndani | **165,274,198,000.00** | **80,820,027,430.46** | **41.56** |
| Fedha za Nje | **29,061,769,000.00** | | |
| **Jumla** | **194,335,967,000.00** | | |

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo, ni wazi kuwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa na Serikali kupitia Wizara hii haiwezi kufikiwa. Hali hii sio nzuri na inaweza kusababisha Sekta ya Mifugo na Uvuvi kushindwa kuchangia vyema katika pato la Taifa, kukuza ajira na kupunguza umasikini miongoni wa Watanzania waliojiajiri kupitia Sekta hizi.

**2.2.3 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa mitatu (3) ya Tanga, Dar es Salaam na Pwani na kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Miradi hiyo ni: -

(i) Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo katika mpaka wa Horohoro, Tanga (Mradi Na. 4486);

(ii) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi Tanzania -(TAFICO); na

(iii) Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo lililopo Vikuge, Kibaha Mkoa wa Pwani.

**2.2.4 Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo, Horohoro, Tanga (Mradi Na. 4486)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo, Horohoro, Tanga una thamani ya **Shilingi 563,079,225.12**. Mradi unalenga kudhibiti utoroshaji wa mifugo kwenda nchi jirani kupitia Mpaka wa Horohoro pamoja na kuimarisha biashara ya mifugo nchini. Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa mnada huo umeanza kutumika kuanzia mwezi Septemba, 2023, ambapo hadi sasa umechangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha **Shilingi 9,428,650**. Aidha, idadi ya mifugo iliyouzwa katika mnada huo ni **809** ikijumuisha ngómbe **359**, mbuzi na kondoo **450**. Vile vile mifugo **278** imesafirishwa kwenda nje ya nchi ikiwemo ngómbe **134** na mbuzi **144**.

**2.2.5 Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya TAFICO Makao Makuu ulihusisha ununuzi wa mtambo wa barafu, ujenzi wa kibanda na ununuzi wa kengevuke. **Shilingi 1,000,000,000.00** zimeidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, hadi sasa mradi umetekelezwa kwa **asilimia 49.** Mradi huu unalenga kuongeza ajira na mapato ya fedha za ndani na za kigeni yatakayowezesha kukuza pato la Taifa. Pamoja na hayo, TAFICO inatarajiwa kuongeza uhamasishaji wa Sekta Binafsi ili kuwekeza zaidi katika uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji, uchakataji pamoja na mauzo ya mazao ya uvuvi hapa nchini kwa kutumia mbinu na teknolojia za kisasa.

**Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji huu ni muhimu kwa kuwa utaiwezesha nchi kunufaika na rasilimali za uvuvi zilizopo katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Miliki (*Exclusive Economic Zone-EEZ*) na Bahari Kuu. Kwa sasa uvuvi kutoka eneo letu la EEZ unafanywa na meli za kigeni.

**2.2.6 Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo - Vikuge Mkoani Pwani**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mradi huu unalenga kuimarisha uzalishaji wa mbegu na malisho kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa mbegu na malisho kwa wafugaji.

**Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelezwa hadi sasa katika Mradi huu ni pamoja na kusafisha pori lenye ukubwa wa **hekta 175** kwa thamani ya **Shilingi 160,539,000.** Jumla ya **hekta 100** kati ya **175** zilisafishwa na kufikia **asilimia 65** ambapo Hati Na. 1 yenye thamani ya **Shilingi 84,063,200** iliwasilishwa Wizarani kwa ajili ya malipo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuzalisha mbegu na malisho (*hay and silage*) ili kuongeza upatikanaji wa malisho, kutoa elimu na kuwajengea uwezo wafugaji kuhusu namna bora ya kuzalisha na kuhifadhi. Aidha, mbegu na malisho yatakayozalishwa yatauzwa kwa wafugaji na wazalishaji binafsi ili kuuwezesha Mradi kujiendesha na kuufanya uwe endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo yameonesha mambo yafuatayo:-

**(a) Mradi wa Ujenzi wa Mnada wa Mifugo - Horohoro, Tanga (Mradi Na. 4486);**

(i) Kumekuwa na utoroshwaji wa mifugo_kwa kupitia njia za panya kwenda nchi Jirani ya Kenya. Aidha, bado idadi ya mifugo inayouzwa katika Mnada wa Horohoro ni ndogo, jambo linalopunguza mapato ya Serikali;

(ii) Ushuru wa mifugo kwenye Mnada wa Horohoro ni mkubwa ambapo ng'ombe mmoja anatozwa **Shilingi 30,000,** hali inayochochea utoroshwaji wa mifugo kupitia njia za panya;

(iii) Pamoja na Halmashauri ya Mkinga na Serikali ya Kijiji kutoa eneo la kujenga mnada bado hawanufaiki na mapato yanayotokana na mnada huo. Hali hii inatokana na utaratibu wa Serikali kuu kuchukua mapato yote yanayotokana na mnada;

(iv) Kukosekana kwa ulinzi katika eneo la mnada kunahatarisha usalama wa watu, mifugo na majengo wakati na baada ya shughuli za uuzaji wa mifugo;

(v) Kukosekana kwa majengo ya ofisi, Kituo cha Polisi na miundombinu ya maji katika eneo la mnada, kunahatarisha usalama na afya za watumiaji wa mnada huo; na

(vi) Pamoja na eneo la mnada kuwa kubwa, hakuna mpango wowote wa kuwa na malisho ya mifugo wakati wafugaji wakiwa wanasubiri kuuza mifugo yao.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto hizo ni dhahiri kuwa lengo la Mradi kuimarisha biashara ya Mifugo na kuongeza mapato haliwezi kufikiwa. Kamati ina maoni kwamba, changamoto hizo zinapaswa kutatuliwa.

**(b) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Shirika la Uvuvi - TAFICO**

(i) Baadhi ya majengo ya TAFICO yaliyo pembezoni mwa Bahari yako hatarini kuanguka kutokana na maji kula kingo za ardhi;

(ii) TAFICO kukabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo na upungufu wa zana za kutosha kama vile meli za uvuvi; na

(iii) Mtiririko usioridhisha wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hali hiyo inasababisha kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ni vigumu kwa Taasisi hiyo kufikia dira yake ya kuwa Kituo Bora cha Utafiti na Ushauri Elekezi katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika. Aidha, TAFICO haitoweza kuendeleza uvuvi wa kibiashara na Sekta ya Uvuvi nchini kama ilivyokusudiwa.

**(c) Mradi wa Shamba la Malisho ya Mifugo - Vikuge Mkoani Pwani**

(i) Ukosefu wa miundombinu ya kukaushia na kuhifadhia mbegu za malisho, hali inayosababisha upotevu wa malisho na mbegu kuharibika;

(ii) Ukosefu wa miundombinu ya kuhifadhia malisho baada ya kuvunwa na kabla ya kuuzwa kwa wanunuzi, hali inayochangia hasara kutokana na malisho kuharibika;

(iii) Ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji, hali inayosababisha shamba kupunguza uzalishaji hasa kipindi cha kiangazi; na

(iv) Uchakavu wa mitambo/vifaa ikiwemo trekta, mashine za kukata majani (*mower*), *bailer, hay rake,* hali inayoathiri ufanisi na tija katika shamba hilo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo, tija ya mradi na manufaa kwa wafugaji hayawezi kupatikana inavyostahili. Kamati ina maoni kuwa, ipo haja ya kuongeza usimamizi wa Mradi huu kwa lengo la kusaidia manufaa makubwa kwa wafugaji. Aidha, Serikali itapaswa kutoa fedha za utekelezaji wa Mradi huu ili kuendelea kupata tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, Kamati inapongeza jitihada za Serikali za kuendelea kuwafikishia wananchi miradi mbalimbali

ambayo ina lengo la kutatua changamoto zinazowakabili hasa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

### 2.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Sekta za Mifugo **(Fungu 99)** na Uvuvi **(Fungu 64)** zilitengewa jumla ya **Shilingi 292,520,933,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyofafanuliwa kwenye **Kielelezo Na. 3**.

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2024**

| **UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA FUNGU (99&64) HADI FEBRUARI, 2024** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha Iliyotengwa kwa Mwaka 2023/2024** | **Fedha Iliyopokelewa hadi Kufikia Februari, 2024** | **Asilimia ya Fedha zilizopokelewa** |
| Mishahara | 39,308,758,000.00 | 20,800,000,000.00 | 52.91 |
| (OC) | 58,876,208,000.00 | 17,050,000,000.00 | 28.86 |
| **Jumla** | **98,184,966,000.00** | **37,850,000,000.00** | **38.55** |

***Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Sekta ya Mifugo - Fungu 99 na Sekta ya Uvuvi - Fungu 64***

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:-

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilipokea **asilimia 38.55** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Matumizi ya Kawaida;

(ii) Pamoja na kuwa Sekta ya Uvuvi ilikadiriwa asilimia 49 ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara, lakini Sekta hiyo

ilipokea asilimia 30 ya fedha zilizopokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida; na

(iii) Sekta ya Mifugo iliyokadiriwa kupata fedha za matumizi ya kawaida, imepata **asilimia 69** ya fedha kidogo za Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha, Sekta zote mbili yaani Sekta ya Uvuvi na Sekta ya Mifugo hazitarajiwi kukamilisha majukumu yake yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Pamoja na kuwa mwenendo wa jumla unaonesha hali ngumu ya upatikanaji wa fedha, Sekta ya Uvuvi imekabiliwa na hali ngumu zaidi ikilinganishwa na Sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo inahatarisha mchango wa Sekta hizo katika Uchumi wa Taifa. Aidha, hali hiyo inaathiri ustawi wa watu ambao shughuli zao kuu za uchumi zimeegemea katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kamati ina maoni kuwa upo umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa fedha zilizobaki kwa ajili ya Sekta hizo zinapatikana kabla ya tarehe 1 Julai, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri fedha zilizoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa wakati ili utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Mifugo na Uvuvi ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa.

**2.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya Ushauri. Mfano wa Ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu uendeshaji wa Vituo vya BBT na ufugaji bora wa kisasa. Taarifa za Wizara zilionesha kuwa Vituo vya BBT vimeanzishwa na Vijana waliopo katika Vituo hivyo wanafundishwa mbinu za ufugaji bora ili kuzalisha mifugo inayokidhi mahitaji ya soko la ndani na la nje.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri, yapo maeneo mengine ya ushauri wa Kamati hayajafanyiwa kazi inavyostahili. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa Serikali ianzishe Mamlaka mpya ya Usimamizi wa Miradi ya Wizara hii lakini taarifa ya Wizara inaonesha kwamba, hatua iliyofikiwa ni maandalizi ya andiko la kuanzisha Chombo Maalum.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijaridhishwa na hatua hiyo kwa kuwa ilitimia miezi isiyopungua nane tangu ushauri kutolewa na Wizara kuendelea kuwa kwenye andiko. Athari yake ni kusababisha fedha za Serikali kupotea, miradi kutokuwa na tija na wananchi kutonufaika na miradi hiyo kama ilivyokusudiwa.

**2.5 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Mifugo na Uvuvi - **Fungu 99** imekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 kama ifuatavyo: -

**2.5.1 Makadirio ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa Makadilio ya Maduhuli yaliyopangwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi - **Fungu 99.** Ili kujenga msingi wa maoni na ushauri kuhusu Maduhuli, Kamati ilichambua maduhuli hayo kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara hii yamepungua kwa **asilimia 14.56** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024;

(ii) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024, lengo linalowekwa

kwa mwaka wa fedha 2024/2025 halina uwezekano wa kutimizwa. Sababu za mtazamo huo hadi kufikia kipindi cha takribani **asilimia 66** ya muda wa utekelezaji, lengo lilifikiwa kwa **asilimia 42.4** tu. Kasi hiyo ya ukusanyaji ilikuwa nyuma ya lengo kwa **asilimia 24** lakini punguzo la lengo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 halifiki **asilimia 24**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kawaida makadirio ya jumla ya bajeti ya nchi, huzingatia makadirio ya makusanyo kwa Sekta moja moja. Uwekaji wa lengo la makusanyo usiozingatia uhalisia unaweza kuathiri uhalisia wa bajeti ya matumizi. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kuwa, ni vizuri kila Sekta inapokadiria ukusanyaji wa maduhuli izingatie uhalisia.

### 2.5.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha majukumu ya Wizara, makadirio ya Bajeti kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ni jambo muhimu. Kutokana na hivyo, Kamati ilichambua makadirio ya Matumizi ya **Fungu 99** – Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio yamepungua kwa **asilimia 2** ukilinganisha na mwaka unaoisha;

(ii) Kutokana na uzoefu wa upatikanaji wa fedha wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaokwisha, kiasi cha fedha kinachokadiriwa kwa matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 kinaweza kisipatikane kama inavyoombwa; na

(iii) Makadirio ya matumizi kwa Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi yamejumuishwa katika Fungu moja – **Fungu 99** - Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Uzoefu huu ni tofauti kabisa na mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo kila Sekta ilikuwa na Fungu linalojitegemea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kubaini kuwa bajeti ya Wizara hii ilipaswa kuendelea kuongezwa. Sababu yake ni kuwa, Ilani ilitambua umuhimu wa kuongeza tija katika ufugaji na uvuvi kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha tofauti na matarajio hayo ya Ilani. Ni maoni ya Kamati kwamba, Sekta ya Uvuvi na Mifugo zinapaswa kupewa kipaumbele.

### 2.5.3 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, uendelezaji wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi kwa kiasi kikubwa unategemea bajeti inayopangwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo chini ya sekta hizo. Kwa madhumuni ya kupata mwelekeo katika Sekta hizo, Kamati ilichambua makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo na kubaini mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yameongezeka kwa **asilimia 79** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024;

(ii) Utegemezi wa vyanzo vya nje kwa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii umeongezeka kwa **asilimia 17** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha unaoisha **asilimia 15** ya bajeti ya maendeleo ilikuwa ni fedha za nje lakini kwa mwaka 2024/2025 **asilimia 32** ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje.

(iii) Pamoja na kuwa uhakika wa upatikanaji wa fedha za nje kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulithibitika kuwa mdogo, ongezeko la uwiano wa fedha za nje haliendani na uhalisia uliojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya mwaka wa fedha wa 2023/2024. Kwa mfano, Sekta ya Mifugo ilipokea **asilimia 0.7** ya makadirio ya fedha za nje; na

(iv) Uzoefu wa jumla wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kuwa, katika kipindi cha utekelezaji cha **asilimia 66,** Wizara ilipata fedha za maendeleo kwa kiasi cha **asilimia 41** ya makadirio. Kwa hali hiyo, uzoefu umeonesha kuwa upatikanaji wa fedha umekuwa mgumu kwa **asilimia 25**. Hali hiyo inathibitisha kuwa ongezeko la bajeti kwa **asilimia 79** linaweza lisiwe na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo, makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yana sura ya kuongeza ufanisi katika Sekta hizo. Hata hivyo, iwapo changamoto za upatikanaji wa fedha zilizojitokeza katika mwaka wa fedha ulioisha hazitapatiwa ufumbuzi, makadirio haya yanaweza yasiwe na maana. Kamati ina maoni kuwa, upo umuhimu wa Serikali kuongeza mkazo katika upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo chini ya Sekta hizi.

### 2.5.4 Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** ili kubaini matokeo ya bajeti inayojadiliwa Fungu 99, Kamati ilifanya mapitio ya maeneo ya vipaumbele katika bajeti ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na mapitio hayo Kamati ilibaini kuwa:-

(i) Maeneo yote ya vipaumbele yaliyobainishwa na Wizara yanaendana na mwelekeo wa nchi na mahitaji ya jamii;

(ii) Iwapo vipaumbele hivyo vitazingatiwa ipasavyo, Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi zitaongeza mchango katika Uchumi wa Taifa, maendeleo ya nchi na ustawi wa watu nchini; na

(iii) Iwapo upatikanaji wa fedha zitakazoidhinishwa kutokana na makadirio hayo utakuwa wa kusuasua, vipaumbele hivyo vitabaki na mwonekano unaovutia lakini usiokuwa na tija.

**Mheshimiwa Spika**, kwa vipaumbele hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inastahili pongezi kwa nia yake ya kuboresha Sekta hiyo. Aidha, Serikali kwa ujumla wake inahitaji kuzingatia umuhimu wa vipaumbele hivyo ili kuboresha zaidi Sekta ya Uvuvi na Mifugo kwa lengo la kupata mchango mkubwa katika Uchumi wa nchi. Kwa mtazamo huo, ipo haja ya kusisitiza zaidi upatikanaji wa fedha zinazoombwa wakati wa utekelezaji, mbali na hivyo, mchango wa Sekta hizo utakuwa mashakani.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kuliwezesha Bunge kujadili Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa namna yenye manufaa kwa Taifa. Ili kufanikisha lengo hilo, Kamati imezingatia matokeo ya uchambuzi na tathmini na kutoa maoni na ushauri kwa namna mbili; ya kwanza ni maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali na ya pili ni maoni na ushauri kwa kila Sekta.

### 3.2 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, maoni na ushauri katika sehemu hii, unatokana na kuzingatia vipaumbele vilivyobainishwa na Wizara kwa kulinganisha na hali halisi ya Sekta. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kama ifuatavyo:-

(a) Wingi wa Tozo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi unakwamisha maendeleo ya Sekta hizo nchini na kusababisha maisha ya wafugaji na wavuvi kuendelea kuwa duni. Ili kutatua changamoto hiyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kupunguza tozo ambazo ni kero na vikwazo kwa maendeleo ya Sekta hizo na kusababisha umasikini kwa wafugaji na wavuvi;

(b) Mtiririko usioridhisha wa fedha kutoka hazina, hususan fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo umekwamisha utekelezaji wa miradi hiyo ukiwemo mradi wa BBT (Mifugo na Uvuvi). Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe kwamba Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Wizara hii zinapatikana kwa wakati;

(c) Utaratibu wa kuanzisha miradi mingi kwa pamoja na kushindwa kuikamilisha, na usimamizi hafifu wa utekelezaji unachangia matokeo yasiyoridhisha ya miradi kaitka Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Ili kukabiliana na changamoto hii Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali iweke na kuzingatia vipaumbele katika utekelezaji wa miradi ili ikamilike kwa wakati na kuepuka ongezeko la gharama za miradi;

(ii) Iandaliwe mikakati ya kusimamia miradi kikamilifu ili tija iliyokusudiwa ipatikane;

(d) Kukosekana kwa Mamlaka za Usimamizi wa Utekelezaji wa Miradi chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ni jambo linalochangia kuzorota kwa Sekta hizo. Aidha, hali hiyo inapunguza mchango wa Sekta za uvuvi na mifugo katika Pato la Taifa, ustawi wa watu na maendeleo kwa ujumla. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ikamilishe mchakatowa kuanzisha Mamlaka Mpya za Sekta za Mifugo na Uvuvi.

### 3.3 Maoni na Ushauri Maalum Kisekta

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutimiza jukumu lake la kuishauri Serikali, Kamati imezingatia tathmini ya jumla ya kila Sekta chini ya Wizara hii na kuilinganisha na hali halisi. Aidha, matokeo ya tathmini hiyo yanaisukuma Kamati kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

### 3.4 Sekta ya Mifugo

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Mifugo Kamati ina maoni na ushauri kama iufuatavyo:-

(a) Utoroshwaji wa Mifugo kwa njia za panya ni jambo lisilofaa kwa uchumi wa nchi. Hali hiyo inaikosesha Serikali mapato, na kuvuruga takwimu muhimu kwa ajili ya mipango ya nchi. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Kamati inashauri kwamba:-

(i) Minada ya mifugo ijengwe katika maeneo ya mipakani na iwekewe ulinzi ili kudhibiti utoroshwaji wa mifugo kwenda nje ya nchi;

(ii) Ushuru unaotozwa katika minada ya mifugo ufanyiwe mapitio kwa lengo la kubaini kiwango cha ushuru kinachoweza kuwavutia wafugaji kuuza mifugo yao kwenye minada hiyo;

(iii) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe kwamba Halmashauri nchini zinaweka mikakati ya kulinda maeneo yote ya Mipaka ili kuzuia utoroshwaji wa mifugo. Aidha, Halmashauri za Wilaya na Vijiji zinufaike na mapato yatokanayo na minada iliyopo kwenye maeneo yao.

(iv) Wizara ya Mifugo na Uvuvi, isukume mazungumzo miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kukubaliana namna bora ya kutumia minada ya mifugo ya mipakani.

(b) Uhaba wa malisho hasa kipindi cha ukame unaathiri mifugo na kusababisha Wafugaji walazimike kutafuta malisho kwa kuhamahama. Hali hii inachangia kupoteza ubora wa mifugo, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na uharibifu wa mazingira. Ili

kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kwamba:-

(i) Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya uanzishwaji wa maeneo ya mashamba ya malisho na mbegu za malisho;

(ii) Miundombinu ya mashamba ya mbegu na malisho iboreshwe ili kuongeza tija katika uzalishaji. Aidha, barabara zinazofika kwenye mashamba ya mbegu na malisho ziboreshwe ili ziweze kupitika wakati wote;

(iii) Serikali itengeneze miundombinu ya kukaushia malisho katika mashamba ili kudhibiti upotevu.

(iv) Sambamba na hilo, maghala ya kuhifadhia malisho baada ya kuvunwa yajengwe na kuendelezwa; na

(v) Serikali ijenge miundombinu ya umwagiliaji, ili kuhamasisha na kuongeza uzalishaji wa malisho hasa kipindi cha kiangazi;

(c) Kutofanyika kwa utambuzi wa mifugo, kunasababisha dosari katika udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, uimarishaji wa usalama wa chakula, dosari za udhibiti wa biashara ya mifugo na mazao yake na udhibiti duni wa wizi wa mifugo. Ili kutatua tatizo hilo, Kamati inashauri kwamba Serikali ifanye utambuzi (sensa) ili kujua takwimu sahihi za aina, idadi, mtawanyiko wake na taarifa nyingine muhimu zinazohusu mifugo nchini. Aidha, Serikali ihakikishe inasimamia utoaji wa Chanjo ya mifugo nchi nzima.

**3.4.1 Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Uvuvi Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Uhaba wa Samaki katika Bahari, Maziwa, Mabwawa na mito unasababishwa kwa kiasi kikubwa na Uvuvi Haramu

ambao unaathiri mazalia na biashara ya Samaki nchini. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri kuwa, Serikali iwahamasishe wadau na Sekta binafsi kushiriki katika udhibiti wa uvuvi na biashara haramu ya samaki;

(b) Upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa (*Post-harvest losses*), unaokadiriwa kufikia asilimia 30 hadi 40 hususan katika maeneo ya vijijini. Upotevu huu umesababisha Sekta hii kutochangia ipasavyo katika Pato la Taifa tofauti na ukubwa wake. Kamati inashauri kuwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi itoe elimu ya namna ya kuhifadhi mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa. Aidha, Wizara ijenge miundombinu ya kuhifadhia samaki kama vile vituo vya kuzalisha barafu katika maeneo ya uvuvi.

(c) Sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu yanapotea kutokana na ukosefu wa nyenzo za uvuvi katika eneo hilo. Aidha, njia ya kukabiliana na ukosefu wa nyenzo kwa kutoa leseni kwa meli za kigeni inaongeza upotevu wa mapato. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kununua meli nne za uvuvi ili zisaidie kufanya uvuvi kwenye eneo la bahari kuu na kuongeza mapato ya nchi;

(ii) Serikali iendelee kuimarisha doria za mara kwa mara kwenye eneo la Uvuvi la Bahari Kuu ili kudhibiti uvuvi haramu;

(iii) Serikali ishirikishe Sekta Binafsi na kuiwekea mazingira rafiki kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya uchakataji na usindikaji wa mazao ya uvuvi ili kukuza mchango wa Sekta katika Pato la Taifa;

(iv) Serikali iongeze bajeti ya TAFICO na kuliwezesha kupata watumishi wa kutosha ili Shirika hilo liweze kutekeleza majukumu yake inavyostahili; na

(v) Uhaba wa vifaranga vya Samaki na chakula bora cha samaki nchini unarudisha nyuma juhudi za Serikali kuhamasisha wananchi kujikita katika ufugaji wa Samaki. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali ishirikishe Sekta Binafsi katika uzalishaji wa chakula na vifaranga vya samaki kwa gharama nafuu ili kusaidia kuhamasisha wananchi hasa vijana kujikita katika ufugaji wa samaki wa vizimba, kupunguza tatizo la ajira na kuongeza pato la Taifa.

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, Sekta za Mifugo na Uvuvi ni za uzalishaji ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa Sekta ya Viwanda. Aidha, Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Ibara ya 9(C), ukurasa wa 7, Serikali iliahidi Kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula na kujitegemea kwa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika Ibara ya 43 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ukurasa wa 54, Serikali imeahidi kuimarisha Sekta ya Uvuvi kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili iweze kuhimili ushindani na kuifanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuachana na uagizaji kutoka nje pamoja na kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025) na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mifugo inachangia **asilimia 7** ya Pato la Taifa. Pato hilo linatokana na uzalishaji wa nyama ya ng`ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Vilevile, Sekta ya Uvuvi inachangia takribani **asilimia 1.8** ya pato la Taifa. Zaidi ya Watanzania **milioni 4.5** wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na shughuli mbalimbali zikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na Baba na Mama lishe. Aidha, Sekta ya

Uvuvi huchangia **asilimia 30** ya protini inayotokana na mazao ya wanyama.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, endapo Wizara ya Mifugo na Uvuvi itapewa fedha ya kutosha kwa ajili ya kufanya uwekezaji kikamilifu na kutumia vizuri rasilimali nyingi zilizopo nchini, Wizara hii ina uwezo wa kufanikisha mipango mbalimbali ya Serikali na kutengeneza faida ikilinganishwa na gharama zitakazowekezwa, hali itakayopelekea Wafugaji kunufaika na mifugo yao.

### 3.5 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao, natamani kuwatambua kwa kuwataja majina yao, lakini kwa kuzingatia ufinyu wa muda, naomba yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Deodatus Mwanyika, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Mzuzuri, Mb, - **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb
5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb
6. Mhe. Dkt. Christine Ishengoma, Mb
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb
10. Mhe. Dkt. Medard Kalemani, Mb
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb
17. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
18. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb

19. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
20. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
21. Mhe. Toufiq Salim Turky, Mb
22. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb
23. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb
24. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mhe. Abdallah Ulega (Mb) na Naibu Waziri - Mheshimiwa Alexander Mnyeti (Mb), kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha kutekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo yake wakiongozwa na Katibu Mkuu - Prof. Riziki Shemdoe, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kuhakikisha Sekta za Mifugo na Uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Deodatus Phillip Mwanyika
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

14 MEI, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Ulega akiwemo Mwenyekiti wa CCM Wilaya, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wote waliokuja kumtembelea Mheshimiwa Ulega simameni kwa ujumla, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyotangaza mwanzo kuna Maelezo ya Serikali kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Iddi Kassim. Mheshimiwa Mchengerwa.

## KAULI YA SERIKALI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 9 Mei, 2024 Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala alieleza masikitiko yake Bungeni kuhusu Maafisa wa Mapato wa Halmashauri ya Msalala kutoza wakulima ushuru wa mazao mashambani. Mheshimiwa Mbunge alieleza kuwa wafanyabiashara wanaobainika kutolipa ushuru wa mazao wamekuwa wakipewa adhabu kali na kupigwa na maafisa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uliagiza Ofisi ya Rais, TAMISEMI, itoe ufafanuzi kuhusiana na suala hili ambalo linasemekana kujitokeza katika halmashauri nyingine pia. Naomba kutoa ufafanuzi wa suala hili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru wa mazao hutozwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa mujibu wa Vifungu (6), (7), (8) na (9) vya Sheria hiyo, ushuru wa mazao ni moja ya vyanzo vya mapato vya Mamlaka za Miji, Halmashauri za Wilaya, Mamlaka za Miji Midogo na Halmashauri za Vijiji. Aidha kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ushuru huu unatozwa kwa asilimia tatu ya bei ya kununulia shambani kwa mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 inatamka kuwa, ushuru huu unalipwa kwa mnunuzi wa zao alilonunua kutoka kwa mkulima kwa kiwango cha asilimia tatu ya bei ya kununulia shambani. Endapo mfanyabiashara atanunua mazao hayo kutoka shambani kwa mkulima atapaswa kulipa ushuru huu katika eneo hilo, ambalo ununuzi umefanyika. Kadhalika ununuzi ukifanyika sokoni, ushuru utatozwa katika soko hilo. Aidha mazao yanapotoka nje ya halmashauri yanapaswa kuwa yamelipiwa ushuru huu. Endapo itabainika mfanyabiashara anayatoa mazao nje ya halmashauri pasipokuwa na risiti halali ya malipo ya ushuru, atapaswa kulipa ushuru wa mazao husika na faini. Aidha mkulima anayesafirisha mazao chini ya tani moja amesamehewa kulipa ushuru huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri waache mara moja kuwatoza wakulima iwapo mazao hayo yakatuwa chini ya tani moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kwa Wakuu wa Mkoa pia Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kusimamia sheria kwa kuzingatia maslahi mapana ya pande zote mbili (upande wa ununuzi na upande wa halmashauri). Halmashauri zetu zinapaswa kukusanya mapato na kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyoelezwa kwao lakini zifanye hivyo kwa kufuata misingi ya sheria, kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa. Aidha ni muhimu kwa wafanyabiashara watambue wajibu wao wa kulipa ushuru uliowekwa kwa mujibu wa sheria zetu. Hivyo, mikoa na wilaya iendelee kutoa elimu juu ya sheria na miongozo mbalimbali juu ya ukusanyaji wa ushuru wa mazao kwa wafanyabiashara waliopo kwenye maeneo yao, ili kuwe na uelewa wa pamoja wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitavumilia ukiukwaji wowote wa sheria na hatua kali zitachukuliwa kwa watumishi wote watakaokiuka taratibu na sheria katika ukusanyaji wa Mapato ya Serikali. Nalitaarifu Bunge lako Tukufu, watumishi

waliohusika na tukio hili tayari uchunguzi unaendelea na hatua zitaendelea kuchukuliwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaingia kwenye mjadala wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tunaanza na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe dakika 10.

Waheshimiwa Wabunge wale ambao hawajachangia kabisa watachangia kwa dakika 10, waliochangia mara mbili mpaka mara saba watachangia kwa dakika tano.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpembenwe unaanza kuchangia kwa dakika 10. Ajiandae Aeshi Khalfan dakika 10. Ajiandae Mheshimiwa Kunambi, dakika tano ana dharura na Mheshimiwa Aida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuwa mchangiaji wa kwanza katika bajeti hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kabla sijaanza kuchangia bajeti hii nichukue nafasi kuwapa pole Wananchi wangu wa Jimbo la Kibiti na wale wajomba zangu wa Rufiji kwa kadhia ya mafuriko ambayo imetukuta. Pia naomba niwaambie tu wananchi hawa wawe na subira kwani *inna-llaha kana `aliiman hakiima* (hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na yeye ndio mwenye hekima). Kwa hiyo, niwaombe wananchi wawe na subira, Serikali ipo kazini na inaendelea kuwashughulikia wananchi hawa ambao wamepatwa na mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya ndani ya nchi hii. Vilevile, kwa kazi ambayo anaendelea kuifanya katika sekta hii. Mheshimiwa Rais amefanya mabadiliko makubwa sana, tunaona uwekezaji wa hali ya juu

sana ambao umeendelea na unaendelea kufanyika. Mfano mzuri upo kwa ndugu yangu, Mheshimiwa Kassinge kule Kilwa. Hivi sasa ninavyozungumza inaenda kujengwa bandari nzuri sana ya uvuvi ambayo inakwenda kuwa bandari ya kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila katika Quran pale, kuna aya inasema kwamba; "*Innallah yarzuqu man yashaau bighairi hisaab*" (Mwenyezi Mungu anamruzuku mambo binadamu bila hesabu yoyote). Mambo haya ameruzukiwa mdogo wangu Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega. Mheshimiwa Ulega ni mbunifu, mchapakazi na anataka matokeo. Haya ni mambo ambayo Mwenyezi mungu amemruzuku. Ndugu yangu hongera sana na naimani sana kwamba wewe ni *institutional memory* katika sekta hii na unakwenda kufanya mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya na kumsaidia ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega. Mheshimiwa Ulega naomba tu nikwambie unatuheshimisha Kaka zako wa Pwani, fanya kazi sisi tuko *very much proud of you. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili tu ya kuchangia katika bajeti hii. Jambo la kwanza linahusiana na masuala mazima ya uwezeshwaji wa vijana katika suala zima la mambo ya kiuchumi hasa katika kuweza kupewa boti. Ndugu yangu, Mheshimiwa Ulega kazi kubwa unaifanya na mimi sina shida wataalamu wako wanakusaidia ipasavyo. Katika mambo ya kutoa boti kwa vijana, Mheshimiwa Ulega mimi nikuombe tu, pale kwa kaka yako Kibiti kuna Kata ya Salale, Kiongoroni, Mbuchi, Msala. Maeneo haya pamoja na Kata ya Mtunda kule chini, haya ni maeneo ya *delta* na wewe unajua sisi tumeathirika kikubwa sana na mambo haya ya mafuriko. Vijana wale hivi sasa mazingira ya kimaisha siyo rafiki. Maeneo yetu ya kilimo wewe mwenyewe unayajua. Kwa hiyo, mimi nikuombe sana tengeneza mpango uliokuwa na uhalisia huku ukiwa unajua kabisa kwamba, kuna wajomba na kaka zako katika Jimbo la Kibiti na pale Rufiji

ambao tumeathirika kwa kiasi kikubwa sana na mambo haya ya mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, wakati anakuja ku-*wind up* hapa utoe tamko maana kuna wababaishaji wanapita pita kule Rufiji na Kibiti, wananza kuwaambia watu sijui wekeni vikundi, changieni hela zinakuja boti, Mheshimiwa Waziri hiki kitu hakikubaliki. Nikuombe sana waambie wananchi wajue kwamba, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan yuko kazini lengo lake ni kuwawezesha wananchi kiuchumi hasa hawa vijana. Kama kuna *agent* mmewaweka huko chini basi mtuambie sisi Wabunge. Mimi ninavyojua sisi tuna vikundi viko tayari. Mheshimiwa Waziri mimi nilishakukabidhi na vijana hawa wanasubiri tu kauli yako useme Kibiti kuna mgao gani? Rufiji kuna mgao gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anisamehe sana nikiwa naitajataja Rufiji wala usishangae, maana sisi Kibiti tumejaziwa ndani ya Rufiji. Rufiji ndiyo baba yetu. Kwa hiyo, sasa nikiizungumzia tu Kibiti peke yangu wale wajomba zangu wa pale Rufiji nikirudi inaweza ikaja ikawa mtihani. Mimi kuweza kutafuta kamba lazima niende Muhoro halafu ndiyo nirudi Kibiti. Kwa hiyo, hili nilikuwa nakuomba sana uweze kulitolea tamko ili sasa tuweze kuona ni jinsi gani vijana hawa wanakwenda kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nililokuwa nataka nilichangie ni eneo zima linalohusiana na sekta nzima ya mambo ya mifugo. Mheshimiwa Waziri wewe unajua sisi ni wahanga namba moja, maeneo haya ya Pwani ya Kusini yote ukianzia Mkuranga ukienda Kibiti, Rufiji, Kilwa, Lindi na kwa Wamakonde kule wewe unafahamu. Sisi ni waathirika wa hali ya juu sana katika suala zima la mambo ya mifugo. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wakati muafaka sasa umefika wa kuweza kuharakisha sera mpya ya mambo ya mifugo, ili sasa tuweze kuona ni jinsi gani tunakwenda kuwa na mifugo ambayo inakwenda kuwa ni mifugo ya biashara. Ni jinsi gani tunakwenda kutenga maeneo ambayo yanakuwa maeneo sahihi kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anajua katika maeneo ya kwetu kule unaamka asubuhi unakutana na ng'ombe 150 na ametoka kuzungumza hapa Mheshimiwa Getere jana, kama sijakosea juzi. Alizungumza hapa kwamba, kule kwake kuna watu wanachomwa mikuki. Mimi nataka niseme tu hao wenzetu wafugaji wote ni Watanzania lakini wenzetu ni wakali sana. Sisi Watu wa Pwani ni waraimu sana, Mheshimiwa Ulega wewe unajua ndugu zetu wako ndani wana ulemavu wa hali ya juu, wengine wamepoteza maisha kutokana na mambo haya kati ya wakulima pamoja na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri na najua nimetoka kusema hapa; *"Innallah yarzuqu man yashao bighairi hisab"* (Mwenyezi Mungu anamruzuku mwanadamu mambo bila hesabu). Najua katika mambo ambayo Mwenyezi Mungu amekuruzuku wewe ni *game changer,* unakwenda kufanya mabadiliko katika Wizara hii. Lete ile sera sasa tuweze kuhakikisha tunakwenda kutunga sheria. Haiwezekani tukawa na mifugo holela holela tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina wakulima pale nyumbani kwangu katika Kata ya Maparoni, hivi ninavyozungumza kuna mifugo ya ng'ombe takribani 1,250. Ile Maparoni ni ndogo na vile ni visiwa na ninyi mnajua taratibu za visiwa jinsi zilivyo, mifugo hairuhusiwi kwenda kule. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wako harakisheni leteni sera mpya ili sasa iweze kutusaidia tuweze kuwa na mifugo yenye tija kama vile Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anavyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kwa sisi wanasiasa. Mheshimiwa Waziri, natamani sana kuona eneo hili ambalo Mheshimiwa Rais amewekeza fedha nyingi sana na anaendelea kuwekeza, basi sasa liweze kuchangia ipasavyo katika *GDP* (pato letu la Taifa). Umetoka kuzungumza katika hotuba yako kuna 1.8% lakini katika miaka miwili au mitatu iliyopita tulikuwa tumekwenda juu zaidi. Kwa hiyo, hapa tafsiri yake ni nini? Tunakimbia mbele katika *speed* ya kurudi nyuma. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri na wewe mdogo wangu mimi

nakujua shughuli yenyewe unaiweza pamoja na wataalamu wako. Kwa hiyo, nikuombe sana kaa kitako na wataalamu wako tunataka kuona sasa hii sekta nzima ya mambo ya mifugo inakwenda kuchangia katika Pato la Taifa na tukifanya hivyo tutakuwa tumemuenzi Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi na jitihada ambazo anaziingiza katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpembenwe. Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly, dakika 10.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia…

**NAIBU SPIKA:** Ajiandae Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayoifanya, pia niipongeze Serikali yote kwa ujumla kwa kweli wanafanya kazi wanajituma na mafanikio na maendeleo tunayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wanajimbo, Jimbo la Nkasi Kaskazini, Kata ya Kagwe kwa ushindi mkubwa tulioupata kwa kukomboa Kata ile ya Kagwe ambayo iliongozwa kwa takribani miaka 27 ikiwa upinzani, lakini mwisho wa siku tumeikomboa na imerudi ndani ya mikono ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi pia kuwapa pole Wakazi wote wa Mwambao wa *Lake Tanganyika* kwa mafuriko waliyoyapata na mimi kama Mbunge na Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa tukimaliza Bunge tutakwenda kuwapa pole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kumekuwa na changamoto ya ufungaji wa Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu au minne. Naomba nishauri au nitoe mawazo ambayo naamini Waziri atayachukua na atakwenda kuyafanyia kazi. Ziwa la Tanganyika huwa linajifunga lenyewe kwa hiyo hatuna sababu ya kulifunga kwa ulazima. Ninaamini hata sasa hivi lile ziwa limejifunga yaani hakuna shughuli yoyote ya uvuvi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kupata mazao ya uvuvi nilitaka nishauri kwamba, tuweke maeneo ya uzalishaji wa samaki. Nitatoa mfano kule *Lake Tanganyika* kuna maeneo yale ya *Mahale National Park.* Pale Mahale pembeni yake mwa ziwa wamezungusha *ring fence* ambayo ni marufuku kwa mtu yeyote kuvua. Nini faida yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yake yamekuwa yakizalisha samaki wengi na dagaa wengi sana. Sasa wanaonufaika ni wale ambao wako jirani Sibwesa na kule Mgambo. Mwisho wa siku wavuvi wengi wanatoka maeneo mengine kwenda kufuata uvuvi wapi? Kule ambako ni maeneo ya karibu na *Mahale National Park.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri kwa nini usichukue mfano huo huo, mkachagua maeneo mengine matano mfano mkaweka maeneo ya Kipili, kule Kasanga, pale katikati Ninde kwa ajili ya uzalishaji wa samaki na dagaa. Yale maeneo mkayawekea sheria kwamba ni marufuku kwa mvuvi yeyote kwenda kuvua maeneo yale. Mwisho wa siku hata gharama ya ulinzi itakuwa ni ndogo kuliko sasa hivi ambako mkifunga ziwa lile kulinda wavuvi wasiende kuvua gharama kubwa kuliko ambavyo tungeweza kutengeneza maeneo ya kuzalisha samaki yakawa ni maalum na tukaweka vifaa vya ulinzi na hatimaye tukatunga sheria kwamba, yeyote atakayekwenda kuvua pale basi akamatwe na achukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilifunga ziwa lote kwa ujumla wananchi wale hawana maeneo mengine zaidi ya kukimbilia kwenda kwenye uvuvi. Kwa mfano, leo hii Mheshimiwa Waziri

baada ya mafuriko mashamba yote ya mpunga yamemevamiwa, mashamba ya mahindi yameharibika. Sasa mvuvi anategeme nini au mwananchi wa Kirando, Kipili, Karema na Kabwe wanategemea uvuvi, ukilifunga ziwa lile umewaua wananchi wale. Ukilifunga ziwa lile wanafunzi hawatapata elimu kwa sababu wazazi wao hawatapata pesa kwa kwenda kuwalipia ada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri kuliko kulifunga ziwa; nakutolea mfano mwingine mdogo tu, Eneo la Kipili lile kuna mzungu pale katikati ana hoteli pale inaitwa *Lake Shore*. Yeye ameweza kudhibiti wavuvi wasiende kuvua maeneo yale. Pale pana samaki na dagaa wengi wa ajabu. Mwisho wa siku wenye maeneo karibu na pale Kipili wanapata wale samaki na dagaa kwa sababu gani? Wameweka sheria ndogo tu ya kuzuia lile eneo wasiweze kuvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ombi langu kwako sasa twende tukatafute maeneo maalum, tutenge kama ambavyo *Mahale National Park* walivyotenga eneo lile, walivyozungusha yale maboya na mwisho wa siku tuweke sheria. Dagaa na samaki watazaliwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwako ni kwamba, sasa tuende tukatafute maeneo maalum tutenge kama ambavyo *Mahale National Park* walivyotenga eneo lile, walivyozungusha yale maboya na mwisho wa siku tuweke sheria, uvuvi wa dagaa zitapatikana pale na samaki zitazaliwa pale na mwisho wa siku, kwa sababau samaki zikiwa nyingi na dagaa zikiwa nyingi zitasambaa kwenda maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu nataka kuishauri Wizara, nimekuwa nikishauriana na wewe muda mrefu, toka mwaka juzi ninakushauri jambo hili unaniitikia, unalifurahia lakini halifanyiwi kazi. Sasa, nakuomba, sisi Wabunge tunaotoka Kigoma, Rukwa na Katavi tukae chini na Wizara tushauriane na mwisho wa siku tukubaliane na vilevile tuyafanyie kazi. Maana yake hatuna sababu ya kuja hapa Bungeni watu tunachangia,

tunapigiwa makofi, Waziri tunakusifia lakini utekelezaji haupo. Tulikuja hapa mwaka jana tukasema hayo hayo, mwaka huu tunasema hayo hayo, mwakani tunasema hayo hayo, utekelezaji haupo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi naomba, nilikuwa nataka kusemea jambo hilo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kabisa ninawashukuru kwamba umesoma bajeti yako nzuri kwamba utaleta boti, utaleta vifaa vya uvuvi, japokuwa sisi kule *Lake* Tanganyika mara nyingi tunakuwa ni wa mwisho, sasa safari hii fedha hizo zikija jitahidi sana na upande wa *Lake Tanganyika* vijana wale na wavuvi wale na wenyewe wapate vifaa vya uvuvi, wapate mikopo waweze kujiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ilikuwa ni hiyo ya kuishauri Serikali sina hoja nyingine, ninaonga mkono bajeti, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kunambi dakika tano.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kweli nasema tu kwa dhati, Mheshimiwa Rais amekuwa akituamini vijana kwa kiasi kikubwa sana, akiwa na imani kwamba kijana atakuwa na fikra mpya katika ulimwengu unaobadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo, tunaambiwa Barani Afrika ni nchi ya pili ukiachana na Ethiopia, lakini ukitazama tija ya mifugo hii kwa Watanzania unaambiwa hapa inachangia kwenye Pato la Taifa kwa asilimia saba, kitu ambacho ninadhani ni sehemu ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo kuwa mingi siyo laana, mifugo kuwa mingi ni uchumi kwa Taifa letu lakini sasa mifugo imegeuka kuwa migogoro kwa wananchi. Leo hii utasikia migogoro baina ya mfugaji na mkulima, leo hii utasikia migogoro ya wafugaji na mamlaka za uhifadhi, kundi hili la wafugaji

limeachwa kama mtoto yatima, wafugaji wameachwa wanajiendesha wenyewe, hatuwezi kufika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwambia Kaka yangu Mheshimiwa Ulega *you are my brother*, wewe bado ni kijana tunaamini utafanya mabadiliko makubwa na msaidizi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelifanyia tafiti ndogo tu kwa wafugaji, wafugaji wanaambiwa punguzeni idadi ya mifugo, haiwezekani! Kwa sababu wafugaji wanasema hivi, mifugo yangu ni sawa na wewe kuwa na akaunti ya benki na mnada ndiyo *ATM* yangu. Sasa, ukiniambia nipunguze mifugo, ah! Mheshimiwa Mbunge kwa nini wewe benki yako usipunguze fedha kwenye akaunti yako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima anasema, mimi mkulima thamani yangu ni mazao yangu, mfugaji thamani yake ni mifugo, sasa wote hawa kila mmoja anapaswa kumheshimu mwenzake lakini kundi hili la wafugaji limeachwa wanajiratibu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano pale Jimboni kwangu, mwaka jana Kata ya Mofu kulikuwa na mapigano kati ya wafugaji na wakulima na wananchi wawili wakapoteza maisha. Ukienda leo hii ninavyozungumza, kuna mgogoro pale Kata ya Utengule eneo la Ndefi, watu wa hifadhi *TAWA* na watu wa kile kitalu chetu pale wanagombana. Sasa, nikafanya tafiti kwa mfano *Ireland* mkulima na mfugaji ni marafiki, walifanyaje tu *Ireland* ninakupa tu elimu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, walichokifanya *Ireland* waliwaambia wakulima kwa kuwa wafugaji, mfugaji hahitaji ardhi niwaambie ukweli, Mfugaji anahitaji malisho na mnielewe tu hapo. Mfugaji haitaji ardhi anahitaji nini, malisho. Sasa, elimu ninayokupa Mheshimiwa Waziri ni kwamba wakulima wapewe elimu kwamba, *okay*, ninyi mnaokaa karibu na wafugaji mashamba yenu limeni nyasi ni biashara, huyu mfugaji

utamkodisha hapa. Inawezekana ikawa biashara baina ya mkulima na wafugaji, uka-*harmonize*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tunazo ranchi mbalimbali, tunayo ranchi ya Mkata na ranchi ya Kongwa. Kwa nini tusiwaambie wafugaji waje pale? Lakini kuna teknolojia wataalam wanasema kila ng'ombe mmoja anakula eneo la hekta moja ni sawa na 2.5 *acres*. Eneo la heka mbili na nusu kila ng'ombe mmoja anapaswa kula kwenye eneo la heka mbili na nusu lakini kuna teknolojia wenzetu wachina wamegundua ya kupanda majani, kwenye 2.5 *acres* unaweza ukalisha ng'ombe 50 mpaka 70, Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi, pale Kongwa mmeanza, sasa kwa nini usi-*disseminate*? Kwa nini isiende kwa hao wafugaji? *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Geter, Mheshimiwa Mbunge ana dakika moja tu iliyobakia.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa ninampa taarifa tu, ni mwenzangu katika kuongea lakini ninampa taarifa kwamba, mashamba ya wakulima pia yana mahitaji kwamba sisi tunahitaji chakula kwa maana ya kuishi na nyasi ni chakula kwa maana ya chakula cha ng'ombe, sasa tukilima mashamba yote nyasi maana yake watu hawataishi isipokuwa wachague maeneo mazuri kwenye maeneo yetu mazuri hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa wewe..

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei hiyo taarifa! Sina maana tuache kulima mazao ya chakula, ninasema kuna maeneo mnawapa elimu wafugaji wachache ambao wanadhani wanaweza kufanya hiyo biashara.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi muda wako umekwisha.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshiiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kusema, dakika moja amechukua muda wangu, nakuomba!

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Maliasili sasa wameacha kulinda majangili wamekuwa wachungaji wa ng'ombe, tutafika kweli? Tuwaache wafanye kazi yao, Mheshimiwa Waziri kazi ya mifugo ni ya kwako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante, mengine ukaandike.

*(Hapa Mhe. Godwin E. Kunambi alizungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Namwita Mheshimiwa Aida, Mheshimiwa Jafari Chege ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia kwa dakika hizo ulizonipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la upumzishaji wa Ziwa au ufungaji wa Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika kwenye mikoa hii mitatu, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma ndiyo shamba letu, ndiyo duka letu, ndiyo maisha yetu. Kwa kuwa shughuli hii ni shughuli halali, mwaka jana tulimshauri Waziri hapa, tulimshauri kwamba jambo hili halikuwa shirikishi. Tunashukuru amechukua hatua ya kwanza kwa kutushirikisha sisi Wabunge, tulikaa naye, pamoja na kushirikisha Wabunge, tulitaka awashirikishe wavuvi, jambo hilo halijafanyika kikamilifu. Tunajua umefanya kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini? Kwa nini tunataka kufunga Ziwa leo? Mheshimiwa Waziri tumefikaje hapa? Kwa sababu Serikali ilikuwepo miaka yote, ni kweli kwamba Ziwa

Tanganyika huwa linajifunga lenyewe na majibu mliyotupatia wakati umekutana na sisi Wabunge ulituambia samaki wamepungua, swali ni kwamba kwa nini wamepungua? Kwa sababu miongoni mwa majukumu yako kama Wizara ni kuendeleza uvuvi pamoja na ufugaji. Sasa, samaki wamepungu na Wizara ipo! Ninaomba nishauri mambo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkataba huo umeusoma hapa, kwa namna ulivyousoma unaanza kutekelezwa kesho tarehe 15, ndiyo mnaanza kutekeleza hilo jambo, wakati mnakwenda kutekeleza, mbadala wa hicho kipindi ambacho wanafunga Ziwa, umezungumza hapa mmetoa vizimba 29 ambavyo bado havijaanza kufanya kazi, huo ndiyo mbadala kwa kipindi ambacho mmefunga Ziwa, sasa hao samaki wana-*mature* baada ya muda gani? Ninataka kuzungumza nini Mheshimiwa Waziri? Yawezekana hiki unachokifanya leo ilitakiwa kianze kufanyika mwaka jana kwa ajili ya maandalizi kama mbadala kabla hatujafunga Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri jambo la kwanza ni lazima tutafute suluhisho la uvuvi halamu ndiyo chanzo cha samaki kupungua, kufunga Ziwa kwa miezi mitatu siyo suluhisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Ofisi ya Rais mnaohusika na mazingira, ni vizuri pamoja na kwamba mkataba huu tumesaini zaidi ya nchi moja, hili jambo linahusu Watanzania, kama linawahusu Watanzania lazima tuwashirikishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo nazungumza hao wavuvi bado wanakata leseni, hawakati leseni kwa ajili ya kuuza maandazi, wanakata leseni kwa ajili ya uvuvi. Sasa, kama tunaenda kufunga na hao watu wanakata leseni, naomba Waziri ukija hapa utuambie mmetenga kiasi gani kwa ajili ya kuwapa hawa wavuvi ambao wamekata leseni na hii ni shughuli halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba ukija hapa utueleze mmetenga kiasi gani kwa Watanzania ambao maisha

yetu ndiyo uvuvi kwa kipindi cha mpito? Kwa sababu kuzaliwa karibu na Ziwa Tanganyika siyo laana ni baraka! Msitufanye tuanze kulaumu kuzaliwa karibu na Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alionekana akimpeleka Rais kuzindua vizimba Ziwa Victoria ni jambo jema sana, lakini kama Ziwa linalofungwa leo ni Ziwa Tanganyika *why* alianza kupeleka Ziwa Victoria? Huoni kama unakwenda kuwachanganya hawa Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo hayastahili hata kidogo. Ukiangalia hapa, tunasema hivyo vizimba, utekelezaji wa maduhuli katika malengo mliyokuwa mmejiwekea ni 42% tu mpaka sasa hivi lakini fedha za maendeleo ni 41%. Hii ni sekta ya uzalishaji tunayoitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo uvuvi ni utajiri, ufugaji ni utajiri. Msifanye hao watu waanze kuona kama hili jambo siyo halali kwao, lazima tuanze kufikiri upya. Jambo la vizimba ninarudia tena, Ziwa Tanganyika lipewe kipaumbele. Mtaenda kufunga kwa sababu ya wingi wa maamuzi ambao tutafanya kwa watu lakini mimi ninasema, hata kama kulikuwa na nia njema, tutafute suluhisho la uvuvi haramu siyo kufunga Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kushauri, kama Kata ina vijiji vinne, tusiende kufunga Kata nzima. Mnaweza mkafunga vijiji viwili, vijiji viwili mkaacha. Mshehimiwa Waziri ukija hapa utueleze, kwa kipindi hiki ambacho mnaenda kufunga, wale watu ambao wanafanya uvuvi wa ndoano kwa ajili ya kitoweo utaratibu gani utatumika wakati haya maisha mengine yanaendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kushauri. Jambo la kwanza, mnapowaambia wakope hivi vizimba, kuna kuandika maandiko, mmetoa elimu kiasi gani kwa hawa wavuvi? Kuandika hayo maandiko ni gharama. Huyu mvuvi wa kawaida anaweza wapi kutoa shilingi laki nne, shilingi laki tatu, shilingi laki mbili? Haiwezekani! Tumeamua kwamba huu ndiyo mbadala, nendeni mkatengeneze mazingira rafiki kwa hao wavuvi. Kwa sababu ukiangalia, ni kwa nini wako 29? Kwa mujibu

wa taarifa yako Mheshimiwa Naibu Waziri ukiwa Sumbawanga ulisema utatoa vizimba 800 lakini leo unazungumzia 29, halafu tunakwenda kufunga Ziwa kesho! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi hata kama nia ni njema kweli, kama hivyo vizimba vimetolewa jana au juzi, Ziwa linafungwa kesho, hao Samaki wata-*mature* lini? Tunakwenda kutengeneza nadharia, jambo ambalo haliwezekani kutekelezeka. Hatutaki kuzalisha vibaka mtaani, hii ni kazi halali ya Watanzania. Sisi ambao tunaamini Ziwa Tanganyika ndiyo shamba letu na ni duka letu, tumeandaa utaratibu gani kwenye kipindi hiki cha mpito? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ninarudia, tusije na majibu mepesi kwenye mambo magumu. Uvuvi haramu upo, hakuna mtu anakataa. Samaki wamepungua ni kweli, nani ametufikisha hapa? Serikali ilikuwa likizo? Ilikuwepo. Kwa nini leo tuwape adhabu hawa Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema, *approach* ambayo inatumika sasa hivi ndiyo ambayo sikubaliani nayo, yawezekana nia ni njema tupate samaki wengi lakini kupata samaki wengi siyo kufunga Ziwa kwa miezi mitatu. Tuandae *operation* maalumu ya kupambana na uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye utitiri wa kodi, utitiri wa kodi, leo kile chombo ambacho mvuvi anatumia mnasema akilipie leseni. Mmiliki dola 55 chombo chenyewe wanakilipia dola 50, halafu na wavuvi wanaokwenda kuvua na wao wanalipia leseni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida muda wako umekwisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili suala la tozo libaki kwa mtu mmoja ambaye ni mmiliki, chombo hakiwezi kujiendesha.

**NAIBU SPIKA:** Mengine mwandikie Waziri kwa maandishi.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, dakika tano halafu Mheshimiwa Sigula ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusimama tena mara nyingine ndani ya Bunge, kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Wiki mbili au tatu zilizopita tulipata ridhaa ya kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu akikabidhi boti ya doria baharini kwa ajili ya kulinda usalama na maslahi ya wavuvi maeneo ya baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kupitia boti hii nachukua nafasi ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea kuwalinda na kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya baharini hasa kwa wavuvi wetu ambao wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwendelezo huo, nachukua nafasi kukuomba sana Mheshimiwa Waziri na nimekuwa nikisema sana ndani ya Bunge, kwa kuwa tayari angalau tumelifanya hili baharini, tufikishie salamu kwa Mheshimiwa Rais na wewe Mheshimiwa Waziri ulione hili namna ambavyo wavuvi wa Mkoa wa Mara ambavyo wamekuwa wakiteseka na kudhulumiwa haki zao maeneo ya ziwani na wanapigwa na wenzetu, kimsingi usalama wao haupo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, kwa kuwa limeanza maeneo ya baharini Mheshimiwa Waziri libebe hili pia lifanyike maeneo ya maziwa ili kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwa wavuvi wetu. Ninafikiri utakumbuka siyo mara ya kwanza kulizungumzia hili, ni changamoto kubwa sana kwa wavuvi maeneo ya Ziwa, niliwahi kukuambia kuna wengine wamefilisika wameacha kazi hizi za uvuvi kwa sababu usalama wao ndani ya Ziwa hauko *stable*, kwa hiyo, nachukua fursa hii kukuomba sana Mheshimiwa Waziri kama tulivyofanya maeneo ya bahari tuone namna tunavyoweza kulifanya kwa Mkoa wa Mara na Kanda ya Ziwa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo kwa sababu dakika ni chache, nitajikita sana kwenye Jimbo langu. Jambo la kwanza ni Chuo cha Gabimori. Mheshimiwa Waziri hiki chuo kwa bahati nzuri nimeona kwenye hotuba yako nimesoma yote sijaona ukikizungumzia mahali popote. Wewe ni shahidi chuo hiki tumekuwa tukikiomba zaidi ya miaka 10, wananchi matumaini yao ni makubwa sana hasa vijana ambao wanahitimu kidato cha nne, matarajio yao ni kwamba chuo hiki kiweze kuimarika waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tazama kwa miaka 10 tunakiimba chuo hiki na hakifanyi kazi, ninakuomba utakaposimama leo jioni, kwa kuwa kwenye hotuba yao hujakizungumza, basi ukitolee majibu ili wananchi kule ndani ya Jimbo la Rorya na Mkoa wa Mara kwa ujumla wake waweze kujua nini hatma ya chuo hiki ambacho tumekiomba zaidi ya miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni soko. Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikuomba sana masoko ya samaki na masoko ya dagaa. Mheshimiwa Waziri umesema sekta hizi ni sekta za uzalishaji lakini kimsingi Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikuambia sana, tuzungumze wewe pamoja na Mawaziri wa TAMISEMI tuone namna ya kuisaidia Wilaya ya Rorya kwa kutengeneza masoko mawili makubwa, Soko la Samaki na Soko la Dagaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavua lakini hatuna soko la uhakika la kuuza bidhaa zetu. Kama unavyojua, uchumi wa Jimbo la Rorya ukiacha kilimo, shughuli kubwa inayofuata ni uvuvi lakini hatuna soko la uhakika. Mvuvi anavua Rorya anapeleka kuuza bidhaa zake Mwanza, anapeleka kuuza bidhaa zake Kenya. Mheshimiwa Waziri lione hili. Tunataka na sisi tupate masoko nasi watu wa Kenya na hao tunaowafuata Mwanza waje kununua mahitaji yetu ndani ya Jimbo letu la Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni vizimba. Ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na wewe mwenyewe kwa vizimba ulivyokabidhi Mwanza, mimi ndani ya Jimbo langu la Rorya wavuvi wangu wamepata vizimba vitatu pamoja na boti tatu, tupelekee salamu, tunashukuru sana kwa

kazi hii nzuri na uendelee kumwomba tena Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sisi shughuli yetu ya uchumi ni uvuvi, tunaomba tupate vizimba vingine na nimekuletea vikundi 15 Mheshimiwa Waziri, ninaomba hivi vikundi 15 uwape vizimba wafanye shughuli ya uvuvi iliyo salama ili angalau na wao waweze kujikwamua kenye uchumi wao. *(Makofi)*

Mhhesimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la majosho. Mheshimiwa Waziri kama unakumbuka toka ukiwa Naibu Waziri nimekuwa nikikufuata sana kuomba majosho na ulinikabidhi kwa mtu mmoja pale Wizarani, ninafikiri anaitwa Ndugu Rutega, toka mwaka 2022 ninakuomba majosho, ninakuomba sasa na hii iwe awamu ya mwisho, josho moja ni shilingi milioni 20 mpaka shilingi milioni 25, siwezi nikawa ninakufuata kila siku kwa miaka mitano kuomba shilingi milioni 25 peke yake kujenga hata josho moja. Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana, kwenye bajeti yako na utakaposimama hapa jioni uwaambie wananchi wa Rorya toka mwaka 2021 ukiwa Naibu Waziri, leo wewe ni Waziri, tunapata lini majosho kwa ajili ya kuboresha na kusaidia wafugaji wetu wanaofanya shughuli hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limekuwa likiendelea ni namna ambavyo, kama ukifuatilia sasa hivi Mheshimiwa Waziri, soko la dagaa kwa sasa hivi, dagaa zimepanda bei, wanaoumia sana ni hawa wananchi wa kawaida kabisa ambao wengine tunatoka nao vijijini, kwa namna ambavyo wanapata yale mahitaji. Mwingine hana uwezo wa kununua nyama, kwa hiyo, chakula chake cha kila siku kwa mwananchi wa kawaida ni dagaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia Kanda ya Ziwa Mheshimiwa Waziri, bei ya dagaa sasa imepanda, kidumu alichokuwa ananunua shilingi 5,000 sasa hivi ni shilingi 10,000 mpaka shilingi 15,000, maana yake bei imepanda. Wale wananchi wa kawaida wanashindwa kumudu gharama za maisha. Mheshimiwa Waziri nini kimetokea? Ni kwa sababu

tumeruhusu wenzetu kutoka nchi jirani kwa maana ya Congo na Uganda kuja kuingia mpaka kwenye Visiwa huko wanakofanya wavuvi kwenda kununua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni walikuwa wananunua wazawa, wanaleta sokoni, hawa watu wageni walikuwa wananunua kupitia masoko ya kawaida, lakini leo wanafuata kulekule ziwani wananunua na wakinunua wananunua kwa bei kubwa. Wakinunua kwa bei kubwa maana yake mlanguzi anaponunua kule anapoleta kwenye masoko ya kawaida, leo ukienda CCM Kirumba Mwanza na maeneo mengine, bei imepanda zaidi ya mara mbili, imepandishwa na nini, kwa sababu ya bei hizi za wenzetu wanaofuata kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitengeneza utaratibu kama alivyotengeneza Waziri wa Kilimo hapa, kwamba wale wageni wasiende kule inakovunwa penyewe kwa maana ya visiwani, wasubiri kwenye masoko wanunue kule bidhaa ili angalau bei iwe linganifu lakini tutawalinda pia wanunuzi wa ndani pamoja na walaji ambao ni wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Chege. Mheshimiwa Sylvia Sigula, dakika saba.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na kusimama hapa leo kuchangia katika Wizara yetu hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara, Kaka yangu Mheshimiwa Ulega na Naibu Waziri wake na wataalamu wote wa Wizara, kwa kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia alitupatia matumaini sana wavuvi pale alipofanya tukio la

kihistoria, tukio ambalo halijawahi kutokea tangu tupate uhuru. Alikabidhi boti zaidi ya 160 na vizimba zaidi ya 120 katika Ziwa Victoria. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi hizi, tunampongeza sana Mheshimiwa Samia na tunaona kazi yake njema inavyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi tulitarajia baada ya matumaini kutoka kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwekeza katika Ziwa Victoria tulitamani kuona uwekezaji ule unahamia katika Ziwa Tanganyika, hayo ndiyo yalikuwa matumaini yetu Mheshimiwa Waziri, lakini kwa masikitiko makubwa sana, tunaona juhudi katika Ziwa Tanganyika bado haziridhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ukienda kwa wavuvi changamoto yao kubwa ni tozo, tozo, tozo, tozo. Mheshimiwa Rais, ukimsikiliza dhamira yake kubwa ni kuhakikisha uwekezaji unafanyika, kutengeneza mazingira wezeshi na mazingira rafiki kwa wawekezaji wetu katika sekta mbalimbali. Leo katika Sekta ya Uvuvi uwekezaji wake umekuwa ni mgumu, ni mgumu na ni mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza, leo hii nikitaka kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi, kwanza kabla sijafanya chochote nitaenda *TASAC*. Nikiwa *TASAC* kule watachukua pesa yao, nikitoka hapo lazima mimi kama mnunuzi wa boti nitakata leseni yangu mimi kama mnunuzi wa boti. Nikitoka hapo nitakata leseni nyingine kwa ajili ya boti lakini boti hiyo moja haiwezi kwenda kuvua ikiwa peke yake, lazima inahitaji *supporting boat* ndogo ndogo na zile boti ndogo ndogo pia na zenyewe zote zikiwa tatu, zikiwa nne, zikiwa mbili zote nitazikatia leseni, hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani katika kazi moja unakuwa na leseni zaidi ya tano, hii haiwezekani Mheshimiwa Waziri, hii siyo sawa. Leo hii mimi nikitaka kuwekeza kwenye Sekta hii lazima nitakuwa na dola 55 kwa ajili ya boti lakini nitalipa dola 50 kwa ajili yangu mimi mnunuzi wa boti, hata kama siendi kuvua lakini pia mvuvi lazima awe na leseni, hii siyo sawa Mheshimiwa Waziri. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, ukae na timu yako kama

ilivyo kwa wamiliki wa magari, akishakuwa na leseni ya chombo hatuoni umuhimu wa kuwa na leseni ya mmiliki na kama ni hivyo inahitajika sana basi zijumlishwe kwa pamoja. Hii kwetu wavuvi ni kero na inatukwamisha sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapotaka kwenda kuvua wewe unafahamu, wewe umesema wewe ni mvuvi unafahamu ile boti moja haiwezi kwenda kuvua ikiwa pekeyake lazima kuwe na boti hizi saidizi, kuna haja gani hizi boti saidizi kuwa na leseni zake kwa kazi ile ile moja? Haiwezekani Mheshimiwa Naibu Waziri. Ninaomba utakapokuja kufanya majumuisho utueleze; ni kwa nini wamiliki wa magari wana leseni moja, wamiliki wa boti tuna leseni zaidi ya nne? Hilo ni jambo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumza, tumeona maziwa mbalimbali yanaelezwa. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri na Wizara yako; hivi mnafahamu kama kuna uwepo wa Ziwa Rukwa? Hatuoni Ziwa Rukwa likizungumziwa popote lakini Ziwa Rukwa lile lipo linafanya kazi lakini hatuoni uwekezaji wa Serikali katika Ziwa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatusikii habari za vizimba Ziwa Rukwa, hatusikii habari za mialo Ziwa Rukwa, nini changamoto hasa Mheshimiwa Waziri? Kama hatufahamu kwamba kuna uwepo wa Ziwa Rukwa basi tuwaeleze wananchi kwamba Wizara haifahamu uwepo wa Ziwa Rukwa tujue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona Ziwa lipo lakini hakuna uwekezaji wowote uliofanyika katika Ziwa Rukwa. Mheshimiwa Naibu Waziri kama itakupendeza tunaomba tupate mialo katika Kata ya Nankanga kama itakupendeza. Pia, katika Ziwa Rukwa pale Muze tunaomba tupate mialo pale. Tunatamani kuona wavuvi pia wa Ziwa Rukwa na wenyewe wanaangaliwa kama wavuvi wengine wa maziwa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia tumeona hapa wavuvi wa Kigoma, Rukwa na Katavi tumepokea hizo vizimba 29. Kwa takwimu na uhalisia wa mikoa hii mitatu kwa idadi ya wavuvi

waliopo bado tunaona vizimba hivi 29 havitoshi Mheshimiwa. Hata kama unasema kwamba hao ndiyo waliojitokeza, imani yetu ni kwamba wananchi bado hawana elimu ya kutosha kuhusu upatikanaji wa hivyo vizimba. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, tuongeze elimu. Pia, tuongeze ushirikishwaji wa wananchi ili waelewe vizimba hivi vinapatikana kwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wananchi wanapiga simu, wanashangaa kuona Serikali inasema walioomba ni wachache vizimba vipo lakini wao wenye uhitaji bado wanaona hawawezi kuvipata. Kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara tutoke ofisini twende kwa wananchi wavuvi tuwafikie waelewe, waelimishwe namna gani vizimba hivi vinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapomwambia mwananchi wa kawaida aanze kuandika maandiko, wengi huwa wanahisi ni jambo kubwa sana. Kwa hiyo turahisishe mambo, kama itawezekana watumie hata fomu. Kwani kuna haja gani ya kuwa na maandiko kama kweli ni mvuvi na anajulikana na uwezekano wa kutumia fomu uwepo? Turahisishe kazi, wavuvi hawa waombe vizimba kwa kutumia fomu, siyo lazima wawe na maandiko. Tunapoanza kusema maandiko ndiyo tunaongeza *chain* ya rushwa.... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa...

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongeza *chain* ya usumbufu... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, ahsante.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula hayupo, Mheshimiwa Mtaturu, jiandae Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ipo mezani. Nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kusimamia maendeleo ya nchi yetu. Sekta zote tumekuwa tukiona anafanya kazi kubwa na hata kwenye Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi tumeona kazi kubwa inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nichukue nafasi hii kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Alhaji Abdallah Ulega kwa kazi kubwa anayoifanya na wenzake Naibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Alexander Mnyeti pamoja na Katibu Mkuu *Professor* Shemdoe na wataalamu wote kwa kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta hii ni Sekta muhimu katika uchumi wa nchi yetu lakini chakula kama ambavyo tumekuwa tukielezwa na leo wanasema ni siku ya protini ambayo ipo kwenye viwanja vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa takwimu hapa na tumesikiliza vizuri Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwamba tunao ng'ombe wengi sana wapatao milioni 37.6 lakini pia tuna mbuzi pamoja na kondoo wa kutosha. Maana yake tukitumia vizuri rasilimali hii tunaweza kubadilisha kabisa uchumi wa nchi yetu na tutaongeza pato la Taifa kupitia kuchangia kwenye *GDP*, ni mipango tu ikiwekwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema nampongeza Mheshimiwa Waziri. Tangu umeingia katika Wizara hii ukiwa Naibu Waziri, tuliona mchango wako lakini sasa ni Waziri kamili, nina amini kabisa tutatumia rasilimali hii vizuri, tutajipanga vizuri kulingana na mipango ambayo umetuambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumpongeze Mheshimiwa Rais, ametuongezea bajeti kutoka shilingi bilioni 169 mpaka sasa ni shilingi bilioni 460, ni zaidi ya 63% imeongezeka bajeti. Maana yake ni kwamba ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba yale

ambayo ni matamanio ya Wizara hii kwenye utafiti, kuwekeza rasilimali watu na mipango mbalimbali, ikifanyiwa kazi vizuri itaongeza uchumi kwa kiasi kikubwa katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hiyo nilitaka tu nitoe mchango wangu kwenye maeneo machache ili niweze kuona namna ambavyo tutafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze kwenye lile suala la kuweka bandari ya Uvuvi pale Kilwa Masoko. Sisi tulifika kama Kamati, ni uwekezaji mkubwa sana zaidi ya shilingi bilioni 286 inaenda kuwekwa pale. Tutakuwa na uwezo wa kupaki meli tatu za mita 100 ambazo zitakuwa na uwezo wa kupakia Samaki na kuzipeleka kule kunakotakiwa. Maana yake ni kwamba tunaenda kuongeza uchumi mkubwa katika Sekta ya Uvuvi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nieleze maeneo machache ambayo nadhani yaweze kuwa kama mchango wangu. Eneo la kwanza nataka niombe kwamba, tumesikia hapa migogoro mingi ya wakulima na wafugaji. Hii ni kwa sababu huenda hatujatenga maeneo halisi ya wafugaji. Ndiyo maana leo wafugaji wanalalamika nchi nzima katika maeneo mbalimbali. Niombe sana Mheshimiwa Waziri kaa na Wizara zingine zinazohusiana na Wizara hii ziweze kusaidia wakulima na wafugaji waondokane na migogoro hii. Mfugaji wa nchi hii asionekane ni yatima kwa sababu kuwa na mifugo mingi kama walivyosikia wengine siyo laana ni sehemu ya rasilimali kila mmoja anajivunia kile alichonacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni kuomba migogoro hii iweze kutatuliwa kwa amani ili wananchi wote waweze kufurahia mifugo yao. Kwenye eneo la wataalamu Mheshimiwa Waziri, unaweza ukawa na mipango mizuri kwenye *level* ya Wizara lakini kule chini kwenye halmashauri hatuna wataalamu wa mifugo, hatuna wataalamu wa uvuvi. Leo hii tunalia kule kwa sababu watendaji wa kata na wa vijiji ndiyo wanafanya kazi kwa niaba ya Wizara yako, niombe sana tuongeze wataalamu ili waende wakafanye *transformation* ya ile mifugo katika maeneo yetu. Kwa hiyo nilitaka niombe sana tuongeze wataalamu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa majosho, kwenye eneo hili Mheshimiwa Waziri una deni na mimi. Nilikuomba majosho manne, umenipatia josho moja katika Kata ya Ntuntu. Kuna josho muhimu lipo katika Kata ya Siuyu, lile josho linatakiwa liondolewe katika maeneo ya Kanisa. Niombe sana lile josho unijengee ili wananchi wale waendelee kupata huduma za kuogesha mifugo yao na kuweza kusaidia mifugo iendelee kunenepa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, niombe sana mifugo katika maeneo ya Isuna, Mang'onyi...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mtaturu...

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Unyahati pamoja na Siuyu nao wanahitaji majosho...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mtaturu...

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili waweze kuboresha mifugo yao. Ahsante sana naunga mkono hoja, nakutakia kila la heri Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo, jiandae Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Naomba na mimi pia nichukue fursa hii kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri lakini pia na kwa hotuba yake nzuri inayoonesha dira ya muelekeo mpya na mzuri wa Sekta yetu hii ya Mifugo na Uvuvi. Pia, nishukuru kwa upande wa Jimboni kwangu tuna shida kubwa ya watumishi wa Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi. Tulipata watumishi 14 kwa ujumla wake lakini bado tunayo changamoto ya watumishi wengi wapatao 93, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri uendelee kututazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata pia vitendea kazi zikiwemo pikipiki nane lakini bado tuna upungufu wa pikipiki 17 kwa hiyo bado tunaendelea kukulilia utusaidie. Pia, huko nyuma tulikuwa tunapata hizi dawa za kuogeshea mifugo, kwa hiyo niendelee kuomba sasa hii huduma iendelee kupatikana kwa sababu mwaka huu hatujapata ile yenye ruzuku. Tunaomba Mheshimiwa Waziri uendelee kutuona katika Wilaya yetu tuendelee kupata dawa za kuogeshea mifugo katika majosho yetu kwa sababu mfugo unapokosa afya hata tija yake inakosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikukumbushe ile ahadi ya majosho 10 ambayo Waziri alituahidi siku ile alivyofika kule kwenye Kijiji cha Mwinkulu, alipokuja kwenye ile timu ya Mawaziri Nane pamoja na hiko Kijiji chenyewe cha Mwinkulu. Alituahidi kwamba angetupatia majosho 10 lakini ile kazi bado haijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mkubwa ningetaka kujikita kwenye maeneo makubwa kama mawili, matatu hapa. Eneo la kwanza ni kuhusu maeneo ya malisho. Nashukuru sana Wizara imejitahidi kutupa mbegu, imejitahidi sana kupeleka mbegu za malisho na kuleta mbegu mpya kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hii ni hatua kubwa lakini bado kuna changamoto kubwa ya maeneo yenyewe ya malisho. Hapa nataka niishauri Serikali, Wizara ianzishe mashamba kwa ajili ya malisho ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee mchango wa Mheshimiwa Kunambi. Amechangia vizuri sana kwenye eneo la kuwekeza kwenye maeneo ya malisho. Malisho ya mifugo kwa sasa ni biashara, wafugaji wanahitaji malisho, wanahitaji majani lakini majani hayapatikani. Watu wengi wanaamini kwamba malisho ni ya Mungu, majani ni ya Mungu lakini majani yenyewe hayaonekani. Ndiyo maana unaona kila mahali sasa hivi kuna migogoro, utakuta migogoro ya wafugaji na wadau wengine wanaohitaji ardhi. Kwa hiyo kumekuwa na shida kubwa kwa sababu hatujawekeza ipasavyo kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaangalia tu kwa tathmini ndogo au kitakwimu. Mkulima au mfugaji akitaka kupanda eka moja ya majani, yeye kazi yake kubwa pale ni kuwa na mbegu, kulima na kupanda. Mavuno yake mpaka mwisho atajikuta robota moja la majani ni shilingi 3,000. Sasa kwa mazingira kama hayo akitoa robota 300 tu anapata shilingi 900,000 lakini ukilima heka moja ya mahindi ukapata gunia 10, gunia moja ni shilingi 40,000, unapata shilingi 400,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaona kwamba ukilima majani faida yake ni mara mbili zaidi na yanahitajika yana wateja. Kwa hiyo natoa wito hapa kwa Serikali na sisi ambao ni wazalishaji wa majani tuwekeze kwenye eneo la mashamba ya malisho ya mifugo na hasa hapa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa umeleta mbegu nyingi basi nikuombe uwekeze kwenye eneo la mashamba sasa. Tushushe chini kwenye wilaya zetu, kwenye ma-*ranch* ili wananchi wanaofuga waweze kupata hii huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Kamati pia imeeleza kuhusu kuanzisha mamlaka kamili ya mifugo pamoja na mamlaka kamili ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ighondo...

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi kama unavyoona *TRA*...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo, ahsante

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA, RUWASA* na kadhalika na huku pia tuweke hili ili kuwe na tija kwenye ufuatiliaji na usimamizi wa Sekta hii ya mifugo. Nakushukuru kwa nafasi na naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus, jiandae Mheshimiwa Janejelly Ntate.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tarehe 17 Septemba, 2023 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya ziara kwenye Jimbo langu la Nachingwea na katika changamoto ambazo alikutana nazo tulimlalamikia juu ya mgogoro wa wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mwezi mmoja ilikuja timu maalum ambayo imetusaidia kuondoa tatizo hilo, mgogoro huo wa wakulima na wafugaji. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nachingwea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi hiyo kubwa na nzuri ambayo ametufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu Waziri na timu yake kwa ujumla wake, wanafanya kazi kubwa na nzuri kweli kweli. Wakati wa mzozo huu, Mheshimiwa Waziri pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani walifanya ziara Nachingwea na kuchukua hatua ambazo walau ziliweza kutatua mgogoro huo kwa awali na baada ya hapo Mheshimiwa Rais alivyokuja akaendelea kuumaliza kabisa huo mzozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mzozo huo wa wafugaji na wakulima pamoja nimeshukuru hapa kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na Serikali, bado imeacha makovu mengi kwenye jamii. Hapa wakati Mbunge mwenzetu anachangia alikuwa anashauri namna ambavyo wakulima wanaweza kupanda majani kwenye mashamba yao ili iwe kama sehemu ya wao pia kuwa na mahusiano mazuri na wafugaji kwa maana ya wafugaji watakuja kulisha kwenye majani ambayo tayari yamepandwa na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kwa kweli kama angekuwa anazungumzia kwenye maeneo yetu, sisi tunaojua hiyo adha iliyotokea kwa sababu ya migogoro hii ya wafugaji na wakulima

wala isingekuwa na afya na wala hakuna mtu ambaye angeweza kusikia kauli ya namna hii. Ni hivi, hawa wafugaji wanavyokuwa wanavamia kwenye maeneo haya kwanza ni maeneo ambayo siyo rasmi kwa ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maeneo ya kilimo, ni maeneo ambayo hayajatengwa kabisa na ufugaji. Sasa wakija wanaacha kabisa kulisha kwenye nyasi wanakwenda kulisha kwenye mazao kwa maana ya mahindi, mbaazi na mazao mengine. Wanayo wenyewe kauli yao wanasema wakilisha haya mazao, hawa ng'ombe wanatoa maziwa mengi na wananenepa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya madhila tunayajua na tunashuhudia sisi ambao tunatoka kwenye maeneo hayo. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri hapa, tuendelee kuchukua hatua. Hii kupongeza ninapopongeza kusiwe kwa muda, muendelee kuchukua hatua ili mgogoro ule usirudie tena, ili wale wafugaji wasirudie tena kwenye maeneo ambayo hayajatengwa kwa ajili ya ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye utatuzi wa mgogoro huu mimi kama Mbunge naishauri sana Wizara kuendelea kuzingatia usawa baina ya wafugaji na wakulima. Kwenye utatuzi wa migogoro hii wapo wakulima ambao wamepata madhila mbalimbali; wapo wengine wameuwawa na wapo wengine wamepata vilema vya kudumu. Hakuna hatua iliyochukuliwa na hakuna mtuhumiwa hata mmoja ambaye kwa sasa yupo mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa na hii nitatolea mfano, wapo wapiga kura wangu tisa ambao sasa zaidi ya mwaka mmoja na nusu wapo ndani na kesi yao haieleweki. Hawa wamekamatwa kwa kesi ambayo haina mlalamikaji. Mimi niiombe sana Serikali kuchukua hatua juu ya vijana hawa ambao sasa zaidi ya mwaka na nusu wapo ndani ili kuleta usawa na amani kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikubaliki leo, hii wala haikubaliki kesho; na maeneo haya hata kufanya siasa ni ngumu kweli kweli kwa sababu wanahisi kwamba hawa wakulima wameonewa. Wapo wakulima ambao wameuawa hakuna mtuhumiwa, lakini huku upande mwingine tumeona hatua zimechukuliwa bila hata kushuhudia huyo aliyeuawa ni nani na alizikwa wapi. Hii haikubaliki, hii sasa tunaonesha ni *double standard;* na kwa kweli tukifanya hivyo hatuwezi kuendelea mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali kupita Mheshimiwa Waziri hapa kuchukua hatua. Kama tunataka maridhiano ni pamoja na kuweka usawa kwenye jamii. Hawa vijana ambao hawana sababu mpaka sasa wapo ndani waone namna ya kuleta maridhiano. Kama upande wa wafugaji hakuna watu ambao wapo ndani na yapo madhila na matukio mbalimbali yalitokea, basi ni vizuri pia ku-*balance* hii hali; hawa vijana watoke nje nao ili waje waungane na jamii zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana na inatia uchungu, vijana hawa wengine ni wadogo wameacha wazazi wanateseka, wameacha wake wanateseka, wameacha watoto ambao kwa sasa hawawezi kusomeshwa. Niiombe sana Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Amandus. Jiandae Mheshimiwa Janejelly Ntate.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** …baada ya Mheshimiwa Ntate, jiandae Mheshimiwa Sabu na baada ya Mheshimiwa Sabu, Mheshimiwa Shangai. *(Makofi)*

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi pia niungane na mwezangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Tukiangalia bajeti ya mifugo na uvuvi katika mwaka tunaoumaliza ilikuwa ni bilioni mbili tisini na mbili *point* tano, lakini leo wanaomba Bajeti ya bilioni 460.3, sawa na ongezeko la 63.5%. Hii ni kwamba Mheshimiwa Rais ana nia thabiti ya kutaka kuendeleza uvuvi na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Ulega na Naibu Waziri wake. Hakika wana nia thabiti ya kuendeleza uvuvi na mifugo na wakiwa na mtendaji wao ambaye ameongoza jahazi la watendaji, Profesa Riziki, hakika wamekuwa wasikivu kwa Kamati. Huwa napenda kauli yake Mheshimiwa Waziri, Kamati ikimwambia anasema hayo ni maelekezo na anakwenda kuyafanyika kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitajikita kwenye kuimarisha ranchi za Taifa, maana wameiweka ni kati ya kipaumbele kwenye vipaumbele vyao 10. Ranchi zetu za Taifa hizi zingeendelezwa huu mchango wa asilimia saba wa mifugo ungeweza kuongezeka zaidi ya hapo. Niwashauri, ranchi zetu nyingi zilikuwa zimetelekezwa na zimeshakuwa ni mapori. Sasa waende wakatengeneze miundombinu kama tunataka Watanzania wa kawaida ndio wawe wawekezaji kwenye hizo ranchi, kwa sababu wanaomba wanawapa. Wanaweza wakampa mtu hekta tano lakini hekta 20 ndizo zipo sawasawa. Pengine ni miti mikubwa ambayo yeye kwa uwezo wake hawezi kuwekeza. Kama watawekeza miundombinu iliyo sahihi *then* ndipo wakawakodisha hawa Watanzania, uzalishaji utaongezeka na manufaa ya hizi ranchi zitaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kwenye ranchi zetu hizi watumishi wengi ni vibarua na ni wa mikataba. Sidhani kama mtumishi kibarua anaweza akaleta tija kwa kujiamini kama hakuajiriwa kwa kazi ya kudumu. Hili nalo waende wakaliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhondo wa ngoma ni sharti uingie ucheze. Leo watumishi wetu wa hizi ranchi hawana hata kitalu cha mfano ili kutuonesha ufugaji bora. Akiwa nacho hicho kitalu ni dhambi na akiwa nacho hicho kitalu ameshaonekana amevunja taratibu na Kanuni. Niwaombe waende wakaliangalie

hili. Hawa watumishi wetu wa kwenye ranchi hizi wawe na vitalu vidogo vya mifano, wafuge kwa mifano ili na wengine tunaofuga nasi twende tukajifunze kutokea kwao. Hili pia liende na kwa Wizara ya Kilimo, hao Maafisa Ugani wetu wawe na mashamba ambayo ni ya mfano. Hii itatufanya kila mmoja kutaka kuingia kwenye tasnia hii ili kuwekeza, kwa sababu watakuwa wanacho cha kutuonesha; lakini sasa wanatuonesha vya kwenye karatasi tu. Atakuja ataniambia namna ya kuchanja mifugo, kulisha lakini yeye hana hata kitalu cha kunionesha au hata mifugo yake ameilishaje na inafananaje. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kama alivyozoea, kwamba ushauri ni maelekezo, akalichakate hili na alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusiana na hivi vitalu ni muda wanaopewa wawekezaji; hebu tujaribu kuona muda. Kuna wengine wakipewa mwaka mmoja atakuwa bado anapambana na visiki, mwaka mmoja bado anapambana na kuweka miundombinu, hawezi akapata faida na hivyo nasi hatuwezi kupata tunacholenga. Tuangalie muda wanaowapa uwe kama muda tunaopewa kwenye hati za umilikaji wa ardhi; uwe ni muda mrefu, mtu awekeze kwa muda mrefu ili Serikali ipate pato na yeye aweze kupata faida kama mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye uvuvi sasa, uvuvi wa kwenye bahari. Leo hii kilimo walituambia hawawezi wakaleta mbolea, hawawezi wakaleta zana za kilimo ndani ya Dar es Salaam, lakini tuna bahari kuu. Katika hili waangaliwe akinamama na vijana wa Mkoa wa Dar es Salaam ili waingie kwa nguvu zaidi kwenye kilimo cha mwani, kufuga majongoo bahari kwenye Bahari yetu ya Hindi ili tuweze kuinua uchumi wao na waweze kupata kipato cha kila siku. Jana tumeona…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ooh! Ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wageni walioko Bungeni mchana huu:-

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; Wageni wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni; Ndugu Wilfred Haule (Mwenyekiti wa Bodi ya *TAFIRI)* na Ndugu Rashid Sound Nassor (Mkurugenzi wa *Farmbase Limited)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ulega, Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni; Wakurugenzi na maafisa wa taasisi zilizo chini ya Wizara, wawakilishi kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB), CRDB, NMB* na *NBC*; wawakilishi kutoka Mashirika ya Kimataifa na Asasi Zisizo za Kiserikali; wafugaji kutoka Chama cha Wafugaji Tanzania, wasindikaji wa mazao ya mifugo na uvuvi, wazalishaji na wasambazaji wa chanjo ya mifugo, vyama vya wadau wa Sekta za Mifugo na Uvuvi; wazalishaji wa kuku; washauri wa Wizara kwa upande wa uvuvi kutoka Ziwa Victoria na vijana wa *Program* ya *BBT*. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Umma kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Wageni hao ni Ndugu Ally Mohamed Sikapo, Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Wilaya ya Mkuranga; Wajumbe Kamati ya Siasa wakiongozwa na Ndugu Zuwena Mtulya; Sheikh wa Wilaya ya Mkuranga, Sheikh Hamas. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sabu, jiandae Mheshimiwa Shangai.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara, inayoongozwa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu wake Mheshimiwa Alexander Mnyeti, pamoja na watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, amekuwa msikivu sana kwenye Kamati. Wakati wote tulipokuwa

tukimshauri amekuwa akitupa ushirikiano. Pia niwapongeze na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Profesa Shemdoe. Kiupekee kabisa niungane na wote waliochukua nafasi kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tunampongeza kwa tukio alilolifanya tarehe 30 Mwezi Januari, 2024 katika Mkoa wa Mwanza, la kuwakabidhi wavuvi boti 160 na vizimba 222. Kiukweli kabisa tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wamenufaika zaidi ya watu 16,000 na hasa wanawake na vijana. Tumeona katika bajeti ijayo zitaongezeka boti 497. Hii ni mara tatu zaidi ya ambazo zimetolewa awali. Kiukweli tunaipongeza sana Wizara kwa maono haya makubwa na mazuri kwa ajili ya wavuvi wanaozungukwa na Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiupekee kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa mambo mbalimbali ambayo wanayafanya, hasa katika eneo la mbegu za malisho. Kama Kamati tumepata fursa ya kutembelea katika eneo la Pwani na Kibaha. Tumejionea namna ambavyo Wizara inatekeleza mradi huu. Kiukweli tunawapa hongera sana. Tusisitize tu, kwamba mbegu hizi za malisho ziwafikie wafugaji wote katika maeneo yote ambayo wanajihusisha na ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza programu ya unenepeshaji wa ng'ombe kupitia *NARCO* ambapo mradi huu umewagusa vijana wa *BBT* na wanawake. Tunashukuru Wizara kwa maono haya mazuri ambayo yatasaidia kuwa na wafugaji vijana katika mradi huu wa unenepeshaji wa ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa Mradi wa Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa. Nafahamu kwamba mradi huu unatekelezwa katika Mkoa wa Kigoma mahususi kwa ajili ya vijana na wanawake. Nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa ajili ya mradi huu. Kama ambavyo tuliahidi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, kwamba, tutatengeneza ajira kwa vijana na wanawake; sasa

nisisitize kwamba mradi huu uendelee kuwa endelevu. Ikimpendeza Mheshimiwa Waziri atafute fedha ili aweze kupeleka katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Simiyu tuna maeneo makubwa na mazuri kwa ajili ya mradi huu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atuletee mradi huu ili uwanufaishe vijana wa Mkoa wa Simiyu kuweza kufuga kisasa, lakini kuweza kufanya ufugaji wa ng'ombe hususani katika upande wa maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa namna ambavyo imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji. Niendelee kusisitiza; na Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake kwamba ana mpango wa kuleta *guest house* kwa ajili ya wafugaji. Nimwombe, kama ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, kwamba tuliahidi kupima maeneo ya wafugaji na kuwamilikisha wafugaji maeneo kama ilivyo katika ilani ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize, kwamba ili kuondoa changamoto ya migogoro ya wafugaji na wakulima, Mheshimiwa Waziri atafute namna ya kutengeneza jambo hili ili kuweza kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji na kuondoa migogoro ambayo imekuwepo. Hii itatuwezesha kuwasaidia wafugaji kupata maeneo mazuri na kuwatengenezea miundombinu bora itakayowawezesha kuondokana na changamoto za migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika hotuba ya bajeti pia kwamba Wizara itaendeleza chanjo na uchanjaji wa mifugo. Niwapongeze mawaziri wa mifugo katika eneo hili. Pia, niendelee kusisitiza kwamba, chanjo za mifugo ni muhimu hivyo ziweze kuwafikia wananchi kwa wakati katika maeneo yote ambayo yanajihusisha na ufugaji wa ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili litatusaidia kuweza kuhakikisha kwamba mifugo inakuwa katika viwango ambavyo ni vizuri ili wale wafugaji ambao wanasafirisha mifugo yao kwa ajili

ya kutafuta masoko ya nje waweze kusafirisha na kufikisha mifugo ambayo ipo katika namna nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa fursa hii. Naunga mkono hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sabu kwa mchango wako.

Waheshimiwa, kuna wageni wengine ambao Mheshimiwa Waziri wa Mifugo anaomba kuwatambulisha. Kwanza ni Mchungaji Adam Kitungulu wa Kanisa la KKKT, Mkuranga na Wenyeviti wa Vijana Wilaya zote za Mkoani Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti wa Vijana Mkoa wa Pwani Ndugu Samaha Seif. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wageni wako hawa tangu asubuhi sijaona kwenda hata kunywa chai, hata chakula cha mchana. Sasa wageni mliokuja kawaida ya Bunge mkiletwa hapa na mwenyeji lazima awalishe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri haya ni maelekezo na uyatekeleze. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Shangai.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi kwa ajili ya mifugo na uvuvi. Tukijaribu kuangalia kwa sasa hivi hatujaona kama Wizara imeweza kusimamia jukumu hili; kwa sababu wafugaji wa Tanzania, kama alivyosema hapa ndugu yangu Mheshimiwa Kunambi, wamekuwa kama watu ambao hawana mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji wa Tanzania kama tunavyowazungumzia na kwenye hotuba yake amesema kwamba mifugo yetu imeongezeka; kwamba sasa hivi tuna ng'ombe milioni 37.6, mbuzi 27.6 *million* na kondoo milioni 9.4. Sasa hii mifugo yote inatakiwa kuwanufaisha wafugaji hao wa Tanzania. Kwa hiyo hao wafugaji ili waweze kunufaika ni lazima wawe na maeneo kwa ajili ya kulishia mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri mwenyewe ajue kwamba katika maeneo yote ambayo Wizara ya Mifugo ilipima kwa ajili ya wafugaji wa Wilaya ya Ngorongoro, Monduli, Kiteto, Simanjiro na Longido. Maeneo yote yaliyopimwa na kuwekwa kwenye Gazeti la Serikali, kama ni maeneo ya malisho, yote yamechukuliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa nini wao kama Wizara ya Mifugo wanayaruhusu haya? Leo ametuletea hoja ya kutaka kuanzisha mamlaka kamili kwa ajili ya mazao na miundombinu ya mifugo ambayo wote tungependa yatokee. Sasa hii mifugo ambayo hatuna maeneo ya malisho tutawalishia wapi kama hatuwezi kusimamia maeneo yao ya malisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kumshauri Mheshimiwa Waziri, ili Watanzania na wafugaji wa Tanzania waweze kunufaika na mifugo yao na ili uchumi wa Tanzania uweze kupanda kutokana na mifugo hiyo ni lazima tuwe na maeneo ya uhakika ya malisho na kuondoa migogoro kati ya wafugaji na wakulima nchini Tanzania. Kwa sababu tusipofanya hivyo hao wafugaji wanakuwa wanatembea kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea kwa mfano Wilaya yangu ya Ngorongoro, eneo la Kijiji cha Engaresero, eneo ambalo lilipimwa ni la Reparkashi. Eneo hilo limechukuliwa na Wizara ya Maliasili, ambalo ni eneo la mifugo, ni eneo ambalo lipo kwenye *GN* ya Serikali kwenye Gazeti la Serikali, lilitangazwa kama eneo la malisho. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kuangalia maeneo ya malisho; kwa sababu wafugaji kama hawana malisho maana yake ng'ombe wao watakufa na uchumi wa Tanzania utashuka kwa sababu hatutanufaika na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, miongoni mwa majukumu mengine ya Wizara ni kuzuia magonjwa mbalimbali ya mifugo. Kwa sasa hivi kuna magonjwa mengi sana, ili sasa tuweze kuzuia ni lazima Wizara ihakikishe kwamba kila kijiji nchini Tanzania kina majosho ya kutosha kwa ajili ya kuogesha mifugo, kama tunataka kuzuia na kutibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba Wizara ije na mkakati na kwenye hili baadaye nitamshikia shilingi; aje na mkakati atuambie sisi wafugaji kwamba Wizara imejipanga vipi na chanjo kwa ajili ya magonjwa mbalimbali Tanzania. Kwa sababu tuna magonjwa mengi sana ambapo tungechanja tungeweza kuzuia magonjwa mengi; lakini kila wakati ukienda kwenye maabara yetu tunasema bado tupo kwenye uchunguzi. Wapo kwenye uchunguzi mpaka lini? Unajua wafugaji wanapoteza mifugo mingapi kwa ajili ya *PPR*? Au unajua kwamba wafugaji wanapoteza mbuzi na kondoo wangapi kutokana na ugonjwa wa *coenurosis,* ugonjwa ambao unatokana na kirusi anayeitwa *taenia multiceps*? Ng'ombe, mbuzi wanapotezwa kwa sababu hatuwezi kuzuia. Tukiweza kuzuia tungeweza kuzuia hawa ng'ombe wasife wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka Mheshimiwa aje atuambie kwamba amejipanga vipi kwa ajili ya chanjo ya *ECFF* kwa wafugaji? Amejipanga vipi kwa ajili ya *PPR*? amejipanga vipi kwa ajili ya *CCPP?* Pamoja na chanjo ya ugonjwa *holimilo* kwa Wamasai wanasema hivyo. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri; yeye kama Waziri wa Mifugo tunataka kuona mbwebwe zake kwa wafugaji wa nchi hii. Tumpongeze sana na niunge mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, jioni tutaanza na Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Shally Raymond. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 Jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa nimeshamtaja Mheshimiwa Nollo, wajiandae Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Raymond. Mheshimiwa Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nchi yetu kwa sasa tuna viwanda karibu 10 vya kuchakata nyama kwa ajili ya kuuza nje ya nchi. Katika viwanda hivi 10 viwanda tisa vyote ni binafsi na kiwanda kimoja tu ni cha Serikali (machinjio ya Serikali) na machinjio hayo yapo hapa Dodoma, Machinjio ya Kizota. Katika viwanda hivi vingine vinavyobaki tisa vingine ni kama nilivyosema vya watu binafsi vingine vya *EPZA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa tatu mfululizo nimekuwa nachangia kuomba Machinjio ya Kizota ipate fedha, nimeomba kwa miaka mitatu mfululizo na wala sio fedha nyingi ni shilingi bilioni mbili tu. Mheshimiwa Ulega ni rafiki yangu, amekuwa Naibu Waziri nikiomba bilioni mbili kwa ajili ya kiwanda kile, amekuwa Waziri naomba bilioni mbili kwa ajili ya machinjio yale na machinjio yale yanasaidia sisi hapa Dodoma. Napata shida kuelewa ni kitu gani kinawapa uzito kukarabati kiwanda kile na wafanyabiashara wetu kwenye maeneo ambayo wanataka wapelekwe wanafanyiwa hujuma, hawawezi kufanya kazi kule na hawawezi kusafirisha. Kwa hiyo, jambo hili sitakuja kulisema tena, lakini ni jambo ambalo linanisikitisha sana na Waziri anajua watu wetu wanavyopata shida na hujuma wanazofanyiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri kukarabati kiwanda kile, kukarabati machinjio yale ili wafanyabiashara wetu waweze kuuza nje ya nchi. Kwa sasa Machinjio ya Kizota yanaruhusiwa kupeleka nyama katika nchi moja tu, nchi nyingine zote wamezuia kutokana na uchakavu na miundombinu ambayo haipo sawasawa. Hili jambo linasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopeleka habari ya kuzuia au waliotoa taarifa katika nchi hizo kwamba kiwanda kile ni chakavu ni washindani wao katika hivi viwanda tisa. Kwa hiyo, tunapata Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, kutoa nyama hapa Dodoma kuipeleka Dar es Salaam inachukua muda mrefu, lakini itakuwa ni dakika 30 unachukua nyama machinjio ya Kizota tunapeleka kwenye uwanja wa Masalato, nyama inaondoka masaa manne ipo Oman, Kuwait au Quatar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kiwanda hiki Waziri amekipeleka *Ranch* ya Kongwa, lakini pamoja na hiyo huu mwaka wa pili na kama nilivyosema uwepo wa Uwanja wa Ndege wa Msalato itakuja kufungua sana machinjio yetu na biashara yetu ya nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Kamati imesema, mnada ule wa Holoholo ushuru wa ng'ombe ni 30,000 na Kamati inapinga kwamba ni hela nyingi. Mimi napinga wazo la Kamati kwamba si hela nyingi, kwa sababu tuna viwanda vya kutosha, vipo 10. Unataka ng'ombe wetu wapelekwe nje ya nchi na wakipelekwa nje ya nchi nao wanafanyiwa *processing*, wanauzwa kwenye masoko ambayo tunaenda kushindana nao, lakini kwako hapo wamechukua bure na wanakuja kununua kwenye minada yetu ya kawaida katika *price* zetu za hapa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema, ushuru pale uwe ni shilingi 100,000, ng'ombe kutoka nje ya nchi. Tena ni hela ndogo sana, walau iwe hata 200,000 kwa ng'ombe. Lengo si kupata ushuru, ng'ombe wako waende nje, tunachotaka ng'ombe wabaki hapa kwa sababu, tuna machinjio ya kutosha ili tuweze kuuza sisi wenyewe lakini mbuzi kupelekwa nje ya nchi kuvuka

pale mpaka wa Namanga ni 6,500, *that is a dumping price,* nataka na mbuzi angalau iwe shilingi 50,000. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wala sio sifa kumuuza mnyama akiwa hai, kuwapelekea nchi jirani, sio sifa na kwa dunia hii ya leo unapeleka mnyama akiwa hai, huwezi ku-*process,* nyama inaenda kwenye nchi Jirani, ng'ombe anachinjwa halafu tunakutana kwenye masoko. Ninachotaka kusema hata 50,000 kwa mbuzi bado kidogo angalau wafanye 100,000, ng'ombe iwe 200,000 iwe 300,000. Lengo ni ku-*discourage,* tusipeleke wanyama wetu wakiwa hai kwenye nchi majirani zetu ambao tena katika masoko yale tunaenda kukutana nao, Mheshimiwa Waziri naomba sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu Jimbo langu nina mambo mawili. Kuhusu wafugaji katika Kata ya Zanka. Kata ya Zanka tumeingiliwa na Serikali. Kuna upande bonde la maji wamechukuwa kwamba wafugaji hawatakiwi kuingia huku. Ukivuka lami kidogo jeshi nao wamechukuwa kwamba ni eneo la mazoezi. Kwa hiyo, wananchi wa Kata ya Zanka hasa hasa Kijiji cha Zanka kimsingi hawana pa kulisha ng'ombe, huku unakutana na bonde mkono wa kushoto, huku unakuta jeshi wanasema wanataka kufanyia mazoezi, sasa na hilo ni jambo la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli kwa dunia ya sasa hivi ufanyie mazoezi hapo Zanka? Urushe mambo yako hapo Zanka? Kwa hiyo, naiomba sana Serikali jambo hili waliangalie walifute. Kama ambavyo Mawaziri wale nane walizunguka hapa ni karibu, waende wakafute ile ni aibu na wananchi wanatushangaa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nollo ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuzungumza kidogo kwenye hii hoja ya Waziri wa Uvuvi na Mifugo. Bahati nzuri nimesikiliza vizuri bajeti yake na nimeisoma. Kusema ukweli imekaa vizuri. Naendelea tu kuwapongeza na kuwapa moyo kwamba waendelee na kazi yao pasipokuwa na shaka yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tu kwenye maeneo mawili; eneo la kwanza ni eneo la uvuvi. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka fedha nyingi. Wameweza kutusaidia kuongeza ajira kwa kuleta vizimba hasa katika Ziwa Victoria na hususan katika Mkoa wangu wa Mara na Mji wangu wa Musoma vilevile wameweza kufaidika na msaada huo. Niwaombe tu, kwa sababu wameahidi wataendelea kutoa vizimba zaidi, nimwambie tu Mheshimiwa Waziri, watu wangu wapo tayari na vikundi vyao vipo tayari na wanasubiri kwa hamu sana ili waendelee kupata ajira kutokana na hii fursa ambayo Serikali ya Mama Dkt. Samia imeamua kuitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu tu mambo mawili yanapaswa yafanyike au kuna changamoto mbili ambazo zinatusumbua. Kwanza kwenye upande wa uvuvi kwa kutumia vizimba. Shida kubwa ambayo tunaipata ya kwanza ni tatizo la chakula. Tatizo la chakula kwa maana kuwa chakula ambacho kinatolewa au kinachouzwa sio chakula sahihi cha kukuza wale samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwa utaratibu kile chakula samaki wanapaswa wale ndani ya miezi sita na wao wameshakuwa na umri wa kuuzwa ambao sio chini ya gramu 500, lakini kwa bahati mbaya sana kwa sababu chakula kinachouzwa sio sahihi unakuta kila mara samaki wanafugwa mpaka miezi 10 lakini wanaishia gramu 300. Kwa hiyo, wanasababisha gharama ziwe kubwa kwa mfugaji na mwisho wanaona kama sio biashara ya kufanya, lakini tukipata chakula sahihi chenye *content* sahihi ni

rahisi sana watu wengi wakaingia kwenye biashara hiyo na biashara hiyo ikaendelea kuwapatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ana kazi ya ziada ya kuhakikisha kwamba wataalam wake kwanza wanakagua vile vyakula vinavyouzwa kulingana na zile *content* ambazo zimeandikwa na kuona kama ni sahihi. Vilevile kututafutia *formula* halisi itakayoweza kutusaidia kuhakikisha kwamba tunapata chakula ambacho ni bora na chakula cha kuwasaidia watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo wakati mwingine ufugaji ule wa njia ya vizimba maana yake ni kwamba ikitokea aina yoyote ya *pollution* kwenye maji kwa maana ya sumu ya aina yoyote ile tafsiri yake ni kwamba wale samaki wote ambao umeweka kwenye ile *cage* moja *either* ni 40,000 au 30,000, matokeo yake wale samaki wanakufa. Hata mwaka jana nakumbuka kule kwetu watu wengi samaki wao walikufa na ilisemekana kwamba kuna sumu ilimwagwa kutoka huko juu, lakini hata wale wavuvi haramu nao imekuwa ni tatizo kubwa maana kila ikitokea tu kwamba wamevua kwa uvuvi haramu inatuathiri na inasababisha hata wale samaki ambao wanafugwa kwa bahati mbaya wanakufa na hii inakuwa ni hasara kubwa kwa yule ambaye ni mtegaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa bure hapo na hili Mheshimiwa Waziri nakumbuka kwenye bajeti iliyopita aliahidi. Tulisema ili tuweze kudhibiti vizuri uvuvi haramu, lakini ili tuweze kuhakikisha kwamba uvuvi unakuwa mzuri tuhakikishe kwamba tunakuwa na mamlaka ya uvuvi ambayo hiyo mamlaka itatusaidia kuhakikisha hiyo shida ya uvuvi haramu inaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa sababu muda wangu umekwisha, nampa Mheshimiwa Waziri hii nakala ya vile viwanda vya nyama, vimebaki viwanda viwili ndiyo vimeruhusiwa ambacho ni Kiwanda cha Bagamoyo na Kiwanda cha Mpakani…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Manyinyi, mengine utaandika.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO**: Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nalo atalifanyia kazi. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, jiandae Mheshimiwa Ole-Lekaita.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu. Nianze kuipongeza Serikali kwanza kwa kuongeza bajeti ambayo inakuja kutekeleza miradi mingi hasa kwenye Sekta ya Uvuvi, lakini niende moja kwa moja kuchangia mchango wangu juu ya kufungwa kwa Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Serikali imefunga Ziwa Tanganyika kuanzia mwezi Mei, lakini zipo changamoto kubwa sana kwenye eneo la mkoa wangu na eneo la Jimbo la Mpanda Vijijini. Ninavyo Vijiji saba vya Karema, Ikola, Itetemya, Shukula, Isengule na Kasangantongwe ambavyo maisha yote ya wananchi wa vijiji hivyo yanategemea shughuli za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana mwaka huu tumepata mafuriko karibu vijiji vyote. Hali ya maisha yao ni duni na shughuli ambazo wanazitegemea ni shughuli za uvuvi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atueleze njia mbadala za kuwasaidia wale wananchi ambao maisha yao yote wanategemea shughuli za uvuvi katika kipindi cha miezi hii mitatu itakayokuwa haiwaruhusu kuvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha kuweka angalizo na katazo la kutokuvua kwenye Ziwa Tanganyika ni uvuvi haramu. Asilimia kubwa ya uvuvi haramu upo kwenye nchi jirani, Nchi ya DR Congo na Nchi ya Burundi ndiyo wanaovua sana uvuvi haramu ambao upo kwenye Ziwa Tanganyika. Kwa bahati mbaya Serikali wameshindwa kudhibiti uvuvi haramu hata kama wale walipewa dhamana ya kusimamia uvuvi haramu kwenye

maeneo hayo ambao ni watu wa Serikali wanashindwa na wanashirikiana na hao hao ambao wanavua uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri waliangalie hili jambo kwa kina na mapana na marefu ili tuone tunatokaje kwenye hili jambo. Mimi binafsi sikatai kwa wazo la *protocol* iliyosainiwa ya Nchi ya Zambia DR Congo, Tanzania na Burundi, lakini tutafute mfumo sahihi ambao tutalinda rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mkoa wa Katavi hatujapata vizimba, tunavyo vizimba viwili tu ndani ya mkoa kwenye eneo la vijiji saba. Nimwombe Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind up* hotuba yake atueleze watu wa Mkoa wa Katavi, wavuvi wale watanufaika vipi na atapeleka vizimba kiasi gani kwenye maeneo hayo. Halikadhalika boti, wananchi wengi ili waweze kunufaika tunahitaji boti za kisasa za uvuvi. Amepeleka kwenye maeneo mengine tofauti kabisa kwenye eneo la Mkoa wa Katavi kuna boti moja tu. Tunaomba kundi la wavuvi wawapelekee boti za kutosha ambazo zitawasaidia kuvua uvuvi wa kisasa. Sambamba na hilo tunaomba boti za doria ili ziweze kusaidia kulinda rasilimali na wale wafanyakazi walionao waweze kufanya kazi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo napenda kuchangia ni suala la wafugaji. Mkoa wa Katavi una ng'ombe wengi, mbuzi na mifugo mingineyo. Kwa bahati mbaya sana bado Serikali haijapeleka vitendea kazi kwa maana ya kuwachimbia mabwawa, malambo, majosho. Kwa hiyo, naomba maeneo haya wayafanyie kazi ili waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Olelekaita wajiandae Mheshimiwa Raymond na Mheshimiwa Mabula

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na timu nzima. Changamoto za wafugaji nchini tunahitaji maeneo ya malisho ya kutosha. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tulisema tutatenga maeneo kutoka hekta milioni 2,700,000 mpaka milioni 6,000,000, lakini kwa trendi ya mambo yanavyokwenda ni kama yanapunguzwa. Sasa wanaopunguza wanatumia Ilani ipi? Tunataka majibu hapo. Maeneo haya yakilindwa kisheria na ng'ombe wakapata sehemu ya kulishwa vizuri, hii sifa wanayosema kila wakati kwamba Tanzania ni Nchi ya pili kwa mifugo itapata tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, tunataka mabwawa kwenye maeneo haya ili wafugaji waweze kutulia. Mheshimiwa Mnyeti wewe unafahamu Kiteto ni kame, Mheshimiwa Waziri ulikuja Kiteto tulipoteza ng'ombe karibu 25,000 lwa ukame. Kwa hivyo lazima tuweke pesa nyingi sana kwenye mabwawa; na Bwawa la Kaiwang Mheshimiwa Waziri anafahamu, tulitembelea na nimeona kwenye bajeti yao hapa, sasa lazima iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni chanjo za mifugo, maeneo yakishatengwa, tukapata mabwawa chanjo ziwepo na tunataka ruzuku ya Serikali tuione kwenye chanjo hizi. Ng'ombe wengi sana wanakufa kwa sababu ya kukosa chanjo za uhakika. Kwa hivyo *it's that time* sasa nchi waanze kutuonesha kwamba chanjo za uhakika zinapatikana wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu mnataka tuboreshe ng'ombe, hizi mbegu mnazoleta zinauzwa ghali sana. Tuuzieni 500,000, 1,000,000 tutanunua lakini kama hampunguzi hatubadilishi. T

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza kuhusu maeneo mengi sana ya wafugaji yanayochukuliwa na hifadhi na nyinyi mpo na Mheshimiwa Mnyeti wewe unafahamu, vurugu za watu wa hifadhi. Sasa inafika mahala inaonekana kwamba ng'ombe sasa sijui hata watoto wanaokuja sasa wanaanza kuona kama mifugo ni mbaya kufuga mifugo wakati ni uchumi kama ilivyo uchumi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo Wizara i-*promote* ili wananchi wafahamu. Kumekuwa na *tendency* fulani watu wana-*generalize* vitu, wafugaji wanafanya hivi, sasa tukienda hivyo hatutajenga taifa imara ambalo kila mtu ana thamani. Kwa hiyo lazima tuwe *careful* na *statement* kama hizo. Hakuna shamba la ujamaa wala hakuna mifugo ya jamii nzima, Ole Kaita akiingiza ng'ombe shambani ni Ole Kaita na anayelima akilima maeneo ya kilimo ni Juma, kama ni Juma, kama ni Ally kama ni nani iwe hivyo. Lakini tukiseme tuki-*generalize* tukisema wafugaji, sijui wakulima, tunafanya nchi tu ionekane kwamba kuna mgawanyiko sio wa lazima sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu minada ya mifugo. Kiteto kuna minada mikubwa mitatu, Dosidosi, Kibaya na Sunya. Tunataka sasa muanze kutengeneza minada hii iwe na hadhi, ili wafugaji wapate sehemu ya kulishia mifugo. Hata leo wakati Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanasema wakulima ukiwa na tani moja hautozwi faini, kuna wafugaji wananiandikia hapa; hivi tani moja ya ng'ombe ni ng'ombe wangapi, ili na sisi tufahamu? Kwamba, ukiwa na ng'ombe wangapi na wewe haulipi kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe na *system* ambazo ni *fair* kwa kila mtu. Kwa hiyo, utatuambia baadaye rafiki yangu kwamba, tani moja ya ng'ombe ni sawa na ng'ombe wangapi, ili na sisi tufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *BBT*. *BBT* ni jambo zuri sana na tunawakaribisha hao wafugaji wapya, lakini msiwasahau wafugaji ambao tayari wako huko wanafanya hizi shughuli. Hebu tafuta pesa sasa za kuwasaidia wafugaji ambao tayari wanafanya hizi kazi za mifugo wakati unaendelea kuwafundisha hawa wapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la majosho na kwenye ilani tumesema hivi, ng'ombe wakiwa na afya watawezesha kufanya biashara hii tunayosema tuondokane na magonjwa. Leo majosho nchini, kwa mfano mimi Kiteto nina upungufu wa

majosho karibu 40 na kitu, ni vyema Serikali iweke hela, ili majosho yapatikane ya kutosha kwa ajili ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamezungumza kuhusu ng'ombe kwenda nje na mtu anasema sijui ni laki tatu sijui? Mahindi pia, yakivuka iwe ni bei gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani, unajua hakuna mtu ana *interest* ya kupeleka ng'ombe huko nje. Masoko yakiimarika hapa na bei ikiwa nzuri kila mtu atauza hapa, lakini haiwezekani tuseme mahindi yapelekwe halafu mifugo sijui tufanye nini? Na tuwe *careful* na lugha kama hizi kwa sababu, zinaleta mkanganyiko ambao siyo wa lazima sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo katika nchi hii ni uchumi kama ulivyo uchumi mwingine wowote. Mheshimiwa Ulega, sijui siku moja na wewe utaanza kutengeneza mazizi tukamate wanyama pori tuwaweke kwa sababu, wanakuja huku wanakula nyasi. Wao wakiondoka hivyo halafu mifugo hakuna mwingiliano. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward, ahsante. Mheshimiwa Raymond, ajiandae Mheshimiwa Mabula.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninakiri kwamba, Mungu ni mwema ametujalia tena wakati mwingine. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yao yote ya Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongeza hiyo hela waliyoomba ikafikia shilingi 460,333,600,002, lakini bado kwangu naona ni kidogo, tena ni kidogo sana. Nilitarajia itakuwa mara tatu au hata mara nne kwa sababu, tunapozungumzia kilimo shilingi trilioni moja na kilimo ni kwenye ardhi tu, hawa mifugo wako juu ya ardhi na kwenye maji na hela yenyewe hii ni kidogo. Namwomba sana Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni msikivu aangalie vizuri hili eneo. Hili eneo ni muhimu kwetu kwa ajili ya chakula tuweze kupata *balanced diet,* lakini pia, kwa ajili ya *export.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia huku ndani kuna waumini wengi wa Janabi. Kwenye ile sahani inatakiwa *three quarters* ndiyo iwe *protein* na kingine iwe *carbs,* yaani *carbohydrates,* na kadhalika. Ukiangalia *protein* inatoka kwenye Wizara hii tu. Sasa watoto wanakuwa na *kwashiorkor*, wazazi tunakuwa na viribatumbo, na kadhalika, tutafika kweli? Maradhi yasiyoambukiza, kama sisi wenyewe hatuli vizuri *proteins*, hatuwezi kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Wizara ya Kilimo wametuambia kuwa, kuna *BBT* ambayo mpaka sasahivi kuna vijana 161 na wametoka kwenye mikoa 26. Ukigawanya ina maana kila mkoa umetoa watu sita, ni kidogo sana, lakini ili *BBT* iwe *sustainable* kwa vile tuna sera, ni kwa nini badala ya kutumia hizo hela kuanzisha ma-*block farms* madogo-madogo, wasipelekwe JKT? Hapo kutakuwa hakuna ugonvi. JKT kuna nidhamu, watafundishika na watarudi hapa wakiwa wamekomaa, litakuwa ni jambo zuri. Kwa hiyo, naishauri hii Wizara waingie mkataba na JKT, ili waweze kuwa-*train* watu wao huko vijana warudi wakiwa wamekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili jambo liletwe hapa tutunge sheria. Leo Mheshimiwa Bashe yuko kwenye hii Wizara ya Kilimo, kesho akitoka anaweza akaja Mheshimiwa Waziri mwingine akaamua anavyotaka. Hayuko tena *BBT* anarukia kwingine, lakini kama ni Sheria na sera ziko mahali pake ni lazima wote tutaendelea na mfumo huo na tutazidi kujikuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze sana wafugaji au watu *private* ambao wanaoendesha shughuli hizi za mifugo, wakiwemo watu wa dini, huko *mission* au kwenye vyuo vya misikiti vya Mabaraza ya Kiislamu, lakini pia hata hao wakubwa. Leo tumekuwa na *ASAS*, tumeona banda zuri pale na wale wengine wote. Nawapongeza wajasiriamali wote ambao wako kwenye hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kuoneshwa na tumeonja mazao yao, lakini nimekuja hapa na ombi na kilio. Kila bajeti huwa nakuja na kilio na ombi hilo. Ni rahisi sana kwa

mwanamke yoyote wa kijijini kufuga kuku, mbuzi, kondoo, wanyama wengine na pia, ni rahisi hao wanyama kuchukuliwa na kutumika nyumbani. Tunapata mayai, samadi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwomba Mheshimiwa Waziri tufanye *cross-breeding*. Imefanyika kule kwenye Jimbo la Vunjo, lakini ng'ombe wetu wale wadogo hawakuweza kubeba yule ng'ombe mkubwa kwa hiyo, nyingi ziliharibika. Wanapotarajiwa kuzaliwa zinaharibika... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond, ahsante.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, jiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nitumie nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Pia namshukuru Mungu kwa kuturuhusu tuendelee tena kuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nichangie katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni la uvuvi wa vizimba na la pili ni la uvuvi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukitazama ongezeko la bajeti ndani ya miaka mitatu, kutoka shilingi bilioni 160 mpaka shilingi bilioni 460 ambayo inaongezeko la zaidi ya shilingi bilioni 291 tafsiri yake ni kwamba, iko kazi kubwa sana ambayo inafanyika kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu, babu yangu na mjukuu wa Wasukuma, Mheshimiwa Ulega. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Naibu

Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu wao na yeye ni mjukuu wa kule Usukumani, Shemdoe, kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nataka kuongelea maeneo mawili. Nimesema hapa tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana aliyoifanya miezi michache iliyopita. Kwa mara ya kwanza uvuvi wa vizimba katika nchi hii ulianzishwa miaka 10 iliyopita pale Nyamagana na Vijana wa Mpanju kwa kutengeneza bwawa la kuchimba. Leo, zaidi ya miaka 10 baadaye, tunazungumzia uvuvi wa vizimba uliotapakaa karibia Ziwa Viktoria lote na maeneo mengine pembezoni mwa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa sana ambayo Mheshimiwa Rais muda mfupi uliopita alikabidhi maboti zaidi ya 160 na vizimba 222 katika tukio lililofanyika pale Nyamagana, tukio hili siyo dogo. Ukitazama uhalisia wake ni tunafahamu vijana kwenye vikundi, makampuni mbalimbali na hata mtu mmoja mmoja wamenufaika na utoaji wa vizimba hivi pamoja na mikopo ambayo kiukweli ukitazama kwenye Sekta ya Uvuvi, vijana wetu wamekwenda kupata ajira. Halikadhalika vijana wametengenezewa mazingira rafiki ambayo yanawafanya wasikimbizane sana na mambo mengine kwenye biashara ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote viwanda vinavyotengeneza hizi *cages* viko Mwanza, pale Nyamagana. Tafsiri yake ni kwamba, vimeendelea. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa sababu, umeendelea kutoa ajira kwa namna tofauti tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwenye hii hatua inayofuata ya *cage* 800 na zaidi ya maboti 490, tungeweza kuamua. Kwa sababu, ya changamoto zilizoko katika maeneo mengine, sio vibaya wakiamua kuchukua miaka mitatu waangalie kwa Ziwa Victoria peke yake na baadaye watoke nje, ili watu wawe wamepata ufahamu vizuri kuhusu *cages* na namna ya kuzifanyia kazi, ili vijana wengi zaidi waweze kupata kwenye Ukanda wa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ni kubwa, namwomba sana Waziri atazame vizuri, hasa tunapozungumzia habari ya chakula, ni kingi, lakini gharama yake ni kubwa sana. Jambo la pili ni, atazame namna watengenezaji wa maboti wanapoanza matengenezo ni lazima mkubali kuwashirikisha wadau wenyewe ambao ni watumiaji wa haya maboti, ili yawe na tija na manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, jambo la pili ni uvuvi asilia. Naomba hapa nishauri vizuri; kama unavyofahamu, pamoja na uwekezaji mkubwa ambao tunaufanya, pamoja na jitihada kubwa ambazo anazifanya Mheshimiwa Rais, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, hatuna mbadala wa uvuvi asilia. Ni lazima tuwekeze nguvu kwenye uvuvi asilia. Ndiko kodi inakopatikana, ndiko kuna ajira nyingi, ndiko kuna mchakato mkubwa... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Mheshimiwa Tabasamu na Mheshimiwa Magessa, mjiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuishukuru Wizara nzima, nasema hongereni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya na kwa hotuba nzuri mliyoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba niongelee kuhusu malisho pamoja na mambo mengine. Mifugo inahitaji chakula, maji na chanjo kusudi iwe na afya. Kwa hiyo, niongelee kwenye upande wa malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, upande wangu wa Morogoro, ili upunguze migogoro ya wafugaji na wakulima ni lazima uwe na malisho mazuri. Kwa hiyo, nasema ingawa Wizara imesema jinsi ya kueneza malisho, naomba sana wafugaji wote waweze kupata elimu ya kuwa na malisho, ili kusudi kupunguza migogoro ya wafugaji na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ni ingawa Mheshimiwa Waziri amesema kuwa mbegu zipo, lakini nasisitiza

kuwa mbegu ziendelee kuzalishwa kwa wingi na ziweze kuonekana madukani. Pia, elimu itolewe, Maafisa Ugani waweze kuwa karibu na wafugaji, ili waweze kupata elimu ya kilimo cha majani haya ya malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni, naongelea kuhusu kuku wa kienyeji. Watu wote humu mnapenda kuku wa kienyeji na watu wengi wanapenda kuku wa kienyeji, lakini sijasikia vizuri kwenye hotuba jinsi ya kuendeleza kuku wa kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake na vijana wengi wanafuga kuku wa kienyeji. Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind up*, naomba aniambie jinsi ya kuendeleza kuku wa kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naongelea kuhusu mambo ya uhaba wa samaki. Uhaba wa samaki ni kwa sababu ya uvuvi haramu. Uvuvi haramu umeanza muda mrefu na kuudhibiti imekuwa kazi. Mheshimiwa Waziri namwamini, kijana wangu namwamini, naomba sana uhaba huu wa samaki usiendelee kutokana na uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhaba wa samaki viwanda mbalimbali vimefungwa, bei ya samaki imekuwa juu na bado nchini tuna utapiamlo. Tumesema, samaki anachangia 30% ya protini, lakini kama bei iko juu watu hawawezi kununua samaki. Kwa hiyo, nakuomba sana, uhaba huu na uvuvi haramu uweze kutokomezwa kabisa. Naomba sana uangalie ufugaji wa vizimba na ufugaji wa mabwawa, ili kusudi tuweze kuwa na samaki wa kutosha ambao wanaweza kuenea na kuwa na protini ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni kuhusu *BBT*. *BBT* ni nzuri sana, ninaomba uiendeleze. *BBT* kwa upande wa unenepeshaji wa mifugo naona mmeanza vizuri kwenye mikoa mbalimbali, ikiwepo Kikurura na Kongwa, jana tumeona wamefanya mambo mazuri sana. Naomba yaendelee, ili kusudi vijana na akinamama waweze kuendelea vizuri kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *BBT* inatoa ajira, inaongeza pato la Taifa, inaongeza pato la familia na vijana wanapata ajira. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie sana kuhusu hiyo *BBT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nikiwa na dakika ya mwisho, naomba niongelee mtiririko wa fedha. Naomba sana mtiririko wa fedha uwekwe vizuri, hela zote ziweze kutoka kama zilivyobajetiwa na miradi yote iweze kutimia vizuri. Naamini kutokana na mifugo, Pato la Taifa litakua kutoka asilimia saba na pato la uvuvi kuwa asilimia moja *point* nane. Namwomba sana Waziri aangalie hilo na Mwenyezi Mungu awabariki Wizara nzima, wafanye kazi nzuri, naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tabasamu. Mheshimiwa Magessa na Mheshimiwa Yustina Rahhi, mjiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi nina maeneo manne tu ya kuchangia, kama dakika moja moja tu Mungu akinijalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni kwamba, ninamshukuru sana Waziri wa Mifugo, Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, pamoja na Naibu Waziri, Ndugu yangu Mheshimiwa Mnyeti. Hawa wote ni ndugu zangu wa karibu sana. Nawashukuru wamekuja Sengerema na wameona changamoto zilizopo Sengerema. Sasa nikiwakumbusha changamoto zilizopo Sengerema haitakuwa sawa kwa sababu, wanazijua. Sasa nitategemea leo hapa wamenipangiaje, kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu yangu Shemdoe naye ni miongoni mwa watu wanaoyajua matatizo ya Sengerema. Tuna Soko letu la Samaki la Nyampurukano, hili ni soko la samaki wabichi. Samaki wale wanatumika sana katika maeneo mengi, Kahama, Misungwi, Kwimba, Nzega, Shinyanga na Tabora

wanategemea samaki kutoka Nyampurukano. Sasa soko hili, kitaalam, sijui wao wanaliona liko katika hali gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna soko ambalo limebeba uchumi wa Sengerema, Soko la Nyakaliro. Soko la Nyakaliro limekusanya zaidi ya visiwa 17 ambavyo vinaleta samaki pale. Hili soko limekuwa na mvutano kati yetu sisi na Kirumba. Soko la Kirumba, wenzetu wanakuwa na wasiwasi, hawa watu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwamba, wakitoa leseni kwa Soko la Nyakaliro ambako kuna uwekezaji mkubwa, Wizara imepeleka pale pesa zaidi ya shilingi milioni 700, tunashangaa kwa nini hawafungui hilo soko? Kwa hiyo, leo tunategemea majibu ya Mheshimiwa Waziri yaje hapa kwamba, tunafungua lini Soko la Samaki na Dagaa la Nyakaliro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuna Soko la pili la Dagaa la Kijiweni. Tumekwenda pale katika hili soko mara mbili na Mheshimiwa Ulega na hata Mheshimiwa Mnyeti amekwenda pale. Kuna ujenzi wa kimagumashi ambao uko pale unaendelea, lakini sitaki kusema sana hapa. Mheshimiwa Waziri anajua kwa sababu, huyo mkandarasi wanajua walikompata. Sasa sisi tunachotaka ni kazi yetu iishe na ule mradi pale ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sehemu ya uanikaji wa samaki wadogo (dagaa). Tumeomba vifaa vya kuanikia wakadai kwamba, tayari kuna wawekezaji, tumepata wataalam kutoka Uganda ambao watakuja kutuwekea namna ya kuanika dagaa pale Chifufu. Wananchi wa Chifufu sasa hivi wako kwenye *TV* wanasubiri kuona mwalo wao wa dagaa utatengenezwa lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuna Mwalo wa Furu wa Bungonya, kote huko tumekwenda na Mheshimiwa Waziri. Sasa tunakuomba jambo hilo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni, nataka kuzungumzia suala la mifugo. Sisi tuna Kituo kinaitwa Kishinda. Serikali ilijenga kituo kile kupitia Mheshimiwa Hayati Lowassa,

wakati ule akiwa ni Waziri wa Mifugo. Kituo kile kilikuwa kinaletewa mitamba pamoja na madume ya mfano yanayokuja kukaa pale. Kwa sababu, yale madume yalikuwa na kilo 500 tulitegemea kwamba, ule mradi ungekuwa ni mradi mkubwa kwa kuwa, ulikuwa ni wa majaribio. Serikali imeutelekeza, watu wa Wizara ya Mifugo wameutelekeza. Sasa tunaomba maelekezo ya Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tuna mabwawa, ameyatembelea haya malambo Ndugu yangu Mheshimiwa Ulega wakati alipokuwa Naibu Waziri leo amekuwa Waziri *Alhamdulillah* dua zetu. Katika watu wanaomwombea dua ni pamoja na mimi sijui anakuwaje? Sasa akanisahau mimi mpaka nikaingia kwenye matatizo jimboni kwa ajili ya haya malambo, mtani wangu inakuwaje ndugu yangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Mamlaka ya Uvuvi, hii Mamlaka ya Uvuvi kama Mheshimiwa Waziri kweli udugu wangu atakomea hapa na wewe kama hatakuja na majibu hii Mamlaka ya Uvuvi na Mifugo inaanza lini? Anaona wenzetu kule wamekuja na *RUWASA*, wamekuja na *TARURA*, leo wanakwenda vizuri, anafeli wapi? Nilimsikia Mheshimiwa Rais anamwita mwanangu Ulega, nikamsikia siku moja tena anamwita Mheshimiwa Mnyeti mwanangu, hawa wanakuwa ni watoto wa kambo kwa mama maana yake sielewi au wanamwogopa wakifika kule hawamwelezi kwamba sisi tunahitaji Mamlaka ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Bunge leo liazimie kuhusiana na suala hili. Wavuvi wanakuwa wanapata matatizo makubwa. Tuna uvuvi kule unaitwa luwa luwa na hawa Wakongo sasa hivi wamevamia Ziwa Victoria. Tunahitaji waje waone hawa *BMU* wanakuja kuwapa mafunzo gani waapishwe wale viapo. Tutengeneze *BMU* yenye nguvu ambayo itafanya kazi na halmashauri pamoja na Serikali za Vijiji ili tukomeshe uvuvi haramu ili Ziwa hili la Victoria liwe ziwa la kunywa maji ya kunywa, kweli inawezekana na siyo limebeba uchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanavyoanza kuchokonoa leo wanaanza kufunga Kigoma, najua wanaelekea kufunga Ziwa

Victoria. Sasa hapa itakuwa hatari kubwa Mheshimiwa Mnyeti ndugu yangu...

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana maana yake nitakwenda mbali zaidi. Mimi namwombea kwa Mungu na nasubiri majibu halali atakayonipa Waziri hapa leo Wanasengerema wanayasubiri. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magessa, wajiandae Mheshimiwa Rahhi na Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Bajeti hii ya Mifugo na Uvuvi. Jimboni kwangu kuna migogoro kati ya wafugaji na wakulima katika sehemu moja inaitwa Ludete na nyingine inaitwa Katangalo kwenye Kata ya Kaseme. Kwa hiyo nimechukua muda kutafuta kwa nini migogoro hii ambayo nimeitoa kwangu na sehemu nyingine ndani ya nchi hii inaonekana kama ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikalichukua eneo zima la Tanzania ambalo ni kilometa za mraba 945,087 ambazo ni sawa sawa na ekari milioni 233,535,723 lakini nikachukua ongezeko ambalo nampogeza Mheshimiwa Waziri kwamba ng'ombe wameongezeka kutoka milioni 36.6 mpaka 37.9. Sasa nikatafuta mahitaji ya hawa ng'ombe bila kuingiza kuku, mbuzi wala kitu kingine chochote katika ile mifugo. Kwa kawaida ukienda kwenye *researches* utagundua kwamba kwenye mazingira yetu ya uoto ng'ombe anaweza kula kuanzia ekari sita mpaka ekari nane. Ukipiga hesabu utagundua kuwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kuchunga hapa nchini kwa hiyo *free range grazing* inatupeleka kwenye milioni 303,200,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kimsingi hata kama ndani ya nchi hii wakabaki ng'ombe peke yao bado ardhi tuliyonayo haitoshi. Kwa hiyo sisi kama Watanzania tunatakiwa tuhame tutafute sayari nyingine, tuondoke na mbuzi na kuku kwa sababu ardhi hii haitoshi. Nataka kushauri nini hapo? Nataka kushauri kwamba tumepewa akili, elimu na maarifa kama wanadamu

maana yake uoto wetu lazima tuuboreshe, malisho yetu sasa yafanyiwe kazi. Tumekuwa na ardhi tumesema kuna matumizi bora ya ardhi yamewekwa sehemu na sehemu lakini hayaheshimiwi kwa hiyo matokeo yake ni kwamba tunatakiwa sasa tuboreshe, wataalam tulionao waboreshe. Tunaona ng'ombe wakiongezeka tunapata mapato zaidi lakini bado malisho yetu hayatoshi na bado uwekezaji huu ambao nimeuona saivi umekwenda kwenye shilingi bilioni 460 hautoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufanya *transformation* ya Wizara ya Uvuvi kwa shilingi bilioni 460, haiwezekani ni ndogo sana. Kwa hiyo tuiombe Serikali iangalie inapoenda kufanya *transformation cost* isije kwa gharama hii ndogo kama tunapata Pato la Serikali kwa asilimia saba kwenye mifugo na 1.8% kwenye Samaki, tuhakikishe kwamba tunaingiza fedha yakutosha kwa sababu tumeshaona ni *reality* ile kwamba tukiingiza fedha nyingi tunapata nyingi. Kwa nini hatuingizi fedha nyingi ili tupate nyingi zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie uvuvi kidogo kwa sababu ya muda. Kule Jimboni Busanda nampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu vikundi kadhaa vimekopeshwa, sasa wanaanza kufanya uzalishaji huu. Wapo baadhi ambao walipewa zile boti za mita tano isivyo bahati nafikiri kuna mahali palifanyika makosa kwenye uvuvi, hazifanyi kazi vizuri ila kwenye vizimba zinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wataalam wakaangalie upya kuona kama wale wanaotaka kuvua kwa hizo boti za mita tano zifanyiwe mabadiliko ili wazitumie tu kwenye vizimba. Vilevile chakula ni changamoto, kama wenzangu walivyochangia ndugu yangu Mheshimiwa Tabasam hapa chakula kina bei ya juu vilevile upatikanaji wake ni adimu. Kwa hiyo watu wetu wamepata mwamko mkubwa mwitikio ni mkubwa sana lakini upatikanaji wa chakula ni changamoto. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri hili utusaidie kule Busanda ili tunapoanza sasa kushughulika na vizimba tushughulike na vizimba na vitu vyote viweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rahhi, wajiandae Mheshimiwa Kamonga na Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya mifugo na mimi moja kwa moja niseme naunga mkono hoja kwa sababu sina shaka kabisa na utendaji kwa Mheshimiwa Waziri mahiri Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Naibu wake lakini pamoja na watendaji wote wa Wizara hii angalau ndoto za wafugaji sasa nafikiri tunaenda kuzifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuongeza bajeti ya mifugo bajeti iliyokuwepo mwaka jana ya shilingi bilioni 292.5 lakini sasa hivi ameenda kuridhia shilingi bilioni 460.33, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu pamoja na uwekezaji huu mkubwa unaofanyika katika mifugo bado hatujaweza kupata tija kabisa kwenye mapato ya ndani, kwenye fedha za kigeni lakini kwenye kaya za wafugaji wenyewe, kwa sababu ya aina hii ya ufugaji unaoendelea nchini kwetu ufugaji wa kuhama hama *(pastoralist)*. Wafugaji wa Arusha, Manyara utawaona mpaka Kilindi, Morogoro, Chalinze mpaka huko kusini. Kwa nini? Kwa sababu wanahangaika kutafuta malisho na maji na kwa sababu hiyo ndiyo chanzo kikubwa kabisa ya migogoro kati ya wafugaji na wakulima, uharibifu wa mazingira na kuendelea kueneza magonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe kabisa kwamba Wizara ilishaanza kutambua maeneo ya malisho na nyanda za malisho kwenye mikoa kadhaa tulishapima hekta 3,189,000. Sasa niombe tu kwamba kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi wafugaji wangemilikishwa maeneo yao ya ufugaji ili kwamba kila mfugaji aweze kufuga kulingana na uwezo wa ardhi *(grazing capacity)*. Hii itawafanya wafugaji waelewe

kuvuna mifugo ili wabaki na mifugo yao michache wanayoweza kuifuga hii itasaidia sana na kupunguza kutembea tembea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwarobaini ambayo Mheshimiwa Waziri amekuja nao wa kusambaza mbegu ya malisho nawapongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa kuna Shamba la Ikunge kule Pwani ambalo kwa msimu uliopita imezalisha tani 127. Leo umewatangazia umma wa Watanzania na wafugaji kwamba mbegu hizo zitapatikana katika maduka yote ya mawakala, mbegu hizi bado ni kidogo wataanza kwenda kule kutafuta hizi mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kabisa Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha katika Wizara hii, kuendelea kuzalisha mbegu za kutosha ziweze kupatikana kwa mawakala kama inavyouzwa mbegu za mahindi kwenye pakiti mbalimbali. Kwa vipando hizi *cuttings* kama majani ya tembo zipelekwe halmashauri na halmashauri watoe kwa wafugaji, wafugaji wanajua kupeana mbegu na mbegu hizi zitaenea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu upungufu wa huduma za ugani. Ni kama tumewaacha wafugaji peke yao wanavyohangaika hasa kwenye kutibu mifugo, wanahangaika wanatumia uzoefu kitu ambacho ni hatari kabisa. Wanavyotumia uzoefu wanatumia dawa kali kwa dozi wanazojua wao na kwa isivyo bahati kabisa kama akiona mifugo haiponi, atachinja hiyo nyama ataleta buchani tutakula wote au kwa vyovyote vile atatibu na pengine maziwa yatakuja sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ku-*promote* vizimba kwenye uvuvi bado hatuna wataalamu wa kutosha kwenye uvuvi na hata hao wachache pengine hawawajibiki. Pamoja na miradi mingi ambayo Wizara inafanya na kuipeleka katika Serikali za Mitaa kama majosho na mengineyo bado inakosa usimamizi. Sasa naona tu suluhisho la huduma hizi za ugani ni kuanzisha hiyo mamlaka ambayo wenzangu wamekwisha kusema: Mamlaka ya Ufugaji na Mamlaka ya Uvuvi. Hizo zinaweza kuwa mwarobaini maana wataajiriwa *para professional* kote katika ngazi ya kijiji na katika ngazi ya kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu utotoshaji wa mifugo, tumeweka uwekezaji mkubwa sana katika sekta hii ya mifugo kwa kweli inasikitisha kabisa tunavyoona mifugo mingi inatoroshwa nje ya nchi na Serikali inakosa mapato. Pamoja na kujenga minada kwenye mipaka kwa mfano mnada wa Horohoro umejengwa kwa shilingi milioni 563 lakini hebu tuone kule wanaotorosha ni Watanzania wenzetu kwa nini hatujajua changamoto, kwa nini wanatorosha hii mifugo na tunakosa mapato. Pengine kuna kila sababu ya Wizara kwenda kukaa na wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo kujua changamoto ni nini? Pengine kuna utitiri mwingi wa tozo na vitu vingine lakini kuimarisha mipaka huko kwenye minada ili tupunguze utoroshaji wa mifugo na Serikali yetu iweze kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nasisitiza kuhusu zoezi la utambuzi wa mifugo ambapo safari hii Serikali itenge fedha za kutosha ili zoezi la utambuzi wa mifugo ifanyike na kufahamu mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kamonga, jiandae Profesa.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii. Kule Ludewa nina kata nane ambazo zimegusa maji, Kata ya Lumbila, Kilondo, Lifuma, Makonde, Lupingu, Lwela, Manda na Ruhuhu wananchi wake hawapungui 30,000 ambao wanategemea shughuli ya uvuvi kwenye maisha yao ili kuweza kupata mkate wa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nipende kuchukua nafasi hii kushukuru sana Wizara hii; Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kupanga mpango wa kujenga soko la samaki pale Manda. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea shilingi milioni 809 kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki ambalo litakuwa na kisasa lina yale majokofu kwa ajili ya

kuhufadhi samaki kwa hiyo nishukuru sana, Wananchi wa Ludewa wamefurahi sana na wanaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kumekuwa na changamoto kwenye lile ziwa ya uhaba wa samaki kutokana na tabia zake. Kwa hiyo niombe Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya tafiti kwenye ziwa hili (Ziwa Nyasa) ili kuweza kujua kwa nini kunakuwa na uhaba wa Samaki. Vilevile niliusikiliza mchango wa kaka yangu Mheshimiwa Mabula niliona anawashauri Wizara kwamba mjikite kwenye Ziwa Victoria kwanza mpaka uzoefu upatikane. Mheshimiwa Waziri mimi napenda nikuhakikishie kabisa Wananchi wa Ludewa wameshajiandaa kufuga samaki kwa njia ya vizimba na kwa kutumia Mfuko wa Jimbo tuliweka kizimba kimoja cha majaribio, matokeo yake Mheshimiwa Waziri yamekuwa mazuri sana. Tulikwenda kwa kushirikiana na watu wa *TAFIRI* walipita maeneo yote, wameainisha maeneo ambayo hayana mawimbi makali ambayo yanafaa kwa ajili ya ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuliweka kizimba cha kwanza kwa kutumia fedha ya Mfuko wa Jimbo, kwa hiyo tumevuna samaki wa kutosha wenye uzito unaoridhisha. Kuhusu vifaranga, tulifuata ushauri wote ambao *TAFIRI* walitushauri, tulikwenda kuchukua pale Ruhila kwa kweli wamefanya vizuri sana. Kwa hiyo naomba kwenye vile vizimba 400 ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema vipo na sisi wa Ziwa Nyasa kule Ludewa tuweze kupewa vizimba vya kutosha kwa sababu tuna maeneo tumeshaainisha pale Lupingu. Kuna maeneo tumeshaainisha Iwela, Manda na maeneo mengine ya Lumbila na Kilondo ambayo yanafaa sana kwa sababu hayana mawimbi makali sana, kwa hiyo yanafaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kuna yale mahema ya kisasa kwa ajili ya kukaushia dagaa, tunaomba sana Mheshimiwa maeneo ya Lifuma wanapata sana dagaa wale wa Ziwa Nyasa na wale dagaa ni wazuri sana na ni watamu mno. Watu wanatoka mpaka kule *DRC* na nchi nyingine jirani wanawafuata pale Makonde na Lifuma. Kwa hiyo tunaomba

sana utusaidie teknolojia ya kuwaanika wale dagaa ili waweze kufaa kwenye soko la ndani na soko la Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuweka hivi vizimba tutasaidia soko lile lipate samaki wa kutosha na hii hoja niliyoisema ya utafiti kuna Mto Ruhuhu ambao unatenganisha Wliaya ya Ludewa na Wilaya ya Nyasa. Ukifika Mwezi wa Sita au wa Saba kuanzia huu wa Tano wavuvi wanapata sana samaki aina ya mbelele lakini samaki wote wale wakivuliwa wanakuwa na mayai tumboni. Kwa hiyo nadhani tafiti zikifanyika wanaweza wakatoa elimu kwa wavuvi huenda ule ndiyo msimu wao wa kwenda kutaga kule kwenye mto au vitu vingine lakini kwa kuwa wavuvi hawajapata elimu ya kutosha wanawavua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa kutafuta eneo Kata ya Ruhuhu kwa ajili ya kituo cha utafiti wa ukuzaji viumbe maji. Eneo hili litasaidia sana kutoa elimu kwa wavuvi juu ya kuhifadhi mazingira ya ziwa nyasa na kuhakikisha samaki wanapatikana wa kutosha. Kumeanza kuonekana samaki wageni ambao inaonekana wanatoka nchi Jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa manufaa ya muda niseme naunga mkono hoja lakini niombe pia Wizara hii...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, ajiandae Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii.  Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu wake na Katibu Mkuu na timu yake na Wizara ya Mifugo kwa kazi kubwa mnayofanya kuna mageuzi makubwa mmeyaleta na tunayaona kusema ukweli kwenye maziwa, Ngozi, kuku, mbuzi, samaki na mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa mradi wa shamba darasa la kuku ambalo lilipatiwa kwenye Kata ya Uru Kaskazini na Kibosho Magharibi nashukuru sana, tunaomba tuje tumalizie ile kazi. Pia nashukuru kwa majosho ambayo tumejengewa kule lakini bado nahitaji josho kwenye Kata ya Arusha Chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anaongeza bajeti ya Wizara hii. Miaka michache iliyopita bajeti ilikuwa ndogo sana lakini sasa hivi tumeona *increase* ya 63% ambapo tunaona wanapata shilingi bilioni 460, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Hii pesa ni muhimu na mimi niseme hapa pesa hii haiwatoshi hawa watu, wanahitaji pesa nyingi ili waje na mageuzi ambayo wametarajia kwenye kuongeza utafiti, kutuletea chanjo, huduma za ugani, mbari za mifugo, malisho, vizimba, *BBT* na mambo mengi. Wana mambo mengi wanataka kufanya kwa hiyo wanahitaji pesa. Niombe Serikali kama Kamati tulivyo-*recommend* iwaongezee hawa watu pesa ili waweze kufanya mageuzi wanayotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie pale alipomalizia Mheshimiwa Rahhi kwamba tunaomba kama Kamati tulivyoshauri tuwe na Wakala wa Mifugo na Wakala wa Uvuvi ili waweze kusimamia hii sekta kwa uhakika zaidi kwa sababu sasa hivi usimamizi nao unaonekana ni shida. Kwa hiyo tukianzisha hizi wakala zitamsaidia Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla kwenye kuwupa *output*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijikite kwenye jimbo langu, Mkoa wa Kilimanjaro umebarikiwa sana, una mazingira yanayoweza kufuga kama Ulaya hivi. Upande wa milimani tunaweza tukafuga ng'ombe wa maziwa wanaoweza kutoa mpaka lita 40 kwa siku na upande wa tambarare Mabogini na Arusha Chini kule tunaweza tukazalisha nyama nyingi sana. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri sisi kule Kilimanjaro tunaomba utusaidie, tupe mbegu bora za mitamba inayoweza kutoa lita 20 hadi 40 kwa siku, uone Mchaga atakavyopambana na Wapare kule. Sisi utatudai maziwa na nyama na kila kitu. Pia, mbegu bora za malisho ili tupeleke kwenye haya maeneo kwa mfano ile

Mbegu ya *Juncao* ni mbegu bora na zile nyingine. Sisi tunakuomba utukopeshe tutakulipa maziwa na nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni samaki, najua Mkoa wa Kilimanjaro una maji mengi na tuna *potential* ya ku-*contribute* kwenye uchumi wa Samaki. Sasa tuna Nyumba ya Mungu pale na wale wavuvi wetu wa Nyumba ya Mungu wangependa sana wawe kwenye *program* ya vizimba. Nimwombe Mheshimiwa Waziri vile vizimba 497 ambavyo ameviweka kwenye *program* hii, sisi tukopeshe vizimba na awafundishe vijana wetu namna ya kufuga samaki kwa kutumia teknolojia ya vizimba. Tusiende tu kwenye maziwa hata Nyuma ya Mungu tunajua tutazalisha samaki wengi halafu sisi atudai samaki na mchango wetu kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, kwenye samaki kuna eneo ambalo lina-*potential* kubwa sana, ukanda wa tambarale tunalima mpunga eneo la Mandaka Mnono, Mabogini na kule Arusha Chini tunalima mpunga, hebu leteni mbegu, anzisheni kuzalisha vifaranga tuwapelekee wakulima wa mpunga, tuwape samaki watupe kule kwenye majaruba uone tutakavyozalisha samaki wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Wizara iajiri Maafisa Ugani wakutosha wawafundishe watu namna ya kufuga samaki kwenye majaruba ya mpunga, siyo Kilimanjaro tu hata maeneo mengine ambayo yanalima mpunga tunaweza tukasaidia sana uchumi wa samaki na ile 1.8 ikaruka ikawa juu ya hapo, tukachangia vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimanjaro tunayo maji mengi, mifugo ina *potential* ya kukusaidia, samaki ina *potential* ya kusaidia Wizara, kwa hiyo tunaomba watukopeshe miradi sisi tutawalipa nyama na samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nimeshakuita Mheshimiwa Mwijage, wajiandae Dkt. Angelina Mabula na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mkutano uliopita nilizungumzia fursa ya samaki kwa kuzingatia maji tuliyonayo *square kilometre 145,000* nilisema tunaweza kupata dola bilioni tatu, leo tunauza milioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika diplomasia ya uchumi amekamata soko la Ghuba, wako tayari kununua nyama kutoka Tanzania, *potential* ya soko lao ni dola bilioni sita, sisi tunauza nje dola 56. Maana yangu ni nini? Pesa tulizowekeza kuchukua masoko haya ni kidogo, soko lipo linatusubiri sisi hatujawekeza pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhifadhi wa Ziwa, tunahitaji kuhifadhi Ziwa. Mkurugenzi wa Uvuvi anajua, samaki wamepungua kwa asilimia 35 na maeneo ya Tanzania yenye matatizo yanajulikana, wakati umefika wa kuanzisha hifadhi, Mamlaka ya kuangalia hili Ziwa. Uvuvi haramu, *overfishing* ni tatizo, hatuwezi kusubiri ili kwamba sasa tuweze kwenda kupata hiyo *potential* ya Vietnam ya dola bilioni tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ufugaji wa samaki. Nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, ninakushukuru Mheshimiwa Waziri, sehemu za Rushonga, Ihumbo, Bugasha, Kamugaza wote umewaweka kwenye *chart* tunakwenda kufuga samaki, lakini kufuga samaki lazima viwanda vyako vile ambavyo nimeelezwa na wataalam vianze mara moja. Tunapaswa tuwe na viwanda vya kutengeneza chakula cha samaki kwa sababu kwenye *co-structure* ya samaki sehemu kubwa ni chakula. Nina uhakika umeshajenga majengo tunataka mitambo ili kusudi tuende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mifugo. Nirudie tena, nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, ule mgogoro umekwisha, mgogoro umekwisha sasa Muleba tumejipanga ili kuanza kufuga na Muleba tutakuwa shule au

darasa la kuifundisha nchi hii namna ya kufuga. Vitalu vyote viwe vya kufuga si kuchunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *NARCO* wasimamie mikataba *to the dots* mtu akikiuka nje. Mheshimiwa Waziri, vitalu hivi sasa vilenge kuwatajirisha Watanzania hata Wabunge wakitaka waje hapa, nitawapa darasa wakati wa kunywa chai waende wafuge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wawekezaji wametangulia kwenye sekta ya maziwa hasa Kagera, namzungumza Kahama *Fresh*. Kahama *Fresh* alindwe atoke kwenye kuchakata lita 20,000 aende kwenye kuchakata lita laki tano. Ni aibu kwa nchi hii kuchakata lita laki mbili na elfu ishirini na nne kwa siku. Uganda kuna kiwanda kinachakata lita laki nane kwa siku. Mtoto wa Mjomba ana kiwanda kinachakata lita 150,000. Serikali impe nguvu Kahama *Fresh. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Heifer International,* namuunga mkono *Heifer International* aanze kugawa mitamba, atupe mitamba sisi tumlipe maziwa *Kahama Fresh.* Tunataka watu wote, na sisi kwetu tunakushukuru sana kwa kuturuhusu kuingiza ng'ombe wa kisasa, wakulima wote wanakupongeza, Ustaadhi Bashe anakupongeza, tulete ng'ombe kama alivyosema mzee Profesa pale, ng'ombe anayetoa lita 40 kwa siku, hao ndiyo ng'ombe tunaowataka, lakini samadi inayotokana na hiyo inatengeneza kahawa, kahawa ya Kagera iweze kukubalika katika *level* za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wote nimeshawaahidi, kuna *collection centre* Nshamba, kuna *collection centre* ya Kahama hizo uzilete pale, halafu Mheshimiwa Waziri wakati namalizia ile *show* tuliyopiga Karagwe tunapaswa tuipige Muleba. Kazi uliyofanya kwa ujumbe uliopewa na Mheshimiwa Dkt. Samia si ya kawaida, tunataka tufanye *show* ya kibabe mtu anapewa ng'ombe anadaiwa maziwa, lakini lengo letu tunaomba pesa ziongezeke kusudi tuweze kupata mapato zaidi na pesa za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa wanaouza nyama nje ya nchi na wanaouza samaki nje ya nchi watuoneshe pesa wanaziweka wapi. Hatuwezi kukaa kwenye namba wakati mtu anauza mnakalia makaratasi halafu angalia wengine wasituuzie *invoice* tunataka *cash* dola. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mabula, jiandae Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa fursa uliyonipa. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais hasa kwa kuwakumbuka sekta ya uvuvi, sekta ambayo kidogo ilikuwa imesahaulika katika vitendeakazi. Sitaki kurudia aliyoyasema Mabula lakini tayari na mimi ni mnufaika kwa maana ya Wilaya ya Ilemela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia suala la mikopo ya boti kwa vikundi vya ushirika ambavyo wamepata, ninaomba sana Serikali iangalie boti mlizowakopesha si zile walizoomba, waliomba boti za uvuvi mkawapa boti za kukusanyia Samaki, kwa hiyo hazifanyi kazi. Pia na zile mlizowapa wavuvi wanadai *horsepower* ni kubwa kuliko mahitaji waliyonayo. Kwa hiyo, unakuta gharama ya uendeshaji ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwakumbushe tu watu wa Wizara ya Mifugo ya kwamba mwaka 2022 tumefanya sensa ya watu na makazi japokuwa na wanyama au mifugo ilikuwa inahesabiwa lakini tungeomba kama Serikali kuwepo na sensa ya mifugo ambayo itakwenda kutupa picha halisi ya idadi ya mifugo tuliyonayo ili kuweza kuona uwekezaji tulionao na namna ya kuweza kuhudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Ugani ni wachache pia kwa sababu hatuna idadi kamili ya ng'ombe, hawa tulionao tunao kwa makadirio lakini siyo, usitarajie mwenye mali akuambie ana ng'ombe 20 wakati ana ng'ombe 200, lakini ukienda *specifically* kwenye sensa ya mifugo tutapata idadi na tutaweza kuwahudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala zima la malisho. Tunayo maeneo ambayo yametengwa, ambayo kwa mujibu wa kumbukumbu umeonesha karibu hekta 81,000 ambazo zimetengwa kwa ajili ya ufugaji, tungeomba pia katika suala zima la namna ya kulisha basi wasaidiwe wale wavuvi na wale walioko kwenye viwanja vyenye *urban farming* wanaruhusiwa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, na wao ni vizuri wakapata namna bora ya kuweza kuandaa malisho ndani ya maeneo yao, kwa sababu wamechukua eneo la *urban farming,* lakini hafanyi hiyo kazi anafanya shughuli nyingine. Kwa hiyo, hao nao ni vizuri wakaweza kupewa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la uvuvi ndani ya Ziwa Victoria ambao unaendelea. Ni vema kweli wanafunga ziwa kwa siku kadhaa, lakini unakuta wale wavuvi wa dagaa siku anazopata kufanya uvuvi ni chache ukilinganisha na wale wanaovua samaki, basi pengine na leseni kwa sababu ziko sawa zingetofautishwa kwa sababu hawa wanafanya kazi siku chache kuliko wale wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *royalty,* watu wa samaki wanatozwa kwa dola, tungekuwa na usawa katika suala zima la utozaji, leseni ziwe za bei ya *Tanzanian shillings* badala wengine kulipa dola wengine wanalipa shilingi halafu anakuwa hana uhakika na kiasi anachotakiwa kulipa maana dola ina panda na kushuka kwa hiyo kwake inakuwa ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ningeomba kwenye suala zima la uwekezaji. Watu tunaowapa maeneo ya uwekezaji ni vizuri Serikali ikaandaa miundombinu ya msingi. Kwa mfano, kuwepo na majosho, malambo kwa ajili ya maji, kuwepo na umeme halafu yeye afanye zile shughuli zingine. Kama ni suala la kuongeza thamani pia itakuwa ni rahisi zaidi kwake yeye kufanya kazi hiyo, lakini tusipofanya hivyo ndiyo unakuta wanalalamika kila siku wanasema mazingira si rafiki lakini tungewaandalia kwa sababu tunazo *ranch* zetu zipo lakini wapo wale ambao wanachukua nje ya *ranch*, kwa hiyo inakuwa ni rahisi zaidi katika

suala zima la kuweza kuwawezesha ili waweze kuwa na miundombinu rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la vikundi ambavyo vimeomba mikopo, mpaka sasa kwenye Jimbo kuna vikundi zaidi ya 36 vimeomba, naishukuru sana Serikali kwa sababu tayari wameweka tengeo kwa ajili hiyo, changamoto iliyopo ni kwamba mikopo pengine inachelewa sana, naomba mikopo hiyo iweze kuharakishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uboreshaji mialo. Tukumbuke kwamba hii mialo katika Ziwa Victoria na maeneo mengine wanauza samaki pia katika soko la *European Union,* sasa kama haijakaa vizuri kidogo itakuwa ni changamoto, naomba katika maeneo yote iweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali, katika Jimbo langu kuna mialo mitatu inayokwenda kuboreshwa ambayo ni mwalo wa Kirumba, Mwalo wa Igombe na Mwalo wa Kayenze Ndogo shilingi bilioni 33.5 zimetengwa ni shukurani kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa uliyonipa Mungu awabariki sana wakachape kazi, mwaafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Dkt. Chaya, wajiandae Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mariam Ditopile na Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lakini kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza kwenye sekta ya mifugo na uvuvi hususan kule kwetu Manyoni Mashariki. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu Ulega pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu Profesa Shemdoe Mwalimu wangu wa Chuo Kikuu cha Sokoine kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kule Manyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara imefanya mambo makubwa sana kule Manyoni. Kwanza, kwenye upande wa majosho ndani ya miaka mitatu Manyoni tumeweza kujenga majosho nane na haya ni mabadiliko makubwa sana kwa Manyoni kwa sababu miaka mitano ya nyuma iliyopita hakuna hata josho moja lililojengwa. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hii juhudi ambayo wameionesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna maeneo ambayo yanauhitaji wa majosho ikiwepo Kijiji cha Kasanii, Kijiji cha Magasai, Kijiji cha Simbanguru, Kijiji cha Dabia vilevile Kijiji cha Udimaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ningependa kuchangia upande wa minada. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, katika Tarafa ya Kintinku Manyoni wamejenga mnada wa kisasa wa zaidi ya milioni 270, tayari mnada umekamilika, kuna mambo machache tu ambayo wanatakiwa kuyamaliza, na niseme Mheshimiwa Waziri Mkoa mzima wa Singida hakuna mnada wa kisasa uliojengwa kama ule wa Manyoni. Nakushukuru sana na tunakusubiri uje Manyoni katika Kata ya Kintinku uje uone ule mnada na uje utufungulie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo ombi moja, pale ndani tunahitaji kukamilisha vyoo, kujenga ofisi kwa ajili ya mapato na kujenga lile eneo dogo kwa ajili ya kutunzia mifugo. Mimi nilete salamu hizi za watu wa Manyoni kwa kazi kubwa ambayo wameifanya, kwa kweli ameweka historia kubwa sana kwa wafugaji wa Manyoni nasi tunamuahidi Mheshimiwa Rais, wafugaji wamenituma mwakani wafugaji wote watamuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabla sijamalizia kuhusu minada. Namshauri Mheshimiwa Waziri, sasa tuachane na suala la kuuza ng’ombe kwa kukisia urefu, uzito na umbile twendeni kwenye kutumia mizani. Amejenga mnada wa kisasa Manyoni, tunataka sasa kwenye ule mnada watu wauze ng’ombe kwa kupima kwenye mizani, huo ndiyo ushauri wangu ambao nampa Mheshimiwa Waziri leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kuhusu mamlaka ya kusimamia sekta ya mifugo, wenzangu wengi wameongelea. Najua hili liko ndani ya uwezo wa Mheshimiwa Waziri, ameipambania Sekta ya Mifugo, bajeti yako imeongezeka tunataka sasa tuanzishe mamlaka ambayo itaenda kuwakomboa wafugaji wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1974 Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipitisha mamlaka ya kusimamia Sekta ya Maendeleo ya Mifugo, Sheria Namba 14 ya mwaka 1974 na aliisaini Julai. Nina maswali machache kwa Mheshimiwa Waziri, ni sheria gani ya Bunge iliifuta mamlaka hii? Nadhani tukipata huo uelewa itakuwa ni rahisi na sisi kujua kwamba, kwa nini ile mamlaka ya zamani ilifutwa na je, hii tunayoenda kuianzisha itatofautianaje na ile mamlaka ambayo ilikuwepo kipindi hicho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni ombi. Nimesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anaanzisha zile *milk collection centre*, vituo vya kukusanyia maziwa. Nimechangia sana hapa Bungeni kuhusu uzalishaji wa maziwa kule Manyoni, namwomba Waziri anapoenda kuanzisha hivi vituo asisahau wafugaji wa Manyoni. Sisi tunafuga sana mifugo, tuna ng'ombe wengi sana zaidi ya laki moja na tisini na tano kule. Kwa hiyo, namwomba Waziri anapoenda kuanzisha vile vituo vya kukusanya maziwa asisahau Manyoni hususan Manyoni Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, narudia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini nikmongeze Mheshimiwa Waziri anafanya kazi kubwa, tunamkaribisha sana Manyoni, karibu sana Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe, wajiandae Mheshimiwa Malapo, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri na Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa afya na uzima kuendelea kuwatumikia wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kutoa pongezi nyingi sana kwa Serikali, nikianzia na Mheshimiwa Rais mwenyewe pamoja na viongozi wa Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wengine wote. Nasema hivyo kwa sababu Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi ni sekta ambayo inachangia pato la Taifa kwa kiwango kidogo lakini ni kwa sababu tulikuwa hatujawekeza kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inaonesha jinsi ambavyo sasa Serikali iko *serious* kutaka sekta hii ichangie kwenye pato la Taifa. Ukiangalia mwaka 2021/2022, bajeti yake ilikuwa bilioni 169 lakini leo tunazungumza bajeti ya 2024/2025 bilioni 460 hii inaonesha kwamba sasa Serikali imeamua kwa dhati kabisa kuwekeza katika mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilisimama katika Bunge hili nikasema maneno makali kuhusu suala la kufunga Ziwa Tanganyika, nilisema nikiwa na sababu. Sababu ya kwanza nilitaka Serikali isishirikiane na Serikali za Nchi za Zambia, Congo na Burundi kufanya maamuzi bila kushirikisha wananchi. Baada ya kusema maneno hayo, namshukuru Waziri huyu msikivu na mwana mapinduzi akaamua kutukusanya wote Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wabunge wote tunaotoka Mikoa hii ya Rukwa, Katavi na Kigoma, tukafanya kikao akaanza kutupa uelewa sisi tukaelewa akashuka akaenda kwa wavuvi wetu kwenye maeneo mbalimbali akakutana nao, wakafanya mikutano ya hadhara kuwaeleza faida tutakazozipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwanasiasa najua kabisa kwamba wakati mwingine siasa inadharaulika mtu unaweza ukafika mahali akasema bwana wee hiyo unayosema ni siasa tu, lakini siasa ndiyo inayoongoza nchi. Lazima sisi wanasiasa tufike mahali tusimame katika uanasiasa wetu kwa ukweli ili kuiheshimisha siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka hapa kabla ya kusema maneno haya ninukuu kwanza maneno ya Hayati Mzee Abeid Aman Karume aliyekuwa kiongozi wa nchi ya Zanzibar. Mheshimiwa Hayati Abeid Karume aliwahi kusema haya, "ni bora kumuudhi mtu siku moja kwa mambo mtakayokuja kukubaliana siku zote kuliko kumfurahisha mtu siku moja kwa mambo ambayo utakuja kumuudhi siku zote." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nikisimama hapa nikataka kufurahisha wananchi wa Kigoma, Rukwa na Katavi kwa kusema Ziwa lisifungwe ili leo wapige makofi lakini watakuja kunichukia siku zote, bora leo niwaambie naungana na Serikali kukubaliana Ziwa lifungwe ili waje wanipende siku zote. Hili nalisema kwa sababu mimi ni mtoto wa mvuvi, mapato tuliyokuwa tunayapata kwenye uvuvi katika Ziwa Tanganyika katika miaka ya 1970, 1980 na 1990 hadi miaka ya 2000, mapato hayo yameshuka kama ni kutoka asilimia mia mpaka asilimia kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi katika Ziwa Tanganyika uko katika hali mbaya sana, kuwaambia wananchi twendeni hivyo hivyo ni kuwadanganya na kufika mahala kuwapotezea muda na siku moja watakuja watuchukie. Ni dhahiri Serikali yetu imefanya utafiti tena utafiti wa kimataifa wakishirikiana na Nchi hizi za Burundi, Zambia na Congo, wameona kwamba kufunga ndiyo njia itakayowasaidia wananchi, hasa kufunga kwenyewe wanafunga katika kipindi sisi tunaita kilimia, yaani mwezi wa tano, mwezi wa sita na mwezi wa saba, ni miezi ambayo Ziwa kwa kawaida huwa linajifunga, mapato yanakuwa madogo sana. Ninawasihi wananchi na ninaishukuru Serikali kwa kuja na utaratibu huu ili mtakapofungua wananchi wapate mapato makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naishauri Serikali kuongeza udhibiti katika uvuvi haramu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ditopile, Mheshimiwa Kassinge na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo wajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Mtwara katika ule mgao wa zile boti za kisasa zimetufikia boti tano; tunaishukuru sana Serikali kwa hilo. Namwomba Mheshimiwa Waziri atume wataalam wake wakaangalie mchakato wa zile boti, kwani inaonekana kama zinasumbua vitu fulani havijakaa sawa sawa. Naomba tu hilo lifanyiwe kazi ili lile lengo ambalo limekusudiwa na Serikali basi liweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namuomba Mheshimiwa Waziri pale katika Manispaa yetu ya Mtwara Mikindani, waangalie kwa jicho la karibu pale *ferry* ambapo samaki wanauzwa, kununulia, kukaangwa, kutayarishwa na kila kitu. Tunaomba miundombinu ya pale *ferry* katika Manispaa ya Mtwara Mikindani paboreshwe. Kwa sababu wanawake wengi wanafanya biashara zao lakini mazingira yaliyopo pale siyo rafiki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *issue* ya nishati bado mpaka leo kuni zinatumika pale kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, kwenye *storage facilities* (sehemu ya baridi ya kuhifadhia samaki) bado uwezo wake siyo mkubwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wafanye kila linalowezekana ili kusudi sehemu ile iweze kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna changamoto kubwa ya mbegu ya majongoo bahari. Mheshimiwa Waziri, mwaka jana nililisema na mwaka huu nalisema. Vijana, wanawake na watu wazima wamehamasika sana kufuga majongoo bahari kwa sababu soko lake ni la uhakika lakini upatikanaji wa mbegu bado unasuasua. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba walitilie mkazo suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, Mheshimiwa Waziri tunasema mchango mdogo wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa. Sababu zinajulikana, ukisoma kwenye hiyo hiyo hotuba amesema uvuvi unachangia pato la Taifa kwa

kiasi kidogo. Akasemaje? Kwa sababu kuna uwekezaji mdogo katika uvuvi wa Bahari Kuu na usindikaji wa mazao ya uvuvi kuna athiri mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwenye mipango yake mingi imeeleza kuboresha uvuvi wa Bahari Kuu kwa kununua meli za uvuvi. Mara ya kwanza walisema watanunua meli nane. Zikaja wakasema watanunua tano, leo nazungumzia nne. Sasa nataka kujua, meli zinanunuliwa au hazinunuliwi? Yaani wanatuachaachaje sisi watu ambao tuko kwenye ukanda wa Bahari Kuu? Watueleze tu, *from* nane kwenda tano na sasa hivi tunaongelea nne. Wananunua au hawanunui? Waziri akija kuhitimisha hapo atueleze. Pia, naomba kama anaenda kununua, basi ya kwanza kabisa ipelekwe Mtwara kwa sababu kuna ukanda mrefu sana wa Bahari ya Hindi ili kusudi uvuvi utekelezeke kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, boti za kisasa za doria. Sitaki kuamini na siamini, bahari yetu ina samaki wengi wakubwa. Tunachokosa sisi ni nyenzo za kuvulia hao samaki. Meli inunuliwe, maboya yanunuliwe lakini wanunue boti za doria za kisasa ili ziweze kufanya kazi ya kuchunga rasilimali ambayo ipo ili tuwezeshe Taifa letu kupata pato kubwa linalotokana na Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki hawajawahi kwisha baharini hata siku moja isipokuwa sisi tunashindwa kuwafikia kutokana na zana duni ambazo tunazitumia kwenda kuvulia. Kwa hiyo, bado nasisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata mshtuko kidogo. Bajeti ya maendeleo kutoka shilingi bilioni 194 mpaka shilingi bilioni 363 wakati iliyopita imetolewa mpaka sasa hivi hata 50% haijafika. Ongezeko hili kubwa kama litakwenda kutolewa, naona mabadiliko makubwa kwenye sekta hii. Kwa hiyo, ombi langu na hoja yangu ni kwamba, fedha hizi zilizotengwa zisiishie kwenye makaratasi. Ziishie kweli kutolewa zikatekeleze miradi ya maendeleo ambayo imekusudiwa kwa manufaa ya nchi yetu na manufaa ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana na namtakia heri kaka yangu Mheshimiwa Ulega. Waende wakayatekeleze haya yaliyopangwa na Serikali itoe pesa ili waweze kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, wageni waliopo Bungeni jioni hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni wanne wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni Uongozi wa Hospitali ya Agha Khan Afrika Mashariki na Tanzania. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mariam Ditopile, atafuatiwa na Mheshimiwa Kassinge, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo ajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Kitabu chetu kitukufu cha *Quran*, kwenye Surat Dhuha Aya ya 11 inatuambia, "*wa amma bi ni'mati Rabbika fahaddith.*" Maana yake neema za Mola wetu tuzitangaze na neema zenyewe za Mwenyezi Mungu ndizo hizi ambazo sisi wanadamu tunazitenda na kuzifanya. Kwa hiyo, kabla sijajikita kwenye ushauri, naomba nitangulize kutoa pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kama wenzangu walivyotangulia, kwa utashi wake wa kisiasa. Pia, hajaishia tu kwenye utashi ila amekwenda kwenye vitendo. Kwanza, kwa kuongeza bajeti ya Wizara yetu na kwa ujumla kwa Wizara hizi zote ambazo zinasimamia sekta ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua umuhimu wa Sekta hizi. Kwanza kwa kuzalisha ajira kwenye nchi yetu lakini kwenye kuchangia kipato cha uchumi wetu na kuingiza fedha za kigeni katika nchi yetu. Hata hivyo, kikubwa sisi ni wawakilishi wa wananchi, kwenda kunyanyua maisha ya mmoja mmoja katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Mheshimiwa Waziri Ulega, hongera sana; kazi unaifanya na tunaiona. Leo hii tunaongelea ajira mpya kupitia *BBT life* ni ubunifu wako na unaendelea kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tulikuwa pale Kongwa kwenye uzinduzi wa Kituo atamizi ambacho kinakwenda kunyanyua vijana wetu na kuwafundisha ufugaji wa kisasa wa mbuzi ili waweze kuuza ndani ya nchi na nje ya nchi. Hayo ndiyo mambo; tulikuwa tunataka Serikali kwenye sekta hizi za uzalishaji wawafikie wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wavuvi wanapewa boti na Serikali, leo wavuvi wanapewa nyenzo na Serikali. Kwa kweli kwa hilo acha tukupe maua yako, tukutie moyo kijana wetu uendelee kuchapa kazi. Sekta hii unaijua kiundani na kwa kweli uliyafanyia kazi mawazo mazuri ya Waheshimiwa Wabunge ambapo lengo wanataka kukusaidia ili na wewe uache alama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kwa kweli Serikali kwenye bajeti tunapitisha fedha kwa ajili ya kuchanja mifugo yetu bure. Sisi hiki ndicho tulichokuwa tunakitaka. Kwa kweli nikutie moyo, chapakazi na usonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wameongelea kuhusu mamlaka. Namwomba Mheshimiwa Waziri aelewe na aielewe Kamati. Inawezekana mengine tukikaa kwenye Kamati tunamweleza yeye, tukiongea hapa Bungeni, tunaongea na Serikali yote. Kama Waziri amekwishafanya kwa nafasi yake, Serikali kwa sehemu nyingine inatakiwa iongezee nguvu, ndiyo maana tunaliongelea hapa kwa nia njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, unaweza ukaanzisha duka kwa mtaji mzuri, biashara nzuri, ukawa pale una meneja, muuzaji na mhasibu mzuri katika eneo zuri. Ukikosa usimamizi ulio madhubuti, huwezi kutengeneza faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi ni Sekta muhimu katika uchumi. Leo tunaona makubwa yanayofanyika kwenye Wizara ya Kilimo lakini yatachukua muda kuyaona. Hata hivyo tujiulize, samaki ni rasilimali kama vile ilivyokuwa miti na misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki hahitaji chanjo, kule kwenye bahari na ziwani samaki hahitaji chakula; anajilisha mwenyewe na anajitibu mwenyewe. Sisi tunakwenda na tukimvua na kumla anatusaidia afya. Unaweza kuwa na walakini kwenye nyama nyekundu lakini kwenye samaki madaktari kila siku wanatuambia tule. Kwa hiyo, tunapopaza sauti kwamba uvuvi tunataka uongezewe wigo kwenye kuusimamia tuna maana yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii anayesimamia mustakabali na maendeleo ya uvuvi na wavuvi hammiliki mvuvi. Mvuvi leo hii anamilikiwa na halmashauri. Afisa uvuvi yuko chini ya Mkurugenzi. Kipimo cha Mkurugenzi ni ukusanyaji wa mapato, kipimo cha Mkurugenzi ni yale mapato yake ameyatumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kumhoji Mkurugenzi kama amemnyanyua mvuvi au uvuvi ndani ya Halmashauri yake. Kwa hiyo, yeye anamchukulia mvuvi kama chanzo cha mapato. Ndiyo maana leo tunaona haya mambo tunaongea kwamba jamani tozo, sijui nini, kwa sababu yule anayemmiliki mvuvi hamuwazi yule mvuvi kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tumekazia kama Bunge kama Kamati ni lazima Mheshimiwa Waziri apate mamlaka ya uvuvi. Vilevile, mimi nimewaza mbali, mwanzoni huko nyuma Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ilikuwa Wizara moja lakini Bunge hili hili liliwaza na tumeona sasa hivi tuna Wizara ya Kilimo na tuna Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Naomba *Hansard* iweke hiyo kumbukumbu yangu. Iko siku tutahitaji hii Wizara ya Uvuvi ibaki yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome nchi kumi Afrika ambazo zinaongoza kwa kuuza samaki na mazao yake duniani.

Tunaanza na Morocco, Namibia, South Africa, Mauritius, Senegal, Tunisia, Seychelles, Mauritania, Madagascar, Uganda ni ya 10, Tanzania hatupo. Tujifananishe na Uganda tu ambayo ina Ziwa Victoria ambalo na sisi tunalo na sisi ndiyo tuna sehemu kubwa ya Ziwa Victoria. Sisi tuna Nyasa, Tanganyika na tuna Bahari, kwa nini hatumo humu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yote huyu hana usimamizi ambao ana umiliki kwa 100%. Mheshimiwa Mwijage ameongea mambo ya msingi namna gani tunaweza, leo hii pamoja na usimamizi mbovu lakini tayari Sekta ya Uvuvi inachangia *GDP* kwa asilimia 1.8. Je, tukiwa na mamlaka hii Wizara ikijitegemea tutafika wapi katika kuingiza kipato kwa nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la kuwa na mamlaka kamili ya kutunza hizi rasilimali zetu zinazotokana na uvuvi hilo jambo haliepukiki. Mheshimiwa Ulega, wewe ni mtaalamu wa Uchumi wa bluu. Umekaa pale na umesoma pale *UDSM*, *Degree* yako na *Masters* umesomea huko. Acha *legacy* kwenye hii Wizara, historia ya hii nchi ikukumbuke. Ili mwanzo uwe mzuri ni lazima Mheshimiwa Waziri asimamie hii mamlaka itimie na ianze kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunatunza misitu kwa nini tusitunze mazao haya ambayo yanakuja kutuongezea mapato na Tanzania itapaa tena kwa haraka? Wala hatuhitaji tena kusubiri sijui miezi miwili, ni sisi kuwawezesha wavuvi wetu wakawa na mazingira mazuri. Kwa sababu vitu vingine ni vya kujiuliza. Ukienda kwa wadau wote ambao wanazunguka Ziwa Victoria, wavuvi wanasema uvuvi haramu hawahutaki, ukienda Serikali inasema uvuvi haramu haiutaki, ukienda kwa sisi wawakilishi wa wananchi uvuvi haramu hatuutaki. Kila mtu anauchukia lakini bado unaendelea; shida iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ndiyo maana tunasisitiza usimamizi uwe thabiti. Hii yote ni katika kuanzishwa kwa mamlaka yetu hii ya uvuvi ambayo matokeo yake tutakuja kuyaona kwa haraka na sisi tuweze kuwa katika ramani kwa hizi rasilimali. Hizi

neema ambazo Mwenyezi Mungu ametupatia sisi kama Nchi ya Tanzania ili tuweze kuleta maendeleo kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nianze tu kwa kuwakumbusha kwamba, ambayo leo tunaiita Wilaya ya Kilwa ni dola ambayo ilikuwepo tangu karne moja. Wakati wa Dola ya Azania iliyokuwa inaundwa na miji mikubwa ya Rufiji na Kilwa kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilwa hii ndiyo dola ambayo ilitengamaa karne ya 11 mpaka ya 15 ikiwa imeweza kujitengenezea fedha zake yenyewe. Mwanahistoria maarufu kutoka Morocco, Ibn Battuta baada ya kuzuru Kilwa anaandika akisema kwamba, "Nimetembea katika Pwani ya Afrika Mashariki na Kati, sijapata kuona Mji uliojengeka wenye dola kamili, wenye ustawi na ustaarabu kama Kilwa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inatupeleka katika kupanda na kushuka kwa masuala mbalimbali ikiwemo miji hii. Kilwa hii ilipanda ikashuka. Karne ya 18 Dola ya Kilwa ikashuka na kuanguka. Imeendelea kuwa hivyo na ndiyo Kilwa iliyosahaulika mpaka karne hii ya 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa wasomaji wa Biblia, turejee Kitabu cha Isaya ile Sura ya Sita mstari wa nane andiko linasema, "Kisha nikasikia sauti ya Bwana akisema nimtume nani? Naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema mimi hapa nitume mimi". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha wa Tanzania, wana Kilwa tulikuwa na kilio cha kusema ni nani atakayerudisha hadhi ya Kilwa kabla ya mwisho wa robo ya karne ya 21? Mama Samia anasema mimi hapa, mimi nitafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja kutujengea Bandari ya Uvuvi Kilwa yenye gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 266 ongeza shilingi bilioni 10; hakuna kama Mama Samia. Kwa wanaosoma Quran rejea Sura ya 27 Surat Naml, Aya ya 40. Nabii Suleiman alikuwa amepatwa na dharura. Dharura hii ndiyo dharura iliyotukuta wana Kilwa. "*Audhu billahi minash shaitwan rajiim, Qalla-lladhi indahu ilimun mina-l-kitabi, anaa atiyka bihi qabla an yartadda ilayka twarfuka.*" Dharura iliyomkuta Nabii Suleiman akatafuta wenye maarifa makubwa ya kufanya jambo la dharura la kuleta Kiti cha enzi cha Malikia Sheba wakati huo Bilqis. Akatokea mwenye elimu kubwa akasema mimi ndiye ambaye nitaleta kiti hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kupepesa jicho, wana Kilwa tunauliza; ni nani atakayerudisha hadhi ya Kilwa kabla robo ya kwanza ya karne ya 21 haijaisha? Mama Samia anasema, mimi hapa nitafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari hii ya Uvuvi ambayao itakuja kuchechemua viwanda vya kusindika samaki na mazao ya bahari pale Kilwa, inakuja kuchechemua miundombinu mingine ya kimataifa ikiwemo uwanja wa ndege wa kimataifa, masoko ya samaki pale Kilwa, vituo vya kuhifadhia samaki, karakana ya kujenga meli ya uvuvi ambayo Mheshimiwa Waziri ametaja katika hotuba yake. Hiyo ndiyo kazi ambayo sisi wana Kilwa tunakuja kuiona kuiona Kilwa ya karne ya 13. Hiyo ndiyo kazi ya Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia amemaliza kazi yake kwetu sisi wana Kilwa, deni limebaki kwetu sisi. Vilevile, sisi wana Kilwa tunasema kabla maeneo mengine hawajamuheshimisha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi Wanakilwa mwaka 2025 tutakuwa wa kwanza halafu wengine watafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna mashaka na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameiheshimisha Kilwa. Bandari ya uvuvi inakuja kuleta mabadiliko makubwa, mapinduzi makubwa ya kiuchumi, mapinduzi makubwa ya ustaarabu na mahusiano mengine ya kimataifa ikiwemo utalii. Sisi Wanakilwa

tunachomuahidi Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mwaka 2025 tutaanza sisi halafu wengine watafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba uniruhusu niwasilishe maombi ya wadau wa Sekta ya Uvuvi kwa Mheshimiwa Waziri. Nikianza na Kilwa Kivinje na Kilwa Somanga wanauliza, ile ahadi ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tulipitisha hapa ya kujengewa masoko Somanga na Kivinje inatekelezwa lini? Nitaomba Waziri anapokuja hapa Wanakilwa wapate majibu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa mwani nao wana hoja yao. Tunashukuru Waziri ametualikia hapa wadau wa mwani kutoka Kilwa na Mafia, tumewatembelea. Pia, wao wanasema kwamba wanaomba Serikali iwatafutie masoko. Kwa sababu hapa Tanzania upande wa Bara kumekuwa na mnunuzi mmoja tu ambaye ame-*monopolize* soko la ununuzi wa mwani. Wanaomba wapanuliwe wigo, wanunuzi wawe wengi zaidi ili kuwe na ushindani na waweze kupata bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho wanaloomba wadau wa mwani ni mashine za kuchakata. Mheshimwa Waziri akipata nafasi atembelee wanamwani hawa, wana ombi mahsusi la kuomba mashine za kuchakata mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge watakapopata fursa, basi watembelee wajasiriamali hawa wanaochakata *products* mbalimbali za mwani hapa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwenye hizi boti za uvuvi ambazo Mheshimiwa Waziri atanunua kutokana na bajeti ambayo si muda mrefu tutaipitisha, zaidi ya mia nne hamsini, tunaomba wale ambao walikosa mara ya kwanza wapewe kipaumbele katika awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa kipekee na mahsusi kabisa ni kwamba, katika vikundi ambavyo tumeviwezesha kuomba mikopo hii ya boti za uvuvi niombe kwa unyenyekevu

mkubwa, pale Kilwa kuna Kikundi cha *BMU* Magengeni, afanye kama *case study* hivi, awakopeshe *BMU* Magengeni boti moja kati ya boti 450 anazokwenda kugawa katika huu mwambao wa Pwani halafu aone matokeo yake. Wao wanasema kwamba wataitumia boti hii kwa ajili ya uzalishaji, doria na kama dharura pale maafa au majanga yanapotokea baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumekuwa tukileta ombi letu mara nyingi la kuomba kujengewa kizimba kwa ajili ya wafugaji wadogo wadogo wanaofuga samaki kando ya Mto Ruaha na katika mabwawa yao ili waweze kujifunza. Tunasikitika ombi letu halijafanyiwa kazi licha ya kuahidiwa kufanyiwa kazi na Mheshimiwa Waziri mwenyewe akiwa Naibu Waziri na sasa ni Waziri kamili. Sasa basi kwa heshima na taadhima tunaomba ombi letu lifanyiwe kazi, tujengewe kizimba ndani ya Manispaa ya Iringa.

Pili, wananchi wa Iringa mmoja mmoja na kwa vikundi wamekuwa wakijishughulisha sana na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na wanyama, hivyo tunaomba katika mpango wa kukopesha au kusaidia ng'ombe nasi pia tukumbukwe. Tunaomba pia kufanyiwa mafunzo ya kunenepesha ng'ombe.

Tatu, Mradi wa Machinjio ya Kisasa Ngelewala ulianza kwa awamu ya kwanza mwaka 2008/2009 hadi 2015/2016; mwaka 2019/2022 ulitekelezwa kama mradi wa kimkakati. Hadi sasa mradi haujakamilika kwa kiwango cha kutoa huduma za uchinjaji wa nyama kwa mfumo wa kisasa ikiwa ni pamoja na kuchakata nyama *(processing)* ikiwa ni kiwanda cha nyama. Tunaiomba Serikali ifanyie kazi ombi letu maalumu la kuomba fedha kiasi cha shilingi 1,902,077,650 yenye Kumb. Na.BC 134/164/01/13 ya tarehe 21 Juni, 2023 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu na kununua

vifaa kwa ajili ya machinjio hii ya Ngelewala katika Manispaa ya Iringa.

**MHE. ZACHARIA PAULO ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi yam waka 2020 hadi 2025 na Serikali nzima ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kupitia Bunge hili ninawathibitishia umma wa Watanzania kuwa katika miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wetu, umejenga madaraja la Mto Gunyoda na Udahaya miradi ambayo imekwama kwa miaka zaidi ya miaka 20 kwa zaidi ya shilingi ilioni tatu, Serikali imejenga Skimu ya Umwagiliaji Endayaya ulioshindikana kwa miaka 40 kwa shilingi bilioni nane, pamoja na miradi mingine mingi sana katika sekta za afya, elimu, maji, mawasiliano, nishati, utawala na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na maoni ya Kamati yetu ya Bunge. Kwanza Serikali iangalie utaratibu wa kuboresha koo za mifugo kwa kuanzisha mashamba darasa ya ufugaji katika halmashauri ambazo zina mifugo wengi ili kuonesha ufugaji wenye tija kwa kuhamasisha wafugaji wachache wenye mwamko na kushiriki maonesho ngazi za wilaya kabla ya Maonesho ya Nanenane.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali ijitahidi kutoa fedha zote zinazoombwa na Wizara hii kwa kuwa ili kufanikisha malengo

na mipango yote kusaidia na kukuza mapato yatokanayo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali ifanye tathmini ya ufugaji wa samaki katika maziwa madogo kama vile Babati na Tlawi katika Mkoa wa Manyara ili kuona mpango mzuri wa kutumia maziwa kama hayo kufanya ufugaji wa samaki kwenye vizimba nchini kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali itoe fedha za majosho matano yaliyopitishwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na kuwa Mheshimiwa Waziri nimekuomba sana mara nyingi kwani ni hitaji la wananchi katika kata kumi za vijijini na huduma hiyo haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali yetu ijitahidi kuajiri maafisa ugani katika sekta ya mifugo na uvuvi kwani kuna upungufu mkubwa sana wa maafisa hao na mfano ni Halmashauri ya Mbulu Mjini ina mahitaji ya maafisa 43 walioko wako saba tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono 100% na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na hadi leo tuko hapa tunaendelea kulitumikia Taifa. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi nikimsaidia kaka yangu Mheshimiwa Ulega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano mkubwa sana ambao amekuwa akinipatia. Yeye kwa kweli ni mwenyeji sana kwenye Wizara hii, amekaa zaidi ya miaka saba. Amekuwa msaada mkubwa sana katika hali ya kunielekeza na kunifundisha.

Mimi sasa nina miezi tisa, bado naendelea kujifunza. Kwa kweli nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Abdallah Ulega kwa namna ya kipekee sana. Nataka niwahakikishie kwamba *boss* wangu ni mtu mwenye roho safi. Unajua wako mabosi wengine roho inakuwa mbaya sana, roho ngumu, mtu anakuwa na roho ngumu, *boss* unakuta amenuna kila siku, sababu inayomfanya anune haieleweki, ukimuuliza hasemi, haeleweki anataka nini, maisha ni magumu wizarani, lakini nataka niwahakikishie sisi Wizara ya Mifugo tuko pamoja na tunafanya kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napokea maelekezo kutoka kwa *boss* wangu na kwa kweli nimejifunza vitu vingi sana kwa *boss*. Kulingana na umri wake, upendo alionao na roho safi aliyonayo naendelea kujifunza kusema ukweli na namhakikishia kwamba nitaendelea kumshauri vizuri, nitaendelea kujua kimo changu kinaishia wapi na maelekezo yake nitayafanya usiku na mchana ili kuhakikisha kwamba gurudumu hili tunalifikisha mahali linapotakiwa kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta hii ya Mifugo ni sekta mtambuka. Sote tunafahamu kwamba sekta hii inapaswa kuwa na mchango mkubwa sana katika ujenzi wa uchumi katika Taifa letu. Kazi ninayoifanya kwa sasa ni kupitia na kurejea *documents* mbalimbali ambazo zimetufanya tunase hapa tuliponasia. Ninachokifanya kwa sasa ni kumshauri Mheshimiwa Waziri, kwamba sasa kwa sababu tulinasia hapa tuanzie hapa ili kunusuru Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi ili iwe na *impact* kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua mambo mengine mengi atakuja kuyasema Mheshimiwa Waziri, mimi nizungumzie mambo machache sana ambayo nimeyaona jioni hii ya leo niweze kuyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kuhusiana na migogoro inayoendelea baina ya watumiaji wa ardhi. Migogoro hii imekuwa ikiripotiwa kutoka maeneo mbalimbali. Watani zangu wa Mikoa ya Kusini wamekuwa wakilalamika sana juu ya wingi wa

mifugo inayoingia katika maeneo yao. Mbaya zaidi mifugo hii imekuwa ikiingia mpaka inaharibu miundombinu ya kilimo kwenye mashamba ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme jambo moja hapa, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri; kwamba tushauri sana katika vijiji vyetu kuhakikisha kwamba tunapanga mipango ya matumizi bora ya ardhi; na mipango hiyo ya matumizi bora ya ardhi ni lazima iheshimiwe na kila mtu anayeishi katika eneo hilo. Mfugaji ajue kwamba shamba hili ni la mkulima na hivyo hapaswi kuingiza mifugo kwenye shamba hilo na mkulima naye ajue kwamba eneo hili ni la wafugaji na kwa hivyo hapaswi kwenda kulima katika maeneo hayo. Serikali za Vijiji, Serikali za Mitaa na kule halmashauri ndani ya zile wilaya wahakikishe kwamba wakishapanga hiyo mipango bora ya matumizi ya ardhi na sisi huku wizarani, Wizara ya Kilimo na sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tupate *documents* za mipango hiyo. Mfugaji anapoingiza ng'ombe zake kwenye shamba la mtu tukienda kwenye ramani tukakuta amefanya kwa makusudi, sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tuko tayari kushirikiana na wasimamizi wa sheria ili achukuliwe hatua za kisheria, tena za kumuumiza ili asirudie kosa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa wizara ya kulalamika kila siku, kwamba sisi tunakuwa sehemu ya kutetea wafugaji wasiofuata sheria. Wafugaji ni lazima wafuate sheria na sisi tutawapenda sana wafugaji. Hapa wako wengine wananisikia, kwamba ni lazima na ni lazima mfugaji yeyote awapo ndani ya nchi hii azingatie sheria, aheshimu mashamba ya watu na aheshimu makazi ya watu. Si kila sehemu tutapeleka ng'ombe, kila sehemu tutapeleka mbuzi ama kila sehemu tutapeleka kondoo, haiwezekeni. Pamoja na kwamba mimi na Mheshimiwa Waziri ni mawaziri wa ng'ombe, ni mawaziri wa kondoo na ni Mawaziri wa mbuzi, lakini hatuko tayari kuwa na ng'ombe wasiofuata sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasema hili nilisisitize na namwona Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro ananiangalia vizuri, nadhani amenielewa vizuri; kwamba ni lazima wafugaji wafuate sheria. Tukikaa bila sheria iko siku tutakutana na ng'ombe

wameingia Bungeni hapa. Hili nalisisitiza kwa sababu limekuwa likilalamikiwa na limelalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana. Tunapokea simu nyingi sana, Wakuu wa Wilaya wanapiga simu nyingi sana wakielezea habari ya hawa ng'ombe, kila kitu ng'ombe, kila kona ng'ombe. Ni kweli tunakubali kwamba sisi ni mawaziri wa ng'ombe lakini ng'ombe wanaofuata sheria. Haufuati sheria haki ya Mungu lazima tukubaliane kwamba sheria inakuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nimelisema sana kwa sababu limekuwa likipigiwa kelele sana na ni lazima kila mtu afuate sheria katika mazingira hayo. Kwa hiyo tunaendelea kusisitiza, Serikali za Vijiji na Serikali za Halmashauri za Wilaya zote zinapaswa kuhakikisha kwamba maeneo yote yenye wafugaji wanapanga mpango bora wa matumizi ili kuepusha hii migogoro ambayo huingiliana katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusiana na vizimba. Imesemwa hapa na Waheshimiwa Wabunge kwamba vizimba kule Ziwa Tanganyika ni vichache, ni kweli, tumepeleka vizimba 29, lakini vizimba hivi vimekwenda kulingana na maombi tuliyoyapokea. Vizimba vipo vya kutosha na kwa hiyo tupo tayari kuendelea kupokea maombi. Tumepokea maombi mengine ya Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa na maeneo mengine. Mheshimiwa Rais ametoa vizimba vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maombi ya awali tuliyoyapokea ndiyo hayo 29, maombi mengine tunaendelea kupokea. Jinsi tunavyoendelea kupokea maombi ndivyo tutakavyowaletea vizimba. Nataka niwahakikishie kwamba Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo pia, kwamba vizimba hivyo vitakuja kadri ya maombi yanavyokuja wizarani na sisi tuko tayari kuendelea kuleta vizimba mpaka wavuvi wa Ziwa Tanganyika watakapotosheka wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maombi hayo ni lazima kuna utaratibu kwa sababu hii ni mikopo. Huwezi kufika tu mahali ukaanza kugawa mikopo kama njugu mawe, kwamba sasa sandakalawe, chukua, lazima kuwe na utaratibu wa maombi

ambayo mtu anaandika. Lazima atupe ka-*concept* kake, kwamba una *concept* gani katika hili baada ya kuwa tumeshampa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima mikopo hii iende kwa utaratibu na ni lazima tufuate utaratibu kwa sababu inakopeshwa na benki. Pamoja na kwamba anapitia kwa fedha za Serikali kutoka wizarani kwetu, lakini kuna utaratibu ambao umewekwa ili kumjua yule anayekwenda kukopeshwa ni nani, anafanyia wapi na kwa faida gani na atapata faida gani. Hii itasaidia sana kumfuatilia ili aweze kupata tija katika shughuli hii anayoifanya. Kwa hiyo naendelea kuwasisitiza wavuvi wale wote ambao wana hamu ya kujua zaidi kuhusu vizimba hivi kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi iko tayari kuendelea kutoa vizimba hivi na iko tayari kuendelea kuwakopesha boti katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusiana na elimu. Hii pia imesemwa sana. Ni ukweli kwamba elimu haina mwisho, ni kweli; na katika hili la vizimba tumekwishatoa elimu kwa kiwango kikubwa sana na kwa kuwa elimu haina mwisho, basi tutaendelea kutoa elimu hii kwa kiwango kingine kikubwa zaidi. Kwa kweli tumejitahidi sana na watalaam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wamekuwa wakienda mpaka vijijini kabisa kule ili kuwaelimisha wavuvi wetu juu ya namna gani vizimba vinatakiwa kuwa na juu ya namna gani boti hizi zinatakiwa kuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Mheshimiwa Anjelina Mabula pale, kwamba boti zingine ambazo zimetolewa *horsepower* yake ni kubwa. Wao wenyewe wavuvi ndio waliochagua, kwa sababu sisi hatuwezi kumkopesha mtu, lazima tukubaliane, kwamba unataka *horsepowe*r ngapi nataka *horsepower* kumi, nataka horsepower 20. Wao wenyewe kulingana na uzoefu wa lile ziwa lenyewe ndio wanachangua wanataka *horsepower* ngapi ili isukume mtumbwi wa mita ngapi. Kwa hiyo kama kuna changamoto yoyote pia ya mtu mmoja mmoja aliyekopa boti hizo tuko tayari kukaa chini na kurekebisha tuone njia nzuri zaidi ya kumsaidia huyo mvuvi ili aweze kupiga

hatua zaidi. Tunaendelea kupokea maombi ya namna hiyo katika picha hiyo katika mazingira ya maziwa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kwamba tunaendelea kutoa elimu na wataalam wetu wataendelea kutoa elimu na hata sasa tunapozungumza wengine wapo katika vijiji vyetu huko wanaendelea kutoa elimu. Waheshimiwa Wabunge tumejitahidi sana kukutana nao na wenyewe tukawapa elimu. Nina uhakika Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika Ziwa Tanganyika kama ni *diploma* au *certificate* ya uvuvi sasa tayari wanayo kwa sababu tumekutana nao mara kwa mara, tukawafundisha na tukawaelimisha njia nzuri ya kufuga samaki kwa njia ya vizimba na kwa kutumia hizi boti. Kwa kweli kama ni cheti tayari wanacho na sisi pale Wizarani tuna profesa wa uvuvi, Profesa Ulega, kwa kweli kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Chaya pale, kwamba kama ni kubobea kwenye suala la uvuvi Mheshimiwa Ulega amebobea, huna chenga ya kumpiga, amebobea sana. Digrii ya kwanza ni ya uvuvi na digrii ya pili ni ya uvuvi. Pale wizarani tuna maprofesa na wao wakileta ile elimu na wenyewe wameshajichanganya, sasa ni Profesa Ulega; tunaendelea vizuri kwa kweli kwa taaluma hiyo hiyo kubadilishana mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu linahusu usimamizi wa miundombinu ya mifugo. Wizara imekuwa ikijenga majosho na malambo. Wizara inapomaliza kujenga majosho na malambo inayakabidhi kwenye halmashauri husika; kama ni halmashauri ya kijiji ama ni halmashauri ya wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha kwamba tunapokuwa tumemaliza kujenga majosho na malambo tunapowakabidhi wenzetu na wenyewe wanayatelekeza. Majosho yanamaliza miezi mitatu yakishaharibika hata ile *service* ya hayo majosho hakuna anayehangaika nayo. Malambo yakijaa kidogo tu anayetakiwa kwenda kutoa hata zile tope hayupo; halmashauri wameyatelekeza Serikali za Vijiji wameyatelekeza, kila mtu ameyatelekeza. Kwa hiyo tukasema kwamba hapa lazima tuwe na chombo kitakachosimamia miundombinu hii ili kunusuru miundombinu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta *service* yake pengine hata ni laki moja au shilingi 50,000, lakini hakuna anayehangaika nayo. Hii ni kwa sababu hakuna usimamizi madhubuti. Sisi tunapojenga tunakabidhi kule ili waweze kusimamia, lakini hakuna anayesimamia. Ndiyo maana tukaja na mpango; kwamba Bunge likisharuhusu habari hii lazima sasa tuwe na chombo kinachosimamia miundombinu hii ili kiweze kuratibu miundombinu hii na hivyo iweze kuleta tija kwa wafugaji wetu walio katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kuhusiana na ufungaji wa ziwa. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri atakuja kulisemea vizuri zaidi, lakini na mimi nigusie kidogo. Kwa wanaotoka maeneo ya Kanda ya Ziwa, wanaotoka maeneo ya Ziwa Tanganyika na maeneo mengine ya maziwa kama Nyasa na Rukwa na maeneo mengine; ukweli ni kwamba samaki wamekwisha ziwani, huo ndio ukweli. Hata hilo Ziwa Victoria. Leo samaki unayemnunua Victoria ana bei ghali kuliko samaki unayemnunua Dar es Salaam; kwa nini? Kwa sababu Dar es Salaam tayari wana mabwawa, wanafuga kwa njia ya mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Victoria kule Mwanza maeneo yote anayoyasema mzee wangu Mheshimiwa Tabasamu ukiuliza bei ya samaki si ile bei ambayo sisi tumekua tukiiona na ukubwa wa samaki wanaopatikana katika maeneo hayo ni samaki wadogo, lakini ni bei ya juu. Kwa nini? Kwa sababu samaki wamepungua ziwani. Ziko sababu nyingi za samaki kupungua ziwani ambazo nikianza kuzielezea hapa nitachukua muda mwingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya muda, niombe sana Wanatanganyika wote waelewe kwamba pamoja na kwamba huu ni mkataba wa kimataifa, lakini samaki wamekwisha na tunakwenda kwa lengo jema sana la kuhakikisha kwamba tunanusuru samaki hawa. Kuna utafiti umefanyika, hatufungi ziwa kiholela tu, kwamba tumeamka tumekurupuka tumefunga ziwa, hapana, utafiti umefanyika na imeonekana kabisa kwamba hapa

bila kufunga ziwa tunaendelea kupoteza mazalia madogomadogo ambayo baadaye yangekuja kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma na mikoa mingine ambao wamelielewa zoezi hili. Tunakwenda kulifunga kuanzia tarehe 15 Mei mpaka tarehe 25 Agosti. Yangekuwa ni matakwa yangu lile ziwa ilipaswa lifungwe hata mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifanya utafiti nchi zote zenye maziwa kama haya huwa zinafunga na kuna nchi huwa zinafunga mpaka miaka kumi. Baada ya hapo mazao yanayopatikana kwenye kufunga huko kama ni samaki huwa ni kuzoa kwa mikono. Fanya utafiti, nenda China, ambako wao wanafunga mpaka miaka kumi; lakini baada ya hiyo miaka kumi wanakuja kuvua kwa mikono, samaki ni wengi mpaka sebuleni, wamejaa, samaki ni wengi. Yaani nataka nikwambie kwamba sisi tumechelewa. Ziwa Tanganyika hili lilipaswa lifungwe kuanzia miaka mitatu minne na kuendelea ili kuwe na tija kwa wafanyabiashara wetu na walaji wa samaki wanaoishi katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kuhusu Mamlaka ya Uvuvi. Hii nayo imesemwa sana na Mheshimiwa Waziri atakuja kulisemea zaidi na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wengi wameonyesha kuunga mkono jambo hili. Ni jambo lenye tija na ni jambo la maana sana kwa sababu ndilo linalokwenda kuwa mwarobaini wa wavuvi haramu na uvuvi usioeleweka katika maeneo yetu ya ziwa. Kwa hiyo niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru sana kwa jinsi ambavyo wanaendelea kutusapoti katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mimi kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba nichukue fursa hii kurejea tena kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini katika Wizara hii. Naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa wasaidizi alionipatia wakiongozwa na Mheshimiwa Alexander Mnyeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme mbele ya Bunge hili leo, wengi wanavyomfahamu Mheshimiwa Mnyeti na yule Mnyeti anayefahamika, ya kwamba ni mtu kama mkorofi hivi. Nataka nikuhakikishie wewe na Bunge lako, kwamba Mheshimiwa Rais ni Mama mwenye maarifa makubwa sana. Ameniletea huyu Mnyeti tufanye kazi; na yeye amesema katika hadhara hii namna ambavyo amekutana uungwana wa kiwango cha juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakati tunafanya mjadala wa kujibu hoja tukiwa mimi na yeye na Katibu wetu Profesa Riziki Shemdoe akaniambia, Mheshimiwa Waziri unafahamu miaka miwili mitatu mpaka juzi tu hapa mimi ustaarabu kwangu ulikuwa mbali sana; lakini kwa hakika nimeingia mahali hapa na baada ya kukutana na wewe na hii timu ya Wizara ya Mifugo na uvuvi niseme namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunileta kufanya kazi na timu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Misungwi wamepata Mbunge, ni mtu mkweli, ni mtu mwenye msimamo na kwa hakika mimi ananisaidia vyema sana. Wakati mwingine ninapoona hapa panahitaji namna ya mtu mwenye haiba yake namtanguliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu anifikishie salamu nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais. Nataka nimwambie kwamba *combination*

tuliyonayo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi ingekuwa ni timu ya mpira, basi ni ile iliyochukua ubingwa siku ya jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kuyasema hayo naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, niseme kwa kunipa *Profesa* Shemdoe. Mwaka jana nilisema hapa kwamba ninayo timu nzuri na nikamsifu. Sikumsifu kwa burebure; ni mtu msikivu na ni mtu anayeelekezeka. Sisi sote ni viongozi na tunafahamu, kwamba uongozi ukiachilia mbali masuala ya kiubunifu, uongozi ni masikilizano. Ikiwa ndani ya nyumba hakuna masikilizano kila mmoja anakwenda kivyake, hakika nyumba hiyo haiwezi kuleta mazao mema. Leo tunazungumzia Wizara ya Mifugo na Uvuvi juu ya *4Rs* za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi tumejikita katika hizo, tumejikita katika Ilani yua Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi; tumejikita katika Mpango wa Taifa (Dira ya Taifa). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *4Rs* zimetafsiriwa katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi, leo nilikuja hapa na katika ujio wangu nilikuja na mbegu ambazo zimekuwa *parked* kutoka Wizarani. Shirika letu la Utafiti wa Mifugo *(TALIRI)*, lakini na mashamba yetu ya mifugo pale tunakwenda kutengeneza uhimilivu. Katika zile *4Rs* liko jambo la *Resilience* na sisi tunakwenda kutengeneza uvumilivu na mimi kwa kuheshimu michango ya Waheshimiwa Wabunge na kwa kuheshimu mchango wa Kamati yetu ya Bunge ambayo ni Kamati mahiri sana na imekuwa ikitushauri vyema wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge hakuna uchawi katika jambo hili. Niko tayari Wabunge wa majimbo yote kuwapatia mbegu za malisho waende nazo kwa ajili kwenda kuhamasisha wafugaji wetu wapande. Tutatoa mbegu za malisho ya nyasi na tutatoa mbegu za malisho aina ya *Jucow* na ninayo furaha kubwa katika ufuatiliaji katika banda letu la wiki ya protini hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana umewaalika Wabunge na wameitika, habari niliyonayo leo wameona namna ambavyo nchi yetu ina mazao ya kutosha ya protini na wale ambao hawakupata, nataka niwaambie ya kwamba wasiwe na

wasiwasi, protini bado tunayo ya kutosha. Tunatengeneza *4Rs,* zile *4Rs* za kustahamiliana na uendelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutengeneza upya Sekta ya Mifugo na Uvuvi katika Bandari ya Kilwa Masoko ambayo ndugu yangu Ally Kassinge ameisema kwa lugha nzuri ya kupendeza sana ni katika kutengeneza upya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Sekta ya Uvuvi iweze kuwa na mchango mpana na mkubwa katika Taifa letu. Yale ndiyo maono na ile ndiyo tafsiri ya zile *4Rs* za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema na haya maneno naomba yachukuliwe na Waheshimiwa Wabunge, hakika migogoro ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine ni lazima sisi sote tuhakikishe kwamba tunakwenda na msimamo huu; kama mfugaji anadhani kwamba yale mahindi ya yule mkulima aliyeyaweka pale shambani kwake ni matamu sana sisi tunayo *Jucow* ambayo ni tamu zaidi ya yale mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi kama mmoja katika wasemaji alivyoshauri hapa akasema, "kwa nini wakulima wasilime nyasi tu ili wawauzie wafugaji?" Mimi nasema Waheshimiwa Wabunge njooni tuwapatie mbegu twende tuwapelekee wafugaji wetu; wajifunze na wakubali kwamba dunia imebadilika na hakuna jambo lingine isipokuwa ni lazima tupande nyasi zetu na tuweze kuvuna kwa ajili ya malisho wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme pia juu ya ufungwaji wa Ziwa Tanganyika, amejibu vyema Naibu Waziri. Ameeleza baadhi ya hoja na amezitolea ufafanuzi mzuri na hili la Ziwa Tanganyika limesemwa hapa na Wabunge wengi wa eneo hili la ukanda wa Ziwa Tanganyika. Kwa kuwa Naibu Waziri wangu ameshalisema jambo hili maelezo yangu yatakuwa ni mafupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge leo tunaomba vizimba viende Ziwa Tanganyika, lakini nataka niwaambie, katika ule mkataba niwajulishe ndugu zangu kwamba kabla ya huu mkataba ambao leo tunauzungumza hapa Bungeni Ziwa

Tanganyika hapakuwa na ruhusa ya kuweka vizimba. Huu mkataba moja ya faida yake katika zile *protocols* zilizosainiwa na kukubaliwa ni pamoja na kukubaliana kuanzisha miradi ya kuweka vizimba. Hili dunia yote inajua *capture fisheries* (uvuvi wa asili) duniani kote unaanguka. Hii ni hoja ya mabadiliko ya tabianchi na hii ni hoja ya ukuaji wa *population* ya dunia. Kwa hiyo, hakuna jambo lingine ni lazima mwanadamu atumie vyema maarifa yake kwa kupanda samaki mle ili kusudi waweze kumpatia mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vizimba ni kitu cha uhakika zaidi kuliko hata hii *capture fisheries.* Wakati mwingine mvuvi anatoka anakwenda katika maji kwa sababu ni mawindo; anakwenda kuwinda, hana uhakika. Anarudi aidha amepata kilo moja, kilo mbili au hakupata kabisa lakini vile vizimba ni kitu cha uhakika. Ukiweka samaki 4,000 wataokufa hawawezi kuzidi 20% ya hao 4,000, watakaobaki wote utawavuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaombe ndugu zangu kwamba, sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan; amefanya kazi kubwa sana mno pale Mwanza, ameianzisha. Ule mwendo aliouanzisha nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa Tanganyika wote. Nikushukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, umesema kwa ufundi wa hali ya juu namna ambavyo hatupaswi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Agosti, nitakwenda Kigoma nitahakikisha pia namwelekeza Naibu Waziri wangu aende Rukwa. Tutakwenda kuwaonesha namna ya mazao yatakavyopatikana mara baada ya kipindi hiki cha ufungwaji wa ziwa na kipindi hiki cha kilimia kitakapokuwa kimepita; kwa namna tulivyojipanga tutakapokwenda tarehe 15 Agosti, hatutakwenda mikono mitupu kwa sababu moja ya tatizo kubwa tulilonalo katika eneo hili ambalo ni tatizo la *cost harvest loss,* upotevu mkubwa sana wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tutakuwa tumezalisha samaki wengi sana nina wasiwasi mkubwa tusije tukawapoteza

samaki wale. Pale Wizarani nimejipanga na timu yangu tunanunua maguduria ya kuhifadhia samaki ili kusudi tukayagawe kwa akinamama wa ukanda mzima wa Ziwa Tanganyika ili watakapovuna yale mazao tarehe 15 Agosti, wakiwemo wale wa Katavi, wa Kigoma na wa Rukwa, wasije wakapoteza mazao yao, hili nataka niwahakikishie tutalifanya, watuunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama viongozi tukiwa na lugha mbilimbili itatusumbua sana na kuwapoteza hawa wananchi. Kama Serikali hatuna nia mbaya kwa sababu ni ukweli wakati wa kipindi cha Mei, Juni na Julai hiki ni kipindi cha baridi na samaki anakimbia. Anafanya *hibernation;* anajificha kutokana na ile baridi. Kwa hiyo, hata hawa wavuvi ukiwaambia wabaki tu. akienda hapati cha maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie, ni utafiti na ni jambo la uhakika siyo jambo la hila; siyo jambo la kusema kwamba tunawafanyia watu hiyana na kuwaonea. Wazo lililotolewa la kwamba tulinde mazalia ndiyo maana nikasema Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika kupambana na vita dhidi ya uvuvi haramu, matumizi ya maarifa ni makubwa zaidi kuliko matumizi ya nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunanunua ndege zisizo na rubani, huyo ndiyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, yaani leo Wizara ya Mifugo na Uvuvi inanunua ndege zisizo na rubani; hiyo ndiyo habari ya mjini. Tuna ndege zisizo na rubani zisizopungua saba, zile ni za *high resolution,* zitakuwa zikitembea umbali wa kilomita 100 kwa masaa mawili. Ndege zile zitapiga picha vyombo vyote vya uvuvi na zitatuma taarifa zile katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tutakuwa tukifanya *tracking* na *traceability,* tunakwenda kuanzisha mradi wa kufunga vyombo maalum katika kila boti ili kusudi tupate takwimu na taarifa za wavuvi wetu ambazo leo hii hatunazo. *This is science* na unajua uvuvi ni *purely science,* hata wale wavuvi walioko kule ni wanasayansi; huo ndiyo ukweli wenyewe. Kwa hiyo na sisi tunaambatanisha hilo jambo. Tunaweka *drones,* zinapiga picha, tukitoka katika kituo tukiwa tunakwenda kumkamata mtu

tunakwenda kwa uhakika kwamba huyo mtu yuko umbali gani, kilomita ngapi, *east or west;* tunaenda *straight* katika lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itatupunguzia matumizi mabaya ya muda, lakini itapunguza pia gharama za mafuta ambazo tumekuwa tukizitumia kwa kiasi kikubwa sana. Tusingetamani kukanyagana na watu wasio na hatia; tunataka tukienda kumshuku mtu awe ni mtu ambaye kweli huyu *records* zinaonesha ni mvuvi haramu. Waheshimiwa Wabunge hili nimeona nilieleze kwa kina sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wamechangia juu ya migogoro ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine. Nimeeleza hapa jitihada ambazo tunazifanya; mmeona kwa mara ya kwanza sisi tunaingiza sokoni mbegu za malisho; kwa sababu hapo mwanzo tulikuwa tunawahamasisha wafugaji wetu kwamba pandeni malisho; lakini mfugaji anakuuliza mbegu ziko wapi? Sasa leo tunapozungumza hapa madukani tutakuwa na mbegu. Kwa hiyo, wafugaji wote waliopo katika Bunge hili nawahamasisha sana kama nilivyosema tunayo *Jucow* na tutakuwa na kampeni madhubuti kabisa ya kupita sehemu moja hadi nyingine ya kupanda hizi *Jucow* na tutapanda na nyasi nyingine ambazo labda zitamea katika hayo maeneo, siyo kila mahali nyasi ambazo zinatakiwa kupandwa zitafanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu lazima tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, nimewasikia hapa baadhi ya Wabunge wakizungumzia juu suala la kwa nini Wizara inakubali maeneo ya wafugaji yaondoke, lakini lazima niseme ukweli, kila mmoja hapa anafahamu juu ya Mradi wa Mawaziri Nane na Vijiji 975, ni katika zile *4Rs* Mheshimiwa Rais amefanya *Reconciliation* kubwa sana. Siyo katika siasa tu, ametoa ardhi kubwa hapa; ardhi ya Serikali imetolewa imepelekwa kwa wafugaji wa nchi hii. Lazima tukubali na wakati tunaomba ni lazima pia tushukuru. Namshukuru sana Mheshimiwa Mwijage, pale Muleba *Ranch* ilikuwa ni mgogoro mkubwa sana. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia akatutuma sisi Mawaziri nane, tulikwenda pale tumeumaliza ule mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo Muleba wanasherehekea na wanataka kufuga kisasa; *this is 4Rs* na hiyo ndiyo nguvu ya *4Rs, reconciliation*. Kwa hiyo, hii hoja ya kwamba maeneo ya wafugaji yanachukuliwa sisi tumeichukua na tutazungumza na wenzetu. Ni lazima Waheshimu *GN* za Serikali. Hilo halina mjadala lakini mle wanakofanya vizuri ni muhimu kushukuru na kupongeza. *Ranch* za *NARCO* zimetolewa nyingi sana kuanzia Ruvu kwenda Mkata na kwenda kila mahali katika nchi hii. *West* Kilimanjaro kote tumemega kwa ajili ya kuwapa wananchi ili kusudi waweze kufanya shughuli zao. Kwa hiyo, hiyo ni nguvu kubwa sana ya utayari wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha kwamba tunaishi kwa maridhiano, tunaishi kwa kuvumiliana; tunaishi kwa umoja na tunajenga uchumi wetu jumuishi, tunajenga uchumi wetu upya na tunasonga mbele kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge Ole-Shangai amesema anataka kunishikia shilingi kama sijasema kuhusiana na chanjo ya mifugo. Mheshimiwa Ole Shangai hana haja ya kushika shilingi yangu kwa sababu tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 25; tunakwenda kuchanja katika nchi hii. Hili jambo la kuchanja tulikuwa tumewaachia sekta binafsi kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukubaliana juu ya kubadilisha mfumo wa uchumi katika Taifa letu miaka ile ya mwanzo wa 90, sekta binafsi ikaachiwa jambo hili la kuchanja. Hapa karibuni tumekubaliana hatuwezi kuwaacha wafugaji wa Taifa hili wawe watu wa kuonewa, kwa sababu huko barabarani kuna vishoka wengi sana. Vishoka ni wengi sana huko mtaani. Mtu mmoja yeye anatembea katika pikipiki yake: yeye ni daktari, yeye ni nesi na yeye ni kila kitu; dawa zenyewe hatuna ithibati nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwaondoa vishoka hawa, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga zaidi ya shilingi bilioni 25 tunakwenda kuchanja. Umetaja *CBPP, PPR* na *Newcatle* zimo. Lazima tukubaliane, akinamama wengi sana kule vijijini wanafuga kuku na kwa hakika kikipita

kideri/mdondo kuku wengi sana wa wale akinamama hufa na wanarudi nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapeleka hizo dawa na tutatoa ajira ya muda mfupi kwa vijana walioko mtaani wasiokuwa na kazi waliosomea shughuli za mifugo. Sisi tutakwenda kuwapa *temporary jobs* katika wakati ule wa kufanya shughuli hii ya chanjo, Rais Dkt. Samia hoyee, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza juu ya uvuvi haramu na Wabunge wengi hapa wamenishauri juu ya kuyalinda mazalia. Nimeeleza katika hotuba ya bajeti ya kitabu ukienda ukasoma mle utakuta tunanunua yale maboya na hizi ni *stainless steels;* tumeshaanza kuyafunga. Mahale kule Kigoma tumefunga, lakini zimefungwa maeneo ya Mgambo pale Uvinza na mimi mwenyewe ndiyo nilikwenda kuzifunga. Zimetengenezwa hapa Tanzania na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *Faculty* yetu ya *Engineering*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda nikiwa Naibu Waziri mwaka 2029, hata juzi nilipokwenda na kuuliza vipi yale maboya, yanaendelea kufanya kazi? Wamenambia zinafanya kazi vizuri sana. Mpaka leo hii ni miaka mitano yale maboya yanafanya kazi vizuri sana. Siyo tu pale Mgambo lakini na Muyobozi mpaka huko Buhingu kama unaenda Kalya; hiyo ni Uvinza na wavuvi wanaheshimu ile mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tutakwenda kufanya hivyo Ziwa Victoria; tutalinda yale mazalia. Tutaendelea kufanya hivyo Ziwa Tanganyika na kwa mwaka huu tumetenga fedha na tunakwenda kununua haya maboya; tunakwenda kulinda yale maeneo yote ya mazalia. Tunayatangaza katika Gazeti la Serikali atakayekwenda kugusa eneo lile ama zake ama zetu hatutamuacha salama kwa sababu tukilinda yale mazalia vizuri *stock* ya samaki wetu itaongezeka sana. Kwa hiyo, nataka tupate ushirikiano na naamini Bunge hili kwa namna lilivyokasirishwa na vitendo haramu vya rasilimali zetu, watatuunga mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vizimba na boti; boti zinatoka kutoka 160, Rais ameridhia tunapeleka mpaka 450, wavuvi wa nchi hii tupewe nini? Zile boti zinafungwa mpaka *tracking systems,* mle ndani kuna nyavu, *GPS* na mpaka kile kipampu cha kutolea maji. Lazima tukubaliane *reformation and rebuilding* ya hii sekta, Rais Dkt. Samia amepania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, wale Wabunge wote ambao wana mahitaji ya hivi vifaa akiwemo ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Mpembenwe, alisema mwanzoni kabisa akanikumbusha kwamba, wale wapiga kura wa kule Maparoni, Kiongoroni, Mbuchi, Mtunda, Salale na Nyamisati wote wanataka haya maboti. Kaka ahakikishe kwamba, anawaandaa wapiga kura wetu wa eneo hilo wakidhi vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hapa katika Bunge hili ya kwamba, kazi ya kuandaa yale maandiko siyo kazi ya wale wavuvi. Mmoja katika wasemaji hapa amesema vizuri, wavuvi hawana hayo maarifa, Mabwana Samaki walioko kule vijijini ndiyo watu wanaopaswa kuwaelekeza wavuvi wetu ni hatua gani ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa maelezo hapa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wetu, bahati nzuri wengi wameipokea hii vizuri sana, wawaelekeze Mabwana Samaki. Isiwe kazi yao wao ni kwenda kunyang'anya ushuru tu. Watoe michango ya kimaendeleo kwa wavuvi wetu ili kusudi wale wavuvi wapate hizi fursa zinazotolewa, wapate kunufaika na hizi fursa ambazo Serikali yetu ya Awamu ya Sita ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inazozitoa. Kwa hivyo, nimewasikia Wabunge wote mnahitaji haya maboti. Maboti 450 ni mengi, nataka niwahakikishie, leteni maombi mumkabidhi Naibu Waziri, mnikabidhi mimi, mumkabidhi Katibu Mkuu na yeyote mnayemjua katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nataka niwahakikishie maboti ya kisasa yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni mtu hakopeshwi boti isipokuwa tunajadiliana anataka boti la *size* gani. Sisi tunayo ya mita tano, mita saba, mita kumi, mita kumi na mbili na mita kumi

na nne kwa hivyo, mvuvi ana-*shop* yeye mwenyewe. Kwa sababu, huu ni mkopo kwa hiyo, sisi hatumlazimishi, sisi hatumuamulii. Wewe unakubaliana na maafisa wetu unataka boti la aina gani na *size* gani, huu ndiyo utaratibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimefurahi sana kwa majibu ya Naibu Waziri aliposema, kama kuna jambo *specific* ambalo Mbunge ameletewa kama malalamiko, sisi tuko tayari kupokea yale malalamiko, ili kusudi yule mvuvi asiende kulipa kitu asichostahiki. Kwa sababu, mwisho wa siku ule ni mkopo na kwa hivyo, anahitajika afanye lile jambo katika utaratibu ulio sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge wameshauri hapa ya kwamba, maeneo ya ukulima wa mpunga tupande na samaki. Namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo, mimi na yeye tumekubaliana Na Kwa kuwa, Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni moja, tunafanya kazi kama mwili mmoja, ndiyo. Nataka niwaambie tunafanya kazi pamoja, kiungo chochote kikipata hitilafu mwili mzima unaharibikiwa, ndivyo kama kidole kimekatika basi mpaka kichwa kinauma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hivi Wizara ya Kilimo inatengeneza skimu za umwagiliaji. Ninayo barua hapa ya mwandamizi, Waziri wa zamani wa Ardhi, mzee wangu Mheshimiwa Lukuvi anasema, Pawaga na pale Isimani, Idodi, wanataka tuwatengenezee mabwawa ya samaki. Sasa kwa sababu, pesa hizi za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, za kutengeneza skimu za umwagiliaji sisi tumefunga mkataba wa kushirikiana. Palipo na skimu ya umwagiliaji tunakwenda na mambo mawili, kila unapoona skimu ya umwagiliaji tunatoa *ember-out* na pia, tunatoa mabirika ya wafugaji kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufanya jambo moja la kuwafaa Watanzania kwa gharama ya Watanzania, huyu anafanya chake na huyu anafanya chake. Tunafanya kwa pamoja ndiyo maana katika miradi hii yote vijiji hivi alivyovitaja

mzee wangu Mheshimiwa Lukuvi, nataka nimhakikishie yeye na Wabunge wengine wote ya kwamba, katika skimu zile za umwagiliaji tunatoa *ember-out* kwa maana ya lile birika la kunyweshea maji. Vilevile, tunaenda mbele zaidi tunapandikiza na samaki, unavuna mpunga na unavuna sato. Halafu ukikaa pale mezani mambo ni mazuri sana kwa hivyo, kila Mbunge mwenye skimu ya umwagiliaji ananidai mbegu za kupandikiza za samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa. Ndakidemi, ameibua hoja hii na wengine wamesema. Mzee aje achukue vifaranga vyake vya samaki, twende tukapandikize, wakiwa wanavuliwa baada ya miezi mitatu, minne tualike au tupigie hata picha tuone ukubwa wa yule sato atakavyokuwa amenenepa. Halafu wakivuna ule mpunga, wakiweka pale mezani inabakia kazi moja tu ya kusubiri mwaka 2025, watu watakichagua tena chama ambacho kinawaongoza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, baadhi ya Wabunge humu wamezungumza juu ya upatikanaji wa maji ya kunywa mifugo yetu. Narudi tena katika hoja ile ile, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. Wakati wote msisitizo wao umekuwa ni tusifanye jambo moja huyu kivyake na yule kivyake. Na sisi tumelishika jambo hili ndiyo maana mimi na ndugu yangu Aweso penye mradi wa maji ya kunywa binadamu tunapeleka na maji ya kunywa mifugo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Aweso ana mabwawa 100, fedha zile ni za kwetu sisi Watanzania. Ya kazi gani mfugaji aliyeko pale ahangaike kwenda kilomita 100 kwenda kuyasaka maji wakati maji yako mahali palepale? Kwa nini, asitengeneze *ember-out*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii miradi yote ya skimu za umwagiliaji, miradi yote ya maji ya kunywa binadamu, kama

iko mifugo pale, imefanyiwa *design* ya kutoa yale maji, kwa ajili ya mifugo yetu. Mifugo yetu ni hazina yetu na utajiri wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ununuzi wa meli. Je, hizo meli ni nane, nne, tano au ngapi? Mheshimiwa Tunza Malapo ameuliza. Meli ni nane, nne Tanzania bara na nne Tanzania Visiwani. Visiwani watanunua upande wa visiwani, Zanzibar, na sisi tutanunua nne za kwetu. Tumekubaliana na ninamshukuru sana Mheshimiwa *Chief Whip* wetu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mama yangu Jenista Mhagama, ametuongoza vizuri sana katika hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefikia makubaliano. Mwanzoni hili jambo lilikuwa linaratibiwa na Wizara moja kwa moja, lakini sasa tumelitoa kwa mashirika yetu Tanzania kwa maana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *TAFICO,* watakwenda kutangaza tenda ya kwenda kununua hizi meli nne. Kwa upande wa Zanzibar, *ZAFICO* watafanya wao wenyewe. Siyo jambo liwe *centralized* Wizarani kwa sababu, tunataka wapate ufanisi. Wapate wanachokitaka, wapate kitu ambacho kitawazalishia na ndiyo maana wakati natoa hotuba hapa nimesema *TAFICO* inafufuka. Kwa hivyo, meli ni nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kilichotuchelewesha ni wahisani ambao tunashirikiana nao, *IFAD*, kwa maana ya wale wanaotukopesha hizi pesa. Hawa wahisani wetu walitaka ni lazima tufanye *environmental and social impact assessment* ya namna ambavyo tutaendesha pamoja na *feasibility study* kwa sababu, *TAFICO* hataendesha yeye mwenyewe pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana itakuwa ni *PPP*, tunakaribisha sekta binafsi. *TAFICO* bado ni Shirika la Serikali, meli ile akiiendesha *TAFICO,* yule mkurugenzi kikiharibika kifaa, yataanza yale yale ya kuanza kutafuta hicho kifaa, dokezo litoke kwangu, liende kwa yule, liende kwa yule, meli imesimama pale. Tunataka sekta binafsi ifanye kazi hiyo. Hakika nawaambia hii ni kwa ajili tu ya kuvutia kwa sababu, hii kazi itafanywa zaidi na sekta binafsi, lakini sisi tunataka tuiaminishe kwanza sekta binafsi ili

ivutike na baadaye ije ituunge mkono, haya ndiyo malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu bila ya sisi wenyewe kuwa na *national fleet*, bila ya kuwa na meli ya kwetu, sisi wenyewe ni nani huyo atakayekuja pembeni akatuamini kwamba, tunayo mazao ya kutosha? Ndiyo maana tukasema *TAFICO* itaanza. Kwa hiyo, dada yangu Tunza na Wabunge wote mjue tu kwamba, kazi hii inaendelea vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wamezungumzia juu ya Mamlaka za Mifugo na Uvuvi. Ni kweli jambo hili Wabunge wamekuwa wakilisema sana na sisi tunafanya jitihada kubwa. Kamati yetu ya Bunge imetusukuma ipasavyo juu ya jambo hili. Jambo limefikia mahali pazuri sana, msiwe na hofu, na sasa tunakwenda katika kulimaliza hili jambo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri omba pesa.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mwisho nimalizie na hoja ya ujenzi wa Bandari ya Kilwa-Masoko. Kwa kweli, tunashukuru sana 53% si haba, na tunakwenda vizuri mno na sasa tunakwenda kuimaliza. Itakuwa ni bandari ya mfano na hiyo inakwenda kutufungulia bandari nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tufungue huu Ukanda wa Mashariki, tuweke viwanda vya kutosha na meli zote za kimataifa zije Tanzania kwa hiyo, tutakuwa na ile ya pale Bagamoyo vilevile. Huo ndiyo mpango wetu, siyo ziende huko kwingine, zitakuja hapa Tanzania. Tunayo maji ya kutosha na tutatumia vyema fursa ya uwepo wa haya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati…

**NAIBU SPIKA:** Aahh, haa. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado? Aah, *okay.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya na ufafanuzi wote nilioutoa hapa, ninayo matumaini. Waheshimiwa Wabunge nawaomba kwa heshima kubwa na taadhima mtuunge mkono twende tukafanye kazi, tukafufue na tukaendeleze vyema sekta hizi za mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi 460,333,602,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 97,215,432,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 363,118,170,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za matumizi ya kawaida ni shilingi 97,215,432,000…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri inatosha, toa Hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Recourses Management Division*…….........……Sh. 6,670,942,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaingia kwenye mshahara na nina orodha hapa ya watu wanne. Tunaanza na Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba ufafanuzi kwenye Fungu 64, hilo ni 99.

**MWENYEKITI:** Hebu sema tena.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi kwenye Fungu 64, la Mshahara wa Waziri. Sasa, sijui kama na hapa inaruhusiwa niendelee tu?

**MWENYEKITI:** Basi subiri. Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka nipate ufafanuzi tu, sikuwa na lengo la kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Ni kuhusu vyuo vya *FETA* nchini, kwa maana ya kwa ajili ya ufundi wa uvuvi na ufugaji kikiwemo Chuo kimoja cha Gabimori. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza, lakini hajazungumzia mpango mkakati walionao, kama Serikali, kuhakikisha kwamba vile vyuo vyote vya ufundi vilivyosimama kwa miaka mingi katika maeneo mengi nchini vinaanza kufanya kazi, kwa ajili ya kuelimisha watoto wetu. Nataka nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na vyuo hivi kikiwemo chuo cha mfano cha Gabimori Wilayani Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu Mheshimiwa Jafari Chege amekuwa akizungumza hoja hii kila mara, juu ya chuo cha mafunzo ya uvuvi, *FETA,* pale Gabimori. Kwa msingi huo na vyuo vingine vyote nchini vikiwemo vile vya Mtwara pale Mikindani, vilevile vya Bagamoyo na Nyegezi. Sasa, nimtaarifu tu kwamba, tumetenga fedha ya kuviendeleza vyuo hivi, ili kusudi tuendelee kudahili wanafunzi wa Kitanzania wengi zaidi, ili waweze kupata hiyo fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Gabimori tunakwenda kumalizia miundombinu. Ni matarajio yetu mpaka kufika mwezi Oktoba, 2024, kile chuo tunakwenda kukifungua. Naomba nimtoe hofu na niwatoe hofu Wana-Mara na Wanarorya wote na wadau wote wa uvuvi kwamba, vyuo hivi hatuvitelekezi, tunavifanyia kazi ya kuvirekebisha ili viweze kutoa elimu kwa vijana wa Kitanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina nia ya kushika Mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini naomba ufafanuzi; Serikali toka kipindi cha nyuma imetenga maeneo kwa ajili ya uzalishaji ng'ombe na maziwa. Kwa maana kuna mashamba kama Kongwa, Ruvu, *Sao Hill* na Shamba la Kitulo, Makete, ambako mimi natoka. Hata hivyo, kwa muda mrefu mashamba haya yamekuwa hayana muendelezo mzuri kwa maana ya uzalishaji wa tija ambao umekusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni upi mkakati au maelezo ya Serikali, ili wananchi na Watanzania wote waujue? Kwa sababu, maeneo haya yamekuwa wazi kwa muda mrefu, uzalishaji wake umekuwa hafifu, ni mdogo; ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, haya maeneo hususan Kitulo, unakuwa na uwekezaji mkubwa na ukaleta tija?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia kwenye takwimu tumeagiza maziwa kutoka nje kwa zaidi ya shilingi bilioni 23 licha

ya kwamba, kwa upande wa nyama tumefanya vizuri kwenda nje. Sasa ni upi mkakati wa Wizara kuona jinsi gani hayo maeneo tunayaendeleza na yanaleta tija, hususan haya mashamba ambayo nimeyataja, ikiwemo Kitulo, Sao *Hill* na maeneo mengine? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Sanga, Mbunge wa Makete. Niseme tu Mheshimiwa Sanga amekuwa akilipigia debe sana Shamba hili la Kitulo, lakini leo ametanua wigo kwa maana ya mashamba yote nchi nzima. Kwanza *NARCO* hapa karibuni mmeiona, imefufuka, imetangaza vitalu. Tumeona palikuwa na kasoro kidogo na watu wengi waliomba vitalu vile hadharani na sasa tumeiondoa ile kasoro. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge *control number* ambazo zilikuwa zimegoma zitapatikana kwa hivyo, mashamba na vile vitalu vyote vilivyotangazwa vitakuwa tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Sao Hill*, tumepokea maombi, *expression of interest* kutoka kwa baadhi ya wawekezaji, wanataka kutufanyia kazi nzuri sana pale. Yale malengo ya msingi ya Serikali ya kutengeneza mitamba na kuigawa kwa wafugaji kwa bei nzuri ya ruzuku hayataondoka, lakini yataongezeka mara mbili yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huohuo wa mfano huohuo wa *Sao Hill*, tutakwenda kufanya Kitulo na Ngerengere, bila ya kuondoka katika ule msingi tulioachiwa na Baba wa Taifa letu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kwamba, haya mashamba yatumike katika kuzalisha mbegu bora zisambae kwa wafugaji nchini. Sisi tunataka tufanye zaidi, kwa ajili ya mahitaji yalivyo makubwa kwa hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, Mheshimiwa *Senator* Sanga na Waheshimiwa Wabunge wengine tunawakaribisha. Hata wewe ukiwa na wazo, tunao uwezo wa kumleta mwekezaji aje afanye jambo hilo hapa, milango iko wazi. Utaratibu wa

kisheria wa *procurement* na kila kitu upo, utafuatwa. Nataka nikuhakikishie kwamba, tuko tayari kufanya uwekezaji. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole Shangai.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi sina nia ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, kama alivyosema, lakini ninahitaji anipe maelezo mazuri. Kwa sababu, amesema kwamba, wametenga shilingi bilioni 25 kwa ajili ya chanjo, lakini kwenye hizo shilingi bilioni 25 zina-*include* mpaka *running cost* pamoja na hereni, nimeona hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hapa ni, kati ya ndama 100 wanaozaliwa Tanzania sasa hivi, ndama 80 wanakufa. Mtu mwenye mbuzi 200 anapoteza mbuzi wawili mpaka watatu kila mwezi kwa sababu ya magonjwa ambayo tungeweza kuwachanja wasingekufa, pamoja na kondoo. Suala lingine ambalo lipo ni, leo unapotuambia kwamba, utachanja kwa shilingi bilioni 25, tuna ng'ombe milioni 37, tuna mbuzi milioni 27 na kondoo milioni tisa, sina uhakika kama hizo fedha zitatosheleza kuchanja mifugo waliopo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Mheshimiwa Waziri, leo unapochanja, mimi nina ng'ombe 100 unapochanja ng'ombe 50 inakuwa kama vile sijachanja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangai, muda wako umekwisha.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka ni, Mheshimiwa Waziri atuambie ni nini mkakati wa Wizara kuhakikisha kwamba, tunachanja mifugo wote waliopo Tanzania ili kuondokana na magonjwa na Watanzania tufaidi mifugo tulionao?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuelewa sana Mheshimiwa Ole Shangai, mfugaji huyu. Kwamba, anachotaka ni kuona mifugo yote inachanjwa. Sisi

tumejipanga kwamba, uchanjaji ni lazima kwa sababu, mifugo ni rasilimali ya nchi hii. Inashikwa na mtu mmoja mmoja, lakini kimsingi ni mali ya taifa letu na ndiyo maana leo tunazungumza hapa kwa kujidai kwamba, mifugo ina mchango katika pato la taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ole Shangai, hii zaidi ya shilingi bilioni 25 niliyokutajia ni *component* ya sehemu moja tuliyoipanga, lakini kwa mfano, tuna Mradi unaitwa *Climate Smart Dairy Transformation Program*. Mradi huu umetokana na kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika hii Mikutano ya *COP28* unayosikia amekwenda, imezalisha mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mradi wenye mabilioni ya fedha, sehemu ya mradi ule ina chanjo. Kama ulinisikia wakati nazungumza mwanzo na ukisoma kitabu cha hotuba, utakwenda kuona ni dozi ngapi zitakazotolewa. Sehemu ya ile shilingi bilioni 25 itaongezea pale katika huo Mradi wa *Climate Smart*. Kwa hiyo, hizi namba nilizozitaja zisikutie hofu, mkakati tumeundaa vyema, tunataka tuhakikishe kwamba, tunawafikia wafugaji katika yale magonjwa ambayo ni kero kubwa sana na labda wafugaji wengi hawana uwezo nayo, kwa mfano, *CBPP*, *PPR*, kama ulivyoyataja hapa, haya tutayafanyia kazi. Wakati huo huo, hatutaacha ile ya kuogesha ambayo inawazuia kupe wasiweze kufanya uambukizaji wa magonjwa kwa ng'ombe wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunafanya *empowerment* ya kiwanda chetu cha *TVLA* yaani maabara yetu na *TVI,* ili chanjo nyingi zaidi zizalishwe. Sasa tuna kiwanda kikubwa *East and Central Africa* kinaitwa *Hester Biosciences*, kiko pale Kibaha. Zote hizi kazi yake ni kuhakikisha kwamba, tuna *streamline,* ili huu mfugo wa Mtanzania uwe salama. Endelea kutuamini na karibu tuendele kushauriana, ili kusudi tuweze kufanikisha kazi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, Wizara hii ina Fungu moja tu 99. Tunaingia kwenye *guillotine*.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Recourses Management Division*……...………Sh. 6,670,942,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*............Sh. 2,280,292,938
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*...........Sh. 2,141,573,750
Kifungu 1004 – *Veterinary Council of Tanzania*…......Sh. 698,773,000
Kifungu 1005 – *Information, Education and Communication Unit*…….….............….…....Sh. 0
Kifungu 1006 – *Fisheries Laboratory Unit*......….......Sh. 2,285,524,000
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*..............................Sh. 695,807,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*......Sh. 993,505,000
Kifungu 1009 – *Legal Services Unit*……………..........Sh. 825,096,000
Kifungu 1010 – *Information and Communication Technology Unit*……………….……....Sh. 931,035,000
Kifungu 1011 – *Environmental Management Unit*……………………………...……..Sh. 550,512,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 1,047,918,000
Kifungu 1013 – *Government Communication Unit*…………………….…..…..…….Sh.1,137,628,000
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*……….....……Sh. 11,316,611,972
Kifungu 7003 – *Infrastructure Development Division*……………..……...…………Sh. 1,067,868,000
Kifungu 7005 – *Research, Training and Extension Services Division*………....…..……..Sh. 27,004,035,166
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing Development Division*…….....……Sh. 8,878,906,044
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Development Division*……..……..Sh. 2,222,656,000
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*…………………...…..……...Sh. 17,883,290,400
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development Division*……………....………………..Sh. 8,583,457,730

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 99 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*..........................................Sh. 0
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*….......Sh. 31,930,522,976
Kifungu 1004 – *Veterinary Council of Tanzania*...........................Sh. 0
Kifungu 1006 – *Fisheries Laboratory Unit*..……...…....Sh. 500,000,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 1,169,808,000
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*..…….….…..…..Sh. 29,700,992,525
Kifungu 7003 – *Infrastructure Development Division*………………..…..………..Sh. 154,443,837,976
Kifungu 7005 – *Research, Training and Extension Services Division*…………………....……….....Sh. 19,455,772,197
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing Development Division*…...…...…....Sh. 32,679,092,934
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Development Division*………...….Sh. 10,569,013,208
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*…………………....………..Sh. 73,416,560,134
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development Division*…………………...…………Sh. 9,252,570,050

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa Hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Ulega, Naibu Waziri na watendaji wenu, Katibu Mkuu na wataalamu wengine hongereni sana. Kwa kweli, umeilezea na inaelekea sekta hii unaifahamu vizuri, hongera sana. *(Makofi)*

Tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji wake wakishirikiana na Serikali nzima, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na viongozi wengine wote. Tusimsahau Waziri wa Fedha ambaye na yeye amesaidia kutoa hizo pesa. Kwa hiyo, hongereni sana, bajeti yenu imepita rasmi. *(Makofi)*

Nataka tu, *for the record* ya Bunge, kuna Mbunge aliomba Mshahara wa Waziri kwa Fungu 64, hatuna Fungu 64. Kwa maana hiyo imekuwa *redundant* na amekosa fursa ambayo, ndiyo kazi za Bunge, tunakwenda kwa kanuni kama *referee,* ukikosea umekosea. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, napongeza tena, lakini naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.47 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 15 Mei, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*